JERUSALEM KATIKA QUR'ANI

Mwandishi: Imran N. Hosein

Tafsiri: Abdul Khamisi Akida

Sura ya Kwanza

UTANGULIZI

KUMBUKUMBU ZA ANSARI NAMBARI 8

Vitabu vingine vilivyojumuishwa kwenye kumbukumbu

1. Umuhimu wa kuzuia *Riba* katika Uislamu; 1977
2. Kukatazwa kwa Riba katika *Qur'ani* na *Sunnah; 1977*
3. Umma mmoja Amiri mmoja: Mpangilio wa Jamii ya Kiislamu katika zama za Majaribu; 1997
4. Dini ya Abrahamu na Nchi ya Israeli – Mtazamo wa *Qur'ani;* 1997
5. Umuhimu wa Mkakati wa Mfungo wa Ramadhani na *Isra* na *Miraj; 197*
6. Umuhimu wa Ndoto na Maono katika Uislamu – Ufunguo kwenye: Ukweli na Moyo; 1997. Toleo la Pili.
7. Khalifa – Hejaz na Nchi ya Wahhabi wa Saudia; 1997.
8. Mfungo na Uwezo Wake; 1997. Toleo la Pili.
9. Utaratibu uliomo kwenye *Qur'ani* wa Kutibu Kutawaliwa na Ulevi wa Pombe na Madawa ya Kulevya; 2000.
10. Jerusalem Katika Qur'ani; 2002. Toleo la Pili 2002.

KUMBUKUMBU ZA ANSARI

JERUSALEM KATIKA QUR'ANI

Mtazamo wa Dini ya Kiislamu juu ya Hatma ya Jerusalem

Ikijumuisha: Majibu ya Waislamu baada ya Shambulio la 9/11

Imran N. Hosein

(Tafsiri: Abdul Khamisi Akida)

Msikiti wa Jami'ah
Mji wa San Fernando
Visiwa vya Trinidad na Tobago

Haki za uchapishaji© Imran N. Hosein 2002
Barua pepe: ihosein@tstt.net.tt, inhosein@hotmail.com
Tovuti: www.imranhosein.org

Kimechapishwa tena 2011

Kimechapishwa na Masjid Jami'ah,
Mji wa San Fernando.
Mtaa wa Mucurapo na. 70
San Fernando.
Visiwa vya Trinidad na Tobago

Kimesambazwa na:
Al-Tasneen Sdn. Bhd
35-1, 1st Floor, Jalan Melati Utama 4
Melati Utama Setapak,
53100 Kuala Lumpur, Malaysia
Simu: 603-4107 2999
Faks: 603-4108 9815
Barua pepe: tasneem@streamyx.com

Msanii mbunifu wa jalada
Habibur Rahman
bouncegraphics@gmail.com

Ubunifu wa jalada umetegemea *Hadith* ya Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*):
"Wakati Dajjal (Mtume wa Uongo au Anti-Christ) atakapoachiwa, ataishi duniani kwa siku arobaini, - siku moja kama mwaka, siku moja kama mwezi, siku moja kama wiki, na siku zilizobaki kama siku zenu." (Sahih Muslim)

Kimechapishwa na
Academe Art and Printing Services Sdn. Bhd.
7, Jalan Rajawali 1A
Bandar Baru Puchong
Batu 8, Jalan Puchong
47100 Selangor

Kwa mwanafunzi wangu mpendwa toka Uturuki

Suat Levant Demirgil

Katika kuenzi mapenzi yake, kujitoa mhanga,
ukarimu wake na kujali kwake, vitu vinavyoashiria
na kunipa hisia mithili ya manukato, ya jinsi alivyonishiba.

MATOLEO YA KUMBUKUMBU YA ANSARI

Vitabu katika Matoleo ya kumbukumbu ya Ansari vinachapishwa kumuenzi Mkufunzi mashuhuri wa Kiislamu, mwanafalsafa na *Sekhe wa Kisufi*, *Maulana* Dk. Muhammad Fadlur Rahman Ansari (1914-1974). Vitabu chini ya mpango huu vimeanza kuchapishwa mwaka 1977 katika kuadhimisha miaka 25 baada ya kifo chake.

Maulana Ansari alikuwa ni Mkufunzi wa Kiislamu, mwalimu na mchungaji wa kiroho ambaye alitumia muda wote wa maisha yake katika kupigania Uislamu katika dunia ambayo imemkifu Mwenyezi Mungu. Jitihada zake katika kujaribu kutimiza lengo hili takatifu lilimlazimu kufanya safari kadhaa kuzunguka sehemu mbalimbali za dunia huku akitoa hotuba na masomo ya dini ya Kiislamu katika miaka ya 1950 hadi 1970. Alikuwa akiondoka kutoka kwenye makazi yake mapya mjini Karachi (baada ya kuhamia hapo kutoka India mnamo mwaka 1947 baada ya kuundwa kwa nchi ya Pakistani) na kuelekea Magharibi, na kisha kurejea nyumbani kwake miezi kadhaa baadaye akitokea Mashariki.

Wito na kujitolea kwake kwenye maisha kulikuwa wazi na wingi wa utakatifu. Aligundua kuwa kuurejesha Uislamu kama Utawala (Nchi), na kama mfumo wa kijamii, kiuchumi na kisiasa, hakuwezekani bila ya kurejesha imani binafsi ya kila mtu. Wakati huo huo, imani hiyo hiyo binafsi ya kila mtu ndiyo imekuwa lengo la mashambulizi makali yanayotumia nyenzo za kisasa, udanganyifu na ya hatari yasiyokuwa na kikomo, kuliko wakati wowote kabla yake katika historia ya binaadamu. Mashambulizi hayo yalianzishwa na mataifa yaliyomkifu Mwenyezi Mungu duniani, mwanzo wake kuanzia Visiwa vya Uingereza, baadaye kufuatiwa na Marekani na mwishowe na Nchi ya Israeli. Lakini, kwa wakati wote huo, mashambulizi hayo yalikuwa yanaendelea kuongozwa na Wazungu ambao wamejivalisha nguo za Wayahudi.

Hususan mapambano haya ndiyo ambayo *Maulana* alikuwa akipigana nayo katika maisha yake yote huku akizunguka dunia nzima – mapambano ya kufufua imani ya Mwenyezi Mungu, Allah, Mtukufu. Alitumia rasilimali kubwa sana aliyojaaliwa kuwa nayo, nayo ni akili timamu ikiambatana na elimu ya kina kikubwa kupigana kielimu kwa niaba ya *Uislamu*. Na alitumia mvuto wa tabia unaotokana na nguvu za kiroho kuigusa mioyo ya wale wote aloweza kukutana nao. Kutokana na kazi na jitihada zake katika kupigania Ukweli, Waislamu wengi waliokuwa Mashariki na Magharibi waliweza kurudisha na kuongeza nguvu juu ya imani zao binafsi katika *Uislamu.* Maelfu wakawa wanafunzi na wafuasi wake kiroho, na wengine wengi wakaingia kwenye Uislamu kufuatia mafundisho na hubira zake.

Maulana alikuwa amehitimu kutoka Chuo Kikuu cha Aligam, India ambapo alisomea Falsafa na Dini. Alipata mafunzo yake ya Falsafa ya Kiislamu na Elimu ya kiroho kutoka kwa Dk. Muhammad Iqbal. Iqbal ndiye mwandishi wa kitabu mashuhuri kuliko vyote katika karne hizi za mwisho katika Uislamu: "*Ujenzi (upya) wa Mawazo ya Kidini katika Uislamu*." Mchango mkubwa na mzito wa *Maulana* Ansari katika Uislamu, "*Misingi na Mfumo wa Jamii ya Kiislamu*", wenyewe ni majibu ya wito wa Dk. Iqbal katika "*Ujenzi (upya) wa Mawazo ya Kidini*."

Alipata mafunzo ya kiroho kutoka kwa *Maulana* Abdul Aleem Siddiqui, msomi wa Kiislamu, *Shekhe wa Kisufi*, na mmishenari mtembezi wa Kiislamu. Na muhimu kuliko yote, alipata mafunzo ya Kisufi ya Epistomolojia kutoka kwa wote wawili, yaani Dk. Iqbal na *Maulana* Siddiqui na akafikisha mafunzo hayo kwa wanafunzi wake. Epistemolojia ya *Kisufi* inatambua kuwa wakati mtu anapokea na

kuukubali Ukweli (anapoukubali *Uislamu*) na akaishi kwa usafi wa roho na ukamilifu wa ibada kwa Mwenyezi Mungu, mwishowe huingia moyoni (*Uislamu* unakua na kuwa *Imani*). Katika Hadithi al-Qudsi inasimulia kuwa Mwenyezi Mungu, Allah amesema:

"*Mbingu zangu na Ardhi yangu ni vidogo sana kuweza Kunitosheleza Mimi, lakini moyo wa mtumishi Wangu muaminifu unaweza kunitosheleza Mimi*." *Hadithi* hii kwa wazi kabisa inaelezea matokeo ya kuingia kwa Ukweli kwenye moyo.

Wakati Ukweli unaingia kwenye moyo, hapo nuru ya Mwenyezi Mungu huingia moyoni (*nurullah*), nuru ambayo inamwezesha muumini na kumpa nguvu za kuangalia na kuona kwa jicho la ndani la hisia za kiroho na kuweza kupenya magamba ya 'nje' na hivyo kuona ukweli halisi wa ndani wa kila jambo. Katika awamu hii ya kukua kwa Ukweli katika moyo, muumini sasa anakuwa anaona kwa kutumia macho mawili – jicho la 'nje' na jicho la 'ndani' (*Dajjal*, Mtume wa Uongo, anaona kwa kutumia jicho moja – jicho la 'nje'). Muumini ambaye anafuata '*Jihad Fillah'* (mapambano kwa ajili ya Mwenyezi Mungu) anabarikiwa kwa kukua kwa Imani kufikia hatua ya *Ihsan*. Hii pia inajulikana kwa jina kama *Tasawwuf*. Kwa kupitia hiyo nuru ya ndani, ndipo moyo wa muumini wa uhakika unapambanua kwa yakini, unazitambua na kuzielewa Alama za Mwenyezi Mungu (*Ayatullah*), na ndiyo njia pekee ya kuweza kuisoma vizuri na kuielewa vyema dunia ya leo. Wale ambao wanaweza kuutambua ukweli halisi wa dunia ya leo wanajua kwamba tunaishi kwenye zama za majaribu (*Fitan*), ikiwa ni Zama za Mwisho kabla ya *Qiyamah* (mwisho wa dunia).

Maulana Ansari alijitolea miaka yake kumi ya mwisho ya maisha yake (1964-1974) katika kuanzisha Taasisi ya Aleemiyah ya Masomo ya *Kiislamu* katika mji wa Karachi ambapo alifanya juhudi za kufundisha kizazi kipya cha wasomi wa *Kiislamu* – wasomi ambao wangeweza kwanza kuielewa dunia ya kisasa kiroho na kielimu kwa kutumia *Qur'ani* na *Hadithi*, na kisha kuweza kutoa majibu muafaka kwa changamoto hizo nzito na kali. Kutokana na jitihada zake, wamefuzu wasomi kama vile Dk. Waffie Muhammad, Dk. Abul Fadl Muhsin Ibrahim, Siddiq Ahmad Nasir, Ali Mustafa, Muhammad Ali Khan, Basheer Ahmad Keeno, Raouf Zaman, Muhammad Saffie, Imran N. Hosein na wengine wengi waliofuzu kutoka katika Taasisi ya Masomo ya Kiislamu ya Aleemiyah, Karachi, Pakistani. Toleo la Kumbukumbu ya Ansari linajumuisha vitabu vinane vifuatavyo, vyote vikiwa vimeandikwa na mmoja kati ya wanafunzi wake walioajwa hapo juu:

- *Jerusalem katika Qur'ani*
- *Dini ya Abrahamu na Nchi ya Israeli – Mtazamo wa Qur'ani*
- *Umuhimu wa kuzuia Riba katika Uislamu*
- *Kukatazwa kwa Riba katika Qur'ani na Sunnah*
- *Ndoto katika Uislamu – Ufunguo kwenye: Ukweli na Moyo*
- *Khalifa – Hejaz na Nchi ya Wahhabi wa Saudia*
- *Umuhimu wa Mkakati wa Mfungo wa Ramadhani na Isra na Miraj*
- *Umma Mmoja Amiri Mmoja – Mpangilio wa Jumuiya ya Kiislamu katika zama za Majaribu*

Toleo hilo, ambalo linaonyesha japo kwa uchache, 'matunda' ya 'mti' ambao ulipandwa na *Maulana*, vimejikita kwa nguvu zote katika kuuelewa 'ukweli' wa dunia ya leo, kuielezea kinaga ubaga, na kujibu changamoto zake ipasavyo. Jitihada hizo, bila ya shaka, siku zote ziko wazi kufanyiwa mapitio na tathmini za kifalsafa za kidini na kielimu.

Mwenyezi Mungu, Mtukufu, amewabariki waumini kwa kuwapa chombo ambacho kwacho wanaweza kupokea uthibitisho kuwa wamebarikiwa na kupewa huo uwezo wa elimu na maarifa ya 'ndani' (elimu na maarifa ambayo moyo inaona). Chombo hicho ni 'ndoto nzuri, za kweli na maono', vitu ambavyo vinajumuisha sehemu ya mwisho ya Utume, *nabuwah*, ambayo bado imebaki duniani baada ya kifo cha Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*). Toleo la Kumbukumbu ya Ansari, hivyo inajumuisha sehemu ndogo ya kazi ya awali katika fani iliyosahaulika, ikimaanisha, "*Ndoto katika Uislamu*."

Ujuzi na maarifa yanayoashiria (kupitia jicho la 'ndani') pia ndiyo chombo muhimu katika kuweza kupenya na kuona kwenye somo lenye mkakati mkubwa wa kisasa kama vile, "*Kukatazwa kwa Riba kwenye Qur'ani na Sunna*." Na "*Dini ya Abrahamu na Nchi ya Israeli – Mtazamo wa Qur'ani",* hivyo masomo hayo yamefanyiwa kazi katika toleo hili. Kwa hakika, ni kweli kusema kuwa, 'kigezo pekee kinachoweza kuchanganua' kuwepo au kutokuwapo kwa nguvu za kiroho katika hizi Zama za Mwisho kinapatikana kenye: i) uwezo wa kuwa na muono unaopenya, ukaelewa na ukatoa majibu ya kukabiliana ipasavyo dhidi ya changamoto nzito za *Riba* katika uchumi wa kisasa wa kidunia (usiokuwa wa Mwenyezi Mungu) na *Shirk* za kisiasa za Nchi zenye mfumo wa kisasa wa kidunia (usiokuwa wa Mwenyezi Mungu), na ii) uwezo wa kuwa na muono unaopenya, ukaelewa na ukatoa majibu ya kukabiliana ipasavyo dhidi ya tukio la ajabu na la kipekee katika siasa za kisasa za kimataifa, tukio la kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu na kuanzishwa kwa Taifa la Israeli. Wasomi wa *Kiislamu* wenye nuru za kiroho katika zama hizi lazima wajikite kwenye jitihada dhidi ya *Rib*a na *Shirk*

Kitu cha kustaajabisha kuliko vyote, chenye fumbo la hali ya juu na kinachokosa maelezo kuliko matukio mengine yaliyowahi kutokea kuanzia mwanzo wa historia ya dini na binaadamu ni kitendo cha kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu miaka takriban 2000 baada ya kuondolewa hapo na Mwenyezi Mungu Mtukufu. "*Jerusalem katika Qur'ani"* inaendeleza somo kuanzia pale ambapo "*Dini ya Abrahamu na Nchi ya Israeli – Mtazamo wa Qur'ani"* ilimalizia katika kujaribu kutumia *Qur'ani* kuelezea hadhi ya ya Jerusalem na kuipitia historia ya mji mtakatifu kama ilivyoelezewa katika *Qur'ani.* Muhimu zaidi, "*Jerusalem katika Qur'ani"* inajaribu kufumbua na kuelezea hatma ya Jerusalem na ile ya Ardhi Takatifu. Kilichojitokeza baada ya uchunguzi wa kina wa jambo hilo ni mchanganuo na maelezo ya kina yanayogusa na kuyahusisha matukio ya kimataifa ya kisiasa na kiuchumi ya zaidi ya karne moja yanayohusiana na tukio hilo ambalo bado linanendelea kujitokeza na kuendelea kupevuka iku hadi siku katika Ardhi Takatifu. Tunagundua pia kuwa, hivi sasa tuko katika hatua ambamo moja ya "*Nchi Tawala*", ikimaanisha Marekani, imo mbioni kubadilishwa na nafasi yake kuchukuliwa na "*Nchi Tawala*" nyingine, ikimaanisha Nchi ya Israeli, katika mfumo kama ule ambapo Uingereza ilibadilishwa kama "*Nchi Tawala*"na nafasi yake kuchukuliwa na Marekani baada ya vita kuu ya Kwanza ya Dunia. Mabadiliko hayo yalifanikishwa kwa kitendo cha kigaidi kilichotokea kiangazi cha mwaka 1914. Mabadiliko hayo hivi sasa yanatokea katika mfumo unaolingana na ule wa kabla yake. Wakati ule, mwaka 1914, wahusika waliwatuhumu Warusi kwa kitendo hicho cha ugaidi. Mara hii, wanaolaumiwa kwa kitendo cha mashambulizi ya mwezi Septemba tarehe 11 ni Waarabu na Waislamu.

Ni kwa kutumia uwezo wa ujuzi wa maarifa yanayoashiria peke yake (Firasa) ndipo mtu anaweza kuthibitisha kuwa sasa tunaishi katika zama za majaribu (*Fitan*), zikiwa ni hatua ya mwisho

katika mchakato na mpito wa historia. Ujuzi na elimu za kisayansia na za majaribio zinaweza tu kudhani, lakini hazitaweza kupenya na kuona moja kwa moja, hali halisi ya zama ambazo hivi sasa tunaishi. Hatua inayofuatia baada ya kuthibitisha kuwa tumo katika zama za majaribu (*Fitan*), ni kuwa jamii za Waislamu wa kweli (*Jama'ah*) wakiwa na *Maimamu / Maamiri* wa kweli, lazima sasa wajikusanye, wawe na washikamane pamoja, kwa nguvu kubwa zaidi hivi sasa kuliko wakati mwingine wowte, na waumini wote lazima washikamane nao kwa *as-sam'u wa-ta'-atu* (kusikiliza na kufuata amri), kwani hiyo ndiyo amri ya Mtume (*rehma na amani juu yake*). Jamii hizo ndogo ndogo za Kiislamu zikiwa na maosko yake madogo madogo zinaweza kuanzishwa vizuri tu ikiwa Waislamu wataiacha miji isiyokuwa na iliyomkifu Mwenyezi Mungu na kuhamia mashambani kuanzisha Vijiji vya Kiislamu. Kitabu, "*Umma Mmoja Amiri Mmoja – Mpangilio wa Jumuiya ya Kiislamu katika zama za Majaribu"* kinaelekeza na kufafanua suala hili muhimu. Kazi nzuri na muhimu sana aliyoifanya Dk. Ansari katika kitabu chake "*Misingi ya Qur'ani na Mfumo wa jamii ya Kiislamu"* iliyo katika sehemu mbili, pia inatoa muongozo mzuri na muhimu wa *Qur'an*i kwa wale ambao wangejikita katika jitihada hizo na ambao wangehitaji misingi ya *Qur'an*i na mfumo wa jamii ya Kiislamu (katika vijiji hivyo au Nchi hizo).

Uislamu katika hatua hizo za Vijiji vya Kiislamu (micro-*Islam*) na masoko yao umependekezwa kwa kuwa 'macro-*Islam*' (*Dar-al-Islam*) haziwezi kuanzishwa katika dunia iliyokuwa imemkifu Mwenyezi Mungu, dunia ambayo imeshikwa na wenye nguvu ambao wamo katika vita kuupiga *Uislamu*. Vita hiyo ilikwishafanikiwa kuuvunja Ukhalifa wa Kiislamu. Hivyo vita hiyo haikuanza Septemba 11 wakati Wayahudi na washirika wao walipoishambulia Marekani na kuwalaumu Waislamu. Kwa muda wote ambapo vita hiyo itakuwa ikiendelea haiwezekani kwa *Uislamu* wa kweli kuchukua Nchi yoyote ile duniani na kuanzisha utawala wa Kiislamu popote pale duniani. Sehemu pekee ambayo hilo linawezekana, ni ardhi au eneo ambalo Mtume (*rehma na amani juu yake*) alilitaja kama *Khorasan* (Afghanistan iko katikati ya *Khorasan*). Muda umefika kwa Waislamu kuamka na kugundua hali halisi na ukweli huu mchungu na kutoa majibu dhidi ya hali hiyo kwa kuelekeza juhudi zao (bila kujali watu wangapi watapoteza maisha yao na itchukua muda gani) kurudisha na kusimamisha upya *Dar-al-Islam* katika ardhi hiyo. Kiini cha wazo la 'Kijiji cha Kiislamu' kimo katika uwezekano wa kulea Waislamu ambao wangeishi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Allah, na ambao, mwisho wake, wangekufa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mmoja, Allah!

Hakuna ambaye ataweza kukabili changamoto hizo bila ya kwanza kufahamu na kuelewa asili na mfumo mzima wa changamoto hizo. "*Khalifa – Hejaz na Nchi na Taif la Wahhabi wa Saudia"* inaelezea historia katika kiwango cha 'macro'-*Islam,* Uislamu Kitaifa ambacho ni kitabu kinachojibu maswali yafuatayo:

- Nani alivunja Ukhalifa?
- Kwanini ulivunjwa?
- Jinsi gani ulivunjwa?
- Kitu gani kiliwekwa badala yake (Ukhalifa)?
- Ni namna gani dunia ya Kiislamu ilijibu tukio la kuvunjwa kwa Ukhalifa?
- Nini hatma ya Ukhalifa?

Uchunguzi wa kina wa matukio na historia kwa kutumia vyanzo visivyo na shaka vimeonyesha kuwa pamefanywa usaliti wa hali ya juu kabisa kwa dini ya *Kiislamu* uliofanywa na *Wahhabi wa Saudia* katika kuvunja Ukhalifa na kuzuia usirudishwe. Hivyo kuna kushabihiana kati ya Nchi ya Israeli (ya kidunia, isiyomtambua Mwenyezi Mungu) katika Ardhi Takatifu na Nchi ya kidunia ya Saudi Arabia katikati ya ardhi ya Kiarabu ambapo ndipo penye moyo wa *Uislamu*. Katika kuanzishwa kwa nchi hizi zote mbili, Waingereza wamejihusisha moja kwa moja. Nchi hizi zote mbili zimeweza kuwapo hadi leo kwa kusaidiwa mwanzo na (visiwa vya) Uingereza na baadaye Marekani. Nchi ya sasa ya Israel, imeanzishwa au imerejeshwa kilaghai, imewasaliti Wayahudi na inawapeleka kwenye kuangamizwa, na Saudi Arabia pia ni Nchi ya kilaghai na inatimiza lengo kama hilo kati ya Waislamu. Nchi zote mbili, Israeli na Saudi Arabia zitapata pigo hilo hilo wakati *Imam al-Mahdi* atakapojitokeza na Ukhalifa wa Kiislamu kurejeshwa, zote zitateketezwa na zitaelekezwa kwenye fuko la takataka la historia. Wafuasi wengi wa Kiislamu wa *Kisalafi* wanakubaliana na mtazamo huu kuhusu historia ya kuvunjika kwa Ukhalifa na usaliti wenye kuangamiza uliofanywa na *Wahhabi wa Saudia*.

Maulana Ansari alimtuza *Shekhe* wake, *Maulana* Siddiqui, kwa kuanzisha Taasisi ya Aleemiyah ya Masomo ya Kiislamu nchini Pakistani, na kwa kutayarisha Toleo la Kumbukumbu ya Aleemiyah. Toleo la Kumbukumbu ya Ansari, linawakilisha jaribio la jitihada za kinyenyekevu katika kufuata mfano huo mtakatifu wenye wingi wa utiifu.

YALIYOMO

Dibaji	xiv
Utangulizi kwa Toleo la Pili	xvii
Utangulizi kwa Toleo la Kwanza	xix
Ismail Raji al-Faruqi juu ya nchi ya Israeli	xxi
Vielelezo	xxii

SEHEMU YA KWANZA

Sura ya Kwanza	Utangulizi	31
Sura ya Pili	Maajabu ya Jerusalem: 'Mji' katika Qur'ani	46
Sura ya Tatu	Mwanzo wa historia ya Jerusalem katika Qur'ani: Jerusalem na Mitume	54
Sura ya Nne	Qur'ani imesema kuwa Ardhi Takatifu, ikiwemo Israeli, walipewa Wayahudi	64
Sura ya Tano	Masharti ya Mwenyezi Mungu ili kurithi Ardhi Takatifu	69
Sura ya Sita	Kuondolewa na Mwenyezi Mungu kwa Wayahudi kutoka Ardhi Takatifu kwa Kuvunja Masharti ya urithi	73
Sura ya Saba	Kugeuka (Qiblah) kutoka Jerusalem kuelekea Makkah	82
Sura ya Nane	Yesu, Mtume wa Kweli, na Dajjal, Mtume wa Uongo	91
Sura ya Tisa	Mirza Ghulam Ahmad: Mtume wa Uongo	115
Sura ya Kumi	Ya'juj na Ma'ajuj katika Qur'ani na Hadithi	124
Sura ya Kumi na Moja	Wayahudi na Waarabu	140
Sura ya Kumi na Mbili	Maelezo ya Qur'ani kuhusu Kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu	151
Sura ya Kumi na Tatu	Qur'ani na Hatma ya Jerusalem	171

SEHEMU YA PILI

Sura ya Kwanza	Ardhi Takatifu na *Shirk* ya kisiasa ya Nchi ya Israeli	179
Sura ya Pili	Ardhi Takatifu na msingi ya *Riba* ya Uchumi wa Nchi ya Israeli	207
Hitimisho		228

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho na. 1	Bahari ya Galilei	235
Kiambatanisho na. 2	Majibu ya Muislamu kwa Shambulio la Marekani	236
Kiambatanisho na. 3	Ibn Khaldun, Iqbal na Jerusalem katika Qur'ani	255
Vielelezo		257
Faharisi		258

Utangulizi

Jerusalem katika Qur'ani ni kitabu cha kusisimua na kimenifurahisha mimi binafsi kwa namna kadhaa. Nimeshangazwa kuona kuwa kitabu ambacho kinatoa maelezo ya kina na kuweka wazi vyanzo vya uchambuzi huo, kimechukua muda mwingi kuweza kuzaliwa na kuuona mwanga wa jua. Ni zaidi ya nusu karne hadi sasa tangu Wazayonisti walipoanza uonevu wao wa aibu na majaribio ya kuwafuta Wapalestina ambao kosa lao pekee ni kujikuta wanaishi kwenye nchi ambayo Wayahudi wanaiona kuwa ni ardhi yao takatifu waliyoahidiwa.

Wazayonisti wameendelea kunukuu maandiko waliyoyabadilisha toka kwenye Taurati (Torah) na Biblia kuhalalisha tabia na vitendo vyao vya kikatili na kuwahamasisha Wayahudi kuunda Taifa la Israeli ambalo litachukua eneo kutoka pembezoni mwa mito Nile hadi Euphrates na Jerusalem ikiwa ni mji mkuu wake. Mfano, David Ben Gurion, waziri Mkuu wa kwanza wa Israeli amenukuliwa akisema kuwa "Biblia ndiyo hati miliki yetu ya ardhi ya Israeli." Wasomi wa Kiislamu, kwa upande wa pili, wameshindwa kudhihirisha uongo huu kwa kutumia vyanzo halisi vya kihistoria na kidini na pia wameshindwa kutimiza wajibu wao wa kidini wa kuelezea suala hili kwa kutumia Qur'ani Takatifu na *Hadithi* za Mtume wetu mpendwa Muhammad (*rehma na amani juu yake*). Kwa jinsi ninavyojua, vyote vilivyoandikwa kuhusu suala hili vimegusia juju juu tu, na vimepaushwa na wingi wa hisia au vimekuwa vikiandikwa kuorodhesha matukio kwa muono baridi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu *Ta'ala* amlipe ndugu yetu katika Uislamu Imran Hosein kwa kuandika kitabu hiki juu ya somo hili kwa uadilifu, kina na uchambuzi wa hali ya juu. Kitabu hiki kitaziba pengo la kifikra na kielimu lililokuwapo na kutoa nafasi ya kielelezo kwa Waislamu katika pande zote za dunia. Ninavyoandika utangulizi huu, wa kitabu hiki ambacho kimeandikwa na kuchapishwa tu mwaka huu, tayari kimeshatafsiriwa kwenye lugha ya kiarabu na Kibosnia. Katika muda mfupi kitatafsiriwa kwenye lugha nyingine za bara la Ulaya na kwenye lugha zilizobaki zinazotumika na Waislamu.

Lazima iwekwe wazi kuwa umuhimu wa kuandika kitabu hiki juu ya Ardhi Takatifu katika Qur'ani havikukosa kuonwa na wataalamu na Wanafalsafa wa Kiislamu kama vile Dk. Kalim Siddiqui, Raisi-Mwanzilishi wa Kitivo cha Kiislamu cha Uchunguzi na Mipango, na Profesa *shaheed* Ismail Al-Farouqi. Nimeshangazwa na mawazo ya msomi niliyemtaja awali alipomshauri Imran Hosein aandike kitabu tangu mwaka 1974. Alimhamasisha kwa kusema kuwa Jerusalem ni ufunguo wa kuelewa mpito wa historia ya Mashariki ya Kati na dunia nzima kwa ujumla. Shekhe Imran ameweza kutimiza zoezi hilo kwa ufanisi baada ya miaka 27. Ingawa inaonekama kama amechelewa, lakini kitabu kimekuja wakati muafaka kwani dunia nzima imeshtushwa na matukio ya Jenin, Sabra na Shatila.

Ismail Al-Faruqi alilizungumzia suala hili kwenye kitabu chake "Uislamu na Tatizo la Israeli." Alisisitiza kuwa Israeli ni tishio kubwa zaidi kwa Waislamu kuliko vita vya krusedi vilivyotayarishwa na Wakristo wa Ulaya kupinga kuenezwa kwa Uislamu vya karne za kati

au hata ukoloni uliofanywa na bara la Ulaya katika miaka ya karibuni. “Israel”, aliandika “si moja kati ya hayo, lakini ni zaidi, na zaidi sana.” Aliwashauri Waarabu na Waislamu wasiikubali nchi ya Israeli kuwa kama ni mojawapo ya nchi unganifu kama sehemu ya nchi za bara la asia na Africa. Pia, aliwashauri wasomi wa Kiislamu wachunguze suala hili kwa kina. Nina hakika kuwa kama hawa wasomi na wanafalsafa mashuhuri wangekuwa hai, basi wangekisifu kitabu hiki na kukitambua kuwa ndiyo hasa kinafikisha ujumbe ambao ulikuwa ni lengo lao.

Nimeshamgazwa na ufundi na mtindo wa kibingwa wa uandishi wa Imran. Japokuwa Jerusalem katika Qur’ani kitabu kilichoandikwa kwa uchambuzi wa kina ulio oanisha nyaraka za kidini na kihistoria na matukio ya kisiasa vikiambatana na tafsiri za qur’ani na Hadithi, kinasomeka kama simulizi. Ukishaanza kukisoma, inakuwia vigumu kukiacha. Huu ni upeo wa ubora wa riwaya. Mtu anayesoma, akimaliza anakitupilia mbali – lakini si kwa hiki kitabu chenye uzito na kuhamasisha fikra ambacho ndugu yetu katika Uislamu, Shekhe Imran Hosein amekiandika. Ni kielelezo ambacho kila mmoja wetu inampasa akiweke na kukisoma tena na tena wakati wowote somo hili linapohitaji kuchunguzwa. Ninaamini kuwa ufundi huu wa kujieleza wa *Shekhe* lazima utakuwa ni ishara ya kipaji alichozaliwa nacho, ambacho amekijumuisha na kukichanganya na juhudi zake zisizokubali kuchoshwa za kuwa mhubiri na *dai’yah* rehma za Mwenyezi Mungu za kuwa msema kweli wa dhati.

Mwisho, bila kujali hali mbaya ya kusikitisha ya Waislamu kwa ujumla, na hasa ile ya Wapalestina, kukisoma kitabu hiki kunamletea mtu wimbi la vuguvugu la matumaini juu ya kipindi kijacho, mwanga mkali ambao unang’ara mwishoni mwa mfereji mrefu wa kiza cha historia yetu. Tunaishi kwenye zama za mwisho. Hiki ni kipindi ambacho utabiri wa Qur’ani Takatifu na Hadithi unafunguka mbele ya macho yetu kuwadhihirishia binaadamu juu ya ukweli wa imani na dini yetu.

Kama alivyotuambia Mtume wetu, tunawaona wachungaji masikini wa kondoo na mbuzi katika Ghuba ya Uarabu waliokuwa wakitembea miguu mitupu wakishindana katika kujenga majumba ya ghorofa ndefu na ndefu zaidi. Pia tumeshuhudia idadi ya Waislamu ikiongezeka kwa kiwango kikubwa wakati kuna upungufu wa imani na tabia za Kiislamu vyote vikifunikwa na mapenzi ya *dunia* na kuogopa kufa ikiwa ni ishara inayothibitisha ukweli uliotabiriwa na *Hadithi.* Pia kama alivyotuambia Mtume wetu, maadui wakubwa wa Waislamu sasa hivi wanazimeza nchi za Kiislamu kama vile vikundi vya waroho vilivyovamia karamu. Na pia kama Mwenye Mungu *Ta’ala* alivyotuambia katika kitabu chake alichotubainishia kupitia kwa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*), Qur’ani Tukufu, Wana wa Israeli, waliosambazwa dunia nzima, wamerudi kwenye Ardhi Takatifu. Kama Qur’ani ilivyoashiria, wamefanya vitendo vingi vya uharibifu na dhulma na wamekuwa wenye nguvu na kujiona, wenye jeuri na majivuno yasiyo kipimo.

Kama vile tulivyokuwa tukiyaangalia matokeo haya, tukiwa kama vile tunaoangalia sinema ya kutisha, ni kweli kuwa tutauona mwisho wake kama vile ilivyotabiri Qur’ani na alivyozungumza Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*). Waislamu wataamka kutoka kwenye usingizi wao mzito na Wayahudi watapata kipigo cha adhabu yao

Waliyoahidiwa na Mwenyezi Mungu. Nchi ya kizayonisti itavunjwa na vyote walivyojenga vitasagwa na kusawazishwa na ardhi.

Kitabu kinatupa na kuchambua kwa kina mlolongo wa matukio hayo kikijumuisha tafsiri mahiri toka kwenye aya za Qur'ani na *Sunna.* Ingawa wengine watapinga tafsiri ya baadhi ya aya za Qur'ani na misemo Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) iliyowakilishwa na mwandishi huyu, hakuna ambaye atashindwa kushuhudia muono wake wa kina, upeo na upenyo wa mawazo yake, ujuzi wake wa dini na kina na upevu wa kukomaa kwake kiroho. Hivyo nakipendekeza kitabu hiki kwa wasomi na wajuvi wa mambo ya dini na pia kwa wale wasiokuwa.

Malik Badri

Mkufunzi
Kitivo cha Kimataifa cha Fikra na Ustaarabu wa Kiislamu
Kuala Lumpur
Malaysia
Novemba 18, 2002; Ramadhan 13, 1423

Utangulizi kwa Toleo la Pili

Toleo hili la pili la '*Jerusalem katika Qur'ani*' limetolewa miezi tisa baada ya kitabu kuchapishwa kwa mara ya kwanza. Katika kipindi hicho, kitabu kimebarikiwa kuweza kuwa kuvunja rekodi za mauzo, 'bestseller'- kikiwa ni cha kwanza kwangu kama mwandishi. Sifa na Shukrani anastahili Allah, Mwenyezi Mungu Mkuu! Toleo hili jipya linajumuisha Utangulizi ulioandikwa na Mkufunzi mashuhuri kutoka Sudan, Profesa Malik Badri, ambaye anafundisha katika Taasisi ya Kimataifa ya Fikra na Ustaarabu wa Kiislamu, Kuala Lumpur, Malaysia. Ni mashuhuri sana kama mwandishi wa kitabu cha awali na kipekee kinachoitwa '*Mtanziko wa Wanasaikolojia wa Kiislamu'*.

Katika Sura ya Saba (*Kugeuka (Qiblah) kutoka Jerusalem kuelekea Makkah*) tumeelezea kuwa kufika kwake Madina na kuwa miongoni mwa Wayahudi, Mtume (*rehma na amani juu yake*) alisali huku akielekea Jerusalem, na alifunga pamoja na Wayahudi katika siku ambazo wao walikuwa wakifunga kufuatana na Sheria za Mfungo zilizomo kwenye Torah (Taurat). Pia tukaeleza kuwa hii ililenga kufikisha ujumbe kwa Wayahudi wa kuthibitisha madai yake kuwa yeye ni Mtume wa Kweli wa Mungu wa Abraham (*rehma na amani juu yake*). Tumeongezea katika toleo hili la pili sababu ya tatu inayohusu r*ajm* (adhabu ya kifo kwa kupigwa na mawe) (angalia sura ya saba). Kuingizwa kwa suala hili la *Rajm* kwenye somo kubwa zaidi la '*Jerusalem katika Qur'ani'* kutamwezesha msomaji wa makini kupata '*mfumo wa mantiki'* ambamo ndani yake ataweza kulisoma na kulielewa vizuri sana somo la Zina (uzinzi) katika Uislamu.

Toleo hili la pili pia linapelekwa kuchapishwa wakati kuna tishio la Marekani kutaka kuivamia Iraq na kubadili Serikali iliyopo na badala yake kuweka Serikali ya ki-*Yankee* mithili ya Serikali za Pakistani/Afghanistan, yakiwa bado hayajatokea. '*Jerusalem katika Qur'ani*' sasa inajaribu kuelezea mkakati unaopelekea kuwapo kwa mashambulizi hayo yanayotarajiwa kufanywa. Katika Sura ya Kwanza tumeitambua mipaka iliyomo kwenye Biblia ya Ardhi Takatifu (*toka mto wa Egypt hadi mto Euphrates)* kuwa ndiyo lengo kuu la eneo ambalo Israeli yenye kiburi na iliyolewa nguvu inahitaji kwa ari zote, na ambayo iko tayari kuanzisha na kupigana vita kubwa kwa ajili yake. Lakini si hulka yao wale ambao wana PhD katika *ulaghai* kupigana vita wakati wakiwa wanaonekana kuwa wao ndiyo wachokozi. Kwa hivyo, mashambulizi ya Amerika nchini Iraq yana lengo, miongoni mwa mengine, kuwasababisha Waarabu wavamie mitaa kufanya maandamano ambayo yatasababisha baadhi ya serikali zilizofungamana na Amerika ziangushwe na badala yake zije serikali za Kiislamu zinazopinga Amerika. Kampeni ya propaganda ndipo itakapoanzishwa kuonyesha picha katika fikra kuwa Nchi ya Israeli inakabiliwa na hatari juu ya usalama na kuwepo kwake kunakosababishwa na kuzungukwa na Waislamu wenye siasa kali. Wayahudi ndipo watakapoanzisha vita yao katika kutafuta kudhibiti kijeshi maeneo *toka mto wa Egypt hadi mto Euphrates.* Tunafafanua na kueleza wazi sasa, katika toleo hili la pili, kuwa, matookeo ya mkakati wa '*mto wa Egypt'* ni Wayahudi kudhibiti mfereji wa Suez na ile ya '*mto Euphrates'* ni kwa Wayahudi kudhibiti Mafuta ya Ghuba. Hayo, pamoja na kuanguka kusikoepukika kwa sarafu ya Dola za Kimarekani na, matokeo yake, uchumi wa Amerika, itasababisha kupanda daraja kwa Israeli kuwa *Nchi Tawala* duniani. Wayahudi watakuwa wamefikia hatua ambayo masishi alipaswa kuwahakikishia.

Kuchapishwa kwa kitabu hiki pamoja na hotuba zangu kuhusu somo hili tayari vimezua majibu yaliyotegemewa. Si muda mrefu uliopita nilinyimwa ruksa ya kutoa hotuba kuhusu Uislamu katika moja ya visiwa baada ya kuwa natoa hotuba nchini humo kwa takriban miaka 14.

Lakini jambo la kusikitisha zaidi kulio yote miongoni mwa majibu juu ya '*Jerusalem katika Qur'ani*' limesababishwa na waheshimiwa *Ulama* wa Kiislamu ambao kwa kifupi wamekikataa kitabu kwa misingi ya hoja kuwa Ya'juj na M'ajuj hawataachiliwa kuingia / kusambaa duniani hadi Mtume wa Kweli (*Nabii Isa rehma na amani juu yake*) atakapomuua *Dajjal*, Mtume wa Uongo (kwani hata kwa kutumia akili ya kawaida kutafakari suala hili, unagundua mara moja kuwa msimamo huo hauleti maana). Hivyo hawataki kabisa kukubali kuwa mfumo wa sasa hivi wa dunia ni ule wa Ya'juj na M'ajuj (au hata kuwa ni ule wa ndugu wa Ya'juj na M'ajuj ukitumia mfano na maelezo aliyotoa Dk Israr Ahmad), na wanasubiri kurejea kwa Mtume wa kweli *Nabii Isa rehma na amani juu yake* kwa kuachiwa kwa Ya'juj na M'ajuj. Inasikitisha kuwa wako kwenye makosa. Kwa hakika wanafanya makosa makubwa mithili ya mlima mkubwa. Makosa hayo yanawasababishia kubaki kwenye kifungo kisichowawezesha kuielewa dunia ya leo, na mbaya zaidi, kutowawezesha kutaraji matukio yanayojitokeza kiwazi katika dunia ya ajabu inayobadilika katika mwendo wa haraka. Hatimaye wanshindwa kuwa na majibu yanayojitosheleza kukabiliana na changamoto nzito za zama hizi ambazo tumo.

Hivi tunavyoelekea kuchapisha kitabu hiki, tafsiri yake katika lugha ya kiarabu inakaribia kukamilika. Tafsiri ya Kibosnia tayari imeshakamilika. Na zile za Kiurdu na Bahasa (Malaysia na Indonesia) zimo mbioni. Ahadi zimetolewa kuhusu tafsiri za Kifaransa na Kihausa. Hayo ni matokeo ya maombi yangu na sala zangu kwa kitabu hiki, kuwa kiweze kutafsiriwa katika lugha zote ambazo wanazungumza Waislamu. Sifa na Shukrani zote anastahili Allah, *Subhanahu wa Ta'al*a. Hakuna Mungu isipokuwa Yeye.

I.N.H.
Kuala Lumpur
December 2002 (Ramadhan 1423)

Utangulizi kwa Toleo la kwanza

Tendo lisilokuwa la kawaida la Ariel Sharon la kuingia kwenye *Masjid al-Aqsa* Jerusalem mnamo mwezi Septemba ya mwaka 2000 si tu lilianzisha sura mpya ya umwagaji damu kwenye ugandamizAJI wa Israeli na upinzani mpya wa Waislamu juu ya ugandamizAJI na uonevu huo, bali pia ilinisbabisha mimi nisimamishe kuandika kitabu change '*Surah al-kahf na Dunia ya (Zama za) Kisasa'* ili niweze badala yake kuandika kitabu hiki chenye kichwa '*Jerusalem katika Qur'ani'.*

Mwaka mmoja baadaye, September 11 mashambulizi ya kigaidi Amerika yalifanyika wakati nikiwa bado ni mkazi wa New York (Hivi sasa natafuta makazi mapya) na nilikuwa nakaribia kumaliza kuandika kitabu hiki. Ukweli ni kuwa kitabu nilikimalizia kukiandika mnano mwezi mtukufu wa Ramadhani nikiwa Kuala Lumpur huku nikiwa nafuatilia kwa uchungu usiosemeka kitendo cha kinyama na kisichokuwa na aibu cha kigaidi cha Wamarekani kushambulia Waislamu wasiokuwa na hatia wa Afghanistan ambao waliamua kuusimamia Uislamu.

Ni kwa bahati nzuri kuwa *Jerusalem katika Qur'ani'* kitawafikia wasomaji wakati muafaka ambamo suala hilo litakuwa liko wazo kwa binaadamu wote wanaliona. Inaonekana kuwa haiwezekani Myahudi au Mkristo aweze kulisoma na kulielewa somo hili la *Jerusalem katika Qur'ani'* na kasha ashindwe kumkubali Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake)* kama Mtume wa kweli wa Mungu wa Abraham, na kuikubali *Qur'ani* kama kitabu cha Mwenyezi Mungu. Hivyo hivyo inaonekana kuwa haiwezekani kwa Ahmadiya (mfuasi wa Mirza Ghulam Ahmad) akubali hoja za msingi na hitimisho la kitabu hiki nab ado abaki kuendelea kuwa Ahmadiya. Inabidi ieleweke wazi kuwa madai ya Mirza Ghulam Ahmad juu ya suala hili yalikuwa si ya kweli!

Kitabu cha *Shekhe* Safar al-Hawali: Siku ya Ghadhabu – "*Je, Intifada ya Siku ya Rajab ni Mwanzo Tu?*" ndiyo tu kimechapishwa na kinajumuishwa na kitabu hiki. Wasomaji wanashauriwa kukipata kitabu hicho kwenye mtandao: (http://www.islam.com/books/intifadha.htm)

Itakuwa msaada mkubwa kwa msomaji ikiwa 'kazi nyingine inayojihusisha' na kitabu hiki kwa jina: *"Dini ya Abraham na Nchi ya Israeli- Mtazamo wa Qur'ani"* kingeweza kusomwa pamoja na kitabu hiki. Kuna mifano kadhaa katika kitabu hicho cha aya za Torah na pia aya za *Qur'ani* ambazo zinatoa mwanga muhimu juu ya masuala mengi yanayojadiliwa katika kitabu hiki.

Maandishi ya kiarabu ya kutoka kwenye Qur'ani Takatifu yamejumuishwa kutilia maanani ukweli kuwa Qur'ani pekee inayotambulika ni ile iliyo katika lugha ya Kiarabu.

Mengi kati ya habari zilizowakilishwa katika kitabu hiki zinazohusu Israeli ya sasa hivi (ya kisasa) zimetoka kwenye gazeti la Kiisraeli '*The Jerusalem Post.'* Tunatambua na kukiri kuwa chanzo cha habari hizo popote msomaji anapokutana nazo kwenye kitabu hiki.

Dondoo kutoka kwenye kitabu muhimu cha Dk. Ismail Raji Faruqi, 'Uislamu *na Tatizo la Isreli'*, zimeambatanishwa kwenye kitabu hiki kwa imani kuwa, miongoni mwa mengine, itasaidia

kurudisha kwa msomi huyo mashuhuri na kwa kazi yake hiyo muhimu, daraja kubwa analostahili kupewa.

Popote linapotumika jina la 'Israeli', kwa mfano 'Nchi ya Israeli' maandishi ya kiingereza yanatumika. Hata hivyo, tunapotumia jina ambalo *Qur'ani* inalitumia kuwataja Waisraeli, '*Banu Israil'* neno (*Israil)* linawakilisha jina la Kiarabu. Aya zote za *Qur'ani* zinawakilishwa kwa kuambatanisha jina la *Sura*, likifuatwa na namba ya *Sura* na namba ya aya husika (mfano, maneno ya aya ya pili ya *Sura* ya kwanza itaonyeshwa kama ifuatavyo: *Qur'ani, al-Fatihah, 1:2)*

Nawashukuru ndugu zangu wawili wa Kiislamu wa hapa Malaysia ambao sitowataja, ambao msaada wao umeniwezesha kuandika na kuchapisha kitabu hiki. Sulaima Dufford, Muhammad Alamgir na Sabeena Watanabe wamesaidia katika kuhakikisha usahihi wa maandishi yote ya kitabu hiki na wametoa ushauri uliosaidia kwa kiasi kikubwa. Jalada la Kitabu hiki limebuniwa na msanii Habibur Rahman wa *Bounce Graphics,* Kuala Lumpur. Mwenyezi Mung awape rehma zake wote hao kwa msaada wao. *Amin*!

Namuomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu kwa anipe msamaha wake, muongozo wake, kinga zake na rehma zake. Na Namuomba Yeye akubali na kubariki juhudi hizi katika kupigania Ukweli na Akilinde kitabu hiki kutoka kwa wale wote wanaojisikia kuwa wanahatarishwa na yale ambayo kinayafichua. *Amin!* Mwenyezi Mungu ambariki mwalimu wangu mpendwa, *Maulana* Ansari (*rahmatullah 'alaihi*), ambaye amenifundisha mimi *Uislamu*, wazazi wangu, Ibrahim na Taimoon Hosein, ambao waliwafundisha watoto wao kuupenda *Uislamu* na mke wangu Aisha Angela, ambaye amesimama nami kwa dhati, kwa uaminifu, kwa kujali na kwa upendo katika jitihada zangu kwenye kupigania *Uislamu. Amin!*

INH
Kuala Lumpur
Juni 2002

Uislamu na Tatizo la Israeli

Ismail Raji Faruqi

[Dk. Faruqi anaamini kuwa Israeli inasababisha hatari kubwa zaidi kwa Waislamu kuliko hatari iliyosababishwa na krusedi za Ulaya-Kikristo za karne zilizopita, au Ukoloni wa Wazungu uliofanywa katika karne za karibuni. Hivyo anapinga wito wa kuikubali Israeli kuwa miongoni mwa wanachama wa 'ulimwengu wa mataifa ya Kiislamu ya Asia-Afrika*.']*

"Tatizo la Israeli linaloukabili Ulimwengu wa Kiislamu leo hii halijawahi kutokea na wala halina mfano wake katika historia. Ulimwengu wa Kiislamu umekuwa ukiliona tatizo hilo kama namna fulani ya ukoloni wa kisasa, au kwa uchache, marudio ya vita vya Crusedi.

Tofauti si kwamba Israeli siyo mojawapo ya hayo, bali ni yote mawili, na mengine mengi zaidi. Kwa bahati mbaya, hakuna vitabu au fikra za Kiislamu (kwenye maandishi) juu ya somo / suala hilo.

Kuhitajika kwa uchambuzi wa tatizo hili, kwa jinsi hali ilivyo, ni muhimu sana katika kipindi hiki wakati ambapo kuna wito kwa, hususan Waarabu na Ulimwengu wa Kiislamu kwa ujumla, kuikubali Israeli kama mwanachama wa ulimwengu wa mataifa ya Kiislamu ya Asia-Afrika."

Isma'il Raji Faruqi

(Dondoo kutoka kwenye kitabu: '*Uislamu na Tatizo la Israeli',* kilichochapishwa na Islamic Council of Europe, London, 1980 ISBN 0 907163 02 5).

MSAMIATI

A

Ahadith:- wingi(zaidi ya moja) wa Hadithi, ikiwa ni maneno au misemo ya Mtume
Ahl al-Dhimmah:- watu ambao wanalindwa na Dar-al-Islam
Al-Ard al-Muqaddasah:- Ardhi Tkatifu
Alim:- msomi, mtu mwenye elimu
Alhamdulillah:- Mwenyezi Mungu, Allah, asifiwe
Al-Haram al-Sharif:- maeneo, miji au wilaya ambamo ipo misikiti mitatu au nyumba za Mwenyezi Mungu zilizojengwa na Mitume Yake, ikiwa ni Makka, Madina na Jerusalem.
Al-Haramain:- maeneo matukufu, miji mitukufu au wilaya tukufu ambamo ipo Misikiti iliyojengwa na Mtume Makka na Madina.
Al-Hijr:- kwa maana ya neon kwa neon ni 'jiwe', ikimaanisha la Ka'aba
Al-Akbar:- mkubwa, mkuu, ikiwa ni Mwenyezi Mungu, Allah.
Al-Ihsan:- daraja la nguvu au uwezo wa kiroho unaowezesha kuona kwa jicho la ndani
Al-Kufru millatun wahidah:- msemo wa Mtume kuwa dunia isiyokuwa na mungu hujumuika na kuwa jamii moja.
Allahu 'alam:- Mwenyezi Mungu, Allah, ndiye anayejua vyema zaidi.
Al-Masih:- Masihi.
Al-Masih al-Dajjal: Mtume wa Uongo.
Al-Qital:- kupigana.
Amin:- na iwe hivyo.
Amir:- mtawala, wakati mwingine inatumika kama Amir al-Mu'minin au Khalifa
Amr bil ma'aruf:- kuamrisha mema
Arafat:- eneo karibu na makka, ambapo mahujaji wanapokuwa wanahiji lazima wajumuike hapo kusikiliza Hotuba ya Haji (miongoni mwa mengine)
As-sam'u wa-ta'-atu:- kusikiliza na kutii
Ayatullah:- alama za Mwenyezi Mungu, Allah.

B

Ba'i:- biashara
Bait al-Maqdis:- Jerusalem
Banu Israil:- Waisraeli (wa asili)

D

Da'abbatul Ard:- neon kwa neon ni kiumbe au mnyama wa ardhi (inawezekana Ardhi Takatifu)
Dajjal:- Mtume wa Uongo
Dar-al-Islam:- eneo lililo chini ya utawala wa Kiislamu
Dhul Qarnain:- neon kwa neon ni mwenye pembe mbili, au anayepatikana katika zama mbili mbili tofauti. Anatajwa katika Sura al-Kahf kama ni mwenye nguvu nyingi na uwezo mkubwa ambao umesimama kwa misingi ya imani. Alijenga kinga ambayo iliwazuia Y'ajuj na M'ajuj

kuweza kuwafikia binaadamu hadi Zama za Mwisho. Wakati ambapo Mwenyezi Mungu Mwenyewe ataivunja hiyo kinga na Y'ajuj na M'ajuj wattakuwa huru kuingia duniani.

Dhul Kifl:- Mtume
Dhulm:- dhuluma, ugandamizaji, uonevu
Din:- Dini, njia au mfumo wa maisha
Dukhan:- moshi
Dunyah:- dunia

F

Fasad:- uharibifu, ubovu unaoharibu
Fatwa:- msimamo wa kisheria
Firasa:- muono wa busara kwa hisia za kiroho
Fisq:- dhambi iliyo kubwa sana
Fitan:- wingi (zaidi ya moja) wa neon fitnah (tazama chini)
Fitnah:- majaribu na changamoto

H

Hadith:- msemo wa au maneno ya Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*)
Hadith al-Qudsi:- maneno ya moja kwa moja ya Mwenyezi Mungu, siyo katika Qur'ani, bali, yale Yaliyofikishwa kwa waumini kupitia kwa Mtume.
Hakimun 'Adil:- wakati Yesu atakaporejea atakuwa mtawala (atakayetawala dunia kutoka Jerusalem) na utawala wake utakuwa wa haki.
Halal:- Halali na iliyoruhusiwa na Mwenyezi Mungu, Allah.
Halim:- mwenye subira na kustahamili.
Haram:- kinyume na sheria na iliyokatazwa na Mwenyezi Mungu, Allah.
Hejaz:- Arabia ya magharibi
Hijrah:- kuhama
Hukum:- sheria na mamlaka ambayo kupitia kwayo sheria inatekelezwa.

I

Ibn Kathir:- mtoa maoni, maelezo wa Qur'ani
Idris:- Mtume
Imam:- kiongozi (kawaida anatambulika kama kiongozi wa dini). Wakati mwingine inatumika Kumaanisha Amir al-Mu'minin au Khalifa.
Imam al-Mahdi:- atokanaye na kizazi cha Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*), ambaye, Atakaporejea Yesu (nabii Isa – *rehma na amani juu yake*), atatimiza jukumu kama ambalo John the Baptist (Yahya Mbatizaji) alilitimiza la kumtambua na kumtangaza Masihi.
Iman:- imani
Injil:- injili
Insha Allah:- Ikiwa kwa utashi wa Mwenyezi Mungu, Kwa ruksa ya Mwenyezi Mungu.
Intifada:- machafuko, upinzani
Ismail:- Ismaili, au Ishmael
Islam:- dini ya kukiri, kukubali na kujisalimisha kwenye wito wa (ki) mungu kuwa ndiyo ufalme wa pekee (usiomtegemea yeyote wala chochote – zaidi ya Allah) na mkubwa na wa juu (kuliko yeyote au chochote – zaidi ya Mwenyezi Mungu – Allah).
Isra na M'iraj:- safari ya kiajabu ya Mtume (*rehma na amani juu yake*) iliyofanyika usiku kutoka Makka kwenda Jerusalem na kisha kupaa mbinguni.

J

Jama'at:- jumuiya

Jassasah:- neon kwa neno ni shushushu, mpelelezi wa siri
Jihad:- neno kwa neno ni bidii au juhudi, kitaalamu ni mapambano ya silaha
Jihad fillah:- bidii, juhudi au kupambana kwa niaba ya, kwa ajili ya Mwenyezi mungu (kwa lengo la kumfurahisha Mwenyezi Mungu na kuweza kupata njia ya kuwa karibu na Allah)
Jizyah:- kodi ya adhabu iliyowalazimu Wayahudi na Wakristo kulipa pale ambapo wanakuwa wakazi Katika Dar-al-Islam

K

Ka'aba:- Msikiti (Masjid au Hekalu) lililojengwa na Abrahamm Uarabuni. Ilikuwa ndani ya Torah Kabla haijaondolewa.
Kafir:- Yule aliyeukataa Uislamu.
Khalifah:- mrithi (anayepewa jukumu la uongozi) wa utawala wa Mtume katika Dar-al-Islam
Khorasan:- Wakati wa Mtume, Khorasan lilikuwa ni eneo kubwa sana lililojumuisha magharibi ya Pakistani hadi mashariki ya Iran ikiwemo eneo lote la Afghanistani na maeneo kaskazini ya Afghanistani.
Khutbah al-Wida:- hotuba ya kuaga ya Mtume (Mitume)
Kufr:- kukataa Ukweli huku akijua

L

Lafif:- wasio wa aina moja (mchanganyiko wa watu)

M

Maryam:- mama yake Yesu (Nabii Isa), Masihi
Masjid al-Aqsa:- Msikiti (au Hekalu) uliojengwa na Solomon Jerusalem.
Maulana:- inatumika sawa sawa na au kumaanisha Alim
Maut:- Wakati roho inapochukuliwa na hairudishwi, ikimaanisha kufa.
Muqaddamah:- utangulizi
Musnad, Ahmad:- mkusanyo (kwenye maandishi) wa Hadithi
Mustadrak, al-Hakim:- mkusanyo (kwenye maandishi) wa Hadithi
Mutawatir:- ripoti iliyokuja au kupatikana kutoka vyanzo (tofauti) zaidi ya kimoja

N

Nabuwwah:- Utume
Nafs:- (mw, w) –enyewe au roho
Nahl 'an al-munkar:- kupinga uovu, kupinga mabaya au matendo ya dhambi
Najd:- sehemu ya mashariki ya Arabia
Nurullah:- Nuru au mwnga wa Mwenyezi Mungu, Allah

Q

Qaryah:- mji au jiji
Qiblah:- mwelekeo / upande (ambao mtu /watu [w]anaelekea wakati wa sala)
Qiyamah:- mwisho wa dunia

R

Radiallahu 'anha:- Mwenyezi Mungu, Allah, yuko radhi naye (akiwa mwanamke)
Radiallahu 'anhu:- Mwenyezi Mungu, Allah, yuko radhi naye (akiwa mwanamume)

Rahman:- baraka au huruma
Rajab:- mmoja kati ya miezi inayofuata (kalenda ya) kuandama kwa mwezi
Rajm:- adhabu ya kuua kwa kupigwa mawe kwa kosa la uzinzi na uasherati
Ramadhan:- mmoja kati ya miezi inayofuata (kalenda ya) kuandama kwa mwezi
Riba:- faida

S

Sahih Muslim:- mkusanyo (kwenye maandishi) wa Hadithi
Sahih Bukhari:- mkusanyo (kwenye maandishi) wa Hadithi
Salafi:- Kikundi cha Waislamu kinachodai kuwa kinafuata Uislamu wa asili wa Waislamu wa Mwanzo. Wasalafi wanaamini kuwa Waislamu waliobaki ni *mushrikiyn* (wale wanaomshirikisha) Mwenyezi Mungu, kwa kufanya *Shirk*)
Salat:- sala au swala
Sallalahu 'alihi wa sallam:- rehma na amani za Mwenyezi Mungu juu yake
Saum:- kufunga
Shaban:- mmoja kati ya miezi inayofuata (kalenda ya) kuandama kwa mwezi
Shaikh:- mtu mzima (kwa umri) au msomi wa kidini
Sham:- Syria
Shirk:- Shirk ni kuabudu yoyote au chochote kisichokuwa Mwenyezi Mungu Mtakatifu, Allah. Kuharibu au kuchafua chochote katika ibada hiyo ya Mungu Mmoja pia ni Shirk. Shirk ni kosa Au dhambi mojawapo ambayo Mwenyezi Mungu amesema kuwa Hatoisamehe.
Shuhada:- shahidi wa dini, aliyekufa katika kupigania (njia, malengo ya) Mwenyezi Mungu
Subhanahu wa t'alah:- Ametakasika na ametukuzwa (Mwenyezi Mungu, Allah)
Sufi Shaikh:- mchungaji wa kiroho anayemuongoza mfuasi kuelekea kwenye njia ya al-Ihsan
Sunan, Abu Daud:- mkusanyo (kwenye maandishi) wa Hadithi
Sunan, Baihaq:- mkusanyo (kwenye maandishi) wa Hadithi
Sunan, Ibn majah:- mkusanyo (kwenye maandishi) wa Hadithi
Sunnah:- mfano au njia au tabia (ya Mtume)
Sura za Qur'ani:
al-'Araf:- milima
al-An'am:- ng'ombe
al-Anbiyah:- mitume
al-Baqarah:- mtamba, ng'ombe
Ale 'Imran:- familia ya Imran
al- Fatihah:- ufunguzi
al-Fatir:- kuumba kutoka kwenye asili (kuumba bila ya kuwa na kitu)
al-Fil:- tembo
al-Fussilat:- maelezo
al-Hadid:- chuma
al-Hajj:- hija
al-Hashr:- mkutaniko
al-Hujurat:- vyumba vya ndani
al-Maidah:- meza iliyotengwa chakula
al-Nahl:- nyuki
al-Naml:- mdudu
al-Nisa:- wanawake
al-Nur:- mwanga
al-Taubah:- kuungama, kukiri dhambi na kuomba msamaha
al-Zukhruf:- marembo katika dhahabu, vito vya dhahabu
al-Zumar:- vikundi (vya watu)
Sad:- kifupi (kifupisho)
Ta Ha:- kifupi (kifupisho)
Yusuf:- Joseph

T

Taliban: Muungano wa Waislamu unaojumuisha Wasomi wa Kiislamu, wanafunzi na Wakufunzi wa Deobandi (Rationalist) wa Seminari za Kiislamu wa Pakistani n Afghanistani ambao walifanya Juhudi za kuiunganisha Afghanistan baada ya kuondoka kwa Warusi chini ya utawala wa Kiislamu. Talibani walionyesha ujasiri na uadilifu wa hali ya juu na walipokataa kutii *amri* ya Kibeberu ya Amerika ya kutaka wamkamate na kuwakabidhi Usama Bin Laden.

Tamim al-Dari:- Mkristo aliyeukubali Uislamu madina na ambaye alimsimulia Mtume tokeo juu ya Dajjal ambalo Mtume alidhihirisha kuwa ni kweli.

Tasawwuf:- ni sawa na al-Ihsan

Tashbih:- kufanya kitu kiwe kichukue sura ya au kionekane kama kitu kingine (au mtu awe) aonekane kama mtu mwingine.

Taubah:- kuungama

Tur:- mlima

U

Ulama:- wasomi wa kidini

Ummah:- jumuiya

W

W'ad:- onyo

Wafat:- kutoa roho, kuchukua roho

Wajib:- kulazimu

Y

Gog & Magog:- Y'ajuj & M'ajuj ni binaadamu ambao waliumbwa na Mwenyezi Mungu ambao wamepewa uwezo ambao hakuna anayeweza kuuzuia na kuvunja nguvu zake isipokuwa Mwenyezi Mungu. Watakapoachiliwa watadhibiti dunia katika utawala ambao utapelekea dunia kuonekana kuwa inakaribia mwisho wa historia. Nguvu na uwezo wao unasimama kwa misingi ya kutomtambua Mungu na uharibifu. Pia watawasababisha binaadamu wote na kuwafanya wawe mithili yao wenyewe kwa kuanzisha jumuiya aina au namna moja kote duniani. Hiyo ndiyo haswa dunia tuliyonayo leo hii!

Yahya:- Yahya au John mbatizaji

Yathrib:- jina la zamani la mji wa Madina

Yunus:- Mtume Yona

Z

Zam Zam:- Chem chem. Ya maji ambayo kimaajabu ilijitokeza na kuwapa maji Hagar na Ismaili baada ya Abraham kutii amri ya Mwenyezi Mungu ya kuwaacha katika Jangwa la Arabia. (Biblia inadai kuwa waliachwa palestina na Zam Zam ni kisima kilichopo Palestina!)

Zina: Kujamiiana baina ya watu wasiokuwa wana ndoa.

****

Sehemu ya Kwanza

JERUSALEM KATIKA QUR'ANI

Mwandishi: **IMRAN N HOSEIN**

Tafsiri: **Abdul Khamisi Akida**

Sura ya Kwanza

UTANGULIZI

قَدْ جَآءَكُم بَصَآئِرُ مِن رَّبِّكُمْ ۖ فَمَنْ أَبْصَرَ فَلِنَفْسِهِۦ ۖ وَمَنْ عَمِىَ فَعَلَيْهَا ۚ
وَمَآ أَنَا۠ عَلَيْكُم بِحَفِيظٍ ﴿١٠٤﴾

"Zimekwisha kuja kwenu hoja (ushahidi, ishara) wazi kutoka kwa Mola wenu. Basi (yeyote) anayeziona (hizo hoja, huo ushahidi) ni kwa faida (ya roho) yake mwenyewe. Na asiyeziona (kipofu wa hizo hoja, huo ushahidi) ni khasara kwake mwenyewe. Nami sipo hapa kama mlinzi kwenu."

(Qur'ani, al-An'am, 6:104)

Qur'ani Inaelezea Vitu Vyote – Ikiwemo Hatma ya Jerusalem

Qur'ani imesisitiza kuwa kazi yake ya kwanza ni kuelezea *vitu na mambo yote*:

وَيَوْمَ نَبْعَثُ فِى كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا عَلَيْهِم مِّنْ أَنفُسِهِمْ ۖ وَجِئْنَا بِكَ
شَهِيدًا عَلَىٰ هَٰٓؤُلَآءِ ۚ وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ ٱلْكِتَٰبَ تِبْيَٰنًا لِّكُلِّ شَىْءٍ
وَهُدًى وَرَحْمَةً وَبُشْرَىٰ لِلْمُسْلِمِينَ ﴿٨٩﴾

"*.....Na Tumekuteremshia hiki kitabu (ewe Muhammad), kinachoelezea kila kitu, ni Muongozo, ni Rehema na Biashara kwa Waislamu*."

(Qur'ani, al-Nahl, 16:89)

Kwa kuwa Qur'ani imetoa maelezo kama yalivyo hapo juu, mtiririko wa mantiki unapelekea kutegemea kuwa ni lazima iweze kuelezea tukio lisilokuwa la kawaida, lisiloelezeka na la kustajaabisha kuliko matukio yote ambayo yameshawahi kutokea katika mpito wote wa historia ya binaadamu, tukio ambalo bado linanendelea kujitokeza na ambalo limeshashuhudia yafuatayo:

- Ushindi wa bara la Ulaya ambalo kiujumla halimjui wala kufuata sheria za Mungu 'kuikomboa' Ardhi Takatifu mwaka 1917-8, ushindi uliopatikana baada ya jitihada za pamoja za Wakristo wa Ulaya jitihada ambazo zilianza karibu miaka 100 iliyopita kwa vita vya krusedi.

  [**Kwanini Ulaya inayofuata mfumo wa kidunia na ambayo haiamini Mungu iamue kukomaa na kung'ang'ania kiubishi kwenye juhudi zilizoanzishwa na Wakristo wa Ulaya takriban miaka 1000 iliyopita ya kukomboa Ardhi Takatifu? Na kwanini Wakristo wa Ulaya, ambao wameshika imani ya dini ya Kikristo zaidi ya miaka 1000 ilyopita, kuwa ndiyo Wakristo pekee ambao wameling'ang'ania hilo suala la kuikomboa Ardhi Takatifu?]**

- Ushindi wa Wayahudi wa Ulaya kuweza kuirudisha nchi ya kale ya Israeli baada ya kuvunjwa na Mwenyezi Mungu zaidi ya miaka 2000 iliyopita – ushindi huu umepatikana baada ya ushirikiano wa hali na mali uliotolewa na Ulaya isiyoamini Mungu.

  [**Kwanini Ulaya isiyoamini Mungu, ing'ang'anie kwa ubishi kutaka kuwasaidia Wayahudi wa Ulaya kuirudisha nchi ya kidini iliyoanzishwa zaidi ya miaka 2000 iliyopita na Mitume David (Daud) na Solomon (Suleyman)? Kwanini Wayahudi wa Ulaya wawe ndiyo Wayahudi pekee walioling'ang'ania suala la kuirudisha nchi ya Israeli?]**

- Kurudi kwa Waisraeli wa asili (Wayahudi wasiokuwa na asili ya Ulaya) kwenye Ardhi Takatifu baada ya kusambaratishwa na Mwenyezi Mungu na ambao walikuwa wakiishi (maajabu) katika sehemu mbalimbali tofauti duniani kwazaidi ya miaka 2000 iliyopita; wayahudi wa Ulaya waliwarudisha Wayahudi wa asili bila ya wao wenyewe 'kurudi' kwenye Ardhi Takatifu kwa kuwa hawajawahi kuwa hapo kwa wakati wowote ule tangu mwanzo wa histotia – walichofanya ni kuhamia tu kwenye Ardhi Takatifu.

  [**Kwanini wakazi wa Ulaya walioingia kwenye dini ya Kiyahudi (Judaism) na baadaye kung'ang'ania jitihada za kuikomboa Ardhi Takatifu na kuwarudisha Waisraeli wa asili kwenye Ardhi Takatifu kwa 'udi na uvumba.'**

Mambo haya yote, ambayo yamejitokeza na ambayo yanaushangaza ulimwengu wote, yanaonekana kwa Wayahudi walio wengi kudhihirisha ukweli wa madai ya Wayahudi kuwa

ni ya Ukweli. Dhana hiyo inakuwa hivyo, kwa kuwa inaonekana kama vile inatimiza ahadi ya Mwenyezi Mungu aliwapa Wayahudi kuwa atawaletea Mtume, ambaye atakuwa akijulikana kama Masihi (*al-Masih* kwa kiarabu), ambaye atawarudishia yote yaliyotajwa hapo juu na mengine zaidi.

Kitabu hiki kinadai na kinaonyesha kuwa *Qur'ani* siyo tu inaelezea matukio haya ya kustaajabisha, bali pia inaendelea na kufunua mwisho na hatma ya Jerusalem. Qur'ani inaonyesha mwisho ambao utaonyesha wazi uwongo wa madai ya Wayahudi kuhusu Ukweli (uliotajwa hapo juu) na inadhihirisha Ukweli aliokuja nao Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*). Mwisho huo utashuhudia Wayahudi wakipewa adhabu kali na Mwenyezi Mungu, adhabu ambayo hajawahi kuwapa binaadamu kabla katika historia.

Kwenye kiini cha ujumbe wa Qur'ani kuhusu hatma ya Jerusalem, na Ardhi Takatifu, ni usemi kuwa awamu ya mwisho kabisa ya zama za mwisho itakapofika, Wayahudi watakusanywa kutoka nje ya nchi ambako walipelekwa na kusambazwa baada ya nchi yao kuvunjwa na kuwa watarudishwa kwenye Ardhi Takatifu kama 'vikundi vilivyochanganywa' (*Qur'ani, Banu Israil, 17:104*). Ahadi hiyo ya Mwenyezi Mungu imeshatimia. Wayahudi wamesharudi kwenye Ardhi Takatifu na wameichukua tena kwa mara nyingine. Ushindi huo unwafanya Wayahudi waamini kuwa nchi ya Israel waliyoiunda ina umuhimu na uhalali wa kidini. Kilichotokea, ni kuingizwa kwa Wayahudi katika udanganyifu mkubwa kupita kiasi, udanganyifu ambao haujawahi kutokea katika historia yote, na kwa sasa, jukwaa liko tayari kwa wao kupewa adhabu ya kali kuliko zote ya Mwenyezi Mungu ambayo haijawahi kuwakuta watu wowote katika historia. Lakni kabla ya adhabu hiyo ya mwisho ya Mwenyezi Mungu haijawakuta *Banu Israil*, kuna matukio makubwa ambayo bado hayajatokea katika Ardhi Takatifu, na kusema kweli, matukio yatakayoikumba dunia nzima. Kitabu hiki kinayachambua baadhi ya matukio ambayo bado yanaendelea kujitokeza.

Lengo la msingi la kitabu hiki ni kufafanua kuwa Uislamu una mtazamo tofauti wa mpito wa historia inavyojitokeza katika Ardhi Takatifu. Ni mtazamo ambao Israeli haina muda wa kutosha. Bahari ya Galilei punde tu itakauka! Yesu atarudi! Na kurudi kwake kutashuhudia kuvunjwa kwa Taifa la Israeli.

Wayahudi walikuwa na Ukweli ule ule ambao Waislamu wanao, isipokuwa wamebadilisha na kuharibu maandiko. Walikuwa na muda mrefu wa kutosha madina (baada ya *Hijrah*) kuweza kupokea ukweli usiokuwa na shaka uliokuja na Qur'ani na kumkubali Muhammad (*rehma na amani juu yake*), Mtume wa mwisho wa Mungu wa Abrahamu, lakini wakakataa kwa kiburi kufanya hivyo. Muda ukawa umepita kwao wakati Mwenyezi Mungu alipobadilisha *Qiblah* (*angalia Qur'ani, al-Baqarah, 2:141-145*). Hapo ikawa vigumu kwao kwa pamoja kubadili hatma yao ambayo inawakabili. Zaidi kuliko tukio jingine lolote yaliyobaki kutokea katika historia, hatma ya Jerusalem na hatma ya nchi ya Israeli, itadhihirisha madai ya *Uislamu* kuwa ndiyo Ukweli usiokuwa na shaka.

Jerusalem katika Uislamu - Matokeo na athari zake kwa Waislamu

Nini ni athari kwa wale Waislamu ambao watasoma kitabu hiki hadi mwisho?

La mwanzo ni kuwa Jerusalem na Ardhi Takatifu inabidi iwe kwenye mioyo na mapenzi yao ya hali ya juu kama vile ilivyo Makkah na Madina – na jitihada za kuikomboa Ardhi Takatifu kutoka kwenye utawala wa nchi isiyo na uhusiano na Mwenyezi Mungu ya Kiisraeli ziwe jitihada muhimu kuliko jitihada zozote kwa Waislamu. Ikiwa Myahudi anaweza kuondoka Marekani au Ulaya au Russia na kwenda kujiunga na Jeshi la Ulinzi la Israeli na kushiriki katika ukandamizaji wa kijeshi wa Waislamu na Wakristo wa Palestina katika Ardhi Takatifu, pia Muislamu awe na uhuru kama huo wa kuondoka popote alipo duniani na kujiunga na majeshi ya kupinga ukandamizaji huo (Jihad) katika Ardhi Takatifu. Waislamu lazima waonywe kuwa, watakapotangaza tu wazi imani yao kuwa nchi ya Israeli ipigwe na jeshi la Kiislamu, na kuweka wazi nia yao na utashi wa kutaka kujiunga na jeshi hilo, watatishwa na hata kuweza kukamatwa ili kuwanyamazisha na kufanywa mfano utakaowakatisha tama wengine.

Pili, pesa, rasilimali na vinginevyo vilivyomo katika mikono ya Waislamu vielekezwe katika kusaidia ukombozi wa Ardhi Takatifu kutoka kwenye ukandamizwaji.

Tatu na muhimu kuliko vyote, Waislamu (wake kwa waume) lazima wasome ujumbe wa Qur’ani kuhusiana na hatma ya Jerusalem, na kasha wawasomeshe wengine. Kitabu hiki kinajaribu kutafuta na kuweka wazi maelezo hayo na muongozo wa Qur’ani

Mkakati wa Wayahudi Wazayonisti

Upande mmoja wa mkakati wa Wayahudi-Wazayonisti umekuwa kujaribu kudhibiti mazingira yanayoizunguka Israeli kwa kujenga ushirikiano wa kujibeba na jumuiya za Kiislamu za Kiarabu zilizo jawa na kuendeshwa kwa rushwa, na mataifa yenye utajiri wa kutosha, zenye mwelekeo wa kibeberu zinazotawaliwa na wachache ambao hawana imani ya Mungu kwa niaba ya Israeli. Wachache hao wanaotawala, wanalazimika kuwa na uhusiano wa kirafiki na Israeli ili kuweza kuendelea kubaki kwenye madaraka, kutawala na kubaki na kigezo cha utajiri. Wayahudi ambao wanaisaidia Israeli wanaendelea kuweka shininkizo kwa wachache wanaotawala kuhakikisha kuwa Waislamu wanakandamizwa ili waache kuipinga Israeli au wahakikishe kuwa upinzani wao kwa Israeli hausababishi athari yoyote kwa Israeli. Wakati Israeli inaongeza ukandamizaji katika Ardhi Takatifu, na Waarabu walio wengi wanakasirishw na vitendo hivyo, hapo hao watawala wanalazimika, ili kuhakikisha usalama wao na kudumu kwao kwenye madaraka, kujiweka kwenye msimamo wa kudai kukasirishwa na vitendo hivyo vya Israeli. Uhusiano huu wa Wayahudi na Waarabu (wachache wanaotawala - elite) leo hii umefikia kiwango ch juu kabisa cha utekelezaji.... ni mkakati wa watu ambao wameacha kufuata moyo wa maadili ya dini ya Abraham (*rehma na amani juu yake*). Mkakati wa Wayahudi Wazayonisti unawalazimu kuwa siku moja wauache huo ushirikiano na watawla wachache wa Kiarabu... na mpango wa kuwaacha kwa kweli umeshaanza kutekelezwa. Hivi tunavyoandika maneno haya, tayari Israeli imeshaanza kupanga na kujitayarisha kwa vita na Waarabu-Waislamu ambao unapelekea kutanuka kwa mipaka ya Israeli. Israeli ndipo itakapoweza kutawala eneo lote la Mashariki ya Kati kama *Nchi Tawala* ya dunia (kwa kuchukua nafasi ya Marekani kama *Nchi Tawala*).

Katika kujibu mikakati hii yote ya Wayahudi ambayo ina lengo la kumpinga Mwenyezi Mungu na waumini, na kujaribu kuepuka kilichopangwa, *Qur'ani* inaeleza kuwa:

"*Na Makafiri (Wayahudi) walipanga mipango na Mwenyezi Mungu akapanga mipango, na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa wenye kupanga*."

(*Qur'ani, al-imran, 3:54*)

Katika kukamilisha mpango huo wa kishetani katika Ardhi Takatifu ndipo Israeli ilipomchukua Yasir Arafat na chama chake cha kidunia cha PLO kama mwenza wao katika mazungumzo ya amani. Mkakati huo ulifanikiwa Egypt, Jordan, Turkey na Saudi Arabia, zote zikiwa ni nchi wateja wa wale ambao hawamjui Mwenyezi Mungu – Marekani. Mkakati huo haukufanikiwa katika Ardhi Takatifu. Pia haukufanikiwa Syria na Yemeni.

Wasomaji wa kitabu hiki wangependa kutafakari juu ya sala ya Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*), ambaye aliomba kama ifuatavyo:

"Imeripotiwa na Ibn Umar: Mtume (*rehma na amani juu yake*) alisema: Ewe Mwenyezi Mungu! Tujaalie Baraka zako juu ya Sham (Syria) na Yemeni yetu. Watu wakasema: *Najd yetu (Najd ni sehemu ya Saudi Arabia ambako ni asili ya watawala wa Saudi Arabia*). Mtume akasema tena: Ewe mwenyezi Mungu! Tujaalie Baraka zako juu ya Sham ba Yemen. Nao wakasema tena: Na Najd yetu pia. Hapo Mtume akajibu: Patatokea matetemeko ya ardhi na majaribu, na kutokea huko (Najd) kutaibuka upande wa kichwa cha shetani."

(Sahih, bukhari)

Nchi ya Kiyahudi ya Israeli hadi sasa imetimiza miaka 50 tangu ianzishwe. Lakini hayo siyo mafanikio "dhidi ya matatizo" kama vile Wayahudi wangetaka tuamini. Wazayonisti ambao kwa ufupi hawamtambui na kuamini Mungu wamewadanganya *Banu Israil*, kwa mlima wa uongo! Moja kati huo uongo ilikuwa ni kauli mbiu "*ardhi isiyokuwa na watu kwa ajili ya watu wasiokuwa na ardhi.*"

Ikiwa Waarabu si 'watu', ikiwa wao ni kama 'mapanzi' kama alivyotamka aliyekuwa Waziri Mkuu wa Israeli Shamir, je, hawakuwaruhusu Wayahudi waishi pamoja nao kwa zaidi ya miaka 2000? Waarabu walihakikisha usalama wa maisha na mali za Wayahudi katika ardhi ya Waarabu kwa zaidi ya miaka 2000. Waarabu walifanya haya, na mengi mengine wakati Wakazi wa Ulaya walifunga milango kwa Wayahudi au waliwaruhusu kwa shingo upande kuishi kwenye mageto. Waarabu walifanya haya yote kwa kuwa walikuwa na 'mabaki' ya dini ya Abraham iliyowafikia kupitia kwa Ishmael (*rehma na amani juu yake*). 'Mabaki' hayo yaliwafundisha kuwa wakarimu. Hadi leo hii, ukarimu wa Waarabu bado upo. Dini hiyo hiyo ya Abrahamu ingepaswa kuwafundisha Wayahudi kuonyesha shukurani kwa ukarimu wa 'mapanzi'.

Wazayonisti wanadai kuwa Ukweli, ambao unapatikana kwenye Judaizm, umewapa Wayahudi ‘haki pekee’, ‘ya milele’ na ‘isiyokuwa na masharti’ ya kumiliki Ardhi Takatifu. Wazayonisti wanadai pia kuwa kufufua nchi ya Israeli, iliyovunjwa na Mwenyezi Mungu takriban miaka 2000 iliyopita, kunahalalisha madai ya Judaizm juu ya (wa kibeberu) Ukweli. Baada ya yote Taurat ilishasema kuwa: “*sehemu yoyote utakayokanyaga kwa mguu wako itakuwa mali yako” (Kumbukumbu ya Taurati, 11:24).* Kwa miaka hamsini tangu ilipoanzishwa nchi ya Israel, dunia imekuwa ikishuhudia kwa mshangao balaa la ‘miguu’ kwenye Israeli ambayo siku hadi siku inazidi kutanuka. Utanukaji huo bado haujaisha. Pamoja na ‘kuonekana’ kama vile Israeli imezungukwa na inahangaika kutaka kuhakikisha kuwa inajilinda vizuri kutokana na mashambulizi ya waarabu, ‘ukweli’ ni kwamba wakati kitabu hiki kinachapishwa (baada ya kuvunjwa kwa kambi ya wakimbizi ya Jenin na kuuawa kwa Waarabu wengi) Israeli inajitayarisha kufanya mashambulizi ya nguvu na vita kubwa kuwapiga Waarabu, matokeo yake ni Israeli kutanua mipaka yake hadi kufikia Ardhi Takatifu ya Biblia, ikiwa ni “*kutoka mto wa Egypt* (ikijumuisha kumiliki mfereji wa Suez) *hadi mto Euphrates* (hii ikimaanisha kuhodhi visima vyote vya mafuta vya Ghuba, ukiacha labda vile vya Iran. Bara lote la Ulaya, Japan na nchi nyingi duniani zinategemea mafuta ya Ghuba kwa kuendesha maisha na uchumi wao).” Vita hiyo, ambayo inapangwa kwa jitihada na uangalifu wa hali ya juu, pia utaifanya Israeli ichukue nafasi ya Marekani kama ‘*Taifa Tawala’* katika dunia.

Hivyo, ukiangalia kwa mtazamo wa Biblia, ushindi wa Wayahudi kuweza kurudisha Taifa la Israeli na kutanua mipaka yake, na pia kuudhibiti mji wa Jerusalem, hapana shaka kuwa madai ya Ukweli wa Judaizm yanathibitishwa.

Swali letu ni: Imewezekanaje kufanya yote haya bila ya msaada wa Masihi? Jibu ni kuwa hayo yote yamewezekana kwa kupitia udanganyifu wa Masihi wa Uongo (*al-Masih al Dajjal!*).

Pia, ukweli usiokepukika na unaotokana na mtiririko wa mantiki, ni kuwa ikiwa kinachoonekana kuwa ni ushindi katika kuifufua nchi ya Israeli kwenye mipaka yake ya asili ya Kibiblia, ni pia kuthibitisha madai ya Wayahudi kuwa Yesu na Muhammad (*rehma na amani juu yao wote*) wote ni wazushi na walaghai.

Ili Israeli ifufuliwe, Judaizm ililazimika kupachika behewa lake kwenye treni mpya, inayoongozwa na wasiomjua Mwenyezi Mungu, wakijulikana kama Utamaduni wa Kimagharibi. Utamaduni huo wa Kimagharibi, ukiongozwa na falsafa ya kutomtambua Mwenyezi Mungu, unatumia nguvu zake, utajiri wake kuwa mchezaji anayetawala katika uwanja wa dunia na kudhibiti bahari, ardhi na anga. Pia nchi ya Israeli isingeweza kudumu bila ya msaada na kinga ya nchi za magharibi zisifuata sheria za, na zisizomjua Mungu:



"*Mpaka watapo funguliwa Juju na Maajuju wakawa wanateremka kutoka kila mlima (kusambaa kwenda pande zote)"*

(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:96)

Wale Wayahudi ambao wanaunga mkono nchi ya Israeli walidai kuwa kilichotokea, na kinachoonekana kwao, ni kurudishwa kwa nchi ya Israeli kwenye mipaka ya kibiblia, lakini hawataki kugusia wala kutambua kuwa hiyo imetokea kwa kufanywa mambo mengi mabaya, ikiwemo kukandamizwa na kudhulumiwa watu wasiokuwa na nguvu, Wapalestina, wakiwemo Wakristo na Waislamu, ambao kosa pekee walilofanya inaonekana ni kuishi kwenye Ardhi Takatifu (ya Wayahudi). Uonevu huo umekuwa ukiongezeka kwa miaka hii 50. Swali letu kwa hao Wayahudi ni: Madai ya Ukweli yanaendana na kutokumtambua Mungu, kuonea, kukandamiza watu wasio na hatia, ubaguzi n.k? Je, mnaweza kupachika behewa lenu kwa wasiomtambua Mungu na kasha kudai kuwa mnafuata amri za Mungu wa Abrahamu?

Wayahudi wa Kizayonisti wananadai kuwa hawakuwafukuza Wapalestina kutoka kwenye nyumba zao, bali waliondoka wenyewe. Kama ni kweli, kwanini hao Wayahudi hawakuwaekea nyumba na mali zao kama sheria inavyowataka na kwanini hawakuwakaribisha warudi majumbani mwao? Badala yake, wayahudi wameendelea kiuchimvi kukataa kwa miaka 50 kuwapa 'haki yao ya kurudi' kwenye nyumba zao.

Utawala wa mabavu na wenye uovu wa Israeli unaendelea kuongezeka ubaya wake siku hadi siku. Israeli punde tu itafikia kilele cha 'utukufu wake wa uongo' itakapokuwa Nchi Tawala duniani. Hata hivyo, kitabu hiki kinatangaza wazi kuwa dunia inashuhudia mwanzo wa mwisho wan chi ya kilaghai ya Israel! Wayahudi wasiwalaumu Wazayonisti kwa matatizo ambayo wamejikuta wameingizwa. Walichofanya Wazayonisti ni kutumia kinyemela kila uongo ulioingizwa kwenye Biblia kwa kutengeneza kwenye kila uongo, milima ya uongo wa ziada.

Jerusalem Haiikutajwa kwa Jina katika Qur'ani

Moja ya sababu ya kuandika kitabu hiki 'Jerusalem katika *Qur'ani*' ni kujaribu kujibu hoja zilizowekwa kwenye makala ya Daniel Pipes iliyochapishwa katika gazeti la Los Angele Times (*Jerusalem ina uzito zaidi kwa Wayahudi kuliko kwa Waislamu, ya tarehe 21, Julai, 2000*). Katika makala hiyo, mwandishi amejaribu kudharau na kuondoa uwezekano wa madai ya aina yoyote ya Waislamu juu ya Jerusalem kwa kusema, miongoni mwa mengine: "Haikutajwa hata mara moja kwenye Qur'ani wala kwenye maandiko mengine ya Kiislamu...) Dk Pipes na wenziwe, wangechukua fursa hii kubadili msimamo wao, ikiwa wataweza kukisoma kitabu hiki.

Mwislamu yeyote ana wajibu wa kujibu makala kama hizo zilizojaa chuki ambazo zinaendelea kujaribu kutoa changamoto kwa *Uislamu* na *Qur'ani*, hasa wakilenga krusedi zao mpya kwa niaba y nchi ya Kiyahudi ya Israeli. Majibu siku zote lazima yawe na misingi ya kurudi kwenye ukweli, kutazama kwenye *Qur'ani.* Qurani inasema kuwa siku zote, Ukweli

ukipelekwa kwenye uongo, Ukweli daima utauzima uongo. Na waumin wameamrishwa kutumia Qur'ani wakati wanapigania haki zao dhidi ya wasioamini.

Bila kijali kama Dk pipes atakubali au atakataa 'Jerusalem katika Qur'ani' ni wazi kuwa somo hili ni msingi wa kuelewa tatizo la Israeli na Uislamu. Na huu ndiyo umuhimu wa awali wa kitabu hiki.

Jerusalem – Ufunguo wa kuielewa Dunia ya Leo

Itakuwa wazi sasa kuwa somo hili ni la umuhimu wa aina yake kwa wale Waislamu wote ambao inawabidi watoe maoni yao juu ya, au wajibu na kukabiliana na sakata linalojitokeza kwa nguvu kuhusiana na mji wa Jerusalem. Mnamo mwaka 1974, hayati Dk. Kaleem Siddique, mwanzilishi na Raisi wa Kitivi cha Kiislamu cha Uchunguzi na Mipango cha London, alimsihi mwandishi huyu kuandika kitabu ambacho kingeonyesha kuwa Jerusalem ni ufunguo wa kuelewa vyema mchakato wa historia na jinsi unavyoonekana leo. *Alhamdulillah* Kazi hiyo hivi sasa imekamilika baada ya miaka 27. Mtazamo wa Qur'ani ambao unajitokeza kwenye kitabu hiki utaonyesha wazi kuwa mtu yeyote hatoweza kuielewa dunia ya sasa bila ya kupenya kifikra kwenye hali halisi ya Jerusalem ya leo!

Nchi za Magharibi zinataka *Uislamu* ufuatwe ambao utaruhusu, miongoni mwa mambo mengine, kuikubali nchi ya Kiyahudi ya Israeli, na kutayarisha mandhari ili Waislamu waitambue na kuwa na amani nayo.... Kitabu hiki kinatoa majibu kwa mkakati huo wa Nchi za Kimagharibi, majibu ambayo yana mzizi na chanzo chake kwenye *Qur'ani* na *Hadithi* za Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*). Kitabu hiki kinafunua ukweli kuwa hapatokuwa na amani wakati wowote ujao baina ya wafuasi wa kweli wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) na nchi ya Kiyahudi ya Israeli, na kwamba wafuasi wa kweli wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) mwishowe watalishinda taifa linalokandamiza la Israel na kuikomboa Ardhi Takatifu kutoka kwenye ukandamizaji huo.

Hakuna sehemu ambayo jitihada za kufundisha *Uislamu* inabidi zifanywe ili kupata matokeo ya maana zaidi (mazuri na mabaya) kuliko kwenye vyuo vya elimu, hususan, kwenye vyuo vya elimu ya juu. Ni wazi kuwa ili elimu ya Kiislamu iweze kushikwa na kueleweka vizuri, akili ya motto na mwanafunzi lazima iwe na misingi imara ya *Qur'ani*. Somo muhimu kuliko yote ambayo yanahusiana na Qur'ani ambalo inabidi lisomeshwe kwenye vyuo vya elimu vya Kiislamu katika ulimwengu wa leo ni somo la '*Jerusalem katika Qur'ani'*. Ni kwa kupitia kwenye somo hili zaidi kuliko somo jingine lolote, ndipo Waislamu wataweza kujibu mashambulizi kutoka kwenye dunia isiyokuwa na Mungu, ambayo inawalazimisha kufanya mabadiliko kwenye imani ya dini ili kuikubali Israeli. Profesa Dk. Isma'il Raji Faruqi (*tazama dondoo kutoka katika kitabu chake*), msomi mashuhuri wa Kiislamu mwenye asili ya Kipalestina na ambaye aliuawa kwa sababu alikuwa kama mwiba unaochoma kwenye ubavu wa Israeli, aliwaonya Waislamu kuhusu hatari hii.

"Tatizo la Israeli kuikabili dunia ya Kiislamu ya leo haijawahi kutokea kabla na pia haina mafano katika historia yote ya Kiislamu. Dunia ya Kiislamu imeelekea kuliona jambo hili kuwa kama ni aina nyingine ya ukoloni, au kwa uchache, basi ni marudio ya krusedi. Tofauti ni kuwa si tu ukweli kuwa Israeli si moja ya hizo, bali ni zote mbili, na zaidi na zaidi. Kwa

bahati mbaya, hakuna vitabu vya Kiislamu vinavyohusiana na somo hili. Mahitaji ya kulichambua suala hili, ni makubwa sana kama vile yalivyo hivi sasa wakati ambao Dunia ya Kiarabu moja baada ya nyingine nchi za Kiislamu kwa ujumla zinashauriwa kuitambua Israeli kama ni mwanachama husika wa Dunia ya mataifa ya Kiislamu ya Asia-Africa."

('Uislamu na Tatizo la Israeli,' Baraza la Waislamu Ulaya, London, 1980. ISBN 0 907163 025).

Dk Faruqi aliweka wazi fikra zake kuwa Israeli ni hatari zaidi kwa Waislamu kuliko hatari inayoletwa na Krusedi za Wakristo wa Ulaya wa karne za zamani, au hata za Ukoloni wa Ulaya wa karne inayopita. Hivyo kukataliwa kwa wito wa kuitambua Israeli kama mwanachama wa 'dunia ianyojumuisha mataifa ya Asia – Africa.'

Kitabu hiki kinajaribu kwa unyenyekevu kujazia kazi ya Dk. Faruqi kwa kuwapatia, hususan, walimu wa Kiislamu mwongozo wa *Qur'ani* unaohusu Jerusalem na hatma yake. Mwalimu wa Kiislamu na Shule za Kiislamu zisiachwe zikashika msimamo usiofungamana kuhusu suala hili la '*Jerusalem katika Qur'ani'*

Wayahudi, Wakristo na Jerusalem katika Qur'ani'

Mwisho, wakati somo la 'Jerusalem katika *Qur'ani*' ni muhimu kwa Waislamu, tulikuwa na hamu sana ya kuwafikishia Wayahudi na Wakristo *Qur'ani* Tukufu. Kadiri muda unavyopita, Saa ya Mwisho inakaribia, inawawia vigumu sana Walimu na Wasomi wa Kiyahudi na Kikristo kutoa majibu yanayohusu *Qur'ani* na *Hadithi* na jinsi zinavyoelezea somo la kitabu hiki, na pia somo la Ju'ju na Ma'juju, Masihi (wa Uongo) na kurudi kwa Yesu (*rehma na amani juu yake*). Huo wote ni ushahidi unaozidi kuongezeka juu ya ukweli wa Qur'ani.

Waislamu wana jukumu la kuliwakilisha somo hili kwa Wayahudi na Wakristo, na tumefanya hivyo kwenye kitabu hiki. Kitabu mashuhuri cha *Shaikh* Safar al Hawali, *"Siku ya Hasira – Je Intifada ya mwezi wa Rajab ni mwanzo tu?"* kinajazia kitabu hiki na kinamruhusu msomaji kujifanyia uchunguzi na kufuatilia kukubaliana au kutokubaliana baina ya utabiri wa *Qur'ani* na ule wa Biblia.

Kitabu hiki kimetofautisha baina ya Wayahudi wa aina mbili. Kuna wale Wayahudi wa Kiisraeli ambao asili yao inatokana na Baba Abraham (*rehma na amani juu yake*). Ni watu wa asili ya Kisemitiki na ukaribu wao na Waarabu uko wazi. Upande wa pili, kuna Wazungu wenye macho ya bluu na nywele za blond ambao waliingia kwenye dini ya Judaizm huko nyuma lakini hawana asili, uhusiano wala si kizazi cha Abraham (rehma na *amani juu yake*). Kwa mawazo ya mwandishi huyu, na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kujua vilivyo, ni kuwa asili ya Ju'ju na Ma'juju kwa uhakika *inapatikana ndani ya vikundi* hivi vya Wayahudi wa Kizungu. Ju'ju na Ma'juju waliupindua utamaduni wa Kikristo wa Ulaya na kuubadilisha kuwa utamaduni uliopo hivi sasa usiokuwa na imani ya Mungu. Ju'ju na Ma'juju ndiyo walioanzisha harakati za Zayonisti na Nchi ya Israeli.

Hakuna shaka kuwa kitabu hiki kitasababisha mshtusho wa kisaikolojia kwa wasomaji wa wenye imani ya dini ya Kikristo, Kiyahudi, wale waliolelewa kwenye

utamaduni wan chi za Kimagharibi na hata kwa baadhi ya Waislamu. Inabidi tuweke wazi bila utata kuwa hatukuandika kitabu hiki kwa lengo la kuwakosea adabu wasomaji hao. 'Ukweli wa ndani' wa dunia ya leo, kama unavyoelezewa na *Qur'ani* ni tofauti kabisa na jinsi dunia hiyo 'inavyoonekana kwa nje' wakati watu wanatumia hilo la pili kujenga hisia na miono yao. Kuna tofauti kubwa sana, ambayo ni kama mbingu na ardhi, baina ya wale wanaotazama kwa kutumia macho mawili na wale ambao wanatazama kwa kutumia jicho moja (kwa kuwa ni vipofu wa jicho la ndani). Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alionya kuwa *Dajjal*, Mtume wa Uongo, ni kipofu kwenye jicho moja: "*Mola wako si mwenye jicho moja!"* Pia alionya kuwa zama za *Dajjal* zitakuwa ni wakati ambapo 'kuonekana' na 'ukweli' vitakuwa vitu viwili tofauti kabisa baina yao. Hakuna atakayeweza kuona 'kwa jicho la ndani' na kupenya kuufikia 'ukweli' katika zama za mwisho isipokuwa wale ambao watamfuata kwa uhakika Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*).

Tuna amini kuwa watakuwapo baadhi ya Wayahudi, ambao baada ya kukisoma kitabu hiki chenye maelezo ya Qur'ani juu ya matukio yanayojitokeza kwenye Ardhi Takatifu, wataweza, *Insha Allah*, kukubali ukweli wa *Qur'ani* na watamkubali Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) kuwa ni Mtume wa kweli wa Mungu wa Abraham.

Tafsiri na Maelezo

Kuna baadhi ya sehemu tumetafsiri maandishi ya Qur'ani sisi wenyewe pale ambapo maandishi hayo hayakuelezewa moja kwa moja aidha na Mwenyezi Mungu, Mjuzi wa Vyote, au na Mtume Wake (*rehma na amani juu yake*). Tumefanya hivyo ili kuyapata maelezo kwa ajili ya somo letu. Popote tulipofanya hivyo, tumetoa mwanya kwa wale wote ambao hawaruhusu tafsiri yoyote ya maandishi matakatifu zaidi ya maana inayotokana na maneno yaliyotumika moja kwa moja kukataa maelezo yetu. Wapo wale ambao hawakubali tafsiri yoyote nyingine zidi ya tafsiri yao wenyewe. Tunawakaribisha wale wote wanaokataa tafsiri zetu watupe 'maelezo' yao ya yale ambayo *Qur'ani* 'inaelezea' kurudi kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu.

Pili, popte tulipotafsiri maandishi ya *Qur'an*i mara zote tumeongezea sharti kuwa Mwenyezi Mungu Ndiye Anayejua Vyema (*Allhu 'alam*). Wafasiri mahsusi wa *Qur'ani* siku zote wamekuwa wakifanya hivyo, na mwandishi huyu naye amefanya hivyo!

Jerusalem na madai ya Qur'ani kuhusu Ukweli

Imekuwa si kitu cha kawaida kwenye karne hii iliyotawaliwa na elimu ya kidunia kuamua kutumia maneno ya Mungu wa Abraham (*rehma na amani juu yake*) kujaribu kuielezea na kuchambua yanayotokea duniani. Hata hivyo, hicho ndicho kilichotokea wakati Nchi ya Israeli ilipojitokeza duniani. Wazayonisti wa Kiyahudi wa Ulaya waliitumia Taurati kuwakilisha madai ya haki (waliyopewa na Mungu) yao ya kumiliki Ardhi Takatifu ili kuifufua Nchi ya Israeli (ambayo awali ilianzishwa na Mtume-Mfalme, David [Daud](*rehma*

na amani juu yake). Waziri Mkuu wa kwanza aliyekuwa na asili ya Ulaya wa Israel, David Ben Gurion, alisema: *Biblia ndiyo hati miliki yetu ya Ardhi ya Israeli*.

Tulikuwa na haki ya kutoa majibu kwa juu ya kisa cha Israeli ya Wayahudi kwa kuwakilisha msimamo unaotokana na maandishi ya *Qur'ani* peke yake. Hakuna ambaye atakuwa na haki ya kutunyima sis haki yetu hiyo, bila kujali ni kiasi gani uamuzi wetu wa kufanya hivyo utakuwa unambughudhi. Kadiri mpito wa historia utakavyokuwa unaendelea kujitokeza katika awamu hii ya mwisho wa historia, na jinsi ambavyo *Qur'ani* inazidi kuongeza uwezo wake wa kufafanua kwa uhakika matukio mbalimbali duniani nay ale yanayotokea Jerusalem leo hii, kufanya hivyo kutaendela kuthibitisha Ukweli wa *Qur'ani*. Na hiki ndicho mabacho kitabu hiki kinaeleza katika Sura ambayo yenyewe inaitwa *al-Fussilat* ("kile ambacho kimeelezewa kwa uwazi"):

سَنُرِيهِمْ ءَايَٰتِنَا فِى ٱلْءَافَاقِ وَفِىٓ أَنفُسِهِمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَهُمْ أَنَّهُ
ٱلْحَقُّ ۗ أَوَلَمْ يَكْفِ بِرَبِّكَ أَنَّهُۥ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ شَهِيدٌ ﴿٥٣﴾
أَلَآ إِنَّهُمْ فِى مِرْيَةٍ مِّن لِّقَآءِ رَبِّهِمْ ۗ أَلَآ إِنَّهُۥ بِكُلِّ شَىْءٍ
مُّحِيطٌ ﴿٥٤﴾

"*Tutawaonyesha Ishara zetu katika(yale yatakayojitokeza) katika upeo wa mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya (Qur'ani) ni kweli. Je! Haikutoshi kwamba Mola wako Mlezi kuwa Yeye ni Shahidi wa kila kitu?"*

"Ama wao wamo katika shaka ya kukutana na Mola wao Mlezi! Ama hakika Yeye ametawala (kuumba, kupanga na kuelewa) kila kitu."

(Qur'ani, al-Fussilat, 41:53-4)

Jerusalem, mji ambao ni mtakatifu kwa Waislamu, Wakristo na Wayahudi unaelekea kuchukua nafasi ya kuwamo kwenye matendo ambayo umuhimu wake haujawahi kutokea katika Mwisho wa Historia kunakojitokeza. Dini za Kiislamu, Kikristo na Kiyahudi zote zinakubaliana juu ya hili. Alama zake zimejaa, na zinaonekana wazi kwa wale waliobarikiwa kuwa na jicho la ndani la kiroho (wale ambao wanaona kwa kutumia macho mawili, jicho la

nje na la ndani) kuwa hivi sasa tunaishi kwenye Zama za Mwisho, zama ambazo zitashuhudia Mwisho wa Historia. Ni muda gani Zama hizi za Mwisho zitachukua? Lini mwishi wake utakuja kutokea? Hakuna anayejua majibu sahihi ya maswali hayo zaidi ya Mwenyezi Mungu, Allah, Mjuzi wa Yote, Mungu wa Abraham (*rehma na amani juu yake*)

Ni muhimu sana kuhakikisha kuwa mtazamo huu wa Qur'ani juu ya somo hili unawekwa wazi na kuwakilishwa mara kwa mara kwa kipindi hiki kwani Jerusalem tayari imeshaanza kuwamo kwenye matendo na matukio yatakayoipeleka kwenye hatma yake. Kitabu hiki kinaelezea matendo na matukio hayo. Ni muhimu pia kuwa nafasi ya Jerusalem katika Mwisho wa Historia inaelezewa mara kwa mara kwa kutumia hisia za jicho la ndani la kiroho kwa kadiri inavyowezekana, kwani nafasi hiyo mara nyingi ni vigumu kuiona na kuielewa kwa namna nyingine yoyote.

Lengo letu lilikuwa kuwalenga wasomaji wa kawaida. Ni muhimu sana kwao kuweza kuelewa hatma ya Jerusalem na Ardhi Takatifu, kama ilivyo katika *Qur'ani* na *Hadithi* (maneno ya Mtume Muhammad *rehma na amani juu yake*), kwa sababu ya madai yanayopingana juu ya hatma ya Jerusalem na kila dai mojawapo likisisitiza kuthibitisha Ukweli wake na kuonyesha uongo wa madai yaliyobaki.

Kwa maneno mengine, hii ina maana kuwa Wayahudi wanaamini kuwa hatma ya Jerusalem ni kuja kwa Masihi. Masihi atakapokuja, atafufua zama za dhahabu (golden age) za judaizm na atatawala dunia kutokea Jerusalem. Hiyo itathibitisha Ukweli wa Wayahudi na kuonyesha kuwa madai yanayopinga si ya kweli. Wakristo pia wana imani kama hiyo. Kuwa Yesu, Masihi atakaporudi, atatawala dunia kutokea Jerusalem na atathibitisha imani ya Utatu n.k. Hivyo Ukweli wa Ukristo utathibitishwa na madai ya waliobaki yatakuwa si ya kweli. Waislamu pia wanaamini kuwa Jerusalem ina hatma ambayo itathibitisha madai ya Uislamu kuwa ni Ukweli na kutibitisha kuwa imani zilizobaki, Ukristo na Uyahudi si za kweli. Kwa kuwa hizi imani tatu za Ukweli, zote zikidai kuwa na asili toka kwa Abraham (*rehma na amani juu yake*) zinatofautiana kwa kiwango kikubwa, haziwezi zote kuwa sahihi.

Mtazamo wa Kiislamu, kama unavyojitokeza kwenye kitabu hiki, ni kuwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) akiwa Masihi wa 'Kweli' atarudi duniani siku moja, na atakwenda Jerusalem na kutawal dunia kama *Hakimun Adil* (mtawala mwema), "*ataoa, atazaa na atakufa" "Waislamu watauswalia mwili wake na atazikwa pembeni mwa kaburi la Mtume Muhammad (rehma na amani juu yake) katika mji wa Madina, Saudi Arabia mabapo Mtume Muhammad(rehma na amani juu yake) amezikwa.* Atakaporudi "*Yesu (rehma na amani juu yake) atauvunja msalaba*" na huo utakuwa ndiyo mwisho wa Ukristo, dini ya msalaba. "*Na atawaua nguruwe*".

Amesema Abu Hurairah: Mtume wa Mwenyezi Mungu alisema: " Yule ambaye Mkononi Mwake ameshika roho yangu, mwana wa Maryamu, muda si mrefu atashuka na kuwa miongoni mwenu kama mtawala mwema. Atauvunja msalaba na atawaua nguruwe na kukataza Jizyah (kodi ya adhabu waliyokuwa wakilazimishwa Wayahudi na Wakristo waliokuwa wakiishi kwenye maeneo yaliyo chini ya himaya ya Uislamu kulipa). Kisha patakuwa na pesa za kutosha na hakuna atakayekubali kupokea zawadi ya msaada.

(Sahih Bukhari)

Neno ‘nguruwe’ haliweza kuchukuliwa kumaanisha kama lilivyo kwa kuwa tafsiri ya namna hiyo haiendani na maana ya sentensi nzima na mtiririko wa mantiki uliokusudiwa. Matumizi ya neno ‘nguruwe’ imekusudiwa kuonyesha hasira nyingi kwa muono wa kiroho. Kitabu hiki kinauliza: Ni nani watakuwa hao ‘nguruwe’ ambao watauawa na Masihi atakaporudi? Ni nani Masihi atakuwa amemkasirikia hivyo? Nani alijaribu kumsulubu?

Waislamu wanayo taarifa ya uhakika kuhusu muda ambamo Masihi Yesu (rehma na amani juu yake) atarudi. Muda huo utakuwa umetimia pale wakati maji kwenye bahari ya Galilee yatakapokuwa yamekauka.

“...Huo ndiyo muda ambapo Mwenyezi Mungu atamleta Kristo, mwana wa Maryam. Atashuka kwenye mnara mweupe upande wa mashariki wa mji wa Damascus, akiwa amevaa vipande viwili vya nguo zikiwa zimetiwa kwa uchache rangi machungwa huku akiwa ameweka mikono yake kwenye mabawa ya Malaika wawili. Atakapoinamisha kichwa chake, patadondoka matone ya jasho, na atakapokiinua, shanga kama hariri zitasambaa kutoka kichwani. Kila asiyekuwa muumini atakaponusa harufu ya mwili wake atakufa na pumzi zake zitafika mbali kiasi upeo wa macho yake. Ndipo atakapomtafuta (Dajjal) hadi atakapompata kwenye lango la Ludd na atamuua. Ndipo watu ambao Mwenyezi Mungu amewalinda watakuja kwa Yesu, mwana wa Maryam na atawasafisha nyuso zao na kuwajulisha vyeo vyao Peponi. Ni katika hali hiyo ndipo Mwenyezi Mungu atakapomfunulia Yesu maneno yafuatayo: Nimewaleta watu wenye nguvu miongoni mwa waja Wangu, watu ambao hakuna atakayekuwa na uwezo wa kupigana nao; wachukue watu hawa kwa amani hadi Tur na ndipo Mwenyezi Mungu atawaleta Ya’juju na Ma’juju na watavamia kutoka kwenye kila kilima. Wa mwanzo atapita kwenye ziwa Tiberias na kunywa maji yake. Wakati wa mwisho atakapokuwa anapita hapo atasema: Kulikuwa na maji hapa...”

(Sahih Muslim)

Bahari ya Galilee (jina jingine ni Ziwa Tiberias au Ziwa Kinneret) ina kina kidogo cha maji leoo hii kuliko wakati wowte katika historia na maji yanazidi kupungua siku hadi siku kwa kuwa Serikali ya Kiyahudi ya Israeli inateka maji kwa wingi zaidi kuliko ambavyo maji hayo kuliko ambavyo maumbile yanaweza kuyaingiza kwenye bahari. Ni rahisi kiasi hicho! Wakati maji yatakapokuwa yamekauka na hapatokuwa na maji ya kunywa, Wazayonisti wa Kiyahudi watakuwa wamefikia kilele cha harakati zao za kuwafanya Waarabu waukubali utawala wa Kiyahudi katika Ardhi Takatifu. Hiyo itamaanisha kumfuata Masihi wa Uongo badala ya Mwenyezi Mungu, Allah, Watalazimika kufanya hivyo ili wapate maji yaliyochujwa chumvi kutoka kwenye viwanda vitakavyokuwa vikifanya kazi hiyo ambavyo vitajengwa na Israeli. Waarabu watakuwa masikini sana kuweza kununua maji hayo.

Kitabu hiki kinaweka wazi kuwa kitu pekee ambacho Wayahudi hao wanapaswa kufanya ili kupima muda uliobaki kabla hawajateketezwa, ni kuangalia kiwango cha maji katika Bahari ya Galilee. Muda ambao wanausubiri, kufuatana na mkakati wao, kuwaletea ushindi wa mwisho, ni muda ambao Mwenyezi Mungu atamrudisha Masihi wa Kweli na Allah atawaangamiza Wayahudi (tazama kiambatanisho na. 1 kuhusu habari zinazoelezea kiwango cha maji katika bahari ya Galilee.)

***

Mfumo wa Kitabu

Kitabu kinaanza, kama ipasavyo, kwa kuelezea ‘maajabu’ ya Jerusalem, ‘mji’, katika *Qur’ani*. Huenda sababu ya kuupa hadhi ya maajabu ni kwa kuwa *Uislamu* unafundisha kuwa mji wa Jerusalem umepangiwa kuchukua nafasi kubwa katika matukio ya Zama za Mwisho.

Sura ya Tatu inatoa utangulizi wa suala hilo kupitia vielelezo vya *Qur’an*i juu ya Ardhi Takatifu.

Sura ya Nne inaelezea matamshi ya *Qur’ani* kuwa Ardhi Takatifu walipewa Wayahudi. Isipokuwa *Qur’ani* inaendelea kufichua ukweli kuwa mara kadhaa Wayahudi walinyimwa ruksa ya kuwa katika Ardhi Takatifu au kwa kuondolewa kutoka hapo. Hii pia ilikuwa hatma ya Ukristo wakati, kwa muda mfupi, walipouteka mji wa Jerusalem na Ardhi Takatifu.

Hayo yanatupeleka kwenye Sura ya Tano ambamo masharti ya Mwenyezi Mungu yaliyowekwa ili kurithi Ardhi Takatifu yameelezewa – masharti ambayo Wayahudi waliyavunja mara kadhaa. Mara ya mwisho waliyavunja pale walipomkataa Yesu (*rehma na amani juu yake)* kama Masihi na kujivuna kuwa wamemsulubu. Waliondolewa kutoka katika Ardhi Takatifu na kupigwa marufuku wasirudi na kuichukua upya na kuifanya mali yao hadi Y’ajuj na M’ajuj watakapowawezesha kufanya hivyo.

Katika Sura ya Sita tunaelezea maelezo ya *Qur’ani* ya kuondolewa kwa *Bani Israil* kutoka kwenye Ardhi Takatifu ikiwa ni matokeo ya kuvunja kwao kwa masharti waliyopewa na Mwenyezi Mungu. Inafuata mtiririko wa mantiki kuwa Sura ya Sita inaweka msimamo wa *Qur’ani* kuwa kuingilia kati kwa Mwenyezi Mungu na kutoa adhabu inabidi kutokee tena kwa mara nyingine kwani hivi sasa kunatokea kutofuatwa kwa misingi hiyo ya urithi wa Ardhi Takatifu!

Sura ya Kwanza nay a Pili ya Sehemu ya Pili ya kitabu inawasilisha sababu za kutosha za kisiasa na kiuchumi zinazoonyesha wazi kuwa mfumo wa kidunia wa kisiasa na kiuchumi wa Nchi ya Israeli wazi unapingana na dini ya Abraham (*rehma na amani juu yake*), na hivyo vinaashiria wazi kuvunjwa kwa masharti ya Mungu ya urithi wa Ardhi Takatifu zilizotajwa kwenye Sura ya Nne ya Sehemu ya Kwanza. Sura hizi ziliwekwa kwenye Sehemu ya Pili ili msomaji aweze kuendelea kupata historia inavyojitokeza bila ucheleweshaji kadiri kitabu kinavyozidi kufunua habari nzima.

Sura ya Saba inajaribu kuelezea athari za kubadilishwa kwa *Qiblah* kutoka Jerusalem kuelekea Makkah. Kubadilishwa huku hakuondoi haja, kwa namna yoyote, kutaka Ummah wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) kutimiza lengo la Mungu la kuivunja nchi ya Kibeberu na ya Kilaghai ya Israeli.

Baada ya Sura ya Saba sehemu iliyobaki ya Sehemu ya kwanza ya kitabu imejikita kwenye kuelezea muono na msimamo wa Kiislamu kuhusu hatma ya Jerusalem. Katika sehemu hii kunapatikana maelezo ya Qur’ani kuwa zitakapofika Zama za Mwisho, wakati ambapo wayahudi watakuwa wamekwisha chelewa kuweza kuomba na kupata msamaha wa Mwenyezi Mungu, Yeye Mwenyewe atawarejesha Wayahudi katika Ardhi Takatifu ili

waweze kuonja moja kati ya adhabu kali kuliko zote. Ili kutimiza hilo, amewatayarisha wale ambao wataifikisha adhabu hiyo kali kwa Wayahudi (hadi siku ya mwisho). *Dajjal*, Mtume wa Uongo, Y'ajuj na M'ajuj na Da'abbatul Ard (Mnyama wa Ardhi) wameumbwa na Allah kutimiza adhabu hiyo.

Mwisho wa mwisho ni pale ambapo Yesu (*rehma na amani juu yake*) atakaporejea na kumuua Dajjal, na Mwenyezi Mungu atakapowaangamiza Y'ajuj na M'ajuj. Wakati huo, amesema Mtume (*rehma na amani juu yake*), jeshi la Kiislamu kutoka Khorasan (ambapo Afghanistan ni moyo [katikati ya] wa eneo hilo) litateka na kuendelea mbele wakati hakuna atakayeweza kulizuia hadi litakapofika Jerusalem. Hapo Ardhi Takatifu itakuwa imekombolewa na dini ya Kweli ya Abraham itakuwa imesimamishwa upya na kutawala katika Ardhi Takatifu.

Masihi wa 'kweli' atweza kutawala dunia kutokea Jerusalem, kama vile ambavyo Wayahudi waliamini kuwa ndivyo itakavyotokea. Lakini hawatoweza kujumuika kwenye kufurahia kutimia kwa utabiri huo kwani *Dajjal*, Mtume wa uongo, amewadanganya. Athari ya kudanganywa huko na kumuamini yeye, kumfuata Masihi wa Uongo, badala ya Yesu, Masihi wa Kweli (*rehma na amani juu yake*).

Sura ya 2

MAAJABU YA JERUSALEM, 'MJI', KATIKA QUR'ANI


وَحَرَٰمٌ عَلَىٰ قَرۡيَةٍ أَهۡلَكۡنَٰهَآ أَنَّهُمۡ لَا يَرۡجِعُونَ ٩٥
حَتَّىٰٓ إِذَا فُتِحَتۡ يَأۡجُوجُ وَمَأۡجُوجُ وَهُم مِّن كُلِّ حَدَبٖ
يَنسِلُونَ ٩٦

"Na tumeweka kizuizi (kwa watu) wa mji Tulioteketeza: kuwa wao (watu wa mji huo) hawatarejea (kuuchukua mji wao) hadi watakapofunguliwa Ju'ju na Ma'juju na (hatimaye) kuteremka kutoka katika kila kilima (au kusambaa kwenda kila upande)."

(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:95-6)

(*Ya'juj na Ma'juj wakishateremka watamiliki na watatawala dunia kwa Mfumo wa Dunia wa Ya'juj na Ma'juj***)**

Ni kitu cha ajabu, cha kushangaza nakisichokuwa cha kawaida... kuwa jina la mji 'Jerusalem' (Kiarabu '*Quds*, au *Bait al-Maqdis*) halipo kwenye *Qur'ani*! Wakati Mitume wengi waliotajwa kwenye Qur'ani wanahusishwa na Mji Mtakatifu, na katika mji huo kuna Nyumba pekee iliyojengwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu, ukiacha zile zilizojengwa Makkah na Madina. Pia si hivyo tu kuwa Nyumba hiyo ya Mwenyezi Mungu (*Msikiti wa al-Aqsa*) haukutajwa kwenye *Qur'ani*, bali hata safari ya kiajabu ya usiku ambamo Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alipochukuliwa kutoka Makkah hadi Jerusalem na kwenye Nyumba hiyo ya Mwenyezi Mungu, haikutajwa kwa jina. Huenda sababu ya kulichukulia jambo hili kwa hali hii isiyo ya kawaida inapatikana kwenye mtazamo wa Kiislamu kuwa Jerusalem imepangwa kuchukua nafasi kubwa na ya umuhimu wa hali ya juu katika Zama hizi za Mwisho. Hivyo, pakawa, inawezekana, umuhimu wa kiroho wa kulificha jina la mji, pamoja na hatma yake, kwa kiwingu cha utakatifu, ambacho hakitafunuliwa hadi muda wake utimie, na Jerusalem ikawa imejitenga na kuwa tayari kuchukua nafasi yake katika matukio ya Mwisho wa Historia.

Hii, huenda, inaelezea kutokuwepo kabisa kwa maandishi na vitabu vya Kiislamu kuhusu somo la hatma ya Jerusalem, kitu ambacho Dk. Ismail Raji Faruqi alichokigusia

alipolalamika: "*Kwa bahati mbaya hakuna vitabu vyovyote vya Kiislamu juu ya somo hili*" (Tazama Sura ya 1). Ukweli ni kuwa hakuna mtu ambaye angeweza kuandika chochote juu ya somo hili hadi muda wake uwe umekomaa kwa kufunuliwa kiwingu kilichofunika.

Wakati Wayahudi walipomkataa Yesu (*rehma na amani juu yake*) kama Masihi na baadaye kujisifu kuwa wamemuua (*Tazama Qur'ani, al-nisa, 4:157*), walibaki na uhakika kuwa bado atakuja Masihi Aliyeahidiwa (ambaye kuja kwake, kutawarudishia Zama za Dhahabu za Judaizm). Waliamini kuwa kurudi kwa Zama za Dhahabu kunahitaji, miongoni mwa mengine, ni mambo yafuatayo:

- kuwa Ardhi Takatifu itakombolewa kutoka kwa Wageni / Mataifa,
- kuwa Wayahudi watarudi kwenye Ardhi Takatifu kutoka nje ugenini na kuichukua tena,
- kuwa Nchi ya Israeli itafufuliwa,
- kuwa Hekalu (au *Msikit*i) utarudishwa (kwa Wayahudi) kwa ibada ya Mungu wa Abraham,
- kuwa Israeli itarudi kuwa *Nchi Tawala* duniani katika hali kama ilivyokuwa wakati wa David [Daud](*rehma na amani juu yake*) na Solomon [Suleyman](*rehma na amani juu yake*),
- kuwa Mfalme wa Kiyahudi, ambaye atakuwa ni Masihi, atatawala dunia kutoka kwenye kiti cha enzi cha ufalme cha David[Daud] (*rehma na amani juu yake*), ikimaanisha, kutoka Jerusalem kama mtawala wa Israeli na mwisho,
- kuwa utawala wake utakuwa ni wa milele.

Mtume Muhammad(*rehma na amani juu yake*) alisema kuwa moja kati ya alama kubwa za Siku ya Mwisho ni kuwa Mwenyezi Mungu atawadanganya Wayahudi kwa kumleta na kuwapelekea atakayejifanya Masihi na kuwafanya waamini kuwa Zama za Dhahabu zinarudi. Lakini, badala yake, Masihi huyo wa Uongo atawafanyia udanganyifu wa hali ya juu na kuwafanya wapewe adhabu kali, adhabu ambayo haijawahi kupewa viumbe wowte miongoni mwa viumbe wa Mwenyezi Mungu. *Al-Masih al-Dajjal* au *Dajjal*, Masihi wa Uongo, ambaye pia anajulikana na Wakristo kama Anti-Christ, aliumbwa na Mwenyezi Mungu na ataachiliwa aingie duniani katika Zama za Mwisho ili kutimiza kazi yake. Hebu angalia yafuatayo:

- ✓ Ardhi Takatifu 'ilikombolewa' (kwa mtazamo wa Wayahudi) kutoka kwenye utawala wa 'wageni' Waislamu wakati Jenerali wa Kiingereza, Allenby, alipoiteka Jerusalem kutoka kwa Waislamu wa Kituruki mwaka 1917;

- ✓ Wayahudi wa Asili hivi sasa 'wamesharudi' na kuihodhi tena Ardhi Takatifu baada ya kufukuzwa kwa amri ya Mwenyezi Mungu na kuwa ugenini kwa miaka takriban 2000. Hii imetokea kama vile ambavyo *Qur'an*i miaka 1400 iliyopita ilielezea kuwa itatokea wakati wa 'Wakati wa Mwisho'. Wayahudi waliobaki wenye asili ya Kizungu pia wanatarajiwa kuelekea huko muda mchache ujao;

- ✓ Nchi ya Israeli ilifufuliwa mnamo mwaka 1948 na inadai kuwa ni endelezo la Nchi ya Israeli ya asili;

- ✓ Israeli ambayo ina silaha za nyuklia inaonekana iko tayari kutumia machafuko ya wapalestina ya Intifada na mashambulizi ya Mossad ya Septemba 11 (ambayo yamesababisha mazingira muafaka kwa Israeli) kwa kuanzisha vita bila kujali matakwa na vipingamizi vya Marekani, nchi za bara laUlaya, Umoja wa Mataifa na duinia nzima, ili kukamata maeneo yote ya nchi zinazoizunguka. Vita hiyo ya Israeli, huenda ikapelekea kutanua ardhi ya Nchi ya Israeli kufikia ile iliyotajwa kwenye Taurati, ikimaanisha kutoka kwenye mto wa Egypt hadi kwenye mto Euphrates. **Kwa kufanikisha vita bila kuijali dunia nzima, ikiwemo Marekani, ukitilia maanani kuanguka kunakotarajiwa kwa Dola ya Marekani pamoja na uchumi wake**, nchi ya Ulaya-Israeli hatimaye itaweza kupanda daraja kutoka nchi tegemezi na kuwa Nchi Tawala duniani kijeshi na kiuchumi na hivyo kuchukua nafasi ya Marekani na Uingereza, hivyo kuhalalisha madai yake ya 'uongozi' wa dunia na kudhibiti dunia kwa mithili ambayo Uingereza wala Marekani hazikuweza kufikia.

- ✓ Kitendo kinachotabirika cha kuvunjwa kwa Masjid al-Aqsa na kulijenga upyaHekalu la Kiyahudi kwenye eneo husika kutatokea. Utabiri wa Mtume Nathan aliyesema "Masihi atajenga Nyumba ya Mungu" (1 Chronicles 17:11-15) kunaonyesha kuvunjwa kwa msikiti uliopo.

Matukio haya yote [itakuwa] yanaonyesha kwa wayahudi kutimia kwa utabiri uliolenga kurejea kwa Zama za Dhahabu wakati Solomon / Suleyman (*rehma na amani juu yake*) alipotawala dunia kutokea Jerusalem. Kwa maoni ya kitabu hiki, juu ya yote, hakuna ambacho kingeweza kutokea bila ya mkono wa *Dajjal*, Mtume wa Uongo. Hivyo, yote yaliyotokea na kutajwa hapo juu ni udanganyifu. Badala yake, Israeli ya Ulaghai imewekwa kuchukua nafasi ya Israeli ya kweli (ambayo mwanzoni ilianzishwa na Mtume Solomon). Ni wazi kwa muandishi huyu kuwa sasa kiwingu cha udanganyifu kimenyakuliwa na "Siku za Mwisho" zimefika na haiwezekani tena kubadilika kwa mwelekeo kwa Wayahudi. Hiyo pengine ndiyo sababu kwanini kuandika kitabu kama hiki kunawezekana. Qur'ani inaelezea matukio haya yote. Maelezo hayo, si rahisi kuonekana na kueleweka kwa urahisi na mara moja. Mengi ya hayo, hata hivyo, yameelezewa katika kitabu chetu, "*Dini ya Abraham naNchi ya Israeli – Mtazamo wa Qur'ani."*

Qur'ani imeizungumzia Jerusalem, mara nyingi, kama 'mji' - lakini bila kuutaja kwa jina.... Hii inawezekana kusababishwa na hicho kiwingu cha kiroho kinacholizunguka suala zima la Jerusalem na umuhimu wake unaotarajiwa katika Zama za Mwisho. Kwa mfano, *Qur'ani* inaelezea kisa cha Wayahudi wa Kiisraeli walipomuabudu ndama wa dhahbu wakati Mtume wao, Musa (*rehma na amani juu yake*), alipopanda juu ya Mlima Sinai baada ya kuashiriwa na kuitwa na Mwenyezi Mungu afanye hivyo. *Qur'ani* ilionya kuwa kuabudu yoyote au chochote zaidi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kutawaletea adhabu ya Mwenyezi Mungu:

إِنَّ ٱلَّذِينَ ٱتَّخَذُوا۟ ٱلْعِجْلَ سَيَنَالُهُمْ غَضَبٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَذِلَّةٌ فِى
ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا ۚ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِى ٱلْمُفْتَرِينَ ﴿١٥٢﴾
وَٱلَّذِينَ عَمِلُوا۟ ٱلسَّيِّـَٔاتِ ثُمَّ تَابُوا۟ مِنۢ بَعْدِهَا وَءَامَنُوٓا۟ إِنَّ رَبَّكَ مِنۢ
بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٥٣﴾

"*Hakika wale walio muabudu ndama (wa dhahabu) (hivyo kutenda Shirk) (na yeyote baada ya hapo atakayetenda shirk – kumshirikisha Mwenyezi Mungu), itawapata ghadhabu ya Mola wao Mlezi na madhila (aibu) katika maisha ya dunia. Na hivi ndivyo tunavyo walipa wazushi (wanaomzulia Mwenyezi Mungu). Isipokuwa wale ambao wanatenda makosa na kisha wakatubu na wakaamini (kikweli) hakika Mola Wako ni Mwenye Kusamehe na Mwingi wa Huruma.*"

(Qur'ani, al-Araf, 7:152-3)

Qur'ani imeendelea kuelezea tukio jingine wakati wakiwa bado Sinai, kabla hawajaruhusiwa kuingia Ardhi Takatifu, na inasema:

وَقَطَّعْنَٰهُمُ ٱثْنَتَىْ عَشْرَةَ أَسْبَاطًا أُمَمًا ۚ وَأَوْحَيْنَآ إِلَىٰ مُوسَىٰٓ إِذِ
ٱسْتَسْقَىٰهُ قَوْمُهُۥٓ أَنِ ٱضْرِب بِّعَصَاكَ ٱلْحَجَرَ ۖ
فَٱنۢبَجَسَتْ مِنْهُ ٱثْنَتَا عَشْرَةَ عَيْنًا ۖ قَدْ عَلِمَ كُلُّ أُنَاسٍ
مَّشْرَبَهُمْ ۚ وَظَلَّلْنَا عَلَيْهِمُ ٱلْغَمَٰمَ وَأَنزَلْنَا عَلَيْهِمُ ٱلْمَنَّ
وَٱلسَّلْوَىٰ ۖ كُلُوا۟ مِن طَيِّبَٰتِ مَا رَزَقْنَٰكُمْ ۚ وَمَا ظَلَمُونَا
وَلَٰكِن كَانُوٓا۟ أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١٦٠﴾

"*Na tuliwagawanya katika makabila kumi na mbili, mataifa mbali mbali. Na tulimfunulia Musa walipo muomba maji watu wake kumwambia: 'Lipige hilo jiwe kwa fimbo yako.' Mara zikatibuka humo chemchem kumi na mbili, na kila watu wakajua mahali pao pa kunywea. Na tukawafunika kivuli kwa mawingu, na tukawateremshia Manna na Salwa. Tukawaambia: 'Kuleni vizuri hivi tulivyo kuruzukuni.' (lakini wakavunja amri tena) Wala hawakutu dhulumu Sisi, bali wamejidhulumu wenyewe."*

(Qur'ani, al-Araf, 7:160)

Ni baada ya tukio hili ndipo *Qur'ani* ikaitaja Jerusalem katika hali ya usiri wa namna fulani kama 'mji':

وَإِذْ قِيلَ لَهُمُ ٱسْكُنُوا۟ هَٰذِهِ ٱلْقَرْيَةَ وَكُلُوا۟ مِنْهَا حَيْثُ
شِئْتُمْ وَقُولُوا۟ حِطَّةٌ وَٱدْخُلُوا۟ ٱلْبَابَ سُجَّدًا نَّغْفِرْ لَكُمْ
خَطِيٓـَٰٔتِكُمْ ۚ سَنَزِيدُ ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿١٦١﴾

"*Na pale walipo ambiwa: Kaeni katika mji huu, na mle humo mpendapo, na semeni: Tufutie dhambi zetu. Na ingieni katika mlango wake kwa unyenyekevu, tupate kukusameheni makosa yenu. Walio wema tutawazidishia*."

(Qur'ani, al-Araf, 7:161)

Pia pana aya nyingine katika *Qur'an*i yenye kutaka kisiri Jerusalem kama 'mji':

وَحَرَٰمٌ عَلَىٰ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَٰهَآ أَنَّهُمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿٩٥﴾
حَتَّىٰٓ إِذَا فُتِحَتْ يَأْجُوجُ وَمَأْجُوجُ وَهُم مِّن كُلِّ حَدَبٍ
يَنسِلُونَ ﴿٩٦﴾

"*Na haiwi (tumewazuia) kwa wana-mji tulio uangamiza (kurejea) [ikimaanisha Jerusalem], ya kwamba hawatarejea"*

"Mpaka watapo funguliwa Y'ajuj na M'ajuj wakawa wanateremka kutoka kila mlima au kusambaa katika kila upande."

(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:95-6)

Wanapokuwa wanateremka kutoka kila mlima au kusambaa katika kila upande, kwa ujumla, wanachukua madaraka na kutawala dunia katika Mfumo wa Dunia wa Ju'ju na Ma'juju.

Ili kutambua ni mji gani unazungumziwa katika aya hapo juu, tumeziangalia kwa kina aya zote za *Qur'ani* na Hadithi zote zinazozungumzia *Y'ajuj na M'ajuj*. Tumegundua kuwa kuna mji mmoja tu unaozungumziwa unaounganisha habari zao. Nao ni mji wa Jerusalem (tazama Sura ya 10, sehemu ya 1). Hivyo tumefikia baada ya kuelekezwa na ishara, na ushahidi wa kutosha kuwa mji unaozungumziwa kwenye aya zilizotajwa hapo juu kwenye *Qur'ani* ni Jerusalem!

Tunapogundua kuwa Jerusalem kuwa ndiyo mji unaokusudiwa, inakuwa wazi kuwa kiwingu kilichopo kwenye *Qur'ani* kitafunuliwa pale ambapo *Y'ajuj na M'ajuj* watakapofunguliwa na kushuka katika kila mlima au kusambaa katika kila upande (na kutawala dunia katika mfumo wa Y'ajuj na M'ajuj. Kurudi kwa Waisraeli wa Kiyahudi kwenye Ardhi Takatifu kunathibitisha kuwa Y'ajuj na M'ajuj tayari wameshaachiwa na *wanmeshateremka kutoka kila mlima au kusambaa katika kila upande,* na hivyo tayari wameshatawala dunia. Mfumo unaotawala dunia ya leo ni mfumo wa *Y'ajuj na M'ajuj*. Kwa hakika ni *Y'ajuj na M'ajuj* ndiyo walioweza kusababisha kutokea kwa kitendo cha Wayahudi wa Asili kurudi Israeli.

Baada ya kujua hilo, sasa tunaweza kujiweka vizuri katika kutaraji mkakati, ambao kwao, *Dajjal*, Mtume wa Uongo, ataendelea kuwadanganya Wayahudi kuwa anawarudishia Zama za Dhahabu. Mkakati huo unaonyesha kuanza kutekelezwa pale ambapo *Dajjal* alipoanzia Uingereza (angalia *Hadithi ya Tamim al-Dari* kwenye *Sahih Muslim*) na kuubadilisha utamaduni wa bara la Ulaya kutoka kwenye imani ya Kikristo na kuliingiza kwenye kutoamini Mungu na kulipa... nguvu na uwezo mkubwa wa kuweza kufanya chochote iachotaka kufanya. Mkakati huo ulishuhudia kuanzishwa kwa ushirika wa Wazayonisti, ambao nao wakaanzisha Taifa la Israeli. Mpango huo unaonyesha pia kujumuisha kutawala eneo lote ambalo limepakana na Ardhi Takatifu, na hiyo ni njia kuelekea kutawala dunia nzima, lengo ambalo *Dajjal* lazima alitimize ili Wayahudi waweze kumkubali kama Masihi wa Kweli. Kiini cha mkakati wote ni kuwepo umuhimu wa kudhibiti mali na maji. Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ameelezea kiunganisho baina ya *Dajjal* na *Rib*a, na kati ya *Y'ajuj* na *M'ajuj* na maji!

Wayahudi wa asili wamerudi kwenye Ardhi Takatifu. Kurudi huko kusingeweza kutokea isipokuwa kwa msaada wa Mataifa ya Kimagharibi (ambamo Uingereza imechukua nafasi kubwa katika kutimiza hilo). Hivyo, inaonekana wazi sasa kuwa Dajjal, Mtume wa Uongo, alianzia kwenye visiwa vya Uingereza, na pia *Y'ajuj* na *M'ajuj* wanapatikana katika bara la Ulaya.

Kutoka 'Jerusalem' hadi kwenye 'Ardhi Takatifu'

Kinachoongeza kushangaza kuhusu Jerusalem katika *Qur'ani*, ni ukweli kuwa Kitabu Kitakatifu mara hutumia jina la mji 'Jerusalem' kikimaanisha 'Ardhi Takatifu' (kama kwenye *Surah al-Anbiyah*, 95-6) na kasha kuendelea kutumia 'Ardhi Takatifu' kwa njia hiyo

hiyo kikimaanisha ‘Jerusalem’. Kwa mfano, katika Sura *Banu Israil*, inaelezea kuwa watatenda *Fasad* (dhambi za uharibifu mkubwa) katika Ardhi Takatifu (*al-Ard al Muqaddasah*) katika nyakati mbili tofauti. Lakini *Qur’ani* haikuitaja katika aya hiyo kwa jina kama Ardhi Takatifu. Hapo *Qur’ani* imeitaja kama ‘ardhi’ au ‘nchi’:

وَقَضَيْنَآ إِلَىٰ بَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ فِى ٱلْكِتَٰبِ لَتُفْسِدُنَّ فِى ٱلْأَرْضِ مَرَّتَيْنِ
وَلَتَعْلُنَّ عُلُوًّا كَبِيرًا ٤

“*Na tukawapa ishara za wazi Wana wa Israili katika Kitabu kwamba: Hakika nyinyi mtafanya fisadi katika nchi mara mbili, na kwa yakini mtapanda kiburi, kiburi kikubwa (na mara mbili watapewa adhabu)!”*

(Qur’ani, Banu Israil, 17:4)

Kisha *Qur’ani* ikalizungumzia jambo muhimu sana juu ya masharti ya kurithi Ardhi Takatifu, na kwa mara nyingine tena, imeitaja kama ‘ardhi’ au ‘nchi’ na siyo ‘Ardhi Takatifu’:

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِى ٱلزَّبُورِ مِنۢ بَعْدِ ٱلذِّكْرِ أَنَّ ٱلْأَرْضَ يَرِثُهَا
عِبَادِىَ ٱلصَّٰلِحُونَ ١٠٥

“*Na hakika tulikwisha andika katika Zaburi baada ya Ujumbe (aliopewa Musa – Kumbukumbu), ya kwamba nchi watairithi waja wangu walio wema.”*

(Qur’ani, al-Anbiyah, 21:105)

Mwisho, *Qur’ani* inaelezea muda ambapo Mwenyezi Mungu ataliinua *D’abatul ard* (mnyama wa ardhi):

۞ وَإِذَا وَقَعَ ٱلْقَوْلُ عَلَيْهِمْ أَخْرَجْنَا لَهُمْ دَآبَّةً مِّنَ ٱلْأَرْضِ تُكَلِّمُهُمْ أَنَّ
ٱلنَّاسَ كَانُوا۟ بِـَٔايَٰتِنَا لَا يُوقِنُونَ ٨٢

“*Na itapo waangukia kauli juu yao(Banu Israil), tutawatolea mnyama katika ardhi atakaye wasemeza, ya kuwa watu walikuwa hawana na yakini na Ishara zetu.”*

(Qur’ani, al-Naml, 27:82)

Huyo ‘Mnyama wa Ardhi’ au ‘Nchi’, ni, kama *Dajjal* na Y’ajuj na M’ajuj, moja ya Alama kuu za Zama za Mwisho. Ni wazi kuwa neno ‘ardhi’ au ‘nchi’ likijumuishwa na Mnyama, linamaanisha ‘Ardhi Takatifu.’

Kwa hiyo, wakati Mwenyezi Mungu akiwa yuko tayari kuanza kutoa adhabu Yake kwa Wayahudi, anamtoa ‘Mnyama’ kwenye Ardhi Takatifu.’ Huyu Mnyama ni rahisi kumtambua kuwa si mwingine zaidi ya Nchi ya Kiyahudi ya Israeli. Hii inakuwa wazi kutoka aya iliyopita ambapo Qur’ani inatambua anayehusika na suala hilo inaposema:



“*Hakika Qur'ani hii inawasimulia Wana wa Israili mengi wanayo khitalifiana nayo.”*

(*Qur’ani, al-Naml, 27:76)*

Hivyo, wakati Mwenyezi Mungu atakapokuwa tayari kuanza kutimiza adhabu yake kwa Wayahudi, Atamwinua ‘Mnyama’ katka Ardhi Takatifu. ‘Mnyama’ huyu ni rahisi kumtambua kuwa si mwingine ila ni Nchi ya Israeli ya sasa.

***

(Kitabu hiki kinaweza kuagizwa kutoka Islamic Book Trust ibtkl@pd.jaring.my)

Sura ya 3

MWANZO WA HISTORIA YA JERUSALEM KATIKA QUR'ANI:

JERUSALEM NA MITUME



"*Na tukamwokoa yeye na Luut'i (binamu yake) tukawapeleka kwenye nchi tulio ibariki kwa ajili ya walimwengu wote."*

(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:71)

Ibrahimu / Abraham (*rehma na amani juu yake*)

Historia ya uhakika kuhusu Jerusalem na Ardhi Takatifu inaanza na Ibrahimu / Abraham (*rehma na amani juu yake*), Mtume wa Mwenyezi Mungu. Alivunja masanamu katika hekalu la watu wake (Ur – kwa sasa iko Iraq) lakini akamuacha sanamu mkubwa kuliko wote amesimama ili kuwapa somo na kuwakosoa wanaoabudu masanamu (*Qur'ani, al-Anbiyah, 21:57-64*). Kama Ibrahimu / Abraham angerudi duniani leo hii na kurudia kitendo hicho, angeshutumiwa na serikali kadhaa na hata waalimu wa kidini pia kuwa kitendo chake ni cha ugaidi na uharibifu wa urithi wa kitamaduni wa Babylon. Umoja wa Mataifa ungeiwekea vikwazo nchi yoyote ambayo ingempa haki ya kuwepo nchini humo. Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) angefanyiwa hivyo hivyo kama naye angerudi na kuvunja masanamu ya Ka'aba.

Ur walikasirishwa sana na kitendo cha kuvunjwa kwa masanamu yao, ikiwemo kufanyiwa dhihaka kwa wanao abudu masanamu. Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*) alipewa adhabu kwa kutayarishiwa moto na kutupwa kwenye moto huo. Lakini Mwenyezi Mungu aliingilia kati na kuuamuru moto "*kuwa baridi*" na "*kuwa salama kwa Ibrahimu*" (*Qur'ani al-Anbiyah, 21:68-69*). Hapo ndipo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliposema kuwa akawapeleka yeye na Lot (*rehma na amani juu yake*) kwenye nchi aliyoibariki kwa binaadamu wote. Hiyo ndiyo Ardhi Takatifu:

"*Na tukamwokoa yeye na Luut'i (binamu yake) tukawapeleka kwenye nchi tulio ibariki kwa ajili ya walimwengu wote."*

Ni kwa hii aya ndipo wazo la Ardhi Takatifu, au Ardhi Iliyobarikiwa, ndipo lilipoanzwa kutajwa na kutumika kwenye *Qur'ani* kwa mara ya kwanza. Je, lina umuhimu gani? Kwanini Mwenyezi Mungu, achague sehemu moja tu ya dunia nzima na kuifanya Ardhi Takatifu Iliyobarikiwa? Na kwanini awapeleke hapo Ibrahimu na Lot (*rehma na amani juu yao*) Mitume Yake na Watumishi Wake, kuhamia kwenye hiyo Ardhi Takatifu? Jibu la maswali hayo linaweza kuwa ni moja tu. Katika binaadamu wote, Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Hekima, alimchagua Ibrahimu (*rehma na amani juu yake)* kama 'rafiki' Yake, au 'mpendwa' (*khalil) (Qur'ani, al-Nisa, 4:125*). Alimjaribu Ibrahimu (*rehma na amani juu yake)* kwa kumpa jaribio kubwa kuliko yote, naye akapasi. Mwenyezi Mungu Mtukufu ndipo alipomchagua kuwa kiongozi wa dini (*Imamu*) wa binaadamu wote (*Qur'ani, al-Baqarah, 2:124*). Inaonyesha kutokana na hilo kuwa Ukweli ni mmoja, na Dini moja kwa binaadamu wote itatokana nao – dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake)*. Hivyo, kuna dini moja tu ya Kweli na zote zilizobaki ni za uongo. Nayo ni dini ya *Imamu* wa binaadamu, dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake).* Hakuna Mchungaji wala Rabbai ambaye anaweza kukataa hilo! Lakini, kila tunaposema hilo, Rabbai wanatushutumu kuwa sisi ni wabaguzi na tunajipendelea.

Wakati Mwenyezi Mungu alipolichagua eneo moja na kulifanya kuwa Ardhi Takatifu na kisha kumpeleka Ibrahimu (*rehma na amani juu yake)* kuhamia hapo, lengo lilikuwa kuifanya Ardhi Takatifu kuwa kama 'kigezo cha majaribio' ya Ukweli. Ni dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake)* peke yake ambayo ingeweza kudumu kwenye Ardhi Takatifu. Nyingine zote zingefukuzwa. Kwa maneno mengine, Ukweli siku zote utakuwa mshindi dhidi ya Uongo, na historia haiwezi kuisha kabla Ukweli haujaweza kuushinda Uongo kwa mara ya mwisho katika ardhi hiyo! Ucha Mungu, Kupenda na Kutenda haki, na Kujitolea kwa Mwenyezi Mungu kama vile mtumwa anavyojitolea kwa bwana wake mmiliki – kunawakilisha kiini hasa chaUkweli na hivyo dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*). Je, dini ya Kikristo, dini ya Kiyahudi, au dini ya *Kiislamu* ni Kweli? Jerusalem tayari inajibu swali hilo! Ni hatma ya Jerusalem kujibu swali hilo na kuthibitisha Ukweli. Na hilo, kwa uhakika, ni jambo moja ambalo kitabu hiki kinahakikisha kuwa kinaliwakilisha kwa msomaji.

Kwa kuwa Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*) na Lot (*rehma na amani juu yake*) walipelekwa hapo kwenye Ardhi Takatifu na Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Busara, ili waishi humo, tokeo la kitendo hicho ni kuwa vizazi vyao pia vitaishi hapo, labda ikiwa watapewa tena amri ya kuhamia sehemu nyingine. Hiyo ardhi ilikuwa, ni mali yao.

Swali ambalo inabidi kujiuliza, hata hivyo, ni je, mwaliko wa kuishi katika Ardhi Takatifu ulikuwa hauna masharti? Je, mwaliko huo utaendelea kuheshimiwa ikiwa vizazi vyao vitaacha kufuata dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*) na kuwa wasioamini Mungu au wajikite kwenye ukahaba au ugandamizaji? Je utaendelea kuwa halali ikiwa Wayahudi wataunda Nchi ya Israeli yenye mfumo wa kidunia katika Ardhi Takatifu ambayo inajengwa kwa misingi ya kuamini kuwa 'mamlaka yote' yako chini ya watawala wa nchi (wa kidunia) badala ya 'Mungu wa Ibrahimu', na kuwa sheria yenye nguvu kuliko zote inayofuatwa katika Ardhi Takatifu ni sheria za nchi na si zile za 'Mungu wa Ibrahimu?' Je, mwaliko huo bado utakuwa halali ikiwa Nchi itaamua kuwa *Halal* (ruksa) kile ambacho

Mwenyezi Mungu ameamrisha kuwa *Haram* (kimezuiwa)? Msomaji inabidi agundue kuwa 'Mungu wa Abraham' (*rehma na amani juu yake*) amekataza kukopesha pesa kwa faida (*Riba).* Wayahudi walibadilisha maandiko ya Torah ili kuhalalisha kukopesha pesa kwa faida kwa wale wasiokuwa Wayahudi. Si *Riba* tu imehalalishwa leo hii katika Ardhi Takatifu, bali pia mambo mengi ambayo Mwenyezi Mungu ameyakataza.

Pili, na pia muhimu, ni swali lifuatalo: Ikiwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, ameibariki Ardhi kwa Baraka kwa ajili ya *binaadamu wote,* je kwa mtirirko wa mantiki si kweli kuwa binaadamu yeyote na binaadamu wote ambao watafuata dini ya Ibrahimu pia watakuwa na haki ya kupata Baraka hizo? Je huu sio usemi wa *ujumla?* Wapi basi kunakotoka madai ya Wayahudi kuwa *wao peke yao* ndiyo wenye haki pekee ya kurithi Ardhi Takatifu?

Wakati tunaendelea kujibu maswali haya muhimu katika kitabu hiki, itasaidia ikiwa wasomaji watatafakari juu ya mazungumzo baina ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*) na Mola Wake:

۞ وَإِذِ ٱبْتَلَىٰٓ إِبْرَٰهِـۧمَ رَبُّهُۥ بِكَلِمَٰتٍ فَأَتَمَّهُنَّ ۖ قَالَ إِنِّى جَاعِلُكَ لِلنَّاسِ إِمَامًا ۖ
قَالَ وَمِن ذُرِّيَّتِى ۖ قَالَ لَا يَنَالُ عَهْدِى ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿١٢٤﴾

"*Na kumbuka Mola wake Mlezi alipo mjaribu Ibrahimu kwa kumpa amri fulani, naye akazitimiza, akamwambia: Hakika Mimi nitakufanya uwe Imam (kiongozi wa dini, wa kiroho wa watu wote". Akauliza (Ibrahimu): Je, na katika vizazi vyangu pia? (Na wao pia watapewa hadhi hii?) Akasema (Mwenyezi Mungu): Ahadi yangu haitawafikia wenye kudhulumu (ikimaanisha wenye kutofuata haki, wagandamizaji, wanaotumia mabavu na waoneaji)."*

(Qur'ani, al-Baqarah, 2:124)

Miongoni mwa vitendo ambavyo *Qur'ani* inavitaja kama ni dhuluma ni pamoja na "*kuwafukuza na kuwaondosha watu kutoka majumbani mwao, kutoka kwenye ardhi yao ambamo wamekuwa wakiishi"* na kufanya hivyo *"bila ya sababu yoyote ya msingi (hakika hakuna sababu zaidi ya) kuwa wanamuamini Allah, Mwenyezi Mungu":*

أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقَٰتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظُلِمُوا۟ ۚ وَإِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ
لَقَدِيرٌ ﴿٣٩﴾


ٱلَّذِينَ أُخْرِجُوا۟ مِن دِيَـٰرِهِم بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّآ أَن يَقُولُوا۟ رَبُّنَا ٱللَّهُ ۗ
وَلَوْلَا دَفْعُ ٱللَّهِ ٱلنَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَّهُدِّمَتْ صَوَٰمِعُ وَبِيَعٌ
وَصَلَوَٰتٌ وَمَسَـٰجِدُ يُذْكَرُ فِيهَا ٱسْمُ ٱللَّهِ كَثِيرًا ۗ
وَلَيَنصُرَنَّ ٱللَّهُ مَن يَنصُرُهُۥٓ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَقَوِىٌّ عَزِيزٌ ﴿٤٠﴾

"*Wameruhusiwa kupigana wale wanao pigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia – (Nao ni) wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila tu kwa kuwa wanasema: Mola wetu Mlezi ni, Allah, Mwenyezi Mungu!.....*

(Qur'ani, al-Hajj, 22:39-40)

Hivi (kwa kuwaondoa waja wa Allah) ndivyo jinsi ambavyo Nchi ya Israeli ilivyoanzishwa.

Qur'ani imetenga kauli nzito ya kulaani kwa watendaji wa vitendo vya dhuluma pale ambapo Neno la Mungu linabadilishwa na uwongo unawekwa badala yake kinyume cha matakwa na amri za Mwenyezi Mungu. Hivyo ndivyo hasa walivyofanya Wayahudi pale walipobadilisha maandiko ya Mwenyezi Mungu kwenye Torah / Taurati na kuweka maneno yao wenyewe:


وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ ٱفْتَرَىٰ عَلَى ٱللَّهِ كَذِبًا أَوْ كَذَّبَ بِـَٔايَـٰتِهِۦٓ ۗ إِنَّهُۥ لَا يُفْلِحُ
ٱلظَّـٰلِمُونَ ﴿٢١﴾

"*Na nani dhaalimu (mtenda dhulma) zaidi kuliko anaye mzulia uwongo Mwenyezi Mungu, na akazikanusha Ishara zake? Hakika madhaalimu hawafanikiwi."*

(Qur'ani, al-An-am, 6:21)

Kitabu chetu kinachoitwa: "*Dini ya Ibrahimu na Nchi ya Israeli"* kimeangalia kwa kina mabadiliko mengi yaliyofanywa kwenye Torah / Taurati.

Musa *(rehma na amani juu yake)*

Sehemu nyingine katika *Qur'ani* ambamo Ardhi Takatifu inatajwa tena ni takriban miaka 500 baadaye wakati Musa (*rehma na amani juu yake*) alipowasihi Wayahudi wapigane ili kuichukua Ardhi Takatifu na iwe chini ya himaya yao. Hii ilikuwa punde tu baada ya kuwakomboa kutoka kwenye utumwa Egypt, na maajabu ya Mwenyezi Mungu yalikwishatokea wakati bahari ilipopasuka na wao kupita huku maadui zao wakazama. Ndipo jitihada zikafanywa kuanzia Sinai ili kuikomboa Ardhi Takatifu:

يَٰقَوْمِ ٱدْخُلُوا۟ ٱلْأَرْضَ ٱلْمُقَدَّسَةَ ٱلَّتِى كَتَبَ ٱللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَرْتَدُّوا۟ عَلَىٰٓ
أَدْبَٰرِكُمْ فَتَنقَلِبُوا۟ خَٰسِرِينَ ﴿٢١﴾

"Enyi watu wangu! Ingieni katika Ardhi Takatifu ambayo Mwenyezi Mungu amekuandikieni. Wala msirudi nyuma, msije mkaondolewa na mkawa wenye kukosa (miongoni mwa mengine haki ya kuishi katika Ardhi hiyo)."

(Qur'ani, al-Maidah, 5:21)

Aya hii ya *Qur'ani* inathibitisha ujumbe uliokusudiwa kwenye *Sura al-Anbiyah, 21:71* iliyonukuliwa hapo juu. Ukitilia maanani ukweli kuwa Wayahudi ni kizazi cha Abraham (*rehma na amani juu yake*) na walikuwa bado wanafuata dini ya Abraham (*rehma na amani juu yake*) chini ya usimamizi na muongozowa Mtume wa Mwenyezi Mungu, Musa (*rehma na amani juu yake*), walikuwa na haki ya kuishi kwenye Ardhi Takatifu. Ilikuwa ni ardhi yao!

Muda baada ya kufa Musa (*rehma na amani juu yake*) Wayahudi walifanikiwa kuingia kwenye Ardhi Takatifu. Lakini makabila yasiyowapenda yalikuwa muda mwingi yakiwabughudhi. Wakati mwingine iliwabidi wakimbie ili kuokoa maisha yao. *Qur'ani* imeyatazungumzia mambo haya, na tama yao ya kuwa na mfalme ambaye angewaongoza katika mapambano kupigania kudhibiti Ardhi Takatifu:

۞ أَلَمْ تَرَ إِلَى ٱلَّذِينَ خَرَجُوا۟ مِن دِيَٰرِهِمْ وَهُمْ أُلُوفٌ حَذَرَ
ٱلْمَوْتِ فَقَالَ لَهُمُ ٱللَّهُ مُوتُوا۟ ثُمَّ أَحْيَٰهُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ لَذُو فَضْلٍ عَلَى
ٱلنَّاسِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَشْكُرُونَ ﴿٢٤٣﴾
وَقَٰتِلُوا۟ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱعْلَمُوٓا۟ أَنَّ ٱللَّهَ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٤﴾

مَّن ذَا ٱلَّذِى يُقۡرِضُ ٱللَّهَ قَرۡضًا حَسَنًا فَيُضَٰعِفَهُۥ لَهُۥٓ أَضۡعَافًا
كَثِيرَةً ۚ وَٱللَّهُ يَقۡبِضُ وَيَبۡصُۜطُ وَإِلَيۡهِ تُرۡجَعُونَ ﴿٢٤٥﴾
أَلَمۡ تَرَ إِلَى ٱلۡمَلَإِ مِنۢ بَنِىٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ مِنۢ بَعۡدِ مُوسَىٰٓ إِذۡ قَالُواْ لِنَبِىٍّ لَّهُمُ
ٱبۡعَثۡ لَنَا مَلِكٗا نُّقَٰتِلۡ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِۖ قَالَ هَلۡ عَسَيۡتُمۡ إِن
كُتِبَ عَلَيۡكُمُ ٱلۡقِتَالُ أَلَّا تُقَٰتِلُواْۖ قَالُواْ وَمَا لَنَآ أَلَّا نُقَٰتِلَ
فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَقَدۡ أُخۡرِجۡنَا مِن دِيَٰرِنَا وَأَبۡنَآئِنَاۖ فَلَمَّا كُتِبَ
عَلَيۡهِمُ ٱلۡقِتَالُ تَوَلَّوۡاْ إِلَّا قَلِيلٗا مِّنۡهُمۡۗ وَٱللَّهُ عَلِيمُۢ
بِٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٢٤٦﴾

"Hukuwaona wale walio toka majumbani kwao kwa maelfu kwa kuogopa mauti? Mwenyezi Mungu akawaambia: Kufeni! Kisha akawahauisha (akawarudisha kuwa hai). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila juu ya watu, lakini wengi wa watu hawana shukurani."

Na piganeni katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba Mwenyezi Mungu ni Msikizi na Mjuzi" (Allah, Mwingi wa Busara, anawataka mpigane na mpinge wanaowagandamiza wanaowafukuza kutoka majumbani mwenu)

"Ni nani atakaye mkopesha Mwenyezi Mungu mkopo mwema ili Allah amrudishie zaidi kuliko alichomkopesha? Mwenyezi Mungu huzuia Anachotoa na huzidishakile Anachotoa. Na Kwake Yeye mtarejea.

Hukuwaona watukufu katika Wana wa Israili baada ya Musa, walipo mwambia Nabii wao: Tuwekee mfalme ili tupigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu? Akasema: Je, haielekei ikiwa mtaandikiwa vita kuwa msipigane? Wakasema: Itakuwaje tusipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na hali tumetolewa majumbani kwetu na watoto wetu? Lakini walipo andikiwa kupigana waligeuka, isipo kuwa wachache miongoni mwao. Na Mwenyezi Mungu anawajua madhaalimu.

(Qur'ani, al-Baqarah, 2:243-6)

Mtume aliongea nao hayo (hapo juu) alikuwa Samuel (*rehma na amani juu yake*). Majibu yao kwake yalikuwa:

"*...Itakuwaje tusipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na hali tumetolewa majumbani kwetu na watoto wetu?...*"

Jibu hili likiwa katika maneno yao wenyewe lililotamkwa kwa ndimi zao wenyewe linathibitisha kanuni kuwa watu wana haki ya kupigana vita dhidi ya wagandamizaji amabo wanawlazimisha kuondoka kutoka kwenye makazi yao wanamoishi. Wakati kanuni hii ni sahihi kwa ardhi yoyote ile, ina uzito zaidi pale ambapo Ardhi takatifu inahusika. Inawezekanaje, kwa Nchi ya Israeli kuanzishwa kwa misingi ya siasa za kuwaondoa watu kwenye nyumba na ardhi zao, watu amabao wanamuabudu Mungu wa Ibrahimu, na kisha bila aibu kuwanyima haki na uhuru wa kurudi kwenye nyumba na ardhi zao kwa zaidi ya miaka hamsini?

Joshua *(rehma na amani juu yake)*

Baada ya Wayahudi kuokolewa kutoka Egypt hatimaye walipewa tena Baraka (kwa mara nyingine tena) ya *kurithi* Ardhi Takatifu. Biblia inatufahamisha kuwa Joshua aliwaongoza kuingia kwenye Ardhi Takatifu. *Qur'ani* haikatai wala haithibitishi msimamo huo wa Biblia kuhusu jina la Joshua:

وَأَوْرَثْنَا ٱلْقَوْمَ ٱلَّذِينَ كَانُوا۟ يُسْتَضْعَفُونَ مَشَـٰرِقَ ٱلْأَرْضِ
وَمَغَـٰرِبَهَا ٱلَّتِى بَـٰرَكْنَا فِيهَا ۖ وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ ٱلْحُسْنَىٰ عَلَىٰ بَنِىٓ
إِسْرَٰٓءِيلَ بِمَا صَبَرُوا۟ ۖ وَدَمَّرْنَا مَا كَانَ يَصْنَعُ فِرْعَوْنُ
وَقَوْمُهُۥ وَمَا كَانُوا۟ يَعْرِشُونَ ﴿١٣٧﴾

"*Na tukawarithisha watu walio kuwa wanadharauliwa ardhi ya Mashariki na Magharibi tuliyo ibariki, kama urithi wao. Na likatimia neno jema la Mola Mlezi wako juu ya Wana wa Israili, kwa vile walivyo subiri. Na tukayaangamiza aliyo kuwa akiyafanya Firauni na kaumu yake, na waliyo kuwa wakiyajenga (kwa majivuno).*"

(Qur'ani, al-Araf, 7:137)

Kabla ta hapo Wayahudi walikataa kupigana ili kuweza kuingia kwenye Ardhi Takatifu wakati Musa *(rehma na amani juu yake)* alipowaamrisha wafanye hivyo. Wakati huo, wawili kati yao walikuwa wametoa amri hiyo kwao, amri ya kupigana ili kuingia kwenye Ardhi Takatifu. Watafsiri wa *Qur'ani* wanamtambua Joshua kuwa ni mmoja kati ya hao wawili:


قَالَ رَجُلَانِ مِنَ ٱلَّذِينَ يَخَافُونَ أَنۡعَمَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِمَا ٱدۡخُلُواْ
عَلَيۡهِمُ ٱلۡبَابَ فَإِذَا دَخَلۡتُمُوهُ فَإِنَّكُمۡ غَٰلِبُونَۚ وَعَلَى ٱللَّهِ فَتَوَكَّلُوٓاْ
إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ ٢٣

"Watu wawili miongoni mwa wachaMungu ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha walisema: Waingilieni kwa mlangoni (kuwashambulia). Mtakapo waingilia basi kwa yakini nyinyi mtashinda. Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni waumini."

(Qur'ani, al-Maidah, 5:23)

Suleyman *(rehma na amani juu yake)*

Kwa mara nyingine tena, takriban miaka 500 baadaye, *Qur'ani* ikaitaja kwa mara ya nne Ardhi Takatifu wakati Allah, Mwingi wa Busara, alipouzumgumzia ufalme wa Suleyman *(rehma na amani juu yake)* kama ifuatavyo:


وَلِسُلَيۡمَٰنَ ٱلرِّيحَ عَاصِفَةً تَجۡرِي بِأَمۡرِهِۦٓ إِلَى ٱلۡأَرۡضِ ٱلَّتِي بَٰرَكۡنَا فِيهَاۚ
وَكُنَّا بِكُلِّ شَيۡءٍ عَٰلِمِينَ ٨١

"*Na tukamsahilishia (kumuwezesha) Suleyman upepo wa kimbunga ili uende kwa amri yake kwenye ardhi Tuliyo ibarikia. Na Sisi ndio tunao jua kila kitu."*

(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:81)

Kufuatia ishara hizi zote za Baraka za Mwenyezi Mungu, ndipo Nchi (ya Kiislamu) ya Israeli ambayo ilitawaliwa na Suleyman *(rehma na amani juu yake)* ikaweza kuwa si tu *Nchi Tawala* duniani, bali pia Nchi maarufu kwa ustawi wa kila namna kupita zote katika historia ya binaadamu. Chini ya Suleyman, Wayahudi walikuwa wakiishi katika Zama za Dhahabu.

Muhammad *(rehma na amani juu yake)*

Mwishowe *Qur'ani* ikaitaja kwa mara ya tano Ardhi Takatifu au Iliyobarikiwa wakati ilipoizungumzia safari ya kimaajabu ya usiku ya Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake)*

Kutoka Makka kwenda Madina na kisha kupaa mbinguni:

سُبْحَانَ ٱلَّذِىٓ أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِۦ لَيْلًا مِّنَ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ إِلَى
ٱلْمَسْجِدِ ٱلْأَقْصَا ٱلَّذِى بَـٰرَكْنَا حَوْلَهُۥ لِنُرِيَهُۥ مِنْ ءَايَـٰتِنَآ ۚ إِنَّهُۥ هُوَ
ٱلسَّمِيعُ ٱلْبَصِيرُ ١

"*Sifa zote anastahiki Allah, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona (vitu vyote).*"

(Qur'ani, Banu Israil, 17:1)

Msikiti (*Masjid, Hekalu*) huo wa mbali ulitambuliwa na Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake)* kama Masjid-al-Aqsa, Msikiti ambao ulijengwa na Mtume Suleyman *(rehma na amani juu yake)* katika mji wa Jerusalem:

"Amesimulia Jabir bin Abdullah: Kuwa alimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu akisema: Wakati watu miongoni mwa Waqureishi walipokataa kuniamini mimi (akimaanisha habari za safari yangu ya usiku), nikasimama al-Hijr na Allah akanibainishia mbele yangu Jerusalem, na nikawa nawaelekeza wao kwa kuwapa maelezo, huku nikiwa naiangalia."

(Sahih Bukhari)

Mtume *(rehma na amani juu yake)* akaamuru kwa Waislamu baada ya hapo, kutofanya safari yoyote takatifu zaidi ya safari za kwenda sehemu tatu takatifu:

"Amesimulia Abu Hurarirah: Mtume *(rehma na amani juu yake)* alisema: Msifanye kufunga safari isispokuwa kwenda kwenye Misikiti (*Masajid*) mitatu ikiwa ni Msikiti wa al-Haram (wa Makka), Msikiti wa Mtume (wa Madina) na Msikiti wa al-Aqsa (wa Jerusalem)."

(Sahih Bukhari)

"Amesimulia Maimunah ibn Sa'ad: Nilisema: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, tupe msimamo wa sheria kuhusu (kutembelea) Bait al-Muqaddas (Jerusalem). Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alisema: Nendeni na mkasali pale. (Isipokuwa) miji yote wakati ule ilikuwa imeandamwa na vita. (Hivyo aliongezea) Kama hamuwezi kutembelea na kusali pale, basi pelekeni mafuta ya taa yakatumike kuwashia taa (akimaanisha pelekeni misaada)."

(Sunan Abu Dawud)

Jeshi la Kirumi chini ya Jenerali Titus liliuvunja Msikiti wa al-Aqsa (au Hekalu lililojengwa na Suleyman *(rehma na amani juu yake)* mwaka 70 AC. Msikiti huo ulikuwa bado umebaki kama gofu wakati majeshi ya Kiislamu chini ya Khalifa Umar (*radhiyallah anhu*) yalipoiteka Jerusalem. Naye ndiye aliyetoa amri ili Msikiti uliopo sasa wa al-Aqsa ujengwe kwenye mabaki ya asili ya Hekalu (*Masjid)* lililojengwa na Suleyman *(rehma na amani juu yake).*

Sura ya Nne

QUR'ANI TAKATIFU IMESEMA KUWA ARDHI TAKATIFU, IKIWEMO JERUSALEM, WALIPEWA WAYAHUDI


وَإِذْ قَالَ مُوسَىٰ لِقَوْمِهِۦ يَٰقَوْمِ ٱذْكُرُوا۟ نِعْمَةَ ٱللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ
جَعَلَ فِيكُمْ أَنۢبِيَآءَ وَجَعَلَكُم مُّلُوكًا وَءَاتَىٰكُم مَّا لَمْ يُؤْتِ أَحَدًا مِّنَ
ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٢٠﴾
يَٰقَوْمِ ٱدْخُلُوا۟ ٱلْأَرْضَ ٱلْمُقَدَّسَةَ ٱلَّتِى كَتَبَ ٱللَّهُ لَكُمْ وَلَا تَرْتَدُّوا۟ عَلَىٰٓ
أَدْبَٰرِكُمْ فَتَنقَلِبُوا۟ خَٰسِرِينَ ﴿٢١﴾

"Na kumbuka pale Musa alipowaambia watu wake: Enyi watu wangu! Kumbukeni neema za Mwenyezi Mungu zilizo juu yenu, alipowateuwa Manabii kati yenu, na akakufanyeni watawala, na akakupeni ambayo hakuwapa wowote katika walimwengu."

"Enyi watu wangu! Ingieni katika Ardhi Takatifu ambayo Mwenyezi Mungu amewapa. Wala msirudi nyuma kwa kutia aibu, mkaangushwa mkawa wenye kukhasirika."

(Qur'ani, al-Maidah, 5:20, 21)

Daniel Pipes, katika makala yake iliyochapishwa katika gazeti la Los Angeles Times (‘*Jerusalem ina uzito na maana zaidi kwa wayahudi kuliko kwa Waislamu’* Julai 21, 2000) anajaribu kudharau madai ya Kiislamu juu ya Jerusalem kwa kudai, miongoni mwa mambo mengine, kuwa: “*Jerusalem haijatajwa hata mara moja katika Qur’ani au sala*.”

Ni kweli kuwa neno ‘Jerusalem’ halitajwi kiuwazi kama lilivyo kwenye *Qur’ani*, lakini hiyo inaonyesha kuwa ni miongoni mwa Busara za Mwenyezi Mungu. *Qur’ani* inaizungumzia na kuitaja Jerusalem katika mfumo wa kimafumbo (na ni vyema kufanya hivyo!) kama *mji* ulioteketezwa, watu wake wakafukuzwa na kisha wakawekewa kizuizi wasiweze kurejea tena ili kuuchukua upya na kuufanya uwe mji wao. Kizuizi hicho kitabaki hadi muda utakapofikia ambapo Ya’juj na Ma’juj watakapokua (*tazama Qur’ani, al-Anbiyah, 21:95-96).* Jina la Kiarabu la Jerusalem ‘*Bait al-Maqdis’* limetajwa mara kadhaa katika Hadithi. Jina la Kirumi ‘Aelia’ pia limejitokeza katika utabiri muhimu sana wa Mtume (*rehma na amani juu yake*).

Kwa hakika, jambo la kushangaza kuwa Dr Pipes ameamua kudharau aya kadhaa za *Qur’ani* ambazo bila ya shaka zimeitaja Ardhi Takatifu (ambamo Jerusalem imo katikati yake) kuwa walipewa Wayahudi na Mwenyezi Mungu Mtukukufu. Wakati Musa (*rehma na amani juu yake*) alipowachukua Wayahudi kutoka kwenye utumwa Egypt, na kuwavusha kimaajabu bahari na kuingia Sinai, Musa (*rehma na amani juu yake*) aliwahutubia na kuwaamrisha wafanye jitihada kuweza kuichukua Ardhi Takatifu. Alisema:

يَٰقَوۡمِ ٱدۡخُلُواْ ٱلۡأَرۡضَ ٱلۡمُقَدَّسَةَ ٱلَّتِي كَتَبَ ٱللَّهُ لَكُمۡ وَلَا تَرۡتَدُّواْ عَلَىٰٓ
أَدۡبَارِكُمۡ فَتَنقَلِبُواْ خَٰسِرِينَ ٢١
قَالُواْ يَٰمُوسَىٰٓ إِنَّ فِيهَا قَوۡمٗا جَبَّارِينَ وَإِنَّا لَن نَّدۡخُلَهَا حَتَّىٰ يَخۡرُجُواْ
مِنۡهَا فَإِن يَخۡرُجُواْ مِنۡهَا فَإِنَّا دَٰخِلُونَ ٢٢
قَالَ رَجُلَانِ مِنَ ٱلَّذِينَ يَخَافُونَ أَنۡعَمَ ٱللَّهُ عَلَيۡهِمَا ٱدۡخُلُواْ
عَلَيۡهِمُ ٱلۡبَابَ فَإِذَا دَخَلۡتُمُوهُ فَإِنَّكُمۡ غَٰلِبُونَۚ وَعَلَى ٱللَّهِ فَتَوَكَّلُوٓاْ
إِن كُنتُم مُّؤۡمِنِينَ ٢٣

"Enyi watu wangu! Ingieni katika Ardhi Takatifu ambayo Mwenyezi Mungu amewapa. Wala msirudi nyuma kwa kutia aibu(kwani huko kutakuwa ni kuisaliti imani yenu), mkaangushwa mkawa wenye kukhasirika (ikiwemo kuikosa Ardhi Takatifu)."

"*Wakajibu: Ewe Musa! Huko wako watu majabari wanaishi. Nasi hatutaingia huko mpaka wao watoke humo. Wakitoka humo hapo tutaingia." (Tazama pia: Numbers 13:32-33)*

"Watu wawili miongoni mwa wacha Mungu (Joshua na Caleb kwa mujibub wa Taurati) ambao Mwenyezi Mungu amewaneemesha walisema: Waingilieni kwa mlangoni (kuwashambulia). Mtakapo waingilia kwa hapo, basi! kwa yakini nyinyi mtashinda. Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu (Allah) ikiwa nyinyi ni waumini."

(Qur'ani, al-Maidah, 5:21-23)

Wayahudi walimjibu Musa (*rehma na amani juu yake*) kwa jibu la kudhalilisha kiasi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu hapo hapo aliwanyima ruksa ya kuingia katika Ardhi Takatifu:

قَالُوا۟ يَٰمُوسَىٰٓ إِنَّا لَن نَّدْخُلَهَآ أَبَدًا مَّا دَامُوا۟ فِيهَا ۖ فَٱذْهَبْ أَنتَ
وَرَبُّكَ فَقَٰتِلَآ إِنَّا هَٰهُنَا قَٰعِدُونَ ﴿٢٤﴾
قَالَ رَبِّ إِنِّى لَآ أَمْلِكُ إِلَّا نَفْسِى وَأَخِى ۖ فَٱفْرُقْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ ٱلْقَوْمِ
ٱلْفَٰسِقِينَ ﴿٢٥﴾
قَالَ فَإِنَّهَا مُحَرَّمَةٌ عَلَيْهِمْ أَرْبَعِينَ سَنَةً ۛ يَتِيهُونَ فِى ٱلْأَرْضِ ۗ
فَلَا تَأْسَ عَلَى ٱلْقَوْمِ ٱلْفَٰسِقِينَ ﴿٢٦﴾

"Wakasema: Ewe Musa! Sisi hatutaingia humo (kwenye Ardhi Takatifu) kamwe maadamu wao wamo humo. Basi nenda wewe na Mola wako mkapigane! Sisi tutakaa hapa hapa."

"Akasema: Mola Wangu Mlezi! Hakika mimi similiki ila nafsi yangu na ndugu yangu. Basi tutenge na hawa watu wapotovu."

(Mwenyezi Mungu) akasema: Basi ardhi hiyo (Ardhi Takatifu) wameharimishiwa muda wa miaka arubaini, watakuwa wakitanga-tanga katika ardhi (Sinai) wakiwa wamechanganyikiwa. Basi wewe (Musa) usiwasikitikie watu wapotovu."

(Qur'ani, al-Maida, 5:24-26)

Qur'ani imethibitisha katika sehemu tofauti kuwa Ardhi Takatifu walipewa Wayahudi:

فَأَرَادَ أَن يَسْتَفِزَّهُم مِّنَ ٱلْأَرْضِ فَأَغْرَقْنَٰهُ وَمَن مَّعَهُۥ جَمِيعًا ﴿١٠٣﴾
وَقُلْنَا مِنۢ بَعْدِهِۦ لِبَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ ٱسْكُنُوا۟ ٱلْأَرْضَ فَإِذَا جَآءَ وَعْدُ ٱلْءَاخِرَةِ
جِئْنَا بِكُمْ لَفِيفًا ﴿١٠٤﴾

"Basi Firauni akataka kuwateketeza (Wayahudi) wasiwepo tena katika dunia. Kwa hivyo Sisi (Allah) tukamzamisha yeye (Firauni) na wote walio kuwa pamoja naye.
Na Sisi (Allah) tukawaambia baada yake Wana wa Israili: 'Kaeni kwa amani katika ardhi (ikimaanisha, Ardhi Takatifu)..."

(Qur'ani, Banu Israil, 17:103-104)

Na tena:

وَأَوْرَثْنَا ٱلْقَوْمَ ٱلَّذِينَ كَانُوا۟ يُسْتَضْعَفُونَ مَشَٰرِقَ ٱلْأَرْضِ
وَمَغَٰرِبَهَا ٱلَّتِى بَٰرَكْنَا فِيهَا ۖ وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ ٱلْحُسْنَىٰ عَلَىٰ بَنِىٓ
إِسْرَٰٓءِيلَ بِمَا صَبَرُوا۟ ۖ وَدَمَّرْنَا مَا كَانَ يَصْنَعُ فِرْعَوْنُ
وَقَوْمُهُۥ وَمَا كَانُوا۟ يَعْرِشُونَ ﴿١٣٧﴾

"*Na tukawarithisha watu walio kuwa wanadharauliwa mashariki na magharibi ya ardhi tuliyo ibariki. Na likatimia neno jema la Mola Mlezi wako juu ya Wana wa Israili, kwa vile walivyoonyesha na kuwa na subira katika dhiki. Na tukayaangamiza aliyo kuwa akiyafanya Firauni na kaumu yake, na waliyo kuwa wakiyajenga (kwa majivuno)."*

(Qur'ani, al-Araf, 7:137)

Inashangaza, kwa hakika, kuwa Wayahudi na Wasomi wa Kizayonisti watadharau na kuacha au kuepuka kunukuu matamko haya yaliyo wazi ambamo *Qur'ani* imesema kuwa Ardhi Takatifu walipewa Wayahudi:

- "Enyi watu wangu! Ingieni katika Ardhi Takatifu ambayo Mwenyezi Mungu amewapa...."

- "Na (Allah) tukawaambia baada yake Wana wa Israili: 'Kaeni kwa amani katika Ardhi (ikimaanisha, Ardhi Takatifu)'....."

- "Na tukawarithisha watu walio kuwa wanadharauliwa Mashariki na Magharibi ya Ardhi tuliyo ibariki."

Wasomaji wetu ambao wanautafuta kwa yakini Ukweli kuhusu hatma ya Jerusalem inawabidi watafakari juu ya msito huu ulio upande wa jumuiya ya Kiyahudi ya Ulaya, Wazayonisti na wasomi wa Kiyahudi katika kutoitamka *Qur'ani* inachosema juu ya somo hili. Kitabu hiki kinatoa maelezo kuhusiana na msimamo huo wa ajabu. Maelezo yamo katika kusita kwao kuonyesha ukweli wa jinsi Taurati ilivyoharibiwa kwa kubadilisha masharti aliyoyaweka Mwenyezi Mungu, Allah juu ya kurithi kwa Ardhi Takatifu. Kughushi huko kulikofanywa katika Taurati kunadhihirishwa katika *Qur'ani.* Je, kughushi huko kuko vipi?

Sura ya Tano

MASHARTI YA MWENYEZI MUNGU (YA KIROHO) ILI KURITHI ARDHI TAKATIFU


وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُورِ مِن بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ ١٠٥

"Na hakika tulikwisha andika katika Zaburi iliyokuja baada ya (andiko Letu kwenye) Kumbukumbu (ikimaanisha Taurati), ya kwamba ardhi (Ardhi Takatifu) watairithi waja wangu wale tu walio wema."

(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:105)

Kama Dk. Pipes angejua aya hii ya *Qur'ani* ambayo imetamka kuwa Ardhi Takatifu walipewa Wayahudi (na haiwezekani iwe hajui) basi ingembidi ajiulize: Waislamu wana haki gani ya kutaka kuwanyang'anya Wayahudi ardhi (na mji ambao umo katikati ya ardhi hiyo) ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu amewapa wao? Sababu iliyomfanya asiulize swali hilo ni kuwa lingefungua 'sanduku la Pandora'. Kwanza, hataki kuruhusu *Qur'ani* ipate kutajwa, kwa kuwa inawazungumzia Wayahudi na Ardhi Takatifu. Pili, jibu la swali hilo limo katika aya nyingine ya *Qur'ani* ambamo Mwenyezi Mungu Mtukufu ametamka kuwa haki ya Wayahudi juu ya Jerusalem na Ardhi Takatifu inakamilika ikiwa tu kwa kutimiza '*masharti' juu ya imani na uadilifu wa tabia na mwenendo.* Imani, bila ya shaka, inamaanisha kufuata na kutimiza matakwa yote ya dini ya Abrahamu:

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُورِ مِن بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ ﴿١٠٥﴾

"Na hakika tulikwisha andika katika Zaburi iliyokuja baada ya (andiko Letu kwenye) Kumbukumbu (ikimaanisha Taurati), ya kwamba ardhi (Ardhi Takatifu) watairithi waja wangu wale tu walio wema."

(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:105)

Ni wazi kuwa *Qur'ani* imetumia neno ardhi au nchi kama hapo juu, haikuwa inamaanisha dunia nzima. Kama ingekuwa na maana hiyo, huo ungekuwa msemo suiokuwa na ukweli ndani yake – si kweli leo na si kweli kwa muda mwingi wa historia. Wale wanaoshikilia na kudhibiti dunia leo, na ambao wawakilishi wao hukusanyika New York kwenye Mkutano wa Milenia, hivi wakati tunaandika kitabu hiki, hao ni wanafiki katika binaadamu. Ni wawakilishi wa mfumo wa kidunia wa kisasa ulio wa kilaghai, unaodidimia kwenye kukosa maadili, wa ugandamizaji na uliomkifu Mwenyezi Mungu. Na wanawawakilisha wachache waliohodhi madaraka na utajiri, wanaonyonya damu za waliobaki ambao kwa sasa wamefanikiwa kuufunga umma wa binaadamu wengi kwenye utumwa wa kiuchumi uliojengwa kwa misingi ya *Riba.*

Lakini, Neno la Mwenyezi Mungu mara zote ni la Kweli. Haliwezi kuwa la uongo! Hivyo neno 'nchi' au 'ardhi' katika aya hiyo halimaanishi dunia nzima. Je, linamaanisha ardhi ipi? Jibu kwa hakika linapatikana katika Taurati na Zaburi. Lipo pia katika Injili (Yafsiri za Injili zimefanywa kwa kiasi huwezi kugundua hilo). Ni 'Ardhi Takatifu'! Lakini tafsiri zote zinatumia neno 'nchi' ('ardhi' au 'dunia'):

"Je ni mtu gani anayemwogopa Bwana? Yeye ndiye atakayemfundisha katika njia atakayoichagua. Roho yake itakuwa na amani; na kizazi chake kitarithi Ardhi (Takatifu). Siri ya Bwana itakuwa na wale wanaomuogopa na kumtii Bwana, na Atawafunulia Ahadi yake."

(Zaburi, 25:12-14)

"Lakini walio watiifu watarithi Ardhi / Nchi (Takatifu) na watafurahia wingi wa amani."

(Zaburi, 37:11)

"Waadilifu watarithi Ardhi/ Nchi (Takatifu) na watadumu humo milele (ikiwa wataendelea kuwa waadilifu.)"

(Zaburi, 39:29)

“Wamebarikiwa watiifu kwani watarithi Ardhi / Nchi (Takatifu).”

(Matayo, 5:5)

Uthibitisho kuwa neno ‘ardhi’ au ‘nchi’ katika maana na mtazamo huu yanamaanisha Ardhi Takatifu unapatikana katika aya za *Qur’ani* ambazo zimeelezea kuwa Wana wa Israili watatenda maovu (*Fasad – ukatili na ugandamizaji wa kinyama*) katika ardhi au nchi katika sehemu mbili tofauti:

وَقَضَيْنَآ إِلَىٰ بَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ فِى ٱلْكِتَٰبِ لَتُفْسِدُنَّ فِى ٱلْأَرْضِ مَرَّتَيْنِ
وَلَتَعْلُنَّ عُلُوًّا كَبِيرًا ﴿٤﴾

“*Na tukawapa maonyo (yaliyo wazi) Wana wa Israili katika Kitabu kwamba: Hakika nyinyi mtafanya fasad (ukatili na ugandamizaji wa kinyama) katika nchi mara mbili, na kwa yakini mtapanda kiburi, kiburi kikubwa (na mara mbili wataadhibiwa!)”.*

(Qur’ani, Banu Israil, 17:4)

Kwa makubaliano ya kijumla inakubalika kuwa neno ‘nchi’ au ‘ardhi’ katika aya hiyo hapo juu inamaanisha Ardhi Takatifu! Hivyo, vitabu vitakatifu vyote vinasema kwa sauti moja, kuwa imani na uadilifu wa mwenendo ndiyo masharti ambayo Wayahudi wangepewa kihalali na kisheria urithi wa Ardhi Takatifu na kuishi humo.
Kuna mtu ambaye amebadilisha maandiko ya Taurati na badala yake ameondoa masharti hayo.
Ameandika:
“Hivyo ujue kuwa si kwa sababu ya uadilifu wenu ndipo Mwenyezi Mungu, Mungu wako, amewapa ardhi hii nzuri ili iwe mali yenu, kwani nyie ni watu wabishi.”

(Kumbukumbu ya Taurati, Deuteronomy, 9:6)

Dk. Pipes huenda hatojisikia vizuri kuweza kufanya jaribio la kuutetea huu mlima wa uongo unaofanywa dhidi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na dini ya Ibrahimu *(rehma na amani juu yake).* Lakini haihitaji nguvu na jitihada nyingi za kifikra, na kwa mtiririko wa mantiki, na busara za maadili, ikiwemo mtazamo wa kiroho, kugundua kuwa usemi wa hapo juu ni uongo. Hauendani na kiwango cha juu kabisa cha uadilifu, wema na haki ambacho kinapaswa kutoka kwa Muumba, Mwingi wa uadilifu, Wema na Haki kuliko yeyote Aliyemuumba. Kwa ufupi, ni ulaghai! Na ilitenegenezwa hivyo ili kuvunja amri waliyopewa Wayahudi ya kuwa waadilifu ili waweze kurithi Ardhi Takatifu. Kama, katika dunia nzima,

ardhi hii ilichaguliwa na Allah na ilipewa Baraka maalum na Yeye, kwanini Awape bila masharti *"watu wabishi"* bila kujali kama wangekuwa waadilifu au wangepinga kufuata viwango vya uadilifu vya tabia na mwenendo mwema?

Pili, mtiririko wa kihistoria unathibitisha kuwa Wayahudi walifukuzwa mara kwa mara, kwa amri ya Mwenyezi Mungu, kutoka Jerusalem na Ardhi Takatifu. Hii iliwatokea kila walipovunja amri na masharti ya kuwa waadilifu na wenye mwenendo mwema. *Qur'ani* imeyataja matukio haya ya kufukuzwa kwao na kisha, baada ya kufukuzwa kwa mara ya mwisho, Mwenyezi Mungu Mtukufu alitamka nia yake ya kuendelea kuwaondoa wakati wowote watakapokuwa wamerudi kwenye Ardhi Takatifu huku wakiwa wamevunja masharti ya 'imani' na 'mwenendo wenye maadili' *(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:105).* Wayahudi wengi wa asilia (ambao hawana asili ya Ulaya) wanakubali mara moja kuwa walijisababishia kuondolewa kwenye Ardhi Takatifu kwa nguvu za Mwenyezi Mungu kwa sababu za mwenendo wao wa dhambi. Wazayonisti wa Ulaya ambao wamemkifu Mwenyezi Mungu hawakubaliani na usemi huo.

Wayahudi wanatujibu kwa madai kuwa yaliyosemwa kwenye Kumbukumbu ya Taurati - (Kumbukumbu ya Taurati, Deuterenomy) 9:6 tuliyoinukuu hapo juu yalimaanisha kuwakumbusha Wayahudi kuwa kupewa kwao kwa arhi kulitokana na imani na uadilifu wa mzazi wao, Ibrahimu *(rehma na amani juu yake).* Kwa maneno mengine, hawakupewa ardhi hiyo na kuirithi kwa sababu ya uadilifu wao.

Hoja hii haivunji mtiririko wa mantiki uliomo kwenye aya hiyo, kuwa Ardhi walipewa bila masharti. Na *Qur'ani* inaeleza wazi kuwa hivyo si kweli. Msimamo wa *Qur'ani* hauna shaka. Ardhi walipewa Wana wa Israili kw masharti. Masharti hayo ni pamoja na kuwa 'wenye kumuamini Mwenyezi Mungu, Allah na kujisalimisha Kwake' na kuwa 'waadilifu na mwenendo mwema' *(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:105).*

Miaka mia sita baada ya kuondolewa Wayahudi kwa mara ya mwisho kutoka kwenye Ardhi Takatifu, Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwawezesha Waislamu kuirithi Ardhi Takatifu wakati jeshi la Kiislamu lilipoiteka na Khalifa Umar alipoombwa aje binafsi kupokea ufunguo wa mji. Siku hiyo, utabiri wa tokeo hilo katika *Qur'ani* ulikamilika:

وَهُوَ ٱلَّذِى جَعَلَكُمْ خَلَٰٓئِفَ ٱلْأَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ بَعْضٍ
دَرَجَٰتٍ لِّيَبْلُوَكُمْ فِى مَآ ءَاتَىٰكُمْ ۗ إِنَّ رَبَّكَ سَرِيعُ ٱلْعِقَابِ وَإِنَّهُۥ لَغَفُورٌ
رَّحِيمٌ ﴿١٦٥﴾

"Naye ndiye aliye kufanyeni makhalifa wa Ardhi (Takatifu), na Amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa kubwa, ili akujaribuni kwa hayo aliyo kupeni (Wana wa Israili walipewa zaidi kuliko watu wengine wowote): Hakika Mola Mlezi wako ni Mwepesi wa kuadhibu, na hakika Yeye ni Mwenye Kusamehe, Mwenye Kurehemu."

(Qur'ani, al-An'am, 6:165)

Mwenyezi Mungu Mtukufu alisema kuwa aliwapangia Waislamu kuwa wnagerithi Ardhi Takatifu. Hapo, Ukweli uliushinda Uongo katika Ardhi Takatifu. Walipoichukua Ardhi Takatifu, waliidhibiti na waliendelea kuitawala (ukiacha muda mchache) kwa zaidi ya miaka elfu moja na mia mbili. Hiyo ilikuwa ni ishara ya wazi kutoka mbinguni! Ilikuwa ni ishara ya kukubalika kiroho na Mwenyezi Mungu kwa utawala wa Kiislamu juu ya Ardhi Takatifu! Wasomi wa Kiyahudi wanapaswa watoe maelezo kwa mlolongo huo wa utawala wa Kiislamu kwenye Ardhi Takatifu kwa kipindi kirefu kama hicho, utawala wa Kiislamu uliokuwa ukimjali, ukimuogopa na ukimuabudu Mwenyezi Mungu, na utawala uliokuwa wa haki na uadilifu.

Wakati Wazayonisti wa Ulaya (wasiokuwa wayahudi wa asili) walipowadanganya Wana wa Israili wajiunge nao katika jitihada za kung'ang'ania kiubishi 'wa nguruwe' kurejea katika Ardhi Takatifu, kwa kile wanachodai mpangilio wa Kimungu wa kurejesha Nchi ya Israeli, kulikuwa na Alama za wazi kwa wana wa Israili kuwa madai ya Wazayonisti ni ya uongo. Ulikuwa ni uongo! Masharti ya Mwenyezi Mungu ya imani katika dini ya Ibrahimu nay ale ya uadilifu na mwenendo mwema yalikuwa wazi yanakosekana katika jitihada hizo za kuirudisha Israeli za Wazayonisti. Na nchi yenyewe ya Israeli ilipoanzishwa, misingi ya Nchi ilikuwa ni ile ile ya nchi za kisasa za mfumo wa kidunia. Misingi ya nchi za kisasa zenye mifumo ya kidunia, ni misingi ya *Shirk* na *Kufr* na hiyo inapingana wazi na dini ya Ibrahimu *(rehma na amani juu yake)* na somo hilo linaelezewa kwa ufasaha zaidi katika Sehemu ya Pili ya kitabu hiki.

Sura ya Sita

KUFUKUZWA KWA WAYAHUDI KUTOKA KWENYE ARDHI TAKATIFU KWA KUVUNJA MASHARTI YA URITHI



وَقَضَيْنَآ إِلَىٰ بَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ فِى ٱلْكِتَٰبِ لَتُفْسِدُنَّ فِى ٱلْأَرْضِ مَرَّتَيْنِ
وَلَتَعْلُنَّ عُلُوًّا كَبِيرًا ﴿٤﴾
فَإِذَا جَآءَ وَعْدُ أُولَىٰهُمَا بَعَثْنَا عَلَيْكُمْ عِبَادًا لَّنَآ أُو۟لِى بَأْسٍ شَدِيدٍ
فَجَاسُوا۟ خِلَٰلَ ٱلدِّيَارِ ۚ وَكَانَ وَعْدًا مَّفْعُولًا ﴿٥﴾
ثُمَّ رَدَدْنَا لَكُمُ ٱلْكَرَّةَ عَلَيْهِمْ وَأَمْدَدْنَٰكُم بِأَمْوَٰلٍ وَبَنِينَ
وَجَعَلْنَٰكُمْ أَكْثَرَ نَفِيرًا ﴿٦﴾
إِنْ أَحْسَنتُمْ أَحْسَنتُمْ لِأَنفُسِكُمْ ۖ وَإِنْ أَسَأْتُمْ فَلَهَا ۚ فَإِذَا جَآءَ وَعْدُ
ٱلْءَاخِرَةِ لِيَسُۥٓـُٔوا۟ وُجُوهَكُمْ وَلِيَدْخُلُوا۟ ٱلْمَسْجِدَ كَمَا
دَخَلُوهُ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَلِيُتَبِّرُوا۟ مَا عَلَوْا۟ تَتْبِيرًا ﴿٧﴾

"*Na tukawapa maonyo (yaliyo wazi) Wana wa Israili katika Kitabu kwamba: Hakika nyinyi mtafanya fasad (ukatili na ugandamizaji wa kinyama) katika nchi mara mbili, na kwa yakini mtapanda kiburi, kiburi kikubwa (na mara mbili wataadhibiwa!) Basi itapo fika ahadi yake ya kwanza kutimia tutakupelekeeni waja wetu wa kali kwa vita. Watakuingilieni ndani ya majumba. Na hii ilikuwa ahadi iliyo timizwa. Kisha tukakurudishieni nguvu zenu dhidi yao, na tukakusaidieni kwa mali na wana, na tukakujaalieni mkawa wengi zaidi. Basi mkifanya wema, mnajifanyia wema nafsi zenu. Na mkifanya ubaya, mnajifanyia wenyewe. Na ikifika ahadi ya mwisho ili wazihariibu nyuso zenu, na waingie Msikitini kama walivyo ingia mara ya kwanza na kuharibu kila walichoteka.*"

(Qur'ani, Banu Israil, 17:4-7)

Sura Banu Israil ya Qur'ani (Sura namba 17) inazungumzia historia ya Jerusalem ambayo inauweka wazi uongo ufuatao ulio katika Taurati:

"Hivyo ujue kuwa si kwa sababu ya uadilifu wenu ndipo Mwenyezi Mungu, Mungu wako, amewapa ardhi hii nzuri ili iwe mali yenu, kwani nyie ni watu wabishi."

(Kumbukumbu ya Taurati, Deuteronomy, 9:6)

Usemi huu ni wa kughushi kwa sababu unaweka misingi ya imani kuwa Wayahudi kupewa Ardhi Takatifu kwa amri ya kiroho kupitia Mitume wao kulikuwa hakuna masharti yoyote kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa maneno mengine, usemi huo unamwezesha Myahudi kudai kuwa Ardhi Takatifu itaendelea kuwa haki yao hata kama hawatokuwa na uadilifu na mwenendo mwema kwani hayo siyo masharti ya wao kupewa Ardhi hiyo. Myahudi atadai kuwa Ibrahimu *(rehma na amani juu yake)* alikuwa muadilifu kwa hivyo kutokana na uadilifu wake, alipewa haki ya Ardhi yeye na vizazi vyake! Baada ya hapo, namna yoyote ya kuvunjwa kwa uadilifu na mwenendo mwema wa imani hakutoweza kuondoa haki yao hiyo waliyorithi. Taurati haikuficha jambo hilo:

"Kwa hivyo kumbuka maneno Yangu moyoni mwako: yafunge kama alama mkononi mwako na yaweke kama alama kwenye paji lako la uso, na wafundishe watoto wako, uyatamke unapokuwa nyumbani, na utakapokuwa safarini, na unapolala na unapoamka, na uyaandike katika nguzo za milango ya nyumba yako na kwenye mageti ili wewe na watoto wako waweze kubaki, kwenye Ardhi (ikimaanisha Ardhi Takatifu) ambayo Bwana aliapa kwa wazazi wako kuwapa, kwa muda wote patakapokuwa na mbingu juu ya ardhi. Ikiwa utafuata amri zote nilizokupa kwa ukamilifu, kumpenda Bwana, Mungu wako, kupita katika njia Zake na kumshikilia Yeye kwa uhakika, bwana atayaondoa mataifa yote: mtayashinda mataifa makubwa na yenye watu wengi kuliko nyinyi. Kila mahali utakapoweka mguu wako, patakuwa mali yako, eneo lako litakuwa kutoka nyika hadi Lebanon na kutoka mto Euphrates hadi bahari ya magharibi. Hakuna mtu takayeweza kusimama kupinga nguvu zako: Bwana, Mungu wako atawaingiza kwenye hofu wakuogope kote ardhini utakapopita, kama alivyokuahidi."

(Kumbukumbu ya Taurati, Deuterenomy, 11:18-25)

(Makala iliyoandikwa na Michael Abi-Yonah katika Encyclopedia ya Kiyahudi, mwandishi anasema kuwa "David / Daud *(rehma na amani juu yake)* alipokuwa akifanya mashambulizi na kujenga himaya yake, aliufanya mji wa Jerusalem kuwa ni makao makuu ya ufalme ambao ulijumuisha maeneo toka Egypt hadi Euphrates, ingawa ni pale tu ambapo mrithi wake alipochukua madaraka, Suleyman, ndipo ukweli huu ulifanyiwa kazi.")

Lakini *Kumbukumbu ya Taurati, Deuterenomy 9:6 na pia 11:18-25* hazisemi ukweli kwani zinaondoa imani, uadilifu na mwenendo mwema kama ndiyo masharti ya kurithi Ardhi Takatifu! *Qur'ani* haikuthitibitisha masharti ya uadilifu na mwenendo mwema peke yake (*Sura Anbiyah, 21:105)* bali pia imeendelea na kuweka wazi ushahidi wa kihistoria kuwa kila masharti hayo yalipovunjwa, basi Mwenyezi Mungu alitoa adhabu ya kuwaondoa kutoka katika Ardhi hiyo. Sura hiyo iliyotajwa hapo juu imeyataja matukio hayo takriban mara mbili wakati Wana wa Israili walipoisaliti dini ya Ibrahimu *(rehma na amani juu yake)* na masharti ya uadilifu na mwenendo mwema na Mweneyzi Mungu alipowaondoa kutika katika Ardhi Takatifu. (Somo hili tumelizungumzia kwa kina zaidi katika kitabu chetu: *Dini ya Ibrahimu na Nchi ya Israeli – Mtazamo wa Qur'ani."*

Kwa mara ya kwanza mwaka 587 BCE, jeshi la Babylon likiongozwa na Nebuchadnezzar liliivamia Jerusalem, mji ukachomwa moto, wakazi wakauawa na Msikiti uliojengwa na Suleyman *(rehma na amani juu yake)* ukavunjwa, na sehemu bora ya jamii ya Kiyahudi wakachukuliwa kama watumwa na kupelekwa Babylon. Mtume Jeremiah aliwaonya kuwa haya yatawatokea *(Jeremiah 32:36),* vile vile kama Mwenyezi Mungu alivyosema katika *Qur'ani* kuwa haiteketezi jumuiya bila ya kuwapelekea onyo (*Qur'ani, Banu Israil, 17:15-16).* Waandishi walioandika Zaburi hawakuelewa adhabu ya Mwenyezi mungu katika kuteketezwa huku kwa Jerusalem na Hekalu, ndipo Zaburi ilipojibu kwa kulalamika:

"Ewe Bwana, mataifa yamevamia urithi wako, yamechafua Hekalu lako takatifu, na wameivunjavunja Jerusalem imebakia magofu."

(Zaburi 79:1)

Walipewa adhabu hiyo kwa kuwa, miongoni mwa mambo mengine, walibadilisha Taurati na kuyafanya *Halali* yale ambayo Allah, aliyafanya *Haramu.* Walibadilisha pia maandishi ya Taurati na kuruhusu kukopesha pesa kwa *Riba* kwa wasiokuwa Wayahudi na kasha kuzuia baina yao wenyewe:

"Hutomkopesha kwa kudai *Riba* ndugu yako (Myahudi); ikiwa ni kumkopesha kwa pesa, au bidhaa (kwa kuwa wakati mwingine bidhaa zilitumika kama pesa) au kukopesha chochote kile kinachokopeshwa kwa Riba (ikimaanisha chochote kinachotumika kama pesa). Kwa mgeni (asiyekuwa Myahudi) unaruhusiwa kukopesha na kudai Riba...."

(Kumbukumbu ya Taurati, Deuterenomy, 23:19-20)

(Vitabu vyetu viwili: '*Umuhimu wa Kuzuia Riba katika Uislamu*' na *Kuzuiwa kwa Riba katika Qur'ani na Sunna'* vinazungumzia somo hili kwa kina)

Kwa mara ya pili waliondolewa tena kutoka katika Ardhi takatifu kwa kuwa waliwaua Mitume ya Mwenyezi Mungu (angalia, kwa mfano, *Qur'ani, al-Baqarah*, 2:61). Walimuua Zakaria *(rehma na amani juu yake)* ndani ya Msikiti. Walimuua mtoto wake, John kwa udanganyifu. Yesu *(rehma na amani juu yake)* alizungumzia mauaji hayo ya Mitume bila kuficha kwa kutumia lugha kali kulaani vitendo hivyo vya kinyama:

"Na ndiyo maana hekima ya Bwana inasema: Nitawatuma Mitume na Watumishi. Wengine watawaua na wengine watawashutumu. Na ikawa damu ya Mitume yote iliyomwagwa katika msingi wa ardhi iwasakame kizazi hiki (cha Wayahudi), kuanzia damu ya Abel hadi damu ya Zakaria, ambaye aliuawa baina ya kibla (altar) na Nyumba ya Mungu – ndiyo, nawaambia, yote itawashutumu kizazi hiki...."

(Luka, 11:49-51)

Mwishowe, walijisifu jinsi gani wameweza kumuua Masihi, Yesu, mwana wa Maryam (lakini Allah, Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Nguvu, alimuokoa kutoka kwenye mtego huo - hawakumuua)

وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا ٱلْمَسِيحَ عِيسَى ٱبْنَ مَرْيَمَ رَسُولَ ٱللَّهِ وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا
صَلَبُوهُ وَلَٰكِن شُبِّهَ لَهُمْ ۚ وَإِنَّ ٱلَّذِينَ ٱخْتَلَفُوا۟ فِيهِ لَفِى شَكٍّ مِّنْهُ ۚ مَا لَهُم
بِهِۦ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا ٱتِّبَاعَ ٱلظَّنِّ ۚ وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًۢا ﴿١٥٧﴾

"Na kwa kusema kwao (kwa kujisifu): Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu - nao hawakumuuwa wala hawakumsulubu, bali walifananishiwa tu (ilionekana tu kwao kuwa wamemuua). Na hakika wanao khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Kwa yakini wala hawakumuuwa."

(Qur'ani, al-Nisa, 4:157)

Ni baada ya hili kutokea ndipo mwenyezi Mungu, Allah alipowapa adhabu kwa mara ya pili. Jeshi la Kirumi, likiongozwa na Jenerali Titus lilivamia Jerusalem mwaka 70 CE. Titus alivunja mji wa Jerusalem, aliwaua wakazi wake na akawafukuza waliobaki watoke kwenye Ardhi Takatifu. Msikiti ulivunjwa tena kwa mara ya pili na askari walibomoa jiwe baada ya jiwe, wakitafuta dhahabu vile vile kama ambavyo Yesu *(rehma na mani juu yake)* alivyowaonya na alivyotabiri "*hata jiwe moja halitoachwa juu ya jingine, yote yatadondoshwa chini.") (Tazama Qur'ani, Banu Israili, 17:4-7)*

وَقَضَيْنَآ إِلَىٰ بَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ فِى ٱلْكِتَٰبِ لَتُفْسِدُنَّ فِى ٱلْأَرْضِ مَرَّتَيْنِ
وَلَتَعْلُنَّ عُلُوًّا كَبِيرًا ﴿٤﴾
فَإِذَا جَآءَ وَعْدُ أُولَىٰهُمَا بَعَثْنَا عَلَيْكُمْ عِبَادًا لَّنَآ أُو۟لِى بَأْسٍ شَدِيدٍ
فَجَاسُوا۟ خِلَٰلَ ٱلدِّيَارِ ۚ وَكَانَ وَعْدًا مَّفْعُولًا ﴿٥﴾
ثُمَّ رَدَدْنَا لَكُمُ ٱلْكَرَّةَ عَلَيْهِمْ وَأَمْدَدْنَٰكُم بِأَمْوَٰلٍ وَبَنِينَ
وَجَعَلْنَٰكُمْ أَكْثَرَ نَفِيرًا ﴿٦﴾
إِنْ أَحْسَنتُمْ أَحْسَنتُمْ لِأَنفُسِكُمْ ۖ وَإِنْ أَسَأْتُمْ فَلَهَا ۚ فَإِذَا جَآءَ وَعْدُ
ٱلْءَاخِرَةِ لِيَسُۥٓـُٔوا۟ وُجُوهَكُمْ وَلِيَدْخُلُوا۟ ٱلْمَسْجِدَ كَمَا
دَخَلُوهُ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَلِيُتَبِّرُوا۟ مَا عَلَوْا۟ تَتْبِيرًا ﴿٧﴾

"*Na tukawapa maonyo (yaliyo wazi) Wana wa Israili katika Kitabu kwamba: Hakika nyinyi mtafanya fasad (ukatili na ugandamizaji wa kinyama) katika nchi mara mbili, na kwa yakini mtapanda kiburi, kiburi kikubwa (na mara mbili wataadhibiwa!) Basi itapo fika ahadi yake ya kwanza kutimia tutakupelekeeni waja wetu wa kali kwa vita. Watakuingilieni ndani ya majumba. Na hii ilikuwa ahadi iliyo timizwa. Kisha tukakurudishieni nguvu zenu dhidi yao, na tukakusaidieni kwa mali na wana, na tukakujaalieni mkawa wengi zaidi. Basi mkifanya wema, mnajifanyia wema nafsi zenu. Na mkifanya ubaya, mnajifanyia wenyewe. Na ikifika ahadi ya mwisho ili waziharibu nyuso zenu, na waingie Msikitini kama walivyo ingia mara ya kwanza na kuharibu kila walichoteka.*"

(Qur'ani, Banu Israil, 17:4-7)

وَكَتَبْنَا لَهُۥ فِى ٱلْأَلْوَاحِ مِن كُلِّ شَىْءٍ مَّوْعِظَةً وَتَفْصِيلًا
لِّكُلِّ شَىْءٍ فَخُذْهَا بِقُوَّةٍ وَأْمُرْ قَوْمَكَ يَأْخُذُوا۟ بِأَحْسَنِهَا ۚ سَأُو۟رِيكُمْ دَارَ
ٱلْفَٰسِقِينَ ﴿١٤٥﴾

"...Nami punde nitakuonyesheni makaazi ya wapotofu (jinsi yalivyokuwa yamevunjwa vunjwa).

(Qur'ani, al-Araf, 7:145)

Qur'ani inalitaja Hekalu ambalo lilivunjwa mara mbili kwa kuliita Msikiti '*al-Masjid.'* Lakini kabla ya kufanya hivyo, *Qur'ani* imeielezea safari ya maajabu ya Mtume *(rehma na amani juu yake)* (*al-Isra* na *Mi'raj)* kama safari kutoka *al-Masjid al-Haram* (wa Makka) kwenda *Masjid al-Aqsa* (ikimaanisha Hekalu la mbali):

سُبْحَٰنَ ٱلَّذِىٓ أَسْرَىٰ بِعَبْدِهِۦ لَيْلًا مِّنَ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ إِلَى
ٱلْمَسْجِدِ ٱلْأَقْصَا ٱلَّذِى بَٰرَكْنَا حَوْلَهُۥ لِنُرِيَهُۥ مِنْ ءَايَٰتِنَآ ۚ إِنَّهُۥ هُوَ
ٱلسَّمِيعُ ٱلْبَصِيرُ ١

"*Sifa zote anastahiki Allah, Ametakasika aliye mchukua mja wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao tumevibariki vilivyo uzunguka, ili tumuonyeshe baadhi ya Ishara zetu. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona (vitu vyote)."*

(Qur'ani, Banu Israil, 17:1)

Msikiti uliotajwa kwenye aya hiyi ya *Qur'ani*, ambao ulivunjwa mara mbili, haukuweza kuwa Msikiti mwingine zaidi ya ule uliojengwa na Suleyman *(rehma na amani juu yake).* Mtume *(rehma na amani juu yake)* mwenyewe alithibitisha hilo. Ni msikiti huo huo uliotajwa kama *Masjid al-Aqsa* ambako Mtume *(rehma na amani juu yake)* alipelekwa katika safari yake ya usiku ya kiajabu. *Qur'ani* inaendelea kusema kuwa alipelekwa huko ili aonyeshwe 'Alama' za Allah, Mtukufu. Zaidi ya yoye, miongoni mwa 'Alama' hizo zinahusiana na hatma ya Jerusalem.

Baada ya kuwaadhibu Wayahudi kwa mara ya pili kwa kuwatoa kwenye Ardhi Takatifu, Mwenyezi Mungu, Allah, Aliendelea kulezea nia Yake ya kuendelea kuwapa adhabu (na kuwaondoa hapo) ikiwa wataendelea kuchafua Ardhi takatifu na kuvunja masharti ya imani, uadilifu na mwenendo mwema:

عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَن يَرْحَمَكُمْ ۚ وَإِنْ عُدتُّمْ عُدْنَا ۘ وَجَعَلْنَا جَهَنَّمَ لِلْكَافِرِينَ حَصِيرًا ﴿٨﴾

"...Na mkirudia (kuvunja masharti yaliyowekwa ya kurithi Ardhi Takatifu) na Sisi tutarudia (adhabu Yetu ikiwemo kuwaondoa hapo mara hadi mara) ..."

(Qur'ani, Banu Israil, 17:8)

Hatma ya Jerusalem iko wazi katika onyo lililotolewa hapo juu na ambalo *Qur'ani* imelithibitisha kwa uhakika. Onyo hilo linabaki hivyo hivyo, bila ya kujali moja au yote kati ya haya yafuatayo:

- Makubaliano yanayofanywa Camp David au popote pale baina ya wasimamizi wa kidunia wa Wapalestina na Wayahudi wa kidunia wa Ulaya ambao wanadhani kuwa wanawawakilisha Wana wa Israeli, au
- Maazimio na maamuzi ya Baraza la Wawakilishi na Wajumbe la Marekani amabyo yamechukua nafasi ya Bunge la Uingereza kuwa kama Msimamizi na Mlinzi wa nchi ya Israeli, au
- Maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa au ya mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambayo yamechukua nafasi ya serikali ya dunia

Hatma ya Jerusalem inaonekana wazi ukichukulia mtazamo wa uozo wa mfumo uliopo hapo wa kisasa wa kidunia wa kilaghai, unaoendelea kudidimia kwenye kukosa maadili ya imani, kiroho, wa ugandamizaji na uovu wa kinyama na uliomkifu Mwenyezi Mungu, mfumo ambao unaichafua Ardhi Takatifu. Baadhi ya haya yameelezewa kwenye Sehemu ya Pili ya kitabu hiki kwenye uchambuzi wa *Shirk* ya Nchi ya Israeli na uchumi wake wa *Riba*. Ni hatma ya Israeli kuwa itapata pigo jingine la adhabu itokayo kwa Mwenyezi Mungu ambalo ilikwisha lipata kabla kwa mara mbili. Mara ya kwanza adhabu ilikuja kwa kupitia jeshi la Babylon lililoivunja Israeli. Mara ya pili ilikuwa ni jeshi la Kirumi. Mara ya tatu nay a mwisho, itakuwa ni jeshi la Kiislamu ambalo litaivunja Nchi ya Israeli.

Miongoni mwa 'Alama' za Mwenyezi Mungu alizoonyeshwa Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake)* wakati wa safari yake ya ajabu alipotembelea

Jerusalem, ‘Alama’ ambazo miongoni mwa mengine, zilimuonesha hatma ya Jerusalem. Jambo hili inaonyesha limemtoka Daniel pipes.

Mtume wa mwisho *(rehma na amani juu yake)* aliona Zama za Mwisho. Aliona, kupitia jicho lake la kiroho, kurejea kwa Wayahudi katika zama hizo kwenye Ardhi Takatifu. Aliona pia kuundwa kwa Nchi ya Kibeberu ya Israeli, na kukosekana kabisa kwa imani ya dini, nguvu za kiroho na kudidimia kwa maadili na mwenendo mema, kukithiri kwa ugandamizaji kutakakoisibu Ardhi Takatifu. Aliona kurejea kwa Yesu *(rehma na amani juu yake)*, mwana wa Maryam, na kuvunjwa kwa Israeli na jeshi la Kiislamu. Na pia aliona Ukweli, Haki na Uadilifu kwenye dini ya Ibrahimu *(rehma na amani juu yake)* ambayo Mtume wa Kweli atairudisha kwenye Ardhi Takatifu pale atakaporejea.

Sura ya 7

GEUKENI KUTOKA JERUSALEM ELEKEENI MAKKA



أَفَلَمْ يَسِيرُوا۟ فِى ٱلْأَرْضِ فَتَكُونَ لَهُمْ قُلُوبٌ يَعْقِلُونَ بِهَآ أَوْ ءَاذَانٌ يَسْمَعُونَ بِهَا ۖ فَإِنَّهَا لَا تَعْمَى ٱلْأَبْصَٰرُ وَلَٰكِن تَعْمَى ٱلْقُلُوبُ ٱلَّتِى فِى ٱلصُّدُورِ ﴿٤٦﴾

"Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kujifunza na kuzingatia yenye busara, na masikio yao yaweze kujifunza kusikia? Kwani hakika si macho yao ambayo hayaoni, bali ni nyoyo zao zilizomo vifuani (ndizo zisizoona na zisizoelewa)."

(Qur'ani, al-hajj, 22:46)

[Je, hawatembei duniani ili nyoyo zao zilizokufa ziweze kuamshwa, ili nyoyo hizo na akili ambazo sasa ziko hai, ziweze kujifunza yaliyo na busara na masikio yao yajifunze kusikia ikimaanisha kusikia kwa ndani? Kwa hakika si macho yao ndiyo hayaoni, bali ni nyoyo zao zilizomo vifuani]

Wasomi wa Kiyahudi waligundua uhusiano uliopo baina ya Ardhi Takatifu, mji wa Jerusalem na Hekalu la Suleyman *(rehma na amani juu yake)* kuwa ni mambo ambayo yameunganika na hali ya 'imani'. Kutokana na imani hiyo wakafikia uamuzi kuwa dini ya Judaizm daima itabaki haijakamilika hadi pale Wayahudi watakaporejea na kuikomboa Ardhi Takatifu, kurejesha Nchi ya Israeli na kuufanya mji Mtakatifu wa Jerusalem kuwa makao yake makuu na kulijenga Hekalu la Suleyman *(rehma na amani juu yake).* Wazayonisti walikuwa hawana uhusiano wowote wa karibu na Ardhi, mji wala Hekalu. Uhusiano wa Wazayonisti na vitu hivi ulikuwa na misingi ya kisiasa, kihistoria, kidunia na kizalendo. Kwa kuwa mtazamo wa kidunia na maadili yanayoendana nayo mara zote hubadilika kufuatana na mabadiliko ya mfumo wa kidunia unaobadilika badilika, mtazamo na maadili hayo huwa ni tegemezi, na daima si mtazamo na maadili yanayojitegemea na yasiyobadilika. Hivyo basi, uhusiano wa Wazayonisti na Wayahudi wa Ulaya na Ardhi Takatifu, mji wa Jerusalem na Hekalu mara zote unaweza kubadilishwa ili ukidhi haja za mahitaji yaliyopo wakati husika.

Hili haliwezekani kwa wasomi wa kidini wa Kiyahudi ambao wamejikita kwenye imani ya msingi iliyotajwa awali hapo juu.

*Qur'ani i*mesema, kwa upande wa pili, kuwa uzito wa dini upo kwenye 'imani' (na mwenendo mwema na uadilifu) – 'imani' juu ya Mwenyezi Mungu, Allah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Yake au Watumishi Wake, Siku ya Mwisho, Kufufuliwa na Hukumu, Pepo na Jahannamu n.k. Allah, Mtukufu ni 'Ukweli.' 'Imani' inapatikana katika moyo wa binaadamu. 'Imani' inapopatikana ndipo 'Ukweli' unapoingia moyoni! Mwenyezi Mungu Mtukufu, Allah, ni mkubwa na muhimu zaidi ya Nchi au Mji au Hekalu. "*Mbingu na Ardhi Yangu haviwezi kunitosheleza Mimi. Lakini moyo wa mja Wangu unaweza kunitosheleza Mimi" (Hadithi al-Qudsi).*

Wakati Mtume wa Mwisho *(rehma na amani juu yake)* alipojitokeza duniani, wasomi wa kidini wa Kiyahudi walikufa ganzi kwenye upande wa kumtambua na kumkubali rasmi kama Mtume kwa sababu ya kung'ang'ania kwao kwenye 'utaratibu wa matendo ya nje' wa kidini badala ya kujali 'umuhimu wa kindani wa kiroho' wa dini. Muhammad *(rehma na amani juu yake),* Mwarabu, hakuwa Myahudi, hivyo, walidai, hawezi kuwa Mtume kwa Wayahudi. Baada ya kuwasili kwa Mtume *(rehma na amani juu yake)* na kuwa miongoni mwao kwenye mji wa *Hejazi* wa *Yathrib* (sasa Madina), alifunga pamoja na Wayahudi katika siku ambazo wao walikuwa wakifunga kufuatana na sheria ya Taurati (maghrib hadi maghrib – kuanzia kuzama kwa jua hadi kuzama kwa jua). Pia alikuwa akisali huku akiwa ameelekea Jerusalem. Ilipojulikana, baada ya miezi kumi na saba kuwa Wayahudi si vile tu wamemkataa Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake)* kama Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Allah na kuwa *Qur'ani* ni neno la Mwenyezi Mungu, bali pia walikuwa wakipanga njama za kuvunja umoja na nguvu za jumuiya ya Waislamu, Mwenyezi Mungu alimuamuru Mtume ageuke kutoka kuelekea Jerusalem kwenye sala na badala yake aelekee Makka.

Mabadiliko haya ya *Qiblah* (mwelekeo wakati wa kusali) kuliwafanya Wayahudi watoe maoni mengi ya kushutumu. Waliona kitendo hicho kuwa ni uchokozi kwao kwani waliamini kuwa kiini cha dini kimo ndani ya kuujumuisha mji wa Jerusalem. *Qur'ani* ilizijibu shutuma zao kwa kudharau:


سَيَقُولُ ٱلسُّفَهَآءُ مِنَ ٱلنَّاسِ مَا وَلَّىٰهُمْ عَن قِبْلَتِهِمُ ٱلَّتِى كَانُوا۟ عَلَيْهَا ۚ
قُل لِّلَّهِ ٱلْمَشْرِقُ وَٱلْمَغْرِبُ ۚ يَهْدِى مَن يَشَآءُ إِلَىٰ صِرَٰطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿١٤٢﴾

"Wapumbavu miongoni mwa watu watasema: Nini kilicho wageuza kutoka kibla chao walicho kuwa wakikielekea? Sema: Mashariki na Magharibi ni ya Mwenyezi Mungu; Yeye humwongoza amtakaye kwenye njia iliyo nyooka."

(Qur'ani, al-Baqarah, 2:142)

Qur'ani ikaendelea kueleza kuwa Wayahudi wamekuwa wafungwa wa imani potofu kuwa Jerusalem ni moyo na imo katikati ya imani kiasi kwamba hakuna chochote duniani kitakachoweza kubadilisha hilo:


وَلَئِنْ أَتَيْتَ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَٰبَ بِكُلِّ ءَايَةٍ مَّا تَبِعُوا۟ قِبْلَتَكَ ۚ وَمَآ
أَنتَ بِتَابِعٍ قِبْلَتَهُمْ ۚ وَمَا بَعْضُهُم بِتَابِعٍ قِبْلَةَ بَعْضٍ ۚ وَلَئِنِ
ٱتَّبَعْتَ أَهْوَآءَهُم مِّنۢ بَعْدِ مَا جَآءَكَ مِنَ ٱلْعِلْمِ ۙ إِنَّكَ إِذًا
لَّمِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿١٤٥﴾

"Na hao walio pewa Kitabu, hata ukiwaletea Alama zote pamoja (hoja za kila namna), hawatafuata Kibla chako....."

(Qur'ani, al-Baqarah, 2:145)

Mwishowe *Qur'ani* ikajibu kwa kutoa maelezo yaliyovunja imani potofu kuwa Jerusalem, kama mji, na Hekalu lake kuwa ni kiini cha dini ya Ibrahimu *(rehma na amani juu yake):*


لَّيْسَ ٱلْبِرَّ أَن تُوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ قِبَلَ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ وَلَٰكِنَّ ٱلْبِرَّ مَنْ
ءَامَنَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةِ وَٱلْكِتَٰبِ وَٱلنَّبِيِّۦنَ وَءَاتَى
ٱلْمَالَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ ذَوِى ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَٰمَىٰ وَٱلْمَسَٰكِينَ وَٱبْنَ
ٱلسَّبِيلِ وَٱلسَّآئِلِينَ وَفِى ٱلرِّقَابِ وَأَقَامَ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَى ٱلزَّكَوٰةَ
وَٱلْمُوفُونَ بِعَهْدِهِمْ إِذَا عَٰهَدُوا۟ ۖ وَٱلصَّٰبِرِينَ فِى ٱلْبَأْسَآءِ
وَٱلضَّرَّآءِ وَحِينَ ٱلْبَأْسِ ۗ أُو۟لَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ صَدَقُوا۟ ۖ وَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ
ٱلْمُتَّقُونَ ﴿١٧٧﴾

"Sio wema, uadilifu na mwenendo mwema wa imani kuwa mnaelekeza nyuso zenu upande wa mashariki au magharibi. Bali wema, uadilifu na mwenendo mwema wa imani kwa anaye muamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii, na (mja) anayetumia mali zake, katika mapenzi Yake (Mwenyezi Mungu) kwa kuwapa, jamaa zake na mayatima na masikini na wasafiri, na wale waombao, na katika ugombozi wa watumwa, na akawa anashika Sala, na akatoa Zaka, na wanao timiza ahadi yao wanapo ahidi, na wanao vumilia katika shida. Hao ndio watu wa Ukweli, wanaomuogopa Mwenyezi Mungu"

(Qur'ani, al-Baqarah, 2:177)

Hivyo pasiwe na shaka kwenye Uislamu itokanayo na kitendo hicho cha kubadilisha mwelekeo kutoka Jerusalem kuelekea Makka, zaidi ya msimamo ulio wazi wa kutaka kurekebisha imani potofu ya wale ambao wanajumuisha kiini cha dini na kukiweka kwenye mipangilio ya kijiografia. Ujumbe wa *Qur'ani* kwa Wayahudi ulikuwa wazi. Wayahudi waliambiwa kuwa japokuwa Muhammad *(rehma na amani juu yake)* hakuwa Myahudi, na japokuwa hakuwa anasali kuelekea Jerusalem, na japokuwa hakufanya juhudi yoyote ya kutaka kuikomboa Jerusalem, lakini bado alikuwa ni Mtume wa Kweli wa Mungu na dini ya Abrahamu, Musa, Daudi, Suleyman, na wa Masihi, mwana wa Maryam. Hivyo kubadilisha kwa *Qiblah* kulikuwa ni jibu la kejeli kwa Myahudi mbishi na mkorofi ambaye alikuwa akidai kuwa Jerusalem ndipo palipo moyo wa kiroho wa dini ya Ibrahimu.

Kama hasira za Mwenyezi Mungu haziku shukia Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake)* baada ya kubadili mwelekeo kutoka Jerusalem, ni wazi kuwa Mtume wa 'kweli' anaweza kubadili mwelekeo nab ado akabaki kuwa Mtume wa 'kweli'. Si tu Muhammad *(rehma na amani juu yake)* hakutokewa na tatizo lolote baada ya kufanya hivyo, bali pia, aliweza bila ya shaka kuwashinda Wayahudi ambao walikuwa wakidai kuwa wao ni 'watu waliochaguliwa' na Mungu wa Ibrahimu.

Hivyo ni wazi kuwa hapakuwa na hasara zozote kisiasa zilizotokana na kubadilishwa kwa *Qiblah* baada ya Uislamu, kama dini, kutokukuwa na kiunganisho chochote na Jerusalem, na kutokuwa na madai yoyote juu ya Jerusalem. Kinyume na hivyo, *Qur'ani* inathibitisha kuwa Muhammad *(rehma na amani juu yake)*, na wafuasi wake, ni wafuasi rasmi na wa kweli wa dini ya Ibrahimu:

إِنَّ أَوْلَى ٱلنَّاسِ بِإِبْرَٰهِيمَ لَلَّذِينَ ٱتَّبَعُوهُ وَهَٰذَا ٱلنَّبِيُّ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ۗ
وَٱللَّهُ وَلِيُّ ٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٨﴾

"Bila ya shaka, miongoni mwa watu, watu wanao mkaribia zaidi Ibrahim (wanaomkaribia katika misingi ya kufuata dini yake) ni wale walio mfuata yeye na Nabii huyu (Muhammad)(rehma na amani juu yake) na walio amini (ikim. waliomuamini Muhammad, na Kitabu alichoteremshiwa):. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mlinzi Rafiki wa Waumini."
(Qur'ani, Al Imran, 3:68)

Maana ya aya hii ya *Qur'ani* iko wazi kabisa. Ni wale tu ambao kwa yakini wanamfuata Muhammad *(rehma na amani juu yake)* ndiyo wenye haki ya kurithi Ardhi Takatifu. Ni hatma ya Jerusalem katika kuthibitisha ukweli huu.

Upenyo kwa Wayahudi kujipatia msamaha wa Mwenyezi Mungu, Allah

Mabadiliko ya *Qiblah* yalikuwa yanaashiria mambo muhimu zaidi kuliko hata hayo yaliyotajwa hapo juu.

Wakati Wayahudi walipomuabudu 'Ng'ombe wa Dhahabu' wakati Musa *(rehma na amani juu yake)* alipokuwa kwenye mlina wa Sinai, na walipobadilisha maandiko ya Taurati na kufanya *Halali* yale ambayo Allah aliyafanya *Haramu* na walipojisifu kuwa jinsi gani wamemuua Masihi, mwana wa Maryam, haya yote yanadhihirisha vitendo vya kiusaliti, kinyama na kikatili vilivyokuwa kinyume na Amri za Mwenyezi Mungu, Allah. Mwenyezi

Mungu aliwajibu baada ya hayo yote kwa maelezo kuwa wanapewa nafasi moja, ikiwa ni ‘upenyo wa pekee’ ambao kwao wangeweza kujiokoa kutoka kwenye ‘adhabu kali kuliko zote’ ambayo ameitayarisha kuwaadhibu. ‘Upenyo’ huo utakuwa ni Mtume wa Kiarabu, Muhammad*) (rehma na amani juu yake)*, ambaye atakuwa ni Mtume wa Mwisho wa Mitume yote. Ikiwa watamkubali na kumuamini watapata msamaha wa Mwenyezi Mungu na Baraka Zake. Ahadi hii imo katika *Qur’ani* katika aya ambamo Anawaambia Wayahudi ambao tayari walikwishapewa Taurati na Injili, hivyo itakuwa wakati ambapo tayari watakuwa wamekwishateremshiwa Injili. Mwenyezi Mungu Aliwakilisha ujumbe wake ukiwa kama majibu ya vitendo vyao vya kuzisaliti amri Zake, kuzibadilisha aya Zake, kuwaua Mitume Wake ifuatavyo:

۞ وَٱكۡتُبۡ لَنَا فِي هَٰذِهِ ٱلدُّنۡيَا حَسَنَةٗ وَفِي ٱلۡأٓخِرَةِ إِنَّا هُدۡنَآ
إِلَيۡكَۚ قَالَ عَذَابِيٓ أُصِيبُ بِهِۦ مَنۡ أَشَآءُۖ وَرَحۡمَتِي وَسِعَتۡ كُلَّ
شَيۡءٖۚ فَسَأَكۡتُبُهَا لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ وَيُؤۡتُونَ ٱلزَّكَوٰةَ وَٱلَّذِينَ هُم
بِـَٔايَٰتِنَا يُؤۡمِنُونَ ١٥٦
ٱلَّذِينَ يَتَّبِعُونَ ٱلرَّسُولَ ٱلنَّبِيَّ ٱلۡأُمِّيَّ ٱلَّذِي يَجِدُونَهُۥ مَكۡتُوبًا
عِندَهُمۡ فِي ٱلتَّوۡرَىٰةِ وَٱلۡإِنجِيلِ يَأۡمُرُهُم بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَيَنۡهَىٰهُمۡ
عَنِ ٱلۡمُنكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيۡهِمُ
ٱلۡخَبَٰٓئِثَ وَيَضَعُ عَنۡهُمۡ إِصۡرَهُمۡ وَٱلۡأَغۡلَٰلَ ٱلَّتِي كَانَتۡ عَلَيۡهِمۡۚ
فَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ بِهِۦ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَٱتَّبَعُواْ ٱلنُّورَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ
مَعَهُۥٓۙ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُفۡلِحُونَ ١٥٧

"…. (Mwenyezi Mungu) akasema: Adhabu yangu nitamsibu nayo nimtakaye. Lakini rehema yangu imeenea kila kitu. Lakini nitawaandikia khasa wanao mchamngu, na wanao toa Zaka, na wale ambao wanaziamini Ishara zetu."

"Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii (Mgeni – asiye Myahudi), asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwenye vitabu vyao - Taurati na Injili, anaye waamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na ana waharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyo kuwa juu yao. Basi wale walio muamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia, na wakaifuata Nuru iliyo teremshwa pamoja naye - hao ndio wenye kufanikiwa."

(Qur'ani, al-A'raf, 7:156-157)

Inakuwa wazi kabisa kuwa ayah ii ya *Qur'ani* inamuhusu Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake).*

Wakati Mtume*) (rehma na amani juu yake)* alipowasili Madina baada ya *Hijrah* 'upenyo' kwa Wayahudi ukawa uko wazi mbele yao. Kama wangemkubali na kumuamini yeye, wangeweza kupata Msamaha wa Mwenyezi Mungu. Lakini kama wangemkataa, 'upenyo' huo wa kupata Msamaha wa mwenyezi Mungu ungefungwa na Adhabu ya Mwenyezi Mungu ingeanza. Huu ulikuwa ni wakati muhimu sana katika historia yote ya Wayahudi. Saa zilikuwa mithili zimesimama huku mbingu na ardhi zikishuhudia matukio yaliyokuwa yanasibu Madina.

Wakati Mtume *(rehma na amani juu yake)* alipowasili Madina alifanya vitu kadhaa ambavyo kiurahisi tu vingeweza kuwasababishia Wayahudi na viongozi wao wa kidini, Rabbai, wamtambue kuwa yeye ni Mtume wa kweli wa mwenyezi Mungu, na kuwa ndiye Mtume waliyekuwa wakimsubiri. Katika miezi kumi na saba ya mwanzo tangu kufika kwake Madina alikuwa akisali huku anaelekea Jerusalem. Alifanya hivyo kwa kuwa hicho ndicho kilichokuwa *Qiblah* ambako Wayahudi walikuwa wakielekea wanaposali, hivyo ni *Qiblah* cha wale wote wanaoabudu kwa mujibu wa dini ya Abrahamu *(rehma na amani juu yake).* Na kwa Mwarabu kufanya hivyo, inambidi aipe mgongo *Ka'aba*, Nyumba ya Mwenyezi Mungu iliyopo Makka ambayo kila Mwarabu anaiheshimu. Kitendo hicho cha Mtume *(rehma na amani juu yake)* kilipaswa pekee kiwatosheleze Wayahudi wamuamini kuwa yeye ni Mtume wa kweli. Na alifanya zaidi ya hilo. Pia alifunga na Wayahudi katika siku ambazo Wayahudi walikuwa wakifunga kwa kufuata sheria za Taurati (kuanzia jua kutua hadi jua kutua). Hakuna Mwarabu aliyekuwa akifunga namna hiyo katika historia yote ya Waarabu. Na jumuiya yote ya Waislamu wa madina wlifunga namna hiyo. Hii ilipaswa iwahakikishie wamuamini kuwa yeye Muhammad *(rehma na amani juu yake)* ni Mtume wa kweli.

Mwishowe, palikuwa na tukio jingine ambalo lingefuta wasiwasi wowote kama bado ungekuwa bado upo. Wayahudi waliwaleta watu wawili kwa Mtume *(rehma na amani juu yake)* ambao walikuwa wamefanya *zina*. Walikuwa wakimpa jaribio waone atafanya nini kwa kumuuliza hukumu yao iweje. Akawauliza, je ni hukumu gani mnatumia. Walimjibu kuwa wanawapaka masizi usoni (kufanya nyuso ziwe nyeusi) na kasha wanawachapa fimbo hadharani. Akawauliza, je hiyo ndiyo adhabu mliyoikuta kwenye Kitabu chenu? Akawaamuru walete Kitabu chao na wamsomee (kwani yeye alikuwa hajui kusoma wala kuandika). Wakati wanamsomea, Rabbai wao, Abdullah bin Salaam, ambaye alikuwa amesilimu (na kuwa Mwislamu) alisimama pembeni ya Mtume *(rehma na amani juu yake).* Msomaji alipofikia sehemu iliyoandikwa *rajm (*kuuawa kwa kupigwa mawe) katika Taurati akaweka kidole chake ili kuficha. Abdullah bin Salaam akamuamuru asite kusoma na aondoe kidole chake kwanza. Hapo ikambidi asome aya inayoitaja *rajm* ikiwa kama ni adhabu ya *zina*. Kusomwa kwa aya hii kuliwaletea taabu sana mioyoni mwa Wayahudi. Walibainika kuwa ni watu ambao wameisaliti amri yao wenyewe takatifu kwa kuificha na kutoitekeleza. Mtume *(rehma na amani juu yake)* ndipo alipoamuru watu hao wauawe kwa kupigwa mawe, hivyo kutumia amri ya Wayahudi amabyo wao wenyewe walikuwa hawaitumii. Hii ilipaswa iwafanye waamini bila shaka kuwa yeye, kwa hakika, ni Mtume wa kweli.

Baada ya kupita miezi kumi na saba tangu Mtume *(rehma na amani juu yake)* kufika Madina ikawa wazi kuwa Wayahudi si tu wamemkataa kumuamini kama Mtume wa kweli wa Mwenyezi Mungu na wameikataa *Qur'ani* kuwa ni Neno la Mungu, bali pia walikuwa wakipanga njama za kuuangusha Uislamu. Hapo ndipo Allah, Mtukufu, alipobadilisha *Qiblah* (geuka toka Jerusalem, elekea Makka!). Na pia alishusha wahyi (aya) zilizoamrisha 'kupigana' (*Qital*) na kufunga (*Saum*) kuwa ni lazima! Wahyi hizo zote tatu zilishuka katika mwezi wa *Shaabani.* Katika kuitangaza Sheria ya Mfungo wa Ramadhani, Mwenyezi Mungu alibadilisha Sheria iliyokuwamo kwenye Taurati. Sheria mpya iliamrisha kufunga kuanzia 'kutoka' kwa jua hadi 'kuzama' kwake. Ruksa ilitolewa kwa kula na kunywa na pia kwa wenye ndoa kujamiiana wakati wa giza. Mwishowe, Mwenyezi Mungu akabadilisha sheria ya adhabu ya *zina*. Sheria mpya ikawa ni kuchapwa hadharani.

Tokeo la kwanza la kubadilishwa kwa sheria hizo ni kuwa kuanzia hapo Sheria za Wayahudi zimefutwa. Hazina tena uhalali wa kutekelezwa.

Lakini tokeo muhimu na la maana zaidi lilionekana, muda mchache baadaye, wakati Mtume *(rehma na amani juu yake)* alipoota au kuona kuwa ameonyeshwa kuwa kitendo cha kuachiwa huru kwa Ya'juj na Ma'juj kimeanza. Pia alithibitisha kuachiwa kwa *Dajjal*, Mtume wa Uongo, wakati alipoenda na Umar (*radhiallahu anhu*) kukutana na mvulana wa Kiyahudi aliyeitwa Ibn Sayyad ambaye alimshuku kuwa ni *Dajjal*. Ujumbe kuwa *Dajjal*

amekwisha achiwa ulipatikana wazi pale ambapo Umar alipoomba ruksa kwa Mtume *(rehma na amani juu yake)* amkate kichwa Ibn Sayyad na Mtume *(rehma na amani juu yake)* akamnyima ruksa kwa kusema: "*Kama huyu ni Dajjal, hutoweza kumuua. Na kama si Dajjal itakuwa dhambi kumuua*."

Ikiwa *Dajjal* amekwishaachiwa, na pia ikiwa Ya'juj na Ma'juj wameshaachiwa, hayo yote ni ishara ya wazi kuwa Zama za Mwisho, au Zama za *Fitan* (majaribu na mitihani) zilianza wakati wa uhai wa Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake)* baada ya kubadilishwa kwa *Qiblah.* **'Mlango' au 'upenyo' kwa Wayahudi kuweza kujipatia Msamaha wa Mwenyezi Mungu kuanzia sasa umefungwa milele na adhabu kali kuliko zote ya Mwenyezi Mungu itaanza.** (Angalia Sura ya 12, kichwa nambari 7)

Daima, haitotokea tena Wayahudi wakawa na haki ya kurithi Ardhi Takatifu. Kipindi pekee ambacho wataweza kurudi hapo na kuichukua tena na kuidhibiti ni pale tu wakati Y'ajuj na M'ajuj watakapokuwa *wamesambaa kwenda pande zote*, hivyo wameidhibiti dunia nzima na kuiingiza kwenye mfumo wa Ya'juj na Ma'juj. Lakini hiyo nayo, itakuwa ni sehemu ya Mpangilio Mkubwa wa Mwenyezi Mungu kwa kupitia kwayo Wayahudi wataadhibiwa kwa adhabu kali kuliko zote ambayo haijawahi kutokea.

Sura ya 8

YESU, MTUME WA KWELI, NA DAJJAL, MTUME WA UONGO

وَنُقَلِّبُ أَفْـِٔدَتَهُمْ وَأَبْصَـٰرَهُمْ كَمَا لَمْ يُؤْمِنُوا۟ بِهِۦٓ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَنَذَرُهُمْ
فِى طُغْيَـٰنِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴿١١٠﴾

"Nasi twazigeuza nyoyo zao na macho yao. Kama walivyo kuwa hawakuamini mara ya kwanza (ujumbe huu), na tunawaacha katika maasi yao (ya kukata ukweli huu) wakitangatanga."

(Qur'ani, al-An'am, 6:110)

[Nasi tutazigeuza (tutazichanganya) nyoyo na macho yao (ya Kiyahudi) ikiwa ni matokeo ya kukataa kwao huko nyuma ujumbe huu, miongoni mwa mengine, kumkataa Masihi, mwana wa Maryam…]

Yesu, Masihi

Mitume ya Mwenyezi Mungu waliwafikishia ujumbe Wana wa Israili ahadi ya Mwenyezi Mungu ya kuwaletea Mtume ambaye atakuwa Mtume wao, atakayejulikana kama Masihi, na mabaye ataitawala dunia kutoka kwenye kiti cha enzi cha Mfalme Daudi *(rehma na amani juu yake).* Hii, kwa ufupi, ilikuwa ni bashira ya kurejeshwa kwa zama za dhahabu za Suleyman *(rehma na amani juu yake).*

Katika 1 Chronicles, 17:11-15, Mtume Nathan aliongea na Mfalme Daudi *(rehma na amani juu yake)* kuhusu Masihi na kumwita *Mwana wa Daudi:*

"Na itakuja kutimia kuwa siku zako zitakapokwisha na ukalazimika kwenda ili kuungana na baba zako, basi nitamsimamisha mmoja kati ya kizazi chako baada yako, ambaye atatokana na wanao, na nitampa ufalme. Naye atanijengea Mimi nyumba, na Nitaufanya ufalme wake uwe wa milele. Nitakuwa baba yake, naye atakuwa mwana Wangu: na sitaondoa Baraka Zangu kwake, kama Nilivyoziondoa kutoka kwa Yule aliyekuwa kabla yako: Nami nitamtuliza katika Nyumba Yangu na Ufalma Wangu milele, na kiti chake cha enzi kitadumu milele na milele."

(1 Chronicles, 17:11-15)

Miaka mingi baadaye Isaiah aliongezea haya yafuatayo:

"Kwetu mtoto atazaliwa, kwetu tutapewa mwana: na Utawala utakuwa mabegani mwake (ikim. Atatawal dunia); na jina lake ataitwa Mwingi wa Maajabu, Mshauri, Mungu Mwingi wa Nguvu, Baba wa Milele, (Mwana wa) Mfalme wa Amani.
Utawala wake na amani hautokwa na kikomo juu ya kiti cha Daudi, na juu ya Utawala wake, kuuongoza, kuujenga kwa maamuzi na haki kuanzia hapo kwa milele. Utashi wa watumishi wa Bwana watafanya hayo."

(Isaiah 9:6-7)

Jeremiah alimtaja kama:
"...tawi la wema, uadilifu na mwenendo mwema la Daudi."

(Jeremiah 23;5-6)

Isaiah aliongezea zaid juu yake:
"Angalia Mtumishi wangu, kwake yeye roho yangu ina furaha: Nimeweka roho yangu kwake: na atafanya maamuzi kwa Wageni.
Hatolia, wala hatainua, na hatopaaza sauti yake ili asikike mtaani.
Jani lililoburuzwa halitokatika, na katani inayotoa moshi hatoizima: ataleta uamuzi kwenye ukweli.
Hatoshindwa wala hatokata tama, 'hadi atakapotenga uamuzi (korti) duniani kote: na visiwa vitasubiri sheria yake.

(Isaiah: 42:1-4)

Pia Nitakupa wewe Mwanga Wangu kwa Wageni, ili uwe uokozi Wangu hadi mwisho wa dunia.

(Isaiah: 49:6)

Na Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake)* alisema kuwa yeye, Masihi, atakuwa *Hakimun A'adil* (Mtawala wa Haki wa dunia):
"Alisikika akisema Abu Hurairah: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alisema: "Kwa Yule ambaye Roho yangu iko Mikononi Mwake (Naapa kuwa) mwana wa Maryam punde atashuka kati yenu kama mtawala wa haki. Atauvunja msalaba na kuwaua nguruwe na kuondoa Jizyah (kodi ya adhabu wanayotozwa Wakristo na Wayahudi wanaoishi kwenye ardhi ya Waislamu). Kisha patakuwa na wingi wa pesa (mali) na hakuna atakayekubali zaka (zawadi za misaada)."

(Sahih Bukhari)

Sura mbili (tofauti) zinazohitilafiana za Masihi

Wayahudi walifurahi sana walipopata habari hizi za Ahadi ya kuletewa Masihi. Lakini walichanganyikiwa kutokana na ukweli kuwa palikuwa na sura mbili tofauti zinazohitilafiana za yeye mwenyewe na kazi yake au ujumbe wake. Ya kwanza ni ile ya Mfalme mshambulizi ambaye atawarudishia 'Watu Waliochaguliwa na Allah' (ambao wakati ule walikuwa Wayahudi) Ardhi Takatifu na atatawala dunia yote kwa amani. Ya pili ni ile ya Masihi aliye mtaratibu na mwenye kupata taabu. Picha hizo mbili zinazohitilafiana zilitajwa wazi katika Isaiah ambaye alimweleza Masihi kuwa kama 'Mtumishi wa Mungu' ambaye atafanikiwa, atainuliwa na kutukuzwa sana:

"Angalia, Mtumishi wangu atapambana kwa busara na hekima, naye atatukuzwa na kusifiwa na atakuwa wa juu sana."

(Isaiah: 52:13)

Na akaendelea katika msemo huo huo kuelezea kuwa 'Mtumishi' atajeruhiwa kiasi kwamba itakuwa vigumu kumtambua kama ni binaadamu, na kuwa atatukuzwa na pia atadhalilishwa:

"Kama vile ambavyo wengi watashangazwa kama wewe, naye ataonekana amebadilika kuliko mtu yeyote, na umbo lake zaidi kuliko wana wa watu."

(Isaiah: 52:14)

Kadiri ilivyokuwa haiyumkiniki, Isaiah alitabiri kuwa 'Mtumishi' atapigwa usoni na mgongoni. Atadhalilishwa kwa kutemewa mate usoni (Isaiah, 50;4-11). Na haya ndiyo yale yale yaliyomtokea Yesu. Mwandishi wa Kikristo, Hal Lindsey, anazungumzia kisa hicho na kusema kuwa hiyo inadhihirisha ukweli wa utabiri wa Isaiah: 52:12 na 53:13:

"Ni jambo linalojulikana sana kuwa haya ndiyo yaliyomtokea Yesu wakati alipokuwa akipelekwa kwenye kesi sita zisizo halali alizokabilishwa. Maafisa katika hekalu la Herod na mlinzi walimtemea mate baada ya kushutumiwa na Sanhedrin. Kisha walimfunga macho na kumpiga usoni. Kasha akavalishwa taji la miba kichwani na akapigwa kwa mkwaju wa Kirumi. Ulikuwa mkwaju wa kikatili wa ngozi ukiwa umewekewa vipande vya mifupa au vyuma ili kuongeza maumivu kwa anayechapwa."

(Hal Lindsey, "Masihi". Harvest House Publishers, Oregon, 1982, ukurasa 108-109.

Isaiah aliendelea kuwatambua kuwa Wayahudi ndiyo watakuwa wale watakaomshutumu na kumtesa 'Mtumishi wa Mungu' (ikim. Masihi). Alifanya hivyo alipomuelezea kuwa Mtumishi-Masihi atakuwa "*aliyedharauliwa, atakayechukiwa na kukifiwa na taifa lote (Isaiah 49:7).* Hal Lindsey analitaja jina 'taifa' likiwa katika umoja na si wingi, na anaendelea kupinga tafsiri isiyo rasmi ya udanganyifu ya aya:

"Ni bahati mbaya sana (na ni udanganyifu) kuwa Bibila toleo la RSV na Maelezo ya Tafsiri ya Kiyahudi ya Soncino vimetafsiri aya hii "Kwake yeye atakayechukiwa na mataifa." Kwa kutafsiri 'mataifa' kwa wingi, inaifanya kama vile Wageni ambao mara zote wanatajwa kama 'mataifa' kuwa ni wale wanaomdhalilisha na kumchukia Mtumishi. Wazo linajengwa hapa kuwa Mtumishi ni Israeli na anachuliwa na Wageni. Wakati hiyo inaweza kuwa ilikuwa kweli kwenye historia ya Wayahudi, wazo hilo haliwezi kuthibitishwa kwa ushahidi uliopo hapa kwenye ayah ii kwa sbabu neno la Kiyahudi lililotumika kama 'taifa' ni 'goi' na liko katika hali ya umoja, na linaweza kutafsiriwa kiuhalali kwa maana ya 'taifa' tu, na katika maana hiyo linazungumzia Israeli peke yake." (Lindsey ukurasa wa 109).

Nakala ya Biblia toleo la KJ (Toleo la Mfalme James) kwa upande wa pili, imetoa tafsiri halali ya aya:

"Naye Mungu akasema, Mwokozi wa Israeli, na Mtakatifu Wake, yeye ambaye anadhalilishwa na watu, ambaye taifa linamchukia, mtumishi wa watawala, Wafalme wataona na watainuka, maprinsi pia wataabudu, kwa ajili ya Mungu ambaye ni muaminifu, Mtakatifu wa Israeli, naye atakuchagua wewe."

(Isaiah, 49:7)

Hata ukirudi nyuma hadi kufikia (kitabu cha) Mwanzo palikuwa na utabiri unaomtaja Yule ambaye kupitia kwake 'utawala' wa dunia, ambao mwanzo ulianzishwa na Daudi *(rehma na amani juu yake)* na Suleyman *(rehma na amani juu yake)* utaendelezwa. Anatajwa kama Shiloh:

"Utawala (jofu la) hautoondoka kutoka (mwana wa) Judah, wala shada la utawala kutoka kati ya miguu yake, hadi Shiloh atakapokuja, na kwake yeye kutakuwa utii wa watu."

(Mwanzo 49:10)

Utabiri huu haukutaja tu kabila ambamo Masihi atatoka, bali pia uliuelezea ukoo wa Wafalme wajao. Tafsiri ya Kirabbai toka nyakati za kale ulilitambua 'Shiloh' kama ni cheo cha Masishi na ilitarajiwa aje kutoka katika kabila la Yudah.

Kuchanganyikiwa kulipatikana pale ambapo waandishi wasiojulikana walipoharibu maandishi ya Isaiah na kusema kuwa Masihi si tu atazaliwa kama motto (hivyo kuwa binaadamu) na kasha atatawala dunia, bali pia kuwa atakuwa Mungu. Maandishi hayo yaliyoharibiwa yalimtaja Masihi kama Mungu na mtu:

"Kwetu mtoto atazaliwa, kwetu tutapewa mwana: na Utawala utakuwa mabegani mwake (ikim. Atatawal dunia); na jina lake ataitwa Mwingi wa Maajabu, Mshauri, Mungu Mwingi wa Nguvu, Baba wa Milele, (Mwana wa) Mfalme wa Amani.

(Isaiah, 9:6)

Miaka elefu mbili iliyopita, wakati Mwenyezi Mungu alipotimiza ahadi yake na kumtuma Masihi, Yesu mwana wa maryamu *(rehma na amani juu yake*) kwa Wana wa Israili (*Banu israil*), aliwakuta wakishikilia matendo ya 'nje' ya kidini wakati wakidharau sehemu ya 'ndani' ya kiroho ambayo ni kiini. Na hata matendo ya nje yalikuwa yameharibiwa kwani waliyabadilisha maandiko kuendana na matakwa yao. Wakati Yesu *(rehma na amani juu yake*) alipothibitisha kuwa yeye ni Masihi aliyeahidiwa, na alipohubiri bila woga umuhimu wa 'ndani' wa kiroho wa dini na kushutumu kuharibiwa kwa matendo ya 'nje', baadhi ya Wayahudi walimkubali lakini wengi zaidi walimkataa. Na wanaendelea kumkataa yeye kama Masihi hadi leo hii. *Qur'ani* inasema kuwa walijisifu (wakati ule) kuwa wamemuua (kwa kumsulubu):

وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا الْمَسِيحَ عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ رَسُولَ اللَّهِ وَمَا قَتَلُوهُ وَمَا
صَلَبُوهُ وَلَٰكِن شُبِّهَ لَهُمْ ۚ وَإِنَّ الَّذِينَ اخْتَلَفُوا فِيهِ لَفِي شَكٍّ مِّنْهُ ۚ مَا لَهُم
بِهِ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا اتِّبَاعَ الظَّنِّ ۚ وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًا ﴿١٥٧﴾

"Na kwa kusema kwao: Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu...."

(Qur'ani, al-Nisa, 4:157)

Wakati walipomuona 'anakufa' msalabani mbele ya macho yao waliona kuwa huo ni ushahidi wa wazi kuwa yeye ni muongo. Waliamini kuwa asingeweza kuwa masihi kwani Taurati inasema kuwa yeyote anayekufa kwa kusulubiwa 'amelaaniwa' na mwenyezi Mungu (Deuterenomy, 21:23). Pili, asingeweza kuwa masihi kwani amekufa kabla hajaikomboa Ardhi Takatifu kutoka kwenye utawala wa wapagani wa Kirumi, na hakutawala dunia kutoka kwenye kiti cha enzi cha Daudi (*rehma na amani juu yake*) (ikim. Jerusalem).

Na ndipo wakaendelea kusubiri Masihi aje. Kila Myahudi aliyemkataa Yesu (*rehma na amani juu yake*) kama Masihi na akaendelea kusubiri toka hapo Masihi aje anahusika, japo si moja kwa moja katika juhudi za kumsulubu Yesu (*rehma na amani juu yake*). Hii inatokana na kumkataa kwao kuwa yeye ni Masihi kunaungana na kifo ambacho wanadhani kilimkuta.

Isipokuwa Mwenyezi Mungu amesema kuwa Wayahudi walidanganyika kwa kudhani kuwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) wamemuua au wamemsulubu:



"Na kwa kusema kwao(kwa kujisifu): Sisi tumemuuwa Masihi Isa, mwana wa Maryamu, Mtume wa Mwenyezi Mungu - nao hawakumuuwa wala hawakumsulubu, bali walifananishiwa tu (ilionekana tu kwao kuwa wamemuua). Na hakika wanao khitalifiana katika haya wamo katika shaka nayo. Wao hawana ujuzi nayo wowote, ila ni kufuata dhana tu. Kwa yakini wala hawakumuuwa."

(Qur'ani, al-Nisa, 4:157)

Hivyo, ni nini kilimtokea Yesu (*rehma na amani juu yake*)? *Qur'ani* imeelezea nini kilimtokea Yesu. Imetoa maelezo tofauti matano:

Kwanza, *Qur'ani* imesema kuwa Wayahudi hawakumuua Yesu:

"*...kwa yakini wala hawakumuuwa....*"

(Qur'ani, al-Nisa, 4:157)

Pili, imesema kuwa hawakumsulubu:

"*...wala hawakumsulubu...*"

(Qur'ani, al-Nisa, 4:157)

Tatu, imesema kuwa Allah alimchukua (ikim. Aliichukua roho yake). Kuna maelezo hayo katika sehemu mbili tofauti za *Qur'ani*:

إِذْ قَالَ ٱللَّهُ يَٰعِيسَىٰٓ إِنِّي مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَيَّ وَمُطَهِّرُكَ مِنَ
ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ وَجَاعِلُ ٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوكَ فَوْقَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا۟ إِلَىٰ يَوْمِ
ٱلْقِيَٰمَةِ ۖ ثُمَّ إِلَيَّ مَرْجِعُكُمْ فَأَحْكُمُ بَيْنَكُمْ فِيمَا كُنتُمْ فِيهِ
تَخْتَلِفُونَ ﴿٥٥﴾

"Pale Mwenyezi Mungu alipo sema: Ewe Isa! Mimi nitakufisha (ikim. Nitachukua roho yako – neno lililotumika ni Wafaat), na nitakunyanyua kwangu, na nitakutakasa na wale walio kufuru, na nitawaweka wale walio kufuata juu ya wale walio kufuru, mpaka Siku ya Kiyama. Kisha marejeo yenu yatakuwa kwangu, nikuhukumuni katika yale mliyo kuwa mkikhitalifiana."

(Qur'ani, Al-Imran, 3:55)

وَإِذْ قَالَ ٱللَّهُ يَٰعِيسَى ٱبْنَ مَرْيَمَ ءَأَنتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ ٱتَّخِذُونِي وَأُمِّيَ
إِلَٰهَيْنِ مِن دُونِ ٱللَّهِ ۖ قَالَ سُبْحَٰنَكَ مَا يَكُونُ لِيٓ أَنْ أَقُولَ مَا لَيْسَ لِي
بِحَقٍّ ۚ إِن كُنتُ قُلْتُهُۥ فَقَدْ عَلِمْتَهُۥ ۚ تَعْلَمُ مَا فِي نَفْسِي وَلَآ أَعْلَمُ مَا فِي
نَفْسِكَ ۚ إِنَّكَ أَنتَ عَلَّٰمُ ٱلْغُيُوبِ ﴿١١٦﴾
مَا قُلْتُ لَهُمْ إِلَّا مَآ أَمَرْتَنِي بِهِۦٓ أَنِ ٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ رَبِّي وَرَبَّكُمْ ۚ وَكُنتُ
عَلَيْهِمْ شَهِيدًا مَّا دُمْتُ فِيهِمْ ۖ فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِي كُنتَ أَنتَ ٱلرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ ۚ
وَأَنتَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿١١٧﴾

"

"Na pale Mwenyezi Mungu atakapo sema (siku ya Qiyama): Ewe Isa bin Maryamu! Ati wewe uliwaambia watu: Nifanyeni mimi na mama yangu kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu? (Na Isa) atasema: Subhanaka, Wewe umetakasika! Hainifalii mimi kusema ambayo si haki yangu. Ikiwa nilisema basi bila ya shaka umekwisha yajua. Wewe unayajua yaliyo ndani ya nafsi yangu, lakini mimi siyajui yaliyo katika nafsi yako. Hakika Wewe ndiye Mjuzi mkubwa wa yaliyo fichikana.
Sikuwaambia lolote ila uliyo niamrisha, nayo ni: Muabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu Mlezi na Mola wenu Mlezi. Na mimi nilikuwa shahidi juu yao nilipo kuwa nao. Na ulipo nifisha(ikim.ulipochukua roho yangu- neno linalotumika ni Wafaat) ukawa Wewe ndiye Muangalizi juu yao. Na Wewe ni shahidi juu ya kila kitu."

(Qur'ani, al-Maida, 5:116-117)

Kama Mwenyezi Mungu angekuwa amechukua roho ya Yesu (rehma na amani juu yake) na asingeirudisha, hicho kingekuwa ni kifo, (*Maut).* Lakini *Qur'ani* inasisitiza kuwa hakuuawa (na wala hakusulubiwa):

"*...kwa yakini wala hawakumuuwa..."*

(Qur'ani, al-Nisa, 4:157)

Je, Mwenyezi Mungu alifanya nini na roho baada ya kuichukua? Inawezekana kuwa, kwa mfano, aliirudisha roho kwenye mwili? Je, kitu kama hicho kinawezekana?

Qur'ani inathibitisha kuwa Allah hurudisha roho baada ya kuzichukua kutoka kwenye miili:



"MWENYEZI MUNGU huzitoa (huzichukua) roho wakati wa kufa. Na zile zisizo kufa (huzichukua) wakati wa kulala kwake (ikim. zile roho ambazo hazikuchukuliwa wakati wako macho, huzichukua wakati wa kulala), huzishika zilizo hukumiwa kufa (ikim. haruhusu zirudi kwenye mwili), na huzirudisha nyengine mpaka ufike wakati (wake) uliowekwa. Hakika katika hayo bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri."

(Qur'ani, al-Zumar, 39:42)

Je hayo yanaweza kuwa ndiyo yaliyomtokea Yesu *(rehma na amani juu yake)?* Majibu yanapatikana katika maelezo yanayopatikana katika sehemu mbili tofauti za *Qur'ani.*

Nne, *Qur'ani* imesema kuwa Allah, Mwingi wa Nguvu, alifanya ionekane kuwa Yesu *(rehma na amani juu yake)* ameuawa. Hii iliweza kutokea aidha kwa kubadilisha 'kitu kimoja' na kuweka 'kingine' au kwa 'kumuweka mtu mmoja' badala ya 'mwingine' (*tashbih*). Hivyo kuwafanya wale waliokuwa wakimshuhudia waamini kuwa Yesu *(rehma na amani juu yake),* kwa hakika, amekufa (*Maut*):

"*...bali walifananishiwa tu kuwa ni hivyo..."* *(Yusuf Ali)*

"...bali ilionekana kwao (kama vile imekuwa wamemuua) ..." *(M. Assad)*

"...bali ilionekana hivyo kwao..." *(M. Pickthal)*

Sasa inawezekana kwa sisi kujibu swali: Je, Mwenyezi Mungu alifanya nini na roho baada ya kuichukua? Jibu moja linalowezekana kukubalika ni kuwa Mwenyezi Mungu alibadilisha *kitu kimoja kwa kingine (tashbih)*

- Mwenyezi Mungu aliichukua roho ya Yesu *(rehma na amani juu yake)* wakati bado akiwa msalabani,
- Mwenyezi Mungu hivyo akawafanya wale waliokuwa wakishuhudia tendo hilo waamini kuwa Yesu *(rehma na amani juu yake)* amekufa,
- Mwenyezi Mungu baadaye akairudisha roho ya Yesu *(rehma na amani juu yake)* baada ya kushushwa msalabani wakati hakuna aliyekuwa akishuhudia. Akamchukua mbinguni ambako siku moja atarejea duniani.

Tofauti pekee kutoka imani iliyokubalika na Wakristo na tafsiri hapo juu ya *Qur'ani* ni kuwa muda ambao ulipita baina ya kitendo cha kuwekwa msalabani na kupaa kwa Yesu *(rehma na amani juu yake)* mbinguni ni pale ambapo Wakristo wanatambua / wanaamini kuwa alikuwa amekufa. Katika tafsiri hiyo hapo juu ya *Qur'ani* kuwa hakutambuliwa kuwa alikuwa amekufa kwani roho yake ilirudishwa kwenye mwili.

Wale ambao wanakataa maelezo hayo ya *Qur'ani* wanadai kuwa Yesu *(rehma na amani juu yake)* hakuwekwa kabisa kwenye msalaba. Wanatafsiri maneno ya *Qur'ani* "*...wala hawakumsulubu..."* kuonyesha kuwa hakuwahi kuwekwa kwenye msalaba.

Wanafikia uamuzi huo kwa msingi wa mawazo yao kuwa kusulubiwa (katika maana ya neno kama inavyotumiwa katika *Qur'ani*) kuna maana ya kuwekwa tu kwenye msalaba na hakuhitaji mtu huyo aliyewekwa hapo afe kutokana na kuwekwa kwenye msalaba huo. Katika kufasiri *Surah al-Maida, 5:36* mfasiri wa *Qur'ani, Ibn Kathir*, ameshika mtazamo kuwa tendo la kusulubiwa kuna maanisha kifo.

Kwa upande wa pili wa uwezekano wa kilichotokea katika tukio hilo, ni kwa Mwenyezi Mungu kumuweka *mtu mmoja badala ya mwingine (tashbih)* ikimaanisha kuwa mtu mwingine alichukua nafasi ya Yesu (*rehma na amani juu yake*). Hii ni nadharia ya 'kubadilisha'. Ni pendekezo la wazo, kama mapendekezo mengine, linalazimika kutiwa katika kundi la: *Allahu 'Alam (*Allah, Mtukufu, ndiye ajuaye vyema!). Kuna wasomi wengi mashuhuri wa Kiislamu, hata hivyo, ambao wanakubali nadharia ya kubadilisha. Wale wanaoukataa mtazamo huu wanadai kuwa unamtupia Mwenyezi Mungu, Mtukufu kuliko chochote na yeyote, na Msimamizi wa Haki, tendo lililo wazi la utovu wa haki kwa kumsababishia mtu asiyetenda kosa lolote (ikim. hakuhusika na makosa aliyokuwa anashutumiwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) ili asulubiwe kwa kumuweka kwenye nafasi hiyo badala ya Yesu (*rehma na amani juu yake).* Wakati Mwenyezi Mungu amesema katika *Qur'ani* kuwa hakuna roho itakayobeba mzigo war oho nyingine *(Al-Anam, 6:164; Banu Israil, 17:15; al-Fatir, 35:18; al-Zumar, 39:7; al-Najm, 53:38).*

Tano, *Qur'ani* imesema kuwa mwenyezi Mungu alimchukua Kwake Yesu (*rehma na amani juu yake):*

وَإِن مِّنْ أَهْلِ ٱلْكِتَٰبِ إِلَّا لَيُؤْمِنَنَّ بِهِۦ قَبْلَ مَوْتِهِۦ ۖ وَيَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ يَكُونُ
عَلَيْهِمْ شَهِيدًا ﴿١٥٩﴾

"Hapana, bali Mwenyezi Mungu alimchukua Kwake, na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye Nguvu, Mwenye Hekima."

(Qur'ani, al-Nisa, 4:158)

إِذْ قَالَ ٱللَّهُ يَٰعِيسَىٰٓ إِنِّي مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَيَّ وَمُطَهِّرُكَ مِنَ
ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ وَجَاعِلُ ٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوكَ فَوْقَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا۟ إِلَىٰ يَوْمِ
ٱلْقِيَٰمَةِ ۖ ثُمَّ إِلَيَّ مَرْجِعُكُمْ فَأَحْكُمُ بَيْنَكُمْ فِيمَا كُنتُمْ فِيهِ
تَخْتَلِفُونَ ﴿٥٥﴾

"Pale Mwenyezi Mungu alipo sema: Ewe Isa! Mimi nitakufisha (ikim. Nitachukua roho yako – neno lililotumika ni Wafaat), na nitakunyanyua kwangu, na Nitakutakasa (kutokana na uongo) na wale walio kufuru..."

Qur'ani inaendelea kuelezea kuwa kila roho (Nafs) lazima ikutane (ionje) mauti:

كُلُّ نَفْسٍ ذَآئِقَةُ ٱلْمَوْتِ ۗ وَإِنَّمَا تُوَفَّوْنَ أُجُورَكُمْ يَوْمَ
ٱلْقِيَٰمَةِ ۖ فَمَن زُحْزِحَ عَنِ ٱلنَّارِ وَأُدْخِلَ ٱلْجَنَّةَ فَقَدْ فَازَ ۗ وَمَا
ٱلْحَيَوٰةُ ٱلدُّنْيَآ إِلَّا مَتَٰعُ ٱلْغُرُورِ ﴿١٨٥﴾

"Kila nafsi itaonja mauti. Na bila ya shaka mtapewa (kwa kazi zenu) ujira wenu kaamili Siku ya Kiyama. Na atakaye epushwa na Moto na akatiwa Peponi basi huyo amefuzu(mtihani wa au lengo la maish). Na maisha ya dunia si kitu ila ni starehe ya udanganyifu."

(Qur'ani, al-Imran, 3:185)

Kwa kuwa Mwenyezi mungu amesema kuwa kila roho (nafsi) lazima ionje mauti, inafuata kuwa Yesu (*rehma na amani juu yake*), pia, kama alikuwa na roho (nafsi0 lazima aonje mauti. Swali hapo linajitokeza: Je, Yesu (*rehma na amani juu yake*) alikuwa na roho (nafsi)? Je, alkuwa ni binaadamu? Na kwa kuwa tunajua kuwa alikuwa mwana wa Maryamu, lazima tujiulize: Je, Maryamu alikuwa binaadamu?

Qur'ani inakuja na jibu la nguvu kabisa linalorhibirisha 'ubinaadamu' wa wote wawili Yesu na Maryamu:

مَّا ٱلْمَسِيحُ ٱبْنُ مَرْيَمَ إِلَّا رَسُولٌ قَدْ خَلَتْ مِن قَبْلِهِ
ٱلرُّسُلُ وَأُمُّهُۥ صِدِّيقَةٌ ۖ كَانَا يَأْكُلَانِ ٱلطَّعَامَ ۗ ٱنظُرْ
كَيْفَ نُبَيِّنُ لَهُمُ ٱلْآيَٰتِ ثُمَّ ٱنظُرْ أَنَّىٰ
يُؤْفَكُونَ ﴿٧٥﴾

"Masihi mwana wa Maryam si chochote ila ni Mtume (wa Mwenyezi Mungu). Wamekwisha pita Mitume wengi kabla yake. Na mama yake ni mwanamke mkweli (na mnyoofu wa tabia – siddiqah). Wote wawili walikuwa wakila chakula. Angalia jinsi tunavyo wabainishia alama zetu (wale wanaokufuru kwa kudai Utatu wa Mungu, kuwa Yesu pia ni Mungu na Maryamu pia ni Mungu) kisha angalia vipi wanavyo geuzwa kutoka kwenye Ukweli".

(Qur'ani, al-Maidah, 5:75)

Kwa sentensi moja fupi na ya kushtusha "*Wote wawili walikuwa wakila chakula" Qur'ani* inaondoa na kufuta kabisa fikra zozote za kuwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) na Maryamu walikuwa chochote zaidi ya kuwa binaadamu.

Qur'ani pia imeeleza kuwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) hakuwa zaidi ya mtumishi na mtumwa wa Mwenyezi Mungu:

يَٰٓأَهْلَ ٱلْكِتَٰبِ لَا تَغْلُوا۟ فِى دِينِكُمْ وَلَا تَقُولُوا۟ عَلَى
ٱللَّهِ إِلَّا ٱلْحَقَّ ۚ إِنَّمَا ٱلْمَسِيحُ عِيسَى ٱبْنُ مَرْيَمَ رَسُولُ ٱللَّهِ
وَكَلِمَتُهُۥٓ ۚ أَلْقَىٰهَآ إِلَىٰ مَرْيَمَ وَرُوحٌ مِّنْهُ ۖ فَـَٔامِنُوا۟ بِٱللَّهِ
وَرُسُلِهِۦ ۖ وَلَا تَقُولُوا۟ ثَلَٰثَةٌ ۚ ٱنتَهُوا۟ خَيْرًا لَّكُمْ ۚ إِنَّمَا ٱللَّهُ إِلَٰهٌ
وَٰحِدٌ ۖ سُبْحَٰنَهُۥٓ أَن يَكُونَ لَهُۥ وَلَدٌ ۘ لَّهُۥ مَا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِى
ٱلْأَرْضِ ۗ وَكَفَىٰ بِٱللَّهِ وَكِيلًا ﴿١٧١﴾

"Enyi Watu wa Kitabu (Wakristo na Wayahudi)! Msipite kiasi (msivuke mipaka) katika dini yenu, wala msimseme Mwenyezi Mungu ila kwa lilio kweli. Hakika Masihi Isa mwana wa Maryamu ni (hakuwa zaidi ya) Mtume wa Mwenyezi Mungu, na Neno lake tu Alilompelekea Maryamu, na ni Roho iliyo toka Kwake. Basi Muaminini Mwenyezi Mungu na Mitume yake. Wala msiseme: Utatu. Acheni! Itakuwa kheri kwenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mungu Mmoja tu. Ametukuka sana Yeye juu ya kuwa na mwana. Ni Vyake Yeye vyote viliomo katika mbingu na katika ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mfanyaji wa kila jambo."

(Qur'ani, al-Nisa, 4:171)

إِنْ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ وَجَعَلْنَاهُ مَثَلًا لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٥٩﴾

"*Kwa hakika hakuwa yeye (Yesu - Isa) ila ni Mtumwa Tuliye Mneemesha na Tukamfanya ni mfano kwa Wana wa Israili."*

(Qur'ani, al-Zukhruf, 43:59)

Hivyo ni wazi kuwa kwa mtazamo wa *Qur'ani*, Yesu (*rehma na amani juu yake*) ni binaadamu. Inafuata mtiririko wa mantiki kuwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) anaguswa na sheria ya ujumla ya kufa. Naye, inabidi aonje kifo, mauti.

Yesu (*rehma na amani juu yake*) **atarejea.**

Qur'ani imesisitiza kuwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) hakufa (ikim. hakuuawa wala hakusulubiwa). Ikaongeza kuwa alipazwa na kuchukuliwa na Mwenyezi Mungu. Na kwa kuwa *Qur'ani* imesema kuwa kila roho (ikiwemo na ya Yesu) lazima ionje mauti, inasibu kuwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) lazima arudi na aonje mauti kama vile kila binaadamu inambidi aonje mauti. Itabidi arudishwe ardhini (ikim. mwili wake itabidi baada ya kifo uzikwe kwenye ardhi, ambayo ndiko ulikotokana nako, ambako ni asilia ya kuumbwa binaadamu wote, tangu Adam) kama binaadamu wengine. Hii kikawaida inakuwa katika hali ya kuzikwa baada ya kufa. *Qur'ani* inamsema:

۞ مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ ﴿٥٥﴾

"Kutokana nayo (ardhi) Tumekuumbeni, na humo(ardhini) Tunakurudisheni, na kutoka humo (ardhini) tutakutoeni tena mara nyengine."

(Qur'ani, Ta-Ha, 20:55)

Lakini *Qur'ani* imetoa onyo kali ilipozungumzia kifo (mauti) ya Yesu (*rehma na amani juu yake).* Onyo hilo ni kuwa Wayahudi na Wakristo itawabidi wote wamkubali na kumuamini yeye (kama vile ambavyo *Qur'ani* imeweka sawa na wazi nafasi na wadhifa

wake kuwa Yesu *(rehma na amani juu yake)* ni Masihi na Mtume wa Mwenyezi Mungu, Allah) kabla 'Yesu' hajafa. Aya hii, hivyo inaweza wazi Mpango wa Mwenyezi Mungu kuwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) siku moja atarudi na kuwa tendo hilo litatokea kabla ya kufa kwake:


وَإِن مِّنْ أَهْلِ ٱلْكِتَٰبِ إِلَّا لَيُؤْمِنَنَّ بِهِۦ قَبْلَ مَوْتِهِۦ ۖ وَيَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ يَكُونُ
عَلَيْهِمْ شَهِيدًا ١٥٩

"*Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao."*

(Qur'ani, al-Nisa, 4:159)

Kwa kusaidia uelewa, fasiri fasaha zaidi, ya aya hiyo hapo juu:

"Na hakutakuwa katika Watu wa Kitabu (ikim.hapatokuwa hata na Myahudi mmoja atakayemkataa Yesu kama Masihi na Mtume wa Allah,na hapatokuwa hata na Mkristo mmoja atakayedai kuwa Yesu inabidi aabudiwe kama Mungu na kama mtoto wa Mungu) na ila hakika watamuamini yeye (Yesu) kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu (dhidi) yao."

(Qur'ani, al-Nisa, 4:159)

Hivyo siku hiyo kila Myahudi itampasa amkubali Yesu kama Masihi na kumuamini yeye, na kila Mkristo itambidi kuacha imani kuwa Yesu ni 'mwana wa Mungu' na ni mmoja kati ya utatu mtakatifu.

Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alisema kwa kusisitiza na uhakika kuwa, Yesu (rehma na amani juu yake) atarejea:

"Imepatikana kutoka kwa Abu Huraira: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu

"Imepatikana kutoka kwa Abu Hurairah: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alisema: "Kwa Yule ambaye Roho yangu iko Mikononi Mwake (Naapa kuwa) mwana wa Maryam punde atashuka kati yenu kama mtawala wa haki. Atauvunja msalaba na kuwaua nguruwe na kuondoa Jizyah (kodi ya adhabu wanayotozwa Wakristo na Wayahudi wanaoishi kwenye ardhi ya Waislamu). Kisha patakuwa na wingi wa pesa (mali) na hakuna atakayekubali zaka (zawadi za misaada)."

(Sahih, Bukhari)

Kwa hakika, kurejea kwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) ni moja kati ya Alama kuu kumi za Siku za Mwisho zilizotajwa na Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*):

"Imepatikana kutoka kwa Hudhayfah ibn Usayd Ghifari:
Mtume wa Allah (*rehma na amani juu yake*) alitokea ghafla kati yetu wakati tukiwa katikati ya majadiliano. Akasema: Mnajadiliana juu ya nini? (Maswahaba) wakajibu: Tunajadiliana kuhusu Saa ya Mwisho. Hapo akasema: Haitotokea hadi mtakapoziona alama kumi kabla (na ndipo) akataja moshi, Dajaal, mnyama wa ardhi, kutoka jua upande wa magharibi, kushuka kwa Yesu mwana wa Maryamu, Y'ajuj na M'ajuj, kupasuka ardhi katika sehemu tatu tofauti, sehemu moja magharibi, moja mashariki na mofa Uarabuni na mwisho wake moto utawaka Yemen, na utawakimbiza watu kwenda kwenye sehemu ya mkusanyiko."

(Sahih, Muslim)

Hivyo, Alama kumi ni kama ifuatavyo:

- **kuachiwa kwa *Dajjal* – Mtume wa Uongo,**
- **kuachiwa kwa Ya'juj na Ma'juj'**
- **kurudi kwa Yesu (***rehma na amani juu yake***) – Mtume wa Kweli,**
- **kutokea kwa moshi (*dukhan),***
- **kutokea kwa** *d'abatul ardh* **- kiumbe cha ardhi (ikim. Ardhi Takatifu),**
- **jua kutoka upande wa magharibi,**
- **kupasuka kwa ardhi na kuwapo mwanya utakaomeza vitakavyomezwa, Mashariki,**
- **kupasuka kwa ardhi na kuwapo mwanya utakaomeza vitakavyomezwa, Magharibi,**
- **kupasuka kwa ardhi na kuwapo mwanya utakaomeza vitakavyomezwa, Uarabuni,**
- **moto utawaka Yemen, na utawakimbiza watu kwenda kwenye sehemu ya mkusanyiko**."

(Msomaji anapewa tahadahari kuwa isieleweke kwamba Alama hizi zimepangwa kufuatana na jinsi zitakavyokuwa zikijitokeza – mfano ya mwanzo juu itatokea mwanzo na ya chini mwisho, **la hasha**)

Qur'ani imethibitisha kuwa kurudi kwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) kama ni "Alama ya Alama zote" za Siku ya Mwisho:

وَإِنَّهُۥ لَعِلْمٌ لِّلسَّاعَةِ فَلَا تَمْتَرُنَّ بِهَا وَاتَّبِعُونِ ۚ هَٰذَا صِرَاطٌ مُّسْتَقِيمٌ ﴿٦١﴾

"Na kwa hakika yeye (ikim. Yesu) ni Alama ya Saa (ya Kiyama)...."

(Qur'ani, al-Zukhruf, 43:61)

Yesu (*rehma na amani juu yake*) mwenyewe alitoa orodha ya alama za kuangaliwa kuashiria wakati ambapo atarejea:

- watajitokeza watu na kujiita Masihi, lakini watakuwa waongo,

- patakuwa na vita na tetesi za vita
- patatokea njaa kali kuliko zote duniani
- magonjwa yataikumba dunia
- patatokea ongezeko kubwa la vurugu na unyama baina ya watu
- matetemeko ya ardhi yataongezeka kwa idadi

Sasa tunapata majibu ya swali kwanini kuna picha mbili tofauti za masihi katika vitabu vitakatifu – ya kwanza Masihi mtulivu, mtaratibu na mnyenyekevu na ya pili shupavu, asiyesita kutumia nguvu. Wakati Yesu (*rehma na amani juu yake*) atakaporejea atakuja kukidhi picha hiyo ya pili.

Lakini Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) aliendelea na kudhihirisha kuwa kabla Yesu (*rehma na amani juu yake*) hajarudi, Mwenyezi Mungu atamfungulia Mtume wa Uongo (al-Masih al-Dajaal) aingie duniani katika Zama za Mwisho.

Dajjal ni nani?

Ndoto kuu kuliko zote ya Wayahudi kwa zaidi ya miaka 2000 ilikuwa ni ndoto ya kurudi kwenye Ardhi Takatifu kama watawala wa hapo ili waweze kufufua Nchi ya Israeli iliyoanzishwa na Mitume-Wafalme, David (Daud) (*rehma na amani juu yake*) na Solomon (Suleyman) (*rehma na amani juu yake*), kulijenga upya Hekalu lililojengwa na Solomon (*rehma na amani juu yake*) katika mji wa Jerusalem, na kumuabudu Mungu wa Abrahamu katika Hekalu hilo. Hiyo ni lazima ikubalike kuwa kwa hakika ni ndoto bora. Watu ambao wanaota ndoto kama hiyo kuwa ni ndoto kuu kuliko zote, ni lazima waw watu ambao wanaweza kufikia kilele cha ufanisi wa kiroho. Wanapaswa kuwa watu ambao wangeweka mbele 'maisha ya baadaye' – akhera badala ya haya ya duniani, na ambao jicho lao la ndani la kiroho lingeweza kupenya kwenye 'magamba' ya uongo na kuweza kuona ndani ya ukweli wa hali halisi ya kila kitu. Katika kiwango cha chini kabisa, wangeweza kugundua kuwa ndoto yao haiwezi kutimia kwa kupitia kuundwa kwa Nchi ya Israeli isiyomtambua Mwenyezi Mungu, yenye mfumo wa kidunia, na kutawala kwa nguvu na mabavu, ugandamizaji katika Ardhi Takatifu kwa zaidi ya miaka hamsini iliyopakwa damu za wanyonge. Haiyumkiniki kuwa ugandamizaji huo utaendelea kwa miaka mingine hamsini kabla hawajapata kipigo kikali kutokana na matendo yao ya uovu.

Hivi sasa Wana wa Israili asilia wote wanaamini kuwa ndoto yao kuu haiwezi na haitowezekana kutimia hadi Mtume maalum anayeitwa Masihi atokee miongoni mwao. *Ataleta uokovu katika mwisho wa zama na atatawazwa kama Mfalme wa dunia.* Utawala huu wa Masihi unarudiwa kila mahali katika vitabu vitakatifu (I Enoch: 45:3; 105:2; 28:29; 13:32-35; 14:9). Inaeleweka wazi na bila shaka kuwa Wayahudi wa Kiulaya ambao ndiyo waanzilishi wa Shirikisho la Wazayonisti hawaguswi kabisa na wala hawajishughulishi na utabiri wowote unaohusu Masihi.

Allah, Mtukufu alipanga kuwa Mtume wa Uongo (*al-Masih al-Dajjal*) atawaletea Wayahudi kiujanja kwa ulaghai kile ambacho watakiona kuwa ni kutimia kwa ndoto yao kuu kuliko zote, ikimaanisha kurejea kwenye Ardhi *yao* Takatifu, kufufuliwa kwa Taifa la Israeli, kuteuliwa kwa mfalme wa kuwatawala: (*Mteue mfalme kwa ajili yetu ili tuweze kupigania njia za Allah – Qur'ani, al-Baqarah, 2:246*). Ukweli ulio wazi kuwa wamedanganyika kikamilifu na kuundwa kwa Nchi ya Israeli ya kibeberu, kunatoa shuhuda iliyo wazi kuwa bado wanaendelea kuwamo katika upofu wa kiroho:

وَٱلَّذِينَ كَفَرُوٓاْ أَعۡمَٰلُهُمۡ كَسَرَابِۭ بِقِيعَةٖ يَحۡسَبُهُ ٱلظَّمۡـَٔانُ مَآءً حَتَّىٰٓ إِذَا
جَآءَهُۥ لَمۡ يَجِدۡهُ شَيۡـٔٗا وَوَجَدَ ٱللَّهَ عِندَهُۥ فَوَفَّىٰهُ حِسَابَهُۥۗ وَٱللَّهُ سَرِيعُ
ٱلۡحِسَابِ ٣٩

"*Na walio kufuru (walio- na wanaoikataa hii Qur'ani na huyu Mtume wa mwisho, miongoni mwa mengine) vitendo vyao ni kama sarabi (mazigazi) uwandani (jangwani). Mwenye kiu*

huyadhania ni maji. Hata akiyaendea hapati chochote. Na atamkuta Mwenyezi Mungu hapo naye Amlipe hisabu yake sawa sawa. Na Mwenyezi Mungu ni Mwepesi wa Kuhisabu."
"Qur'ani, al-Nur, 24-39)

Nchi ya Israeli leo hii iko katika hali hiyo hiyo inayotajwa hapo juu kwenye aya: mtu ambaye ameshikwa na kiu ya maji jangwani na anakimbilia sarabi akidhani ni maji.

"*Hakika Qur'ani hii inawasimulia Wana wa Israili mengi wanayo khitalifiana nayo. Nayo hakika ni Uwongofu na Rehema kwa Waumini."*
(Qur'ani, al-Naml, 27:76-77)

'Gamba' lililopo leo hii ni kuwa 'ndoto kuu kuliko zote' takriban imekwisha kamilika. Wana wa Israili asilia wamekwisha rejea kwenye Ardhi Takatifu, au wako huru kufanya hivyo, wakitokeo popote pale duniani ambapo wapo. Nchi ya Israeli ilifufuliwa mnamo mwaka 1948 na sasa ni nchi halisi. Kilichobaki tu ni kuteuliwa kwa mfalme na kuvunjwa kwa msikiti wa al-Aqsa (Masjid al-Aqsa) ili kuwezesha kujengwa kwa Hekalu:

"Mtakapokuja kwenye ardhi amabyo Mungu, Bwana wenu amewapa, na mkaidhibiti, na mkaishi humo, na mkasema: 'Nitamteua mfalme juu yangu, kama mataifa yote yaliyonizunguka', ndipo mtamtawaza mfalme ambaye Mungu, Bwana wako atamchagua (hapa inaelekezwa kwenye imani kuwa atatoka kwenye Nyumba ya David (Daud))
(Kumbukumbu ya Taurati, Deuterenomy, 17:14-15)

Baada ya hapo Israeli ni lazima iwe *Nchi Tawala* duniani na Mfalme wa Israeli lazima *atawale* dunia kutokea Jerusalem.

Ushahidi pekee unaotokana na mtiririko wa mantiki ni kuwa haya yote yasingeweza kutokea bila ya mchnago wa Masihi. Hili ndilo 'gamba'. Je, 'ukweli halisi' uko wapi?

'Ukweli halisi' wa yote haya, yakitazamwa kwa mtazamo wa *Kiislamu,* ni kuwa *Dajjal,* Mtume wa Uongo, amewadanganya Wayahudi kuamini kuwa baraka za Mungu zimewaleta karibu kabisa na kutimiza ndoto yao kuu kuliko zote. 'Ukweli halisi' ni kuwa upofu wao wa kiroho umewapeleka kwenye mtego wa kiroho ambapo kwa sasa hakuna tena jinsi ya kujiepusha nao. Wanashutumu ugandamizaji na uonevu duniani lakini wanahalalisha ugandamizaji na uonevu wao wenyewe kwa wengine. Wanafanya hivyo kwa misingi ya kuwa wao wana daraja maalum kwa Mungu, daraja mabayo watu wengine hawana. Na kwa kuwa wanaamini kuwa Ardhi Takatifu ni mali yao, wanaamini pia kuwa wna haki ya kuikomboa kutoka kwa wale ambao wameishi humo kwa karne kadhaa. 'Matokeo' au 'lengo'

linahalalisha ‘namna (yoyote)’ itakayotumika kutimiza lengo hilo. ‘Ukweli halisi’ ni kuwa wamedanganywa na wamepotezwa na *Dajjal*.

Dajjal, Mtume wa Uongo, ni *kiumbe* aliyeumbwa na Allah, Mtukufu, Mwingi wa Hekima, ambaye atajifanya Masihi na kuwadanganya Wayahudi wamuamini kuwa yeye ni Mtume wa Kweli. *Dajjal* amepewa na Mwenyezi Mungu, mwingi wa Hekima, nguvu nyingi na uwezo mkubwa wa ajabu, uhodari usio na kikomo na uwezo mkubwa sana na ujanja wa kupanga kudanganya na kughilibu. Wakristo wanamjua kwa jina la *AntiChrist. Dajjal*, kiumbe wa shari aliyeimbwa na Allah siku moja atajitokeza duniani kama binaadamu. Atakapofanya hivyo, atakuwa Myahudi, atakuw kijana kwa rika, mwenye umbo la kuashiria kuwa na nguvu nyingi mithili ya mwanariadha shupavu na pia atakuwa na nywele zilizojipindika pindika. Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake)* alimshuku kijana wa Kiyahudi, Ibn Sayyad, ambaye alikuwa ni mkazi wa Madina, kuwa ni *Dajjal*. Mtume *(rehma na amani juu yake)* kwa kufanya hivyo alithibitisha kuwa *Dajjal amekwishaachiwa aingie duniani na* siku moja atajitokeza kama:

- binaadamu
- Myahudi
- Kijana

Mtume wa Kweli, kama vile Solomon (Suleyman *(rehma na amani juu yake)*, atatawala dunia kutoka katika kiti cha enzi cha David (Daud) *(rehma na amani juu yake)* ikimaanisha kutokea Jerusalem. Ili aweze kufanya hivyo, inampasa kwanza atimize mambo yafuatayo:

- aikomboe Ardhi Takatifu kutoka kwenye utawala wa wale ambao hawamuabudu Mungu wa Ibrahimu,
- awalete ‘watu wateule (waliochaguliwa) (ambao, wakati wanabashiriwa na kupewa ahadi hiyo ya kiroho walikuwa Wayahudi) kwenye Ardhi Takatifu,
- alifufue Taifa la Israeli lililoanzishwa na David / Daud *(rehma na amani juu yake)* na Solomon / Suleyman *(rehma na amani juu yake)*,
- aifanye Israeli iwe *Taifa Tawala* duniani.

Hapo tu ndipo itakapokuwa inawezekana kwa Mtume wa Uongo kuitawala dunia kutoka kwenye kiti cha enzi cha Daud *(rehma na amani juu yake)* ikim. kutoka Jerusalem.

Ikiwa kama *Dajjal*, Mtume wa Uongo, anataka afaulu kujifanya Mtume wa ukweli, na aaminike, ni wazi kuwa inambidi ayatimize yote hayo yaliyoorodheshwa hapo juu.

Swali linaloibuka kufuatana na msimamo huu ni: Ikiwa *Dajjal*, Mtume wa Uongo, au *AntiChrist* anahusika katika udanganyifu huu mkubwa kupita kiasi wa Wayahudi, na mengine mengi, na kama amekwishaachiwa na tayari yumo duniani, je, yuko wapi? Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake)* alizungumza (katika hili linaloweza kutambulika kama ni mama wa 'mafumbo yote') kwa kusema yafuatayo kuhusu *Dajjal*, Mtume wa Uongo:

Amesikika al-Nawwas ibn Sam'an: …Tukasema: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu *(rehma na amani juu yake)*, je, ni muda gani atakuwa Duniani? Akajibu: Kwa siku arobaini, siku moja kama mwaka, siku moja kama mwezi, siku moja kama wiki na siku zilizobaki zitakuwa kama siku zenu...."

(Sahih, Muslim, Sunan, Tirmidhi)

Ni pale tu ambapo atakuwa yuko katika kumalizia maisha yake duniani, ndipo *siku za Dajjal itakuwa kama siku zetu.* Pili, *Dajjal*, Mtume wa Uongo, atakuwa kwenye 'eneo-upeo' (*dimension*) la wakati wetu pale ambapo '*siku yake' itakuwa kama 'siku yetu'.* Hivyo, atakuwa kwenye dunia 'yetu' mwishoni mwa maisha yake wakati atakapoingia kwenye dunia 'yetu' ili kukamilisha zoezi lake la kuchukua kilaghai nafasi ya Masihi. Ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kuwa Masihi atatawala dunia kutokea kwenye kiti cha enzi cha David *(rehma na amani juu yake),* ikimaanisha Jerusalem ambayo itakuwa ni katikati ya Nchi ya Israeli. Hivyo ni wazi kuwa Dajjal atakuwa yupo Jerusalem kimaumbile mwishoni mwa maisha yake, na wakati huo ambapo '*siku yake' itakuwa kama 'siku yetu'* itawezekana kwetu sisi kumuona kwa macho. Wakati huo tutamuona kama Myahudi, kijana, mwenye umbo shupavu akiwa na nywele zilizopinda panda n.k. Pia itambidi awe Mtawala wa dunia atakayetawala kutokea Jerusalem. Hili ndilo jibu la swali linalohusu mpango maalum na umuhimu wa Jerusalem katika mwisho wa historia.

Kabla ya hapo, atakuwa yuko nasi kama vile ambavyo malaika na majini walivyo nasi na ilhali hawamo katika dunia 'yetu' u 'eneo-upeo' letu (katika siku kama siku yetu) na hivyo hawaonekani. Atakuwa siku zote anatushambulia ili kuijaribu imani yetu. Atakuwa akitandika wavu wa mtandao wake wa udanganyifu, lakini hatutoweza kumuona yeye kwa kutumia nyenzo zetu za kawaida kwa kuwa '*siku yake' si sawa na 'siku yetu'*. Je, ni wapi *duniani Dajjal* atakuwa pale ambapo ataachiwa na Mwenyezi Mungu katika *siku kama mwaka* na baadaye katika *siku kama mwezi* na kisha katika *siku kama wiki*? Tunajua kuwa atakuwa duniani, lakini je, ni wapi hapa duniani?

Kwa bahati njema, tunalo jibu la swali la kwanza, na jibu hilo, litafungua uwezekano wa kutafuta na kupata majibu ya maswali mawili yaliyobaki. Jibu la swali la kwanza linapatikana katika *Hadithi* inayojulikana kama *Hadithi* ya Tamim al-Dari. Tamim al-Dari alikuwa ni Mkristo ambaye alisilimu na kuwa *Muislamu* Madina. Siku moja alikuja kwa Mtume *(rehma na amani juu yake)* na kumsimulia jambo lililomtokea linalomhusu *Dajjal*. Hakuna uhakika kama hii ilikuwa ni ndoto, au njozi au ni tendo lililomtokea maishani mwake. Mtume *(rehma na amani juu yake)* aliwasihi waumini wabaki msikitini baada ya sala ili aweze kuwasimulia kile ambacho Tamim kimemtokea kuhus *Dajjal.* Akawaelezea kuwa

kile ambacho Tamim al-Dari amemsimulia, kinathibitisha yale ambayo yeye Mtume *(rehma na amani juu yake)*, amekuwa akiwaambia kuhusu *Dajjal*. Hii ndiyo Hadithi yenyewe:

"Amesimulia Fatimah bint Qays, dada yake ad-Dahhak ibn Qays:
Amir ibn Sharahil ash-Sha'bi alisema: Fatimah bint Qays alikuwa miongoni mwa wanawake wa mwanzo katika kuhama. Nikamuuliza anisimulie mimi Hadithi ambayo aliisikia moja kwa moja kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu *(rehma na amani juu yake)* na palikuwa hapana kiunganisho chochote cha ziada baina yao. Akasema: Vizuri sana, kama unataka, niko tayari kufanya hivyo. Akamwambia: Sawa, nisimulie. Akasema: Niliolewa na mtoto wa Mughirah na alikuwa kijana mteule wa ki-Quraysh wa wakati ule, lakini alikufa kama shaheed katika vita vya kwanza vya Jihad (ktk kupigania upande wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu *(rehma na amani juu yake).* Nilipobaki mjane Abdurrahman ibn Awf, mmoja kati ya maswahaba wa Mtume, alinitumia posa na kutaka kunioa. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu *(rehma na amani juu yake)* pia akanitumia posa kwa ajili ya mtumwa wake aliyemwachia, Usama ibn Zayd. Zilifika kwangu habari kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu *(rehma na amani juu yake)* alisema: Yeyote anayenipenda mimi, inambidi pia ampende Usama. Wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu *(rehma na amani juu yake)* alipoongea nami (kuhusu jambo hili), nilisema: Maswala yangu yako mikononi mwako. Unaweza kuniozesha kwa yoyote utakayemchagua. Akasema: Ni vizuri uhame uende kwenye nyumba ya Umm Sharik. Umm Sharik alikuwa ni mwanamke tajiri miongoni mwa Ansar. Alikuwa akitumia mali yake bila kusita katika kupigania jina la Allah na alikuwa mkarimu sana kwa wageni. Nikamwambia: Sawa, nitafanya kama utakavyo. (Lakini mara) yeye (akabadilisha mawazo juu ya hilo) akasema: Usifanye hivyo kwa sababu Umm Sharik ni mwanamke ambaye mara nyingi anatembelewa na wageni na nisingependa kichwa chako kiwe wazi au uwe umeondoa kizuizi na wageni wasijekuona yale mbayo wewe utachukia wakiyaona. Nivyema uende kweny nyumba ya binamu yako, Abdullah ibn Amr ibn Umm maktum. Alikuwa ni mmoja wa Banu Fihr, tawi la Quraysh, na alikuwa ni kabila lake (la Fatimah). Hivyo nikahamia kwenye nyumba hiyo, na muda wangu wa kusubiri ulipotimia, nikamsikia sauti ya muezzin akitangaza kuwa sala itakuwa kwenye msikiti (ambapo) sala ya jamaa hufanyika. Hivyo nikaenda msikitini na nikasali pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu *(rehma na amani juu yake)* na nikawa kwenye safu ya wanawake iliyo karibu na safu ya wanaume. Wakati Mjumbe wa Mwenyezi Mungu *(rehma na amani juu yake)* alipomaliza sala yake, akakaa kwenye mimbari, akatabasamu na kusema: kila muumini abaki kwenye nafasi yake. Kisha akasema: Je, mnajua kwanini nimewaomba mkusanyike? Wakasema: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu *(rehma na amani juu yake)* ndiye anayejua vyema. Akasema: Naapa kwa Allah, sikuwaita kwa ajili ya kuwapa mawaidha wala kuwasihi / kuwaonya. Nimewakusanya hapa kwa sababu Tamim Dari, Mkristo ambaye amesilimu na ameukubali Uislamu, ameniambia jambo ambalo linakubakubaliana nay ale niliyokuwa nikiwaambia kuhusu Dajjal. Ameniambia kuwa alikuwa anasafiri kwa meli na watu thelathini wa Banu Lakhm na Banu Judham na wakapigwa na mawimbi baharini kwa mwezi mzima. Kisha mawimbi yakawafikisha karibu na ardhi iliyo katika bahari (kisiwa) muda wa jua kuzama. Wakaingia kwenye boti dogo wakaelekea kwenye hicho kisiwa. Pakawa na mnyama mwenye manyoya mengi (kiasi kwamba) hawakuweza kujua kichwa wala mkia uko upande upi. Wakasema: Ni nani wewe? Akawajibu: Mimi ni al-Jassasah. Wakasema: Jassasah ni nini? Akawajibu: Enyi watu, nendeni katika monastery kuna mtu ana hamu sana anataka kuonana nanyi. Yeye (msemaji) alisema: Alipomtaja huyo mtu tuliogopa isije ikawa ni Shetani. Kisha tukaharakisha kwenda kwenye monastery na tukamkuta mtu mwenye umbo shupavu huku mikono yak ikiwa imefungwa shingoni na minyororo ya chuma imefungwa miguu yake kwenye mafundo ya miguu. Tukasema: Je, wewe ni nani? Akajibu: Mtanifahamu muda si mrefu, niambieni ninyi ni nani? Tukajibu: Sisi ni watu kutoka uarabuni, na tulifanya safari kwa boti ila mawimbi yakatuchukua kwa muda wa mwezi mzima na yakatuleta karibu na kisiwa hiki. Tukachukua maboti madogo tukafika hapa. Hapo mnyama mwenye manyoya mengi sana akatulaki, na hatukuweza kutambua kichwa wala mkia uko upande gani. Tukamwambia: Je, wewe ni nani? Akajibu: Mimi ni al-Jassasah. Tukamwuliza: al-Jassasah ni nini? Akajibu: Kuna mtu katika monastery ana hamu kubwa kutaka kuwaona, nendeni pale. Ndipo tukaja kwa haraka tukiwa na hofu kuwa labda inaweza kuwa ni Shetani. Yeye (aliyefungwa minyororo) akasema: Niambieni kuhusu mitende ya Baysan. Tukasema: Unataka habari gani kuhusu hiyo mitende? Akasema: Nawauliza kama mitende hiyo inazaa matunda au la? Tukasema: ndiyo. Hapo akasema: nadikiri kuwa hiyo haitozaa matunda.

Akasema: Nipeni habari juu ya ziwa Tabariyyah? Tukasema: Unataka habari gani kuhusu ziwa Tabariyyah? Akasema: Bado lina maji? Wakasema: limejaa maji mengi sana. Hapo akasema: Nadhani muda si mrefu litakauka. Kisha akasema: Nipeni habari za chemchem ya Zughar. Wakasema: Unataka habari gani kuhusu chemchem ya Zughar? Yeye (aliyefungwa minyororo) akasema: Je ina maji na yanatumika kumwagia mashamba? Tukasema: ndiyo, ina maji mengi sana na wakazi (wa Madina) wanayatumia kumwagilia mashamba yao. Akasema: Nipeni habari za Mtume asiyejua kusoma na kuandika, amefanya nini? Tukasema: Ameondoka Makka na amehamia Yathrib (Madina). Akasema: Je, Waarabu wanapigana naye? Tukasema: Ndiyo. Akasema: Je, jinsi gani anajibu mashambulizi yao? Tukasema: Amewashinda wale ambao walikuwa majirani kwake na wamejisalimisha kwake. Hapo akatuambia: kama ndivyo, ni vizuri kwao wakimtii na kumsikiliza. Sasa nitawaeleza habari zinazonihusu mimi. Mimi ni Dajjal na punde nitaruhusiwa kuondoka. Hapo nitaondoka na kuzunguka ardhini na sitoacha kuingia miji yote ambapo sitofika katika siku arobaini isipokuwa Makka na Tauba (Madina). Hizi mbili (sehemu) nimezuiliwa na sitojaribu kuingia. Malaika mwenye upanga mkononi atanikabili mimi na kuzuia njia yangu na malaika watalinda kila njia inayoelekea huko. Ndipo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu *(rehma na amani juu yake)* alipopiga kwa mwisho wa fimbo yake juu ya dawati la mimbari akasema: Hii inaonyesha Tayba ikimaanisha Madina. Je, sikuwasimulia habari (za Dajjal) kama hivi? Watu wakasema: Ndiyo, na hii habari ilivyosimuliwa na Tamim Dari niliipenda kwani inakubalina na habari niliyowapa kuhusu (Dajjal0 Madina na Makka. Angalieni yeye (Dajjal) yuko katika bahari ya Syria (Mediterranean) au bahari ya Yemen (bahari ya Arabia). Hapana, kinyume chake, yuko mashariki, yuko mashariki, yuko mashariki na akanyoosha kidole chake kuelekea mashariki. Mimi (Fatimah bint Qays) nikasema: Nikayahifadhi katika kumbukumbu yangu (masimulizi haya ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu *(rehma na amani juu yake)*

Sahih Muslim

Ni wazi kutokana na *Hadithi* hii kuwa wakati *Dajjal* alipofunguliwa kuingia duniani alikuwa katika kisiwa hicho kijiografia, na itakuwa kutokea kwenye kisiwa hicho ndipo atakapoanza jitihada zake za kutaka kujifanya au kuchukua kiulaghai nafasi ya Masihi kwa kuikomboa Ardhi Takatifu kutoka kwenye utawala wa wasio-wayahudi n.k. Je, ni kisiwa gani hicho?

Kisiwa ni Uingereza

Kwa mtazamo wetu kisiwa kinachozungumziwa kwenye *Hadithi* hiyo ni Uingereza. Ushahidi unaothibitisha madai yetu ni wa kushtusha. Hebu tafakuri yafuatayo. Mnamo mwaka 1917 serikali ya 'visiwa' vya Uingereza ilitangaza Azimio la Balfour ambamo ilitangaza na kuushtusha ulimwengu mzima kuwa Serikali ya Uingereza inadhamiria kuunga mkono kuanzishwa kwa Makazi ya Taifa la Wayahudi katika Ardhi Takatifu. Kisha mwaka 1917 – 1918 lilikuwa ni jeshi la Kiingereza chini ya uongozi wa Jenerali Allenby lililoliangusha jeshi la Kituruki na kuikomboa Ardhi Takatifu hivyo kuikomboa kutoka kwenye utawala wa Kiislamu. Kutoka 1919 hadi 1948 Uingereza ilitawala Ardhi Takatifu ikiwa kwa misingi ya Ruksa ya Baraza la Mataifa (League of Nations). Wakati huo, dunia ilishuhudia uhamiaji mkubwa sana wa Wayahudi wa Ulaya kuhamia kwenye Ardhi Takatifu.

Chuki kubwa sana ya Wajerumani dhidi ya Wayahudi kwa kuwasaliti katika vita kuu ya kwanza ya dunia (Wayahudi wa Kijerumani walikuwa na makubaliano ya siri na Uingereza ambayo kwayo wangeisababisha Marekani iingie vita kwa upande wa Uingereza, ikiwa Uingereza, kama malipo, itaahidi kuwasaidia kuwapa Ardhi Takatifu baada ya kushinda vita) na ushindi wa Hitler ukasababisha kushutumiwa na kusakamwa kiujumla kwa Wayahudi kukasababisha kuongezeka kwa kiasi kikubwa sana kukimbia na kuhamia kwa Wayahudi

katika Ardhi Takatifu wakitokea Ulaya. Mwishowe, mwaka 1948 Uingereza ilikuwa mithili ya 'mkunga' kwa mtoto kuzaliwa, ikim. kutamkwa rasmi kuwa taifa la Israeli limepata uhuru. Tungependa kupigia mstari chini ya ukweli kuwa, kisiwa cha Uingereza kipo baada ya kuvuka bahari ya Mediterranean, takriban safari ya mwezi mmoja kutoka Uarabuni! Pia ni muhimu kugundua kuwa Waingereza ni mashuhuri katika uwanja wa ujasusi. Sherlock Holmes na James Bond ni hadithi za kubuni zilizo sawa na kulingana na Lawence wa Arabia.

Inawezekana kuwa watakuwapo wale ambao bado hawatokubaliana na mtazamo wetu ambamo tumekitambua kisiwa cha Uingereza kuwa ndicho kinachotajwa katika *Hadithi.* Watu hao tunawaambia, kwa wingi wa heshima, na kuwakaribisha ili kwa unyenyekevu watusahihishe. Na ili wafanye hivyo, inawapasa, wao wenyewe watutambulishe kisiwa na watoe ushahidi ambao utathibitisha madai yao au chaguo lao litakalovunja pendekezo letu.

Kisha tukagundua kuwa palikuwa na kipindi hapo nyuma, ambapo katika namna isiyokuwa ya kawaida na kiajabu, Uingereza ilisita kuwa 'Taifa Tawala' katika dunia na nafasi yake ikachukuliwa na Marekani (USA). Tokeo hili la mabadiliko lilionekana kuanza kutokea ikiwa ni matokeo ya vita moja, ikim. Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, na kukamilika na vita nyingine, ikim. Vita Kuu ya pili ya Dunia. Mtazamo na msimamo wetu ni kuwa kipindi kati ya vita hizo mbili kuu za dunia kumeshuhudia kuhama kwa *Dajjal* kutoka *siku kama mwaka* kwenda kwenye *siku kama mwezi*.

Kitendo cha kigaidi katika kiangazi cha mwaka 1914 katika mji wa Sarayevo kilisababisha kuuawa kwa Arch Duke Franz Ferdinand wa Austria-Hungary. Mtuhumiwa alikuwa ni Mserbia, lakini alama za ushahidi zilizoachwa zilielekeza kufikirika kuwa Urusi imehusika. Yeyote aliyepanga mauaji hayo, na aliyepandikiza ushahidi huo ulioelekeza Urusi, alitaka Austria-Hungary iitangazie vita Urusi. Lengo halisi la mauaji halikuwa Urusi, bali swahiba wa Urusi, kwa jina Uingereza. Lengo la pili lilikuwa ni Taifa la Kiislamu la Ottoman. Taifa hilo la Kiislamu la Ottoman, lilikusudiwa livunjwe na Uingereza ndiye ingekuwa mvunjaji. Punde tu Austria-hungary ilipoitangazia vita Urusi, Uingereza na Ufaransa mara moja waliingia vitani kwa upande wa Urusi. Na Ujerumani ikaingia vitani kwa upande wa Austria-Hungary. Mpango huo maalum wa mauaji ni kutaka kuuangusha uchumi wa Uingereza kwa kuiingiza Uingereza kwenye vita hivyo kusababisha kupoteza nafasi yake ya *Taifa Tawala* na kufungua mlango wa Taifa jingine kuchukua nafasi hiyo. Watendaji wa tendo hilo la kigaidi walikuwa na mpango wa siri uliopangwa kwa ujanja wa hali ya juu na kishetani kiasi kwamba pamoja na hayo yote waliweza pia kuuvamia utawala wa Ufalme wa Kiislamu wa Ottoman. Utawala huo ulikuwa ni kikwazo kikubwa katika kuikomboa Ardhi Takatifu, na kulifufua Taifa la Israeli. Njia nzuri kuliko zote ya kukiondoa kikwazo hicho ilikuwa ni vita. Hivyo Ufalme wa Kiislamu wa Ottoman ulilazimika, kwa njia ya kiujanja wa ndani kwa ndani, kuingia kwenye vita kwa upande wa Ujerumani. Uingereza ikatumika sit u kwa kuupiga na kuuvunja Ufalme wa Kiislamu wa Ottoman, bali pia Ukhalifa wa Kiislamu. (Tazama kitabu chetu: "*Ukhalifa Hejaz na Nchi-Taifa la Wahhabi wa Saudia".)*

Lakini kuanzia mwaka 1914 hadi 1916 vita ilikuwa ni janga kwa Uingereza. Kwanza manowari za Ujerumani zikanyakua na kudhibiti mapigano ya baharini kutoka kwenye himaya ya Waingereza. Pili, Ujerumani, ikachukua Ufaransa na kuweka Serikali

iliyofungamana na Ujerumani kutawala Ufaransa. Tatu, majeshi ya Kirusi yalikuwa yakikimbia vita na kurudi nyuma. Na mwisho, hadi kufikia mwaka 1916, Uingereza ilifikia hali mbaya kiuchumi kiasi kwamba kulitokea tishio la njaa. Ndipo lilipotokea badiliko la nguvu mnamo mwaka 1916. Wayahudi waliikabili Serikali ya Kiingereza na kuipa ahadi kuwa wangeweza kusababisha kuiingiza Marekani vitani kwa upande wa Uingereza, ili kuisaidia, ikiwa kama Uingereza, *nipe nikupe* (*quid pro quo*), itaahidi kuwapa Wayahudi Ardhi Takatifu baada ya vita kwisha. Waingereza walilikubali wazo hilo. Wayahudi ndipo walipofungua mashine yao ya propaganda Marekani na kufanya kila waliloweza hadi kufanikiwa kuiingiza Marekani kwenye vita mwaka huo huo kuisaidia Uingereza. Mwaka mmoja baadaye, Waingereza walitoa tamko la Azimio la Balfour. Mwaka huo huo ulishuhudia kumalizika kwa ushindi na ufanisi mkubwa shughuli za majasusi wa Kiingereza katika Ghuba ya Kiarabu.

Waingereza walifanikiwa kukamilisha mambo mawili muhimu, na yote yaliupelekea kipigo kikubwa Ufalme wa Kiislamu wa Ottoman. Jambo la kwanza ni kupatikana kwa Mkataba wa Makubaliano ya Kupeana Msaada na Kutofungamana (na adui wa mwenzio) kati ya Uingereza na ‘Abdul ‘Aziz Ibn Saud (aliyekuwa akitawala Riyadh). Gharama yake ilikuwa ni ndogo sana kwa Waingereza, kiasi cha paundi za Kiingereza 5000 kwa mwezi, ambazo Abdul Aziz angepata kutoka katika Hazina ya Waingereza. La pili lilikuwa ni kufanikiwa kumfanya *Sharifu* Husain, aliyeteuliwa na Ufalme wa Ottoman kama *Sharifu* wa Makka na *Hejaz*, amuasi Khalifa wa Ottomanna kujitangazia uhuru. Gharama kwa Uingereza ilikuwa ni paundi Sterling milioni 7 (Angalia kitabu chetu: *Ukhalifa Hejaz na Nchi-Taifa la Wahhabi wa Saudi.”)*

Hivyo mwaka 1916 ulibadilisha mwelekeo wa vita na mwishowe uliwapatia ushindi Marekani, Uingereza na Wayahudi. Siyo Ujerumani tu peke yake ilishindwa vita hivyo, bali pia Ufalme wa Kiislamu wa Ottoman uliparaganywa na nafasi yake ikazaliwa Taifa (lenye mfumo wa kidunia) la Uturuki. Viongozi wake mara moja waliwekeana *mkataba wa ulinzi na ushambulizi* na hiyo hiyo Uingereza ambayo ilikuwa imefanya jitihada kubwa katika kuuangusha Ufalme wa Kiislamu wa Ottoman. Hata hivyo Uingereza ilikuwa imeathiriw sana na vita hivyo kiasi kuwa Marekani ikachukua nafasi ya *Taifa Tawala* la dunia. Hili lilithibitishwa katika kipindi kilichopita kati ya vita hizo mbili za dunia, na haswa baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Kwa mfano, wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia ni jenerali wa Kimarekani, Dwight Eisenhower ndiye aliyekuwa kiongozi wa majeshi ya Muungano. Kisha mwaka 1944 Mkutano wa Bretton Woods uliopelekea kupitishwa kwa Makubaliano ya Mfumo mpya wa Fedha wa Kimataifa uliashiria kushuka kwa daraja la Uingereza pale ambapo Dola ya Kimarekani iliteuliwa kuwa ni sarafu ya Kimataifa badala ya paundi ya Kiingereza. Shirikisho la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia zikachukua nafasi ya Benki Kuu ya Uingereza kama ni vyombo viongozi vya masuala yote ya kifedha duniani. Na Washington ikachukua nafasi ya London kama mji mkuu wa masuala hayo, hivyo kudhibiti masuala yote ya fedha duniani. Baada ya vita, ilikuwa ni Marekani iliyochukua jukumu la kuyajenga upya mataifa yaliyoathirika kwa vita ya Ulaya, ikiwemo Uingereza, kwa kupitia Mpangowa Marshall. Mnamo mwaka 1956, wakati wa tatizo la Suez na baadaye wakati wa

matatizo ya makombora ya Cuba ya mwaka 1963, Marekani bila ya shaka iliithibitishia dunia nzima nafasi yake ya kuwa *Taifa Tawala*.

Katika namna ile ile ambapo Uingereza ilionekana kuwa imepagawa na Ardhi Takatifu (mfano, Azimio la Balfour) na Waingereza wenyewe hawakuweza kuelezea kupagawa huko kwa ajabu, ndivyo hivyo ilikuwa kwa *Taifa* hili jipya *Tawala*, kiajabu limepagawa kwenye mambo yote yanayoihusu Ardhi Takatifu, na Wamarekani wenyewe hawawezi kutoa maelezo ya kupagawa huku. Kwa mfano, Marekani ilikuwa ni nchi ya kwanza duniani 'kuitambua' Israeli ilipotangaza uhuru wake mwaka 1948. Kuanzia hapo, Marekani imekuwa ikiibeba Israeli 'kwa hali na mali'! Marekani inaipa Israeli kiasi kikubwa sana cha missada ya kipesa, kiuchumi, na ya kijeshi. Ukweli ni kuwa msaada ambao Marekani inaipa Israeli, unazidi misaada yote inayotoa kwa nchi zote zilizobaki duniani! Baadhi ya misaada ya Marekani kwa Israeli inepelekwa kwa kupitia Serikalini, lakini pia kuna misaada inayokwenda Israeli kupitia Wayahudi ambao wanaishi Marekani. Baadhi ya misaada ya kijeshi inapelekwa kihalali kupitia 'mlango wa mbele', lakini ipo misaada inayopelekwa kupitia 'mlango wa nyuma' (tukio la Jonathan Pollard, aliyepeleka Israeli, siri za silaha za nyuklia za Marekani, ni moja tu ya matukio yanayojulikana sana). Matokeo yake ni kuwa Israeli imekuwa inahodhi silaha za nyuklia na thermo-nyuklia sawa sawa na nchi nyingine zenye silaha hizo duniani.

Uhusiano wa kiajabu, usio wa kawaida, usioelezeka baina ya Marekani na Israeli ulijionyesha tena kwa nguvu kabla tu ya shambulizi la mwezi Septemba tarehe 11, Marekani. Mkutano wa Dunia juu ya Ubaguzi wa Rangi uliishutumu Israeli kwa ugandamizaji wake wa Wapalestina. Israeli ilijibu shutuma hizo kwa kutoka kwa ujumbe wa Israeli nje ya ukumbi wa mkutano huo. Ni nchi moja tu iliyojumuika nayo (Israeli) katika kuunga mkono kitendo hicho cha kutoka nje ya mkutano. Nayo, wajumbe wake wakatoka nje! Nchi hiyo ilikuwa Marekani!

Kutokana na hayo yote, tunafikia uamuzi kuwa *Dajjal*, kijiografia yuko Marekani katika kipindi chake cha maisha duniani akiwa katika awamu ya '*siku yake (moja) kama mwezi*'. Tunaendela kuweka wazi katika kitabu hiki kuwa hivi sasa tuko katika kile kipindi ambacho Dajjal yuko tayari kuhama na kuingia kwenye awamu ya maisha yake hapa duniani '*siku yake (moja) kama wiki*', ambako tutashuhudia Israeli kuchukua nafasi ya Marekani na kuwa *Taifa Tawala* duniani. Na kwa hakika tumegundua kuwa shambulizi la Septemba 11 marekani lilikuwa ni sura ya kwanza katika sakata ambamo mabadiliko hayo ya Taifa Tawala yanapangwa kupitia (*Tazama kiambatanisho 2 – Jibu la Kiislamu kwa shambulio la Marekani')*

Kwa uzito wa ukweli kuwa *Qur'ani* imejitamkia kuwa 'inaelezea mambo yote' (*Qur'ani, al-Nahl, 16:89*), ina uwezo wa kuelezea hili jambo la kustaajabisha ambalo halijawahi kutokea katika historia yote ya kidini ya binaadmu, ikim. kufufuliwa kwa Taifa la Israeli katika Ardhi Takatifu, takriban miaka 2000 baada ya kuvunjwa na Allah, Mtukufu.

Lengo letu katika kurudi kwenye *Qur'ani* na kupata maelezo hayo ni kuelekeza macho, fikra na ufahamu kwenye mwongozo wa kiroho ambao ungewasaidia Waislamu kote

duniani kuwa na majibu sahihi kwenye matukio ya ajabu yanayojitokeza katika Ardhi Takatifu.

Kabla hatujarudi kwenye kuuchunguza huu utabiri usio wa kawaida mabao tayari umekwishatimia, ikim. Mwenyezi Mungu, Allah, Mtukufu, atawarudisha Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu wakati wa ‘Zama za Mwisho’, ni muhimu kwetu kulizungumzia suala la Mirza Ghulam Ahmad, ambaye ni mdanganyifu wa hali ya juu kabisa duniani ambaye hajawahi kutokea kabla yake aliyejaribu kujihusisha na utabiri wa kurejea kwa Masihi.

Sura ya 9

MIRZA GHULAM AHMAD: MTUME WA UONGO

Imepatikana kwa Abu Huraira: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alisema: "Kwa Yule Ambaye roho yangu iko Mikononi Mwake, kwa hakika (Yesu), mwana wa Maryamu punde atashuka na kuwa miongoni mwenu na atahukumu walimwengu kwa haki (kama mtawala wa haki), atauvunja msalaba na atawaua nguruwe na hapatokuwa na Jizyah. Pesa zitakuwa nyingi kiasi hakuna atakayekubali kuzipokea, na kumsujudia mara moja Mwenyezi Mungu (kwa sala) kutakuwa bora kuliko chochote kilichokuwa duniani." Abu Huraira akaongeza, "Na kama ukitaka, unaweza kusoma (aya hii ya Kitabu Kitakatifu):

"Na hawi katika Watu wa Kitabu ila hakika atamuamini yeye kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao." (Qur'ani, al-Nisa, 4:159)

(Sahih Bukhari)

Mirza Ghulam Ahmad alikuwa ni Muislamu wa Kipanjabi aliyekuwa akiishi katika mji wa Qadian, india mwanzoni mwa karne ya ishirini. Alifariki takriban wakati inaanza Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia. Hakuishi kuweza kuona kuhama kwa dola kutoka *Taifa Tawala* moja (Uingereza) kwenda kwa la pili (Marekani) kulikotokea wakati wa vita hiyo. Pia hakuishi na kuweza kuona kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu na kuundwa kwa Taifa la Israeli mwaka 1948. Pia hakuishi na kuweza kuona kile ambacho punde tu tutaweza kuwa mashahidi wake, ikim., kuhama kwa dola kutoka Marekani kwenda kwenye *Taifa Tawala* jingine – Nchi ya Kiyahudi ya Israeli. Kitabu hiki kinatarajia kutokea kwa hilo katika miaka mitano hadi kumi ijayo, au pengine mapema zaidi ya hapo.

Mirza aliushtusha ulimwengu pale alipotangaza madai kadhaa yanayohusu utabiri wa kurejea kwa Masihi. Akaanzisha Shirikisho la Ahmadiyyah nchini India na mara likaanza juhudi za nguvu kubwa kuwabadilisha watu wa Ulaya kuwaingiza kwenye Ahmadiyyah. Shirikisho hilo pia lilifanya jitihada maalum kuelekea kwa Waislamu wa Kimarekani weusi wa Taifa la Kiislamu waliokuwa wakiongozwa na Elijah Muhammad. Matokeo yake, Mirza alifanikiwa kuwaghilibu Waislamu wa Marekani wenye asili ya Kiafrika ambao leo hii wanaongozwa na *Imam* Warithuddin Muhammad au Louis Farakhan, kuhusu suala la kurudi kwa Masihi. Kwa sababu hizo, imekuwa muhimu kwetu kutenga sura ya kitabu hiki kuzungumzia madai ya Mirza.

Kadiri mtiririko wa historia unavyofuata mkondo wake katika Zama hizi za Mwisho, inabidi iwe wazi kwa wafuasi wake na pia kwa wale ambao walifuata mafundisho yake kuwa madai yafuatayo ya Mirza yalikuwa siyo sahihi na kwa ufupi yalikuwa ya uongo:

- Kuwa yeye ni *Imam-al-Mahdi* ambaye atakuwa kiongozi wa Waislamu wakati ambapo Masihi atarejea,

- Utabiri wa kurejea kwa Masihi ulitimia kwake yeye

- Yeye ni Mtume teule anayetokana na njia ya Utume wa Muhammad (*rehma na amani juu yake*)

Tuna matumaini kuwa Ahmadiyyah watapokea mwaliko wetu, ambao hapa tunauwakilisha kwao, kuitumia *Qur'an*i na *Hadithi* kuelezea matukio ambayo yametokea baada ya kifo cha Mirza (niliyoyataja hapo juu) na hasa kurejea kwa Wayahudi katika Ardhi Takatifu na kuundwa kwa Taifa la Israeli. Ikiwa watafanya hivyo, tuna hakika watagundua na kuyaelewa upya masomo la *Dajjal*, Mtume wa Uongo, Y'ajuj na M'ajuj, *Imam-al-Mahdi* na kurejea kwa Masihi (Yesu, Mwana wa Maryamu) – ambao utakuwa ni uelewa mpya wa aina yake tofauti kabisa na walivyopokea kutoka kwa Mirza Ghulam Ahmad.

Kitabu hiki kimeandikwa kuwasaidia wa-Ahmadiyyah wakiwa wanafanya jitihada za kuuelewa mtazamo wa *Qur'ani* unavyoelezea kitendo cha ajabu kabisa katika matukio yote ya kidini ya binaadamu, ikim., kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu. Si rahisi kwa mfuasi wa Ahmadiyyah kuelewa na kukubali sababu za msingi zinazowakilishwa kwenye kitabu hiki na hapo hapo kuendelea kukubali madai ya Mirza Ghulam Ahmad kuwa ni Masihi ambaye siku moja atarejea, *Imam-al-Mahdi* na kasha kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu. *Na Mwenyezi Mungu humuongoza kwenye mwanga Wake yeyoye ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumuongoza.*

Wayahudi si watu pekee ambao wamedanganywa na *Dajjal*. Waislamu safi wengi, ambao wanaonyesha utiifu wa hali ya juu kabisa wa kushangaza katika kuitafuta imani, pia walidanganywa. Kwa uaminifu wakaingia kwenye Shirikisho la Ahmadiyyah na wakaamini kuwa wamejiunga na imani pekee ya kikweli inayowakilisha *Uislamu* duniani. Badala yake, wameingia kwenye mtego uliotegwa na *Dajjal*. Je, ni vipi walidanganywa?

Shirikisho la Ahmadiyyah linaamini kuwa utabiri unaohusu kurejea kwa Masihi umetimia kwa kuja kwa Mirza Ghulam Ahmad. Kuna sbabu kadhaa kwanini madai haya si ya kweli. Kwanza, *Hadithi* inayozungumzia 'kurejea kwa Masihi' inaonyesha wazi kabisa bila kuficha kuwa Masihi anayetarajiwa kurejea atakuwa ni 'mwana wa Maryamu'. Tatizo, Mirza Ghulam Ahmad ni mwana wa mwanamke wa

Kipunjabi. Pili, Ikiwa Mirza ni kweli anawakilisha kutimia kwa kurejea kwa Masihi, basi yeye, Mirza, angemuua *Dajjal*, Mtume wa Uongo, katika maisha yake kama Masihi ikiwa ni moja ya vitu anavyotarajiwa kuvifanya. Ufuatao ni usemi wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) juu ya suala hilo. Tunainukuu *Hadithi* nzima kwa manufaa ya wasomaji:

Imepokelewa kutoka kwa al-Nawwas ibn Sam'an:

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*) alimtaja Dajjal siku moja asubuhi. Mara nyingine alimzungumzia kama hana umuhimu na mara nyingine aliyazungumzia (matatizo yake) kama ni muhimu sana (na tukahisi) kama vile yuko kama matawi ya mnazi. Tulipokwenda kwake (kwa Mtume) jioni na akaona (ishara za wasiwasi) nyusoni mwetu, akasema: Mna tatizo gani? Tukasema: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*) ulimtaja *Dajjal* leo asubuhi (wakati mwingine ukimzungumzia) kama hana umuhimu sana na wakati mwingine kuwa ni muhimu sana, hadi tufikia kufikiria kuwa kajificha kwenye matawi (ya karibu) ya minazi. Ndipo akasema: Nina wasiwasi juu yenu kwa mambo mengi mengine ukiacha *Dajjal*. Ikiwa atakuja wakati ningali niko nanyi, nitakabiliana naye kwa niaba yenu, lakini akija wakati sipo miongoni mwenu, kila mtu itambidi akabiliane naye kwa niaba yake mwenyewe na Allah atamlinda kila Mwislamu kwa niaba yangu (na kumlinda na athari zake). Naye (*Dajjal*) atakuwa ni kijana, mwenye nywele zilizosokoteka, na kipofu wa jicho moja. Namfananisha na Abd al-Uzza ibn Qatan. Yeyote atakayekuwa hai kumuona asome aya za mwanzo za sura al-kahf. Atajitokeza baina ya Syria na Iraq na atasambaza uharibifu kila mahali kulia na kushoto. Ewe mja wa Allah! Shikilia (njia ya Haki). Tukasema: Mjumbe wa Allah (*rehma na amani juu yake*), ni muda gani atakuwa Duniani? Akasema: Siku arobaini, siku moja kama mwaka, siku moja kama mwezi, siku moja kama wiki na siku zilizobaki zitakuwa kama siku zenu. Tukasema: Mjumbe wa Allah (*rehma na amani juu yake*), je sala ya siku moja itatosha kwa sala za siku kama mwaka mmoja? Hapo akasema: Hapana, lakini inabidi mkadirie muda (na kisha mfanye maombi kwa sala). Tukasema: Mjumbe wa Allah (*rehma na amani juu yake*) atakuwa anatembea Duniani kwa mwendo gani? Hapo akasema: Kama mawingu yakiendeshwa kwa upepo. Atakuja kwa watu na kuwakaribisha na kuwaingiza (kwenye dini ya uongo); watamuamini na kumfuata. Kisha atatoa amri kwa mawingu: na mvua itanyesha Ardhini na mazao yatastawi. Kisha jioni wanyama wao watarudi wakiwa wameshiba, wakiwa wamejaa maziwa na matumbo yao yamejitokeza kwa kuvimba kila upande. Kisha atakuja kwa watu wengine na kuwakaribisha. Lakini watamkataa, naye ataondoka, nao watakuwa na ukame na hakuna kitakachobaki kama utajiri. Kisha tatembea jangwani na kuliambia jangwa. Onyesha utajiri wako. Utajiri utajitokeza na kujikusanya mbele yake kama kundi la nyuki. Kasha atamwita mmoja akiwa katika ujana, atampiga kwa panga, na kumkata vipande viwili (na kuviweka vipande hivyo mbali mbali, kiasi umbali wa mpiga mshale na bango la lengo lake). Kisha atamuita (kijana Yule) na atakuja huku akicheka na uso wake ukimeremeta (umejaa furaha). Hapo ndipo Allah atamtuma masihi, mwana wa Maryamu. Atateremka kwenye mnara mweupe mashariki ya Damascus, akiwa amevaa shuka mbili zikiwa zimetiwa rangi ya *safarani isiyokoza* akiwa ameweka mikono yake kwenye mabawa ya Malaika wawili. Atakapokuwa akiinamisha kichwa chake, pataanguka matone ya jasho kutoka kichwani, na atakapokiinua, matone mithili ya lulu yatapukutika. Kila kafiri atakayepata harufu ya mwili wake atakufa na harufu yake itafika mbali kiasi cha upeo wa macho yake. **Kisha atamsaka yeye (Dajjal) hadi atakapomkamata katika lango la Ludd na kumuua**. Kisha watu ambao Allah atakuwa amewalinda watakuja kwa Yesu, mwana wa Maryamu, na atawfuta nyuso zao na kuwapa habari za daraja zao katika pepo. Itakuwa katika hali hiyo wakati Allah atakapomfunulia Yesu Masihi maneno haya: Nimewaleta kutoka miongoni mwa waja Wangu watu ambao hakuna atakayeweza kuwashinda, wapeleke watu hawa kwa usalama hadi Tur, kasha Allah atawaleta Ya'juj na Ma'juj na watateremka kutoka katika kila mlima. Wa mwanzo watapita katika ziwa Tiberias na kunywa maji yake. Wakati wa mwisho akiwa anapita, atasema: Hapa zamani palikuwa na maji. Yesu na watu wake watazungukwa hapo (wakiwa Tur, na watasakamwa sana) kiasi kichwa cha ng'ombe kitakuwa ghali kuliko dinari mia moja. Mjumbe wa Allah, Yesu mwana wa Maryamu (*rehma na amani juu yake*), na wafuasi wake watashuka ardhini na na

hawatokuta kipande cha ardhi kisichokuwa kimeoza na kuwa na harufu. Mjumbe wa Allah yesu mwana wa Maryamu (*rehma na amani juu yake*) ndipo atakapomuomba Allah ambaye atawaleta ndege wenye shingo ndefu mithili ya ngamia wa Bactriani na watawachukua na kuwatupa pale ambapo Allah atawajaalia. Kisha Allah ataleta mvua kubwa ambayo hakuna nyumba ya udongo (au hema) la ngozi ya ngamia litakaloweza kuikinga na litasafisha Dunia na iwe kama kioo. Kisha ardhi itaamrishwa itoe matunda yake na kurudisha rehema zake, na kutokana na hiyo yatastawi (matunda makubwa ya kokomanga) kiasi kwamba kundi la watu linaweza kula tunda moja na kushiba na kupata kivuli kwenye ganda lake, na ng'ombe mmoja wa maziwa atatoa maziwa mengi kutosheleza kunywa kundi la watu kwenye tamasha. Ngamia wa maziwa atatoa maziwa (mengi kutosha) kunywa kabila zima na kondoo wa maziwa atatoa maziwa mengi kutosheleza familia nzima kunywa. Wakati huo Allah atatuma upepo mpole na wa baridi utakaowaburudisha (waja wake) na wasikie raha hata kwenye kwapa zao. Atayachukua maisha ya kila Muislamu na kuwaacha wadhalimu peke yao ambao watakuwa wakifanya zina kama punda na Saa ya Mwisho itawakuta."

(Sahih Muslim)

Hadithi iko wazi. Yesu, Masihi wa Kweli, atamuua Dajjal, Mtume wa Uongo: "*Kisha atamsaka yeye (Dajjal) hadi atakapomkamata katika lango la Ludd na kumuua.*" Kama Mirza Ghulam Ahmad ni kweli anawakilisha kutimia kwa kurejea kwa Masihi kama ilivyo kwenye Hadithi, basi naye ingebidi awe amekwishamuua *Dajjal,* Mtume wa Uongo. Pasingekuwa na uwezekano, wa Dajjal, Mtume wa Uongo, kuendelea na kazi yake baada ya kifo cha Mirza. Wakati Mirza, alifariki mara baada ya kuzaliwa kwa Shirikisho la Kizayonisti, na hakuweza kuishi na kuona moja ya mafanikio makubwa kabisa ya *Dajjal,* kwa jina, kuzaliwa kwa Taifa la 'Kibeberu' la Israeli na kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu. Katika historia yote ya kidini, hakujawahi kutokea tukio la ajabu kulinganisha na hili likiwa ni la ushindi wa *Dajjal,* Mtume wa Uongo (angalia sura iliyopita).

Tatu, kuna ushahidi wa kutosha (unaoonekana na wale wanaoona kwa macho mawili) *kuwa bado tunaishi katika zama za Dajjal,* Mtume wa Uongo. Kuna mifano mingi kama ifuatavyo:

- *Shirk* (kumshirikisha Allah) ya kifalsafa katika mfumo wa kisasa wa kidunia wa *materialism* ambamo umetimia utabiri wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) ambaye alitamka kuwa *Dajjal* atajaribu kuwadanganya binaadamu ili wamuabudu yeye badala ya Allah. Kiini cha mashambulizi hayo ya mfumo huo yalijitokeza mwanzoni kwenye visiwa vya Uingereza. *Hadith*i ya Tamim Dari iliyomo kwenye *Sahih Muslim* ilionyesha wazi kuwa Dajjal atakapofunguliwa atakuwa katika kisiwa na kuanzia kisiwani hapo ndipo atakapoanza jitihada zake za kuwashambulia binaadamu na Wayahudi. Tumeonyesha wazi kwa ushahidi kuwa kisiwa hicho kisingeweza kuwa kingine chochcote zaidi ya kisiwa cha Uingereza.

- *Shirk* (kumshirikisha Allah) ya kifalsafa ya mfumo wa kisasa wa elimu ya elimu (*epistemolojia*) wa nchi za kimagharibi ambao unakataa kuwapo kwa na kupatikana kwa elimu kwa 'jicho la ndani la hisia za kiroho' ambapo kuna ushahidi wa wazi kwenye usemi wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) kuwa *Dajjal,* Mtume wa Uongo, anona 'kwa jicho moja' wakati 'Mola wako si mwenye jicho moja.' Elimu hii ya jicho moja ya *epistemolojia* ilikubalika kwenye mfumo wa kisasa wa mataifa ya magharibi na kasha ukahamishiwa kwenye mataifa yaliyobaki duniani kwa kupitia kwenye mfumo wao wa elimu ya kimagharibi. Kwa mara nyingine tena, ni Uingereza ndiyo iliyokuwa ikiongoza kwenye mashambulizi haya ya epistemolojia.

- *Shirk* (kumshirikisha Allah) ya kijumla ya kisiasa iliyosambaa duniani katika mfumo wa kisasa wa Mataifa (Jamhuri za kidunia) ambamo pia umetimiza utabiri wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) ambaye alitamka kuwa *Dajjal*, Mtume wa Uongo, atajaribu kuwadanganya binaadamu ili wamuabudu yeye badala ya kumuabudu Allah. Utamaduni wa kisasa wa kimagharibi umebuni mfumo wa Taifa la kidunia, ambamo Taifa linadai kuwa huru, utawala wa kitaifa ndiyo utawala unaopaswa kufuatwa na wote na wa mwisho, ukiwa juu ya tawala zote, na sheria zinazopitishwa kitaifa ndizo sheria kuu zinazopaswa kufuatwa, zikiwa juu ya sheria nyingine zozote zile. Hapo, Allah anaweza kutaja kuwa jambo fulani ni *Haramu*, lakini Taifa lialifanya jambo hilo kuwa *Halali*. Hii ni *Shirk* iliyo wazi, lakini jambo la kustaajbisha ni kuwa hata Waislamu wanakuwa wagumu kulielewa na kulitambua. Pia, ilikuwa ni Uingereza iliyoongoza katika mashambulizi haya. Dunia nzima hivi sasa imekumbatia utawala wa kidunia na Umoja wa Jumuiya ya Mataifa inayoongoza mfumo huo. Haya yote yalikuwa hayajatokea wakati Ghulam Mirza Ahmad alipokufa.

- Mfumuko wa maendeleo uliofuatana na mapinduzi ya kisayansi na teknolojia ambao umeiletea dunia usafiri wa anga na ule wa nje ya anga letu, simu na namna nyingine za kisasa za mawasiliano, n.k. umeweza kiulaghai kuchanganya yale ambayo bila shaka yana faida kubwa kwa binaadamu na yale ambayo yana hatari kubwa na athari nyingi kwa binaadamu. Sehemu ile ya mapinduzi ambayo bado haijatokea bado yana akiba ya matendo ya kiugunduzi wa kiajabu na ya kushangaza ambayo yatafanywa kwa lengo la kuwadanganya binaadamu ili kuwanasa kwenye mtego wa *Dajjal*. Ugunduzi huo unaofanyika kupitia mapinduzi ya kisayansi na teknolojia yana uhusiano wa moja kwa moja na *Dajjal* kwa ushahidi unaopatikana kwenye Hadithi isemayo, kwa mfano, *Dajjal* atasafiri kwa kumpanda punda ambaye atasafiri haraka mithili ya mawingu na ambaye atakuwa na masikio yaliyokuwa yamevutika (na kuwa marefu) kwa upana. Hii inaashiria ndege za kisasa za abiria na za kijeshi.

- Mwenyezi Mungu, Allah alimuumba binaadamu na kasha kuwataarifu malaika kuwa anadhamiria kumuweka duniani ili awe kama Khalifa (atakayejiendesha kwa niaba Yake, akiwa chini ya amri Zake) wake. Dola za Kiislamu za *Khilafah* (Ukhalifa) zilikuwa zikifanya na kutimiza hayo. Zilikuwa zikiutambua na kufuata bila kuongeza wala kupunguza Utawala, Uhuru na Sheria za Mwenyezi Mungu kuwa ndizo kikomo cha juu kabisa cha Utawala, Uhuru na Sheria zinazopaswa kufuatwa na binaadamu. Dola hizo za Kiislamu zilivunjwa na utamaduni wa kimagharibi baada ya kifo cha Mirza Ghulam Ahmad na badala yake kuundwa kwa Mataifa ya kisasa ya kidunia yanayojengwa kwa misingi ya *Shirk*. Mfumo wa Taifa hilo jipya la kisasa la kidunia ulikumbatiwa na Uturuki wakati ikiwa ni makao makuu ya *Khilafah*. Mfumo huo ukaendelea kuivamia ghuba ya Uarabuni, ikiwa ni kiini cha *Uislamu* kabla ya kuzimeza nchi zote zilizobaki za *Kiislamu* duniani, hivyo kuuingiza ulimwengu wote wa *Kiislamu* katika *Shirk*. Hii ilikuwa ni kazi ya *Dajjal*. Nayo ilitokea baada ya kifo cha Mirza.

- Uchumi wote wa dunia uliokumbwa na *Riba* ambao umetimiza pia utabiri wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) ambaye alitamka kuwa zama za *Dajjal*, Mtume wa Uongo, zitakuwa ni zama za kusambaa kwa *Riba* kwa kiasi kikubwa mno. Mtume (*rehma na amani juu yake*) pia alitabiri kuwa wakati utafika ambapo hutoweza

kumpata binaadamu hata mmoja ambaye hatokuwa akila *Riba* au kitokanacho na *Riba*, na kuwa hata akitokea atakayedai kuwa hali *Riba* au kitokanacho na *Riba*, "kwa hakika vumbi la *Riba* litakuwa limempata". Utabiri huo, hivi sasa umekamilika. *Riba* hivi sasa imekamata uchumi wote duniani. Lakini *Riba* ilikuwa haijaukamata uchumi wa dunia wakati Mirza Ghulam Ahmad alipofariki dunia.

- Mapinduzi ya kisasa ya Wanawake na jitihada zake za kumkomboa mwanamke ambayo yametimiza pia utabiri wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) ambapo aliwazungumzia wanawake kuwa 'watakuwa watu wa mwisho kuja kujiunga na *Dajjal*, Mtume wa Uongo'.
"

"Watu wa mwisho kuja kujiunga na *Dajjal* watakuwa wanawake, kiasi kwamba mtu (mwanamume) itambidi arudi kwa mama yake, mwanawe wa kike, dada yake na shangazi yake na kuwafunga kwa nguvu ili wasije wakaenda kujiunga naye (*Dajjal*)"

(Kanz al-'Ummal, Toleo la 7, Hadith ya 2116)

"Wengi kati ya wale wanaomfuata yeye (Dajjal) ni Wayahudi na wanawake"

(Kanz al-'Ummal, Toleo la 7, Hadith ya 2114)

Wanawake wa Kiingereza waliongoza juhudi hizo za kutaka 'kujikomboa'. Ni pale tu katika karne ya ishirini, baada ya kifo cha Ghulam Mirza Ahmad ndipo mapinduzi hayo ya wanawake yalipoweza kuingia kwenye ulimwengu wa *Kiislamu.*

- Uchafuzi wa mazingira ambayo yanasababisha mabadiliko ya hali ya hewa ambayo Mtume (*rehma na amani juu yake*) aliyazungumzia kuwa yatatokea katika zama za *Dajjal*, Mtume wa Uongo. Haya yanatokea hivi sasa, hata hivi tukiwa tunaandika, wakati Mirza, amefariki muda mrefu uliopita.

- Udanganyifu mkubwa uliokithiri katika dunia ya kisasa ambamo 'kuonekana' na 'hali halisi' viko tofauti kabisa baina yao, na njia ya haki inayompeleka binaadamu peponi kuonekana kama ndiyo njia ya jahannamu na mwenendo wa jahannamu kuonekana kama ndiyo mwenendo wa peponi ni ushahidi kuwa *Dajjal* bado yumo kazini! Mtume (*rehma na amani juu yake*) alisema kuwa *Dajjal* atatenda hilo!

- 'Kukombolewa' kwa Ardhi Takatifu kutoka kwenye mikono na utawala wa wasiokuwa Wayahudi (ikim. Waislamu), kurejea kwa Wayahudi kwenye ardhi hiyo, na kuundwa kwa Taifa la Israeli, yote hayo yaliweza kukamilishwa kupitia mchango wa 'kisiwa' cha Kikristo cha Uingereza ambacho kipo umbali wa takriban mwendo wa mwezi mmoja kutoka ghuba ya Kiarabu (kama ilivyotajwa katika *Hadithi* ya Tamim al-Dari). Haya yote, pia yamekamilika baada ya kifo cha Mirza. Huu ni ushahidi wa nguvu kuwa *Dajjal* alikuwa kazini akiwashambulia Wayahudi kutoka kwenye kisiwa cha Uingereza, muda mrefu baada ya kifo cha Mirza.

- Kuna uwezekano kuwa Taifa la Israeli punde litachukua nafasi ya Marekani kama Taifa Tawala duniani na litanadi kuwa Zama za Dhahabu za Solomon (*rehma na amani juu yake*) zimerejea. Hili bado halijatokea. Lakini litakapojitokeza, litakuwa ni ushahidi mwingine kuwa *Dajjal* yumo mbioni katika kutekeleza azma yake ya kujifanya Masihi. Haya yote yatajitokeza punde, lakini Mirza amekwisha iaga dunia takriban karne nzima iliyopita.

Hayo yote ni matunda ya kazi ya *Dajjal*, Mtume wa Uongo, *ambaye bado yu hai*, wakati Mirza tayari amekwishakufa. Uhakika ni kuwa matukio hayo yote yamejitokeza duniani na kuwa matukio yaliyotambulika kipindi kirefu baada ya kifo cha Mirza Ghulam Ahmad. Ikiwa kama Mirza alimuua *Dajjal*, Mtume wa Uongo, je, vipi na kwa jinsi gani wafuasi wa Mirza wanaweza kutoa maelezo ya matukio hayo? Huenda ikawa kuwa wafuasi wa kweli wa Mirza Ghulam Ahmad hivi sasa wakagundua ukweli na hali halisi katika dunia ya leo, na hivyo kugundua kuwa Ukweli halisi unatofautiana na madai ya Mirza Ghulam Ahmad. Amin!

Sura ya 10

YA'JUJ NA MA'JUJ KATIKA QUR'ANI NA HADITHI

قَالُوا۟ يَٰذَا ٱلْقَرْنَيْنِ إِنَّ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ مُفْسِدُونَ فِى ٱلْأَرْضِ فَهَلْ نَجْعَلُ لَكَ
خَرْجًا عَلَىٰٓ أَن تَجْعَلَ بَيْنَنَا وَبَيْنَهُمْ سَدًّا ﴿٩٤﴾

"Wakasema: Ewe Dhul-Qarnaini! Hakika Juju-wa-maajuju wanafanya uharibifu katika nchi. Basi je, tukulipe ujira ili utujengee baina yetu na wao ngome?"

(*Qur'ani, al-Kahf, 18:94*)

Mwalimu wetu, mwenye baraka za kumbukumbu, *Maulana* Dk. Muhammad Fadlur Ansari (Mwenyezi Mungu amrehemu), alitufundisha somo muhimu sana linalofungamana na kutafuta elimu – hususan ikihusiana na kutafuta elimu ya Ukweli. Alitufundisha kuwa 'sehemu' (ya elimu) isisomwe pekee, ikichanganuliwa au kuachwa peke yake, kutoka kwenye 'somo zima' ambako 'sehemu' hiyo inatokana nako. Pili, alitufundisha kuwa katika kukusanya elimu inayohusiana na somo linalohusika kunahitaji kujumuisha 'sehemu' zote husika na kuzipanga ili kupata kitu kizima. Lakini hilo halitawezekana hadi upate kugundua kanuni ya umoja inaziunganisha sehenu hizo kuwa kitu kimoja kizima. Akaiita kanuni hiyo ya umoja 'mfumo wa maana'. Ni mfumo huu wa maana ndiyo ambao inatubidi tuugundue ili tuweze kulisoma na kulielewa somo la Ya'juj na Ma'juj. Bila ya kutumia njia hii katika kulisoma somo hili, ukweli ni kuwa hata walimu wenye ujuzi na elimu kubwa ya kidini wanaweza kupotoshwa.

Katika hadithi pekee inayopatikana katika kitabu cha Sahih Muslim, kuna ishara kuwa dunia haitopata athari za Ya'juj na Ma'juj hadi baada ya kurejea kwa Yesu (*rehma na amani juu yake*):
"Itakuwa katika hali hiyo ndipo Mwenyezi Mungu atamdhihirishia Yesu maneno haya: Nimewaumba miongoni mwa waja Wangu watu ambao hakuna atakayeweza kuwashinda kwenye mapambano; wapeleke watu hadi Tur kwa usalama, na hapo Allah atawaleta Ya'juj na Ma'juj na watateremka kutoka katika kila kilima."

(Sahih Muslim)

Hata hivyo, ushahidi wa wazi unapatikana kwenye *Qur'ani* na pia kuna hadithi za *Sahih Bukhari* zisizopungua nane zinazopingana na hadithi hiyo hapo juu. Zote zinathibitisha kuwa kuachiwa kwa Ya'juj na Ma'juj kulitokea wakati wa zama za Mtume (*rehma na amani juu yake*), muda mrefu kabisa kabla ya kurejea kwa Yesu (*rehma na amani juu yake*).

Ya'juj na Ma'juj wametajwa mara mbili tu katika *Qur'ani*. Hivyo basi, nguvu zetu za awali inatupasa tuzielekeze katika kutafuta kanuni ya umoja itakayoziunganisha hizo aya mbili za *Qur'ani* zinazowataja Ya'juj na Ma'juj.

Aya ya kwanza inapatikana katika *Surah-al Kahf* na ya pili inapatikana katika *Surah al-Anbiyah*. Hii ni sura ya kwanza:

قَالُوا۟ يَٰذَا ٱلْقَرْنَيْنِ إِنَّ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ مُفْسِدُونَ فِى ٱلْأَرْضِ فَهَلْ نَجْعَلُ لَكَ
خَرْجًا عَلَىٰٓ أَن تَجْعَلَ بَيْنَنَا وَبَيْنَهُمْ سَدًّا ﴿٩٤﴾

Wakasema: Ewe Dhul-Qarnaini! Hakika Juju-wa-maajuju wanafanya uharibifu katika nchi. Basi je, tukulipe ujira ili utujengee baina yetu na wao ngome? (ili iwe kinga kwetu?)"

(Qur'ani, al-Kahf, 18:94)

Hivyo basi inaonyesha wazi kuwa wanapotajwa kwa mara ya mwanzo katika *Qur'ani*, Ya'juj na Ma'juj wanaonekana kuwa ni maajenti wa *Fasad* (tazama maana yake juu). Mtume (*rehma na amani juu yake*) alifafanua kuwa Ya'juj ni jumuiya ya binaadamu waliotokana na Adamu. Ni hivyo hivyo pia kwa Ma'juj. Hadithi inaijazia maelezo ya ziada *Qur'ani* na kuonya kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Allah, amewajaalia binaadamu hawa kwenye jumuiya zinazowajumuisha maajenti wa *Fasad* nguvu na uwezo mkubwa kiasi kwamba, kwa kipimo cha kidunia, hawana mshindani:
"Itakuwa katika hali hiyo ndipo Mwenyezi Mungu atamdhihirishia Yesu maneno haya: **Nimewaumba miongoni mwa waja Wangu watu ambao hakuna atakayeweza kuwashinda kwenye mapambano**; wapeleke watu hadi Tur kwa usalama, na hapo Allah atawaleta Ya'juj na Ma'juj na watateremka kutoka katika kila kilima. Wa mwanzo watapita katika ziwa Tiberias (ikim. Bahari ya Galilee) na watakunywa maji yake. Wakati wa mwisho atakapokuwa akipita atasema: Hapa zamani palikuwa na maji. Yesu na wafuasi wake watazungukwa hapo (Hapo Tur, na watakuwa na hali ngumu) kiasi kuwa kichwa cha ng'ombe kitakuwa na thamani kubwa kuliko dinari mia moja. Yesu (*rehma na amani juu yake*) Mtume wa Mwenyezi Mungu, na wafuasi wake watamuomba Mwenyezi Mungu, Ambaye atawapelekea wadudu (ambao watazishambulia shingo

zao) hadi asubuhi wataangamia kama mtu mmoja. Yesu (*rehma na amani juu yake*) Mtume wa Mwenyezi Mungu, na wafuasi wake ndipo watakaposhuka duniani na hawatoweza kupata hata sehemu moja amabyo haitokuwa na uozo na harufu mbaya. Yesu (*rehma na amani juu yake*) Mtume wa Mwenyezi Mungu, na wafuasi wake ndipo atakapomuomba Mwenyezi Mungu amabye Atawatuma ndege ambao shingo zao zitakuwa kama shingo za ngamia wa Bactriani na watawachukua na kuwatupa pale watakapoamrishwa na Allah."

(Sahih Muslim)

Surah al-Kahf inatufahamisha kuwa *Dhul Qarnain* alijenga ngome baina ya watu walimuomba afanye hivyo na maajenti wa *Fasad.* Alitumia mapande ya 'chuma' na kisha akayaziba kwa 'shaba iliyoyeyushwa'. Kisha akaiita ngome kuwa ni *Rahmah* (tendo la rehma) kutoka kwa Mola na kuwa Allah Mwenyewe ataivunja kinga hiyo na kuwaachia Ya'juj na Ma'juj pale ambapo *W'ad* (onyo) la Mola (wa *Dhul Qarnain*) litakapotimia:

قَالَ هَٰذَا رَحْمَةٌ مِّن رَّبِّي ۖ فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ رَبِّي جَعَلَهُ دَكَّاءَ ۖ وَكَانَ وَعْدُ رَبِّي حَقًّا ﴿٩٨﴾

"Akasema: Hii ni rehema itokayo kwa Mola wangu Mlezi. Na itapo fika ahadi ya Mola wangu (kuhusu Zama za Mwisho) Mlezi atauvunja vunja. Na ahadi ya Mola wangu Mlezi ni kweli tu."

(Qur'ani, al-Kahf, 98)

Je, ni onyo (*W'ad*) lipi linalozungumziwa hapa? Jibu linapatikana wazi kabisa katika hadithi maarufu ya Mtume (*rehma na amani juu yake*) ambamo anazitaja Alama kuu za Zama za Mwisho. Miongoni mwa Alama hizo kuu kumi, mojawapo ni kuachiwa kwa Ya'ajuj na Ma'ajuj:

"Amesimulia Hudhayfah ibn Usayd Ghifari:

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*) alijitokeza kwetu ghafla na kutukuta tunajadiliana. Akauliza: mnajadili kitu gani? (Masahaba) wakasema: Tunajadiliana kuhusu Saa ya Mwisho. Hapo akasema: Haitokuja hadi mtakapoona alama kumi na (kuhusiana nazo) akataja 'moshi', 'Dajjal', 'Mnyama', 'jua kutokea magharibi', 'kushuka kwa Yesu (rehma na amani juu yake) mwana wa Maryamu', Ya'juj na Ma'juj', Mapasuko ya ardhi sehemu tatu tofauti, moja mashariki, la pili magharibi na la tatu Arabia' ambapo mwisho wake moto utawaka kutka Yemen na utawapeleka watu kwenye sehemu ya mkusanyiko'."

(Sahih Muslim)

Kwa maneno mengine, wakati ngome inavunjwa na Ya'juj na Ma'juj wanaachiwa, hiyo itakuwa ni moja ya alama kuu kuwa binaadamu wameingia kwenye Zama za Mwisho. Swali ni: je,

tutajuaje kuwa ngome imevunjwa na Ya'juj na Ma'juj wameanza kuachiwa? Hebu kwanza tuziangalie *hadithi* hizi nane ambazo zote zinapatikana katika *Sahih Bukhari*. Msomaji asishangazwe na kurudia rudia. Hizi si *Hadithi* tofauti. Isipokuwa kinachozungumziwa ni kile kile. Pia, wasimulizi ni watu tofauti na hivyo kuna tofauti kidogo katika mapokezi yake. Matokeo yake ni kuwa *Hadithi* inakuwa *mutawatir* na hivyo kunaifanya *Hadithi* kuwa ya nguvu na kuaminika kwa hali ya juu kabisa:

"Amesimulia Abu Huraira:

Mtume akasema: Tundu limefunguliwa katika bwawa la Ya'juj na Ma'juj. Wuhaib (msimulizi mdogo au wa kati) akafanya ishara ya namba 90 (kwa kidole chake cha shahada na gumba)."

(Sahih Bukhari)

"Amesimulia Zainab bint Jahsh:

Siku hiyo moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimjia akiwa na hali ya kushikwa na hofu kubwa na akasema: Hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah! Msiba kwa Waarabu unaotokana na ubaya mkubwa unaowakabili. **Leo,** tundu kama hivi limetobolewa katika ngome / bwawa la Y'ajuj na M'ajuj. Mtume akaonyesha ukubwa wa tundu kwa ishara ya kuchora kwa kidole cha shahada na gumba. Zainab bint Jahsh akasema: O Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je, tutaangamizwa ilhali kutakuwa na watu wema miongoni mwetu? Mtume akasema: Ndiyo, ikiwa idadi ya wabaya (watu) itaongezeka."

(Sahih Bukhari)

Hadithi hii inarudiwa tena katika *Sahih Bukhari*, ikiwa na maneno tofauti kidogo kama ifuatavyo:

"Amesimulia Zainab bint Jahsh:

Mtume alitoka usingizini huku uso wake ukiwa mwekundu na akasema: Hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah! Msiba kwa Waarabu unaotokana na ubaya mkubwa unaowakabili. **Leo,** tundu limetobolewa katika ukuta wa Y'ajuj na M'ajuj (Sufyan aliashiria kwa kuonyesha namba 90 au 100 kwa vidole vyake). Ikaulizwa: Je, tutaangamizwa japo kna watu wema miongoni mwetu? "Mtume akajibu: Ndiyo, ikiwa uovu utaongezeka."

(Sahih Bukhari)

"Amesimulia Zainab bint Jahsh:

Siku hiyo moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alimjia akiwa na hali ya kushikwa na hofu kubwa na akasema: Hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah! Msiba kwa Waarabu unaotokana na ubaya mkubwa unaowakabili. **Leo,** tundu kubwa kama hivi (akionyesha kwa vidole viwili kufanya duara) limetobolewa katika ukuta wa Y'ajuj na M'ajuj. Zainab akasema: 'O Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je, tutaangamizwa japo miongoni mwetu kuna watu waadilifu?' Akasema: 'Ndiyo, ikiwa uovu utaongezeka.'

(Sahih Bukhari)

"Amesimulia Zainab bint Jahsh:

Siku moja Mtume alimjia akiwa na hali ya kushikwa na hofu kubwa na akasema: 'Hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah! Msiba kwa Waarabu unaotokana hatari inayowakabili. Tundu limetobolewa katika ukuta wa Y'ajuj na M'ajuj (akifanya duara kwa kidole gumba na shahada). Zainab bint Jahsh akasema: 'O Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je, tutaangamizwa japo miongoni mwetu kuna watu waadilifu?' Akasema: "Ndiyo, ikiwa watu waovu wataongezeka."

(Sahih Bukhari)

Amesimulia Umm Salama:

Mtume aliamka na kusema: Atukuzwe Allah: Mali ngapi (kiasi gani) zimeshushwa na maafa makubwa (kiasi gani) yameshushwa!"

(Sahih Bukhari)

"Amesimulia Abu Huraira

Mtume alisema: Allah ametoboa tundu kwenye ukuta wa (watu wa) Y'ajuj na M'ajuj kama hivi (na akaashiria kwa kutumia vidole vyake.)"

(Sahih Bukhari)

"Amesimulia Ibn Abbas:

Mjumbe wa Mweneyzi Mungu alifanya Tawaf (kuzunguka Kaaba akiwa amepanda ngamia wake, na kila mara alipofikia kona (yenye jiwe jeusi) alilinyooshea kidole na kusema: '*Allah Akbar*.' Zainab akasema: Mtume akasema: 'Tundu limetobolewa katika ukuta wa Y'ajuj na M'ajuj kama hivi' (akifanya namba 90 kwa kidole cha shahada na gumba)

(Sahih Bukhari)

Hadithi hizi nane za Sahih Bukhari amabazo zimepatikana kutoka kwenye vyanzo vinne tofauti, Abu Hurarira, Zainab bint Jahsh, Umm Salama na Abdallah ibn Abbas (*radhiallahu anhu*), zinaweka wazi na kwa uhakika kuwa kuachiwa kwa Ya'juj na Ma'juj kulitokea katika zama za Mtume (*rehma na amani juu yake*). Ukweli ni kuwa yeye mwenyewe alisema kuachiwa huko kumetokea "**leo**"! Hivyo Zama za Mwisho, au Zama za *Fitan,* zilianza wakati wa uhai wa Mtume (*rehma na amani juu yake*). Na huu ndiyo ufunguo wa msemo wake kuhusiana na 'Saa ya Mwisho.':

"Amesimulia Sahl bin Said:

Nilimuona Mjumbe wa Allah akionyesha kwa kidole cha shahada na cha kati akisema: Muda wa kuja kwangu na Saa (ya Mwisho) ni kama vidole hivi viwili. Maafa Makubwa (akim. Zama za Fitan) yatakumba na kutawala kila kitu."

(Sahih Bukhari)

Qur'ani imeendelea kuwapa waumini ushahidi wa nguvu na Alama kubwa ambayo si tu itawawezesha kuwa na uhakika wa kuachiwa kwa Ya'juj na Ma'juj, bali pia, watakuwa na uthibitisho kuwa dunia sasa iko chini ya utawala wa Ya'juj na Ma'juj. Wataweza kugundua na kutambua kuwa Y'ajuj na M'ajuj kama ni Nguvu ya Dola (Watawala) wa Dunia. Hii inapatikana pale wanapotajwa Y'ajuj na M'ajuj katika *Surah al-Anbiyah*:



"Na haiwi kwa wana-Mji tulio uangamiza, ya kwamba hawatarejea (wakazi wake) mpaka watapo funguliwa Ya'juj na Ma'juj(kutoka kwenye kizuizi chao) wakawa wanateremka kutoka kila mlima (au kusambaa kuelekea kila upande).

(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:95-96)

Wakati Ya'juj na Ma'juj wameachiwa na, *wakawa wanateremka kutoka kila mlima au kusambaa kuelekea kila upande,* ndipo wakati huo watu au wakazi wa Mji walioadhibiwa na Mwenyezi Mungu, na kufukuzwa kutoka kwenye mji wao (ambao uliteketezwa na Mwenyezi Mungu), wataweza kurudishwa kwenye mji huo. Ni mji mmoja tu ambao (uliteketezwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu) ambao umetajwa kwenye Hadithi unaoambatanishwa na Ya'juj na Ma'juj. Nao ni mji wa **Jerusalem.**

Hadithi ifuatayo inawataja Ya'juj na Ma'juj wakipita pembezoni mwa Bahari ya Galilee, ambayo ipo kwenye Ardhi Takatifu:

"Amesimulia al-Nawwas ibn Sam'an: ..... Itakuwa kwenye mazingira kama hayo ndipo Allah atakapoyadhihirisha maneno haya kwa Yesu (*rehma na amani juu yake*): Nimewaumba miongoni mwa waja Wangu watu ambao hakuna atakayeweza kuwashinda kwenye mapambano; wapeleke watu hadi Tur kwa usalama, na hapo Allah atawaleta Ya'juj na Ma'juj na watateremka kutoka katika kila kilima. Wa mwanzo watapita katika ziwa Tiberias (ikim. Bahari ya Galilee) na watakunywa maji yake. Wakati wa mwisho atakapokuwa akipita atasema: Hapa zamani palikuwa na maji. Yesu na wafuasi wake watazungukwa hapo (Hapo Tur, na watakuwa na hali ngumu) kiasi kuwa kichwa cha ng'ombe kitakuwa na thamani kubwa kuliko dinari mia moja..."

(Sahih Muslim)

Wakati Ya'juj na Ma'juj wanapita pembezoni mwa Bahari ya Galilee wataelekea Tur (mlima) ambao umetajwa katika Hadithi kuwa ni mlima uliopo **Jerusalem:**

"Y'ajuj na M'ajuj watatembea hadi watafika kwenye mlima wa al-Khamr, na ni mlima wa **Bait al-Maqdis** (ikim. Jerusalem), na watsema: Tumewaua wale ambao wamo duniani. Hebu sasa tuwaue wale ambao wako mbinguni (mawinguni). Watarusha mikuki yao kuelekea mbinguni na mikuki itawarudia ikiwa imeenea damu."

(Sahih Muslim)

Kwa kuwa hakuna mji mwingine wowote (ulioteketezwa na Allah) zaidi ya Jerusalem unaotajwa kwenye Hadithi zinazowahusu Ya'juj na Ma'juj, tumefikia uamuzi na hitimisho kuwa mji unaokusudiwa na kutajwa kwenye *Surah al-Anbiyah* (aya za 95 na 96) hapo juu ni pekee mji wa **Jerusalem**.

Kutokana na hitimisho hili na utambuzi huo wa mji, mtiririko wa mantiki unatupeleka kwenye kugundua kuwa kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu, ambako kumekwishatokea, ni ushahidi wa uhakika kuwa kizuizi kilichowekwa kimevunjwa na Allah Mtukufu, na kuwa sasa tunaishi kwenye zama za Ya'juj na Ma'juj, hivyo tumo kwenye Zama za Mwisho.

Jambo la umuhimu zaidi linalotokana na kurejea kwa Wayahudi kwenye 'mji' (Jerusalem) na kuundwa kwa Taifa la Israeli ni kuwa Ya'juj na Ma'juj hadi hapo wametimiza ile awamu ya lengo lao iliyotajwa kwenye *Surah al-Anbiyah, 21: 96*, ya kuwa wameteremka kutoka kila mlima (au kusambaa kuelekea kila upande) na wameidhibiti dunia. Mfumo wa dunia mabao unawarudisha Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu ni mfumo wa Ya'juj na Ma'juj! Ni nani hao? Je, tunaweza kuwafahamu? Mpangilio wetu wa kutafuta majibu ya maswali hayo unabidi utuongoze katika kutafuta watu ambao wataonyesha, tabia ya kupagawa katika ushirikiano wao na Wayahudi na Ardhi Takatifu, mabadiliko ya ajabu ya tabia hizo ukilinganisha na kipindi cha kabla ya Mtume Mtukufu *(rehma na amani juu yake)* ukilinganisha na kipindi baada ya Mtume *(rehma na amani juu yake).*

Kupagawa kwa ajabu kwa Wazungu wa Ulaya kuhusiana na Ardhi Takatifu

Wakati Abraham *(rehma na amani juu yake)* alipofanya *Hijrah* kwa kwenda kwenye Ardhi Takatifu, na Babylon, Persia, Egypt na China walikuwa wamefikia kiwango cha juu cha ustaarabu, na Falme za Kigiriki na Kirumi zilikuwa bado hazijaibuka, Ulaya walikuwa wakiishi kama 'makabila ya mwituni'. Hapakuwa na biashara, au kama ilikuwapo basi ni kwa kiwango kidogo sana baina ya Ulaya na dunia iliyokuwa imeshastaarabika. Hapakuwa pia na kiwango chochote kinachopimika cha safari za matembezi baina yao. Matokeo ya kutengana huku kusiko kwa kawaida, watu duniani hawakuweza kuzielewa lugha za watu wa Ulaya, na pia bara hilo halikuweza kuwa na nafasi yoyote

muhimu katika masuala yaliyokuwa yanahusu na kuathiri dunia. *Qur'ani* inalizungumzia jambo hili linalolihusu bara la Ulaya katika *Surah al-Kahf* wakati *Dhul Qarnain* alipofanya safari yake ya tatu na kuwafikia watu ambao lugha yao hakuweza kuielewa (*Surah al-Kahf, 18:93*)

Mapinduzi ya ajabu na yasiyoelezeka kwa urahisi yakalikumba bara la Ulaya. Ustaarabu usiomjua Mungu wa Kigiriki na Kirumi ukajitokeza na cha ajbu ni kuwa mara moja falme hizo zikajikita katika kushambulia na kuteka maeneo mengi duniani kwa kadiri zilivyokuwa zikiweza kuteka. Falme hizo zote mbili, zikaonyesha kuwa na kufanya bidii maalum juu ya Ardhi Takatifu. Alexander 'the Great' aliiteka Jerusalem na kuonyesha kuvutiwa na Judaizm, na Ufalme wa Kirumi uliitawala Jerusalem hadi wakati wa Yesu *(rehma na amani juu yake)* na hata baada ya kipindi hicho. Pili, hapakuwa na mshikamano na mapenzi na miungu yao (ya kike na kiume) na mfumo wao wa kipagani wa maisha. Miungu hiyo ya kike na kiume ya Wagiriki na Warumi haikuweza kuendelea kuwepo kama vile miungu ya kike na kiume, mfano ya Wahindi wa India. Badala yake, imani hizo za kipagani, kiajabu kama vile zilivyojitokeza, pia kiajabu zikatokomea na kuacha kufuatwa kama zilivyojitokeza karne kadhaa nyuma yake.

Kisha, kiajabu bara la Ulaya likaukumbatia Ukristo, kwa sababu zaidi za kisiasa, nako kukapelekea kujitokeza kwa Kanisa Kristo la Ulaya na Roma ikawa ndipo makao makuu ya kanisa hilo jipya. Ni Ukristo ndiyo ulioibua sehemu kubwa ya bara la Ulaya kutoka kwenye kiwango cha historia cha 'makabila ya mwituni' na kuiunganisha Ulaya chini ya Ukristo. Kanisa jipya la Kikristo likaweka umuhimu mkubwa sana katika kujitofautisha na Ukristo wa zamani kiasi kufikia hata kuchagua tarehe yao peke yao ya kusherehekea kuzaliwa kwa Yesu *(rehma na amani juu yake).* Tarehe mpya ya Krismasi ya Wakristo wa Ulaya ikawa Disemba 25.

Lakini cha ajabu ni kuwa Ukristo wa Ulaya ukawa na tofauti kubwa ukilinganisha na Ukristo wa jadi wa zamani wa Byzantium. Mara tu baada ya Ukristo mpya kujiimarisha katika kulikamata bara la Ulaya, ukaendelea kuonyesha hali ya kupagawa na Ardhi Takatifu, kitu ambacho hakikuwapo na hakipo kwenye tabia ya Wakristo wengine wote waliobaki. Mashambulizi ya kikrusedi hayakuwa tu ya Kikristo. Yalikuwa ni ya Wakristo wa Ulaya. Yalifanywa moja baada ya jingine dhidi ya Waislamu katika jitihada zilizokosa mafanikio ya kuweza kunyakua Ardhi Takatifu kutoka mikononi mwa Waislamu. Ukombozi uliopatikana haukudumu muda mrefu kwani ulimalizwa na pale ambapo Sultani Salahuddin alipowashinda Makrusedi wa Kikristo na kurudisha utawala wa Kiislamu juu ya Ardhi Takatifu.

Kitu kilichokuwa ni cha muhimu zaidi kuliko vyote kuhusiana na mashambulizi ya Krusedi, ni ukweli kuwa yalikuwa yakiwahusu na yakifanywa na Wakristo wa Ulaya peke yao. Japokuwa iliwalazimu kupita kwenye himaya za Wakristo wa Byzantine, wasiokuwa Wakristo wa Ulaya hawakushiriki katika Krusedi hizo. Hivyo basi, kupagawa na Jerusalem na Ardhi Takatifu, ni kupagawa kwa watu wa bara la Ulaya, na si kupagawa kwa Wakristo. Kitabu hiki kinaliweka wazi swali: Kwanini, na kunatokana na nini kupagawa huku kwa Wakristo wa Ulaya?

Pili, pindi wapiganaji wa Krusedi walipofanikiwa kutwaa madaraka dhidi ya mji wa Jerusalem kutoka mikononi mwa Waislamu, kwa kipindi kifupi walifanya mauaji na umwagaji damu mkubwa sana ambao haukuwa na uwiano wowote na misingi na kanuni za Ukristo. Waliwaua na kuwachinja wakazi wote wa Jerusalem, wakiwemo wanawake na watoto. Nchi, himaya na waumini wa dini ya Kikristo dunia nzima walishikwa na mshangao mkubwa kwa kushuhudia uovu na unyama ulioonyeshwa na waumini wa dini ya Kikristo waliokuwa na asili ya Ulaya ambao walijikita kwenye jitihada za kiroho na kidini za kutaka kuikomboa Ardhi Takatifu. Ilidhihirika wazi kuwa Ukristo ulitumika kama vazi hadaa la mbwa mwitu kujivisha imani ya dini ya Kikristo kama ngozi ya kondoo kwa makusudi ya kutimiza malengo yao. Krusedi ilidhihirisha ukweli wa msimamo wa wakazi wa Ulaya uliojaa ukatili na unyama unaotisha usio na imani ya Mungu, hazikuwa za Kikristo na zilihusisha makabila yenye unyama mwingi wasiokuwa wastaarabu. Lakini pia walionyesha dalili za kuwa na nguvu nyingi zilizokosa utiifu. Kadiri muda ulivyokuwa ukipita ilidhihirika kuwa na uwezo mkubwa sana wa kuficha uhalisia na malengo yake na kujionyesha na kuonekana kinyume na ukweli ulivyo.

Mazingatio ambayo Waislamu walipaswa kuyaelekeza kwenye matukio haya ya mwenendo wa kiajabu wa wakazi wa bara la Ulaya yalichepushwa kiajabu wakati wa mashambulizi ya watu kutokea Mongolia yaliyokuwa pia ya kinyama na kikatili yaliyofanywa dhidi ya umma wa Waislamu ambayo hayakuwa tofauti na yale yaliyofanywa na Wakristo wa Ulaya. Laiti mashambulizi haya ya watu wa Mongoli yasingefanywa, wanazuoni wa Kiislamu wangegundua kujitokeza kwa mwenendo wa kiajabu wa waumini wa Kikristo wanaotoka bara la Ulaya.

Ndiyo sababu hasa iliyopoteza mwelekeo wa mtazamo wao na iliyowakosesha Waislamu kugundua mwenendo wa kiajabu uliokuwa unajitokeza katika historia ya bara la Ulaya ambamo bara zima lilikuwa likigeuka kiajabu kusikokuwa na maelezo kutoka kwenye utamaduni wa enzi za kati wa Kikristo na kuingia kwenye mapinduzi ya kileo ya magharibi yanayomkana Mwenyezi Mungu. Mapinduzi hayo yalililetea bara la Ulaya mapinduzi ya viwanda na sayansi yakijumuisha mfumo wa

uchumi uliofungamana na *Riba* uliopelekea bara la Ulaya kuwa na nguvu na uwezo mkubwa kuliko sehemu nyingine zozote za dunia zikijumuishwa na kushika nafasi ya kwanza ya mtawala wa dunia bila mpingamizi. Katika bara jipya la Ulaya, Uingereza, ikiwa kisiwa kidogo kilicho umbali wa mwendo wa takriban mwezi mmoja kutoka Ardhi Takatifu kwa mwendo wa kutumia bahari, kilithubutu kuzishinda himaya zote zenye nguvu katika bara la Ulaya na kujitokeza kuwa kiongozi wa Ulaya na mtawala wa dunia nzima.

Lakini Ulaya mpya iliyojitokeza kwa kuwa na mwelekeo na mtazamo wa kumkana Mwenyezi Mungu, ikijifanya ni ya Kikristo, iliendelea kuonyesha tamaa na mshikilio wa Ardhi Takatifu kama ule ulioonyeshwa na Ulaya ya zamani iliyopigania ardhi hiyo kwa Krusedi. Iliendelea na kujiunga na wasioamini Mungu wanaojifanya Wayahudi wa Ulaya wa Khazari katika mwendelezo wa kutaka kuikomboa Ardhi Takatifu. Watu hawa wa aina hizi mbili wameendelea kubaki kwenye mshikamano usiokuwa na utakatifu wa kiajabu na usioelezeka tangu enzi hizo.

Ilikuwa ni kisiwa cha Uingereza ambacho kilitoa tamko (linalojulikana kama Tamko la Balfour) mnamo mwaka 1917 kuwa litajikita kwenye harakati za kupigania kupatikana kwa Makazi ya Kitaifa ya Wayahudi ndani ya Palestina. Waingereza waliendeleza juhudi zao na miaka miwili baadaye waliweza kuikomboa Ardhi Takatifu kutoka mikononi mwa utawala wa mataifa (Waislamu) wasiokuwa Wayahudi. Hii ilitokea mwaka 1917 wakati Jenerali wa Kiingereza, Allenby, alipoliongoza jeshi lililonyakua ushindi dhidi ya jeshi la Kituruki lililokuwa likilinda Jerusalem na Ardhi Takatifu. Wakati ambapo Krusedi, zilizofanywa na wanaojifanya Wakristo wa Ulaya, zilishindwa, krusedi mpya, zilizofanywa na Ulaya inayomkana Mungu, zilishinda. Jenerali Allenby mwenyewe alithibitisha hili kwa usemi wake unaokumbukwa alioutoa wakati anaingia Jerusalem kama mshindi kwa kusema: "*Leo hii Krusedi zimefikia mwisho wake*." Hivyo basi ni wazi kuwa jitihada za kuikomboa Ardhi Takatifu zilikuwa hazina uhusiano wowote na dini. Badala yake zilikuwa na kila uhusiano na mwenyeji mpya kwenye jukwaa la dunia, bara la Ulaya!

Uingereza ikajinyakulia madaraka ya udhamini juu ya Ardhi Takatifu chini ya kivuli cha Shirikisho la Mataifa na ikaendelea kutekeleza harakati zake aenye lengo la kuunda Makazi ya Taifa la Wayahudi. Kitabu hiki kinawakilisha swali: kwanini panajitokeza tamaa na mshikilio wa ajabu wa bara la Ulaya unaohusiana na Ardhi Takatifu, bara ambalo hivi sasa limejichagulia msimamo wa uyakinifu na mwelekeo wa kidunia wa kumkana Mwenyezi Mungu, na huku Ukristo wake ukiwa siyo wa dhati?

Ikiwa bara la Ulaya kuukumbatia Ukristo ulikuwa wa kiajabu, basi ukumbatiaji wake wa dini ya Uyahudi umepitiliza maajabu yote. Ilikuwa mnamo karne ya saba, huenda, ndipo makabila ya Kikhazeri ya Ulaya ya Mashariki yalipojiunga na dini ya Kiyahudi. Walifanya hivyo kwa sababu za kisiasa. Imani ya kidini haikuwa kabisa kwenye kiini cha uamuzi huo. Hata kabla hawajajiunga na dini ya Kiyahudi, makabila haya ya Kikhazeri ya Ulaya yalionyesha kuwa na nguvu zisizokuwa za kawaida zilizowawezesha kushinda na kuhimili kuingia kwa Uislamu katika bara la Ulaya.

Kama walivyo Wakristo wa Ulaya, hawa Wakhazeri wa Ulaya pia walitofautiana sana kimuonekano na Wayahudi wa Israeli. Tofauti na Wayahudi wa Israeli, hawa Wayahudi wa Ulaya walishikilia kinaganaga lengo la kupokonya madaraka ya kuikamata Ardhi Takatifu. Ilikuwa ni Wayahudi wa Ulaya ndiyo walioanzisha Ushirika wa Wayazonisti na kujikita kwenye kupigania kile kile ambacho Wakristo wa Ulaya walikuwa wakikipigania kwa Krusedi, nacho ni, lengo la kuikomboa Ardhi Takatifu. Kitabu hiki kinauliza swali: Kwanini panajitokeza mshikilio wa mshikamano wa Wayahudi na Wakristo wa Ulaya kwenye Ardhi Takatifu?

Uingereza iliusaidia Ushirika wa Wazayonisti katika “kuwarudisha” Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu, jambo ambalo mwishowe lilifanikishwa baada ya kuundwa kwa Taifa la Israeli mnamo mwaka 1948. Wakati Uingereza, ikiwa kama mkunga, ilisaidia kukamilisha tendo la uzazi wa mtoto “Israeli” na dunia ikashuhudia kile kinachoonekana kuwa ni kulirudisha upya taifa la Kiisraeli la jadi ambalo lilivunjwa na kuteketezwa na Mwenyezi Mungu Mtakatifu Zaidi ya miaka 2000 iliyopita.

Baada ya Uingereza kuitawala dunia kwa karne kadhaa mabadiliko ya kiajabu yalijitokeza ambapo taifa kubwa jingine lenye nguvu na utajiri mkubwa lilipojinyakulia haki na hadhi ya kuitawala dunia. Ushahidi wa Dhahiri ulijitokeza wakati wa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia wakati jeshi la Kimarekani lilipojiingiza vitani na kuiokoa Uingereza kutoka kwenye kipigo kilichotishia kuishia kwenye kushindwa. Ikawa Dhahiri Zaidi kwenye Vita Kuu ya Pili ya Dunia wakati Jenerali wa Kimarekani, Eisenhower, alipochaguliwa kuwa Kmanda Mkuu wa Majeshi yote ya kirafiki yalioungana na kupigana kwenye Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Eisenhower, Mmarekani mwenye asili ya Kijerumani, hakuwa hata na asilia ya Kiingereza.

Pia baadaye mnamo mwaka 1944, huko Bretton Woods, kwenye jimbo la New York, mkutano wa kimataifa uliitishwa ukiwa na lengo la kuunda mfumo wa kimataifa wa kusimamia fedha na uwiano wa sarafu duniani. Sarafu ya Kiingereza ya paundi ambayo ilikuwa ikitambulika duniani kwenye ulimwengu wa sarafu bandia za makaratasi iliondolewa kutoka kwenye nafasi yake na badala

yake dola ya Kimarekani ikachukua nafasi hiyo. Hivyo hivyo, mji wa New York ukaupiku mji wa London na ukachukua nafasi mpya kama kiini na makao makuu ya mfumo mpya ulioundwa wa sarafu bandia za makaratasi.

Taifa hili kubwa jipya ambalo lilijitokeza katika mazingira ya kiajabu lilitokana na utamaduni ule ule wa bara la Ulaya ambalo huko nyuma lilipigana kwa njia ya Krusedi kupigania Jerusalem na Ardhi takatifu, likiwa limejipa jukumu la awali katika kutekeleza kuundwa kwa Makazi ya Taifa la Wayahudi katika Ardhi Takatifu. Taifa hili kubwa jipya, lilianzia pale ambapo taifa kubwa la awali lilipoachia juhudi na mshikamano wa kiajabu usio wa kawaida na Ardhi Takatifu na Taifa la Isrseli. Hata Taifa la Israeli lilipotangazwa kuwa ni nchi huru mwaka 1948, nchi ya kwanza duniani kulitambua Taifa la Israeli ilikuwa ni Marekani.

Taifa hili jipya lilihakikisha kuwa linaweka wazi kabisa kuwa limechukua nafasi ya Uingereza na kuwa ni mshirika mpya wa kimikakati wa Taifa la Israeli. Kwa kweli, liliendelea kufanya hivyo hadi kuliadhiri na kulivunjia heshima Taifa la Uingereza. Palitokea mapinduzi nchini Egypt mwaka 1952 na jeshi la Egypt lilimuondoa mfalme na kuchukua madaraka ya kuiongoza nchi hiyo. Mwaka 1956, Kanali Gamal Abdel Nasser alichukua nafasi ya Jenerali Muhammad Naguib kama Kiongozi wa Taifa na mara moja alichukua hatua za kuonyesha uzalendo wake kwa kutaifisha Mfereji wa Suezi. Israeli ikaona kuwa hili ni tishio kwenye usalama wa Taifa la Israeli na Waingereza, upande wa pili, wakaona kuwa nafasi yao kama Taifa Kubwa inatiwa kwenye majaribu na mtihani.

Katika kampeni ya pamoja iliyoendeshwa na majeshi ya Kiingereza, Kifaransa na Israeli bila kuwajumuisha Wamarekani, majeshi hayo yalilishambulia jeshi la Egypt na kulitoa kwenye Mfereji wa Suezi. Raisi wa Marekani alijibu kwa kutoa amri kwa majeshi hayo ya Kiingereza, Ufaransa na Israeli kujitoa kutoka kwenye ardhi ya Egypt. Uingereza, likiwa kama taifa kubwa la awali, lililazimika kuyatoa majeshi yake na serikali ya Uingereza iliyokuwa ikiongozwa na Anthony Eden ilianguka na kuachia madaraka. Baadaye, kuanzia kipindi hicho hadi leo hii, Marekani imekuwa mlezi nambari moja wa Taifa la Israeli. Kitabu hiki kinauliza swali: kwanini panajitokeza hali hii ya kiajabu ya mshikamano wa Ulaya-marekani kwa Ardhi Takatifu.

Ikiwa tunastaajabu mshikilio huu wa Ardhi takatifu kunakoonyeshwa na wakazi wa Ulaya na Marekani (wakijumuika na Wakristo wa Ulaya na Wayahudi wa Ulaya), basi tujitayarishe kwani siku zijazo zinaashiria kutuletea yale yanayostaajabisha Zaidi ya haya tunayoyaona hivi sasa. Mtazamo

wetu unaashiria kuwa dunia itashuhudia kujitokeza kwa Taifa la Kizungu la Israeli (Israeli iliyoundwa na Ushirika wa Wazayonisti) kama taifa kubwa na lenye nguvu kuliko mataifa yote duniani ambalo litachukua nafasi ya Uingereza na Marekani. Taifa hili la kizungu la Israeli tayari linamiliki silaha za kutosha za nyuklia na nyukliajoto zinazoiwezesha kutambulika kama Taifa kubwa lenye nguvu duniani. Zaidi, teknolojia yake ya kijeshi tayari inalingana kiushindani na mataifa yanayoongoza kwenye fani hiyo duniani. Mwisho, mabepari stadi wa kizungu wa Kiyahudi na wamiliki wa mabenki makubwa duniani tayari wanao uwezo wa kutwaa mfumo na usimamizi wa fesha duniani kwa kufanya tendo jepesi la kuisababishia kuanguka kwa sarafu ya dola ya kimarekani. Kuanguka huko kwa dola, kutauporomosha mfumo mzima wa pesa za makaratasi duniani. Muanguko huu wa sarafu ya dola unaweza ukaoanishwa na onyesho la nguzu za kijeshi la taifa la kizungu la Israeli lisilo la kawaida kushambulia Wapalestina na nchi jirani za Kiarabu. Israeli itaweza kutojali msimamo wa dunia nzima na kuendelea kwa ushindi kushikilia matunda ya shambulio lake kwa nchi za Kiarabu na kwa kufanya hivyo, kujitokeza na kujiimarisha kama taifa kubwa linalotawala dunia. Kutokea kwa jambo hili, kwa hakika kutaonekana kwa Wayahudi wa Kiisraeli (*Banu Israel*) kuwa sasa wanashuhudia kurudishwa kwa zama za dhahabu, enzi ambapo Israeli iliyokuwa chini ya utawala wa Solomon ilikuwa ikitawala dunia nzima.

Je, *Qur'ani* ina maelezo yoyote kuhusu haya, na kama ndivyo, maelezo yake ni yapi?

Tungependa kukiri mwanzoni kabisa kabla ya maelezo yoyote kuwa kitabu hiki kisingeweza kuandikwa laiti kama Wayahudi wangekuwa hawajarejea kwenye Ardhi Takatifu. Na hiki inaonyesha kuwa ni kitabu cha kwanza kuandikwa tangu tukio hilo litokee. Hivyo basi, tutakapokuwa tunatumia *Qur'ani* na *Hadithi* kuelezea hili matukio haya ya ajabu, maelezo yetu bila ya shaka yatawashangaza wengi wakiwemo hata wanazuoni wa *Kiislamu*. Zaidi inaonekana kwa mwandishi huyu, kuwa maelezo ya *Qur'ani* ya matukio haya yote yasiyokuwa ya kawaida yaliyotokea Ulaya na katika Ardhi Takatifu, ni mtazamo unaotumia elimu ambayo huenda hadi hivi haijawahi kuelezewa kwa namna hii kote duniani. Hivyo basi, inamlazimu mwandishi huyu, wakiwemo wale wote ambao kwa sasa wanaukubali 'ukweli' ambao kitabu hiki unauelezea, wakiwemo pia wale ambao walikwishabarikiwa kwa kuujua ukweli huu, kumsujudia kwa unyenyekevu Mwenyezi Mungu Mtakatifu ambaye pekee ndiye mwenye "*elimu na ujuzi wa kila kitu*" na "*Ambaye humuelekeza kwenye nuru Yake, yeyote Amtakaye*."

Wale ambao watakataa maelezo ya *Qur'ani* yanayotolewa kwenye kitabu hiki basi wanalazimika aidha kusema kuwa *Qur'ani* haitoi maelezo kuhusu kurudi kwa Wayahudi kwenye

Ardhi Takatifu na kuzaliwa upya kwa Taifa la Israeli, au basi pana maelezo mbadala tofauti na haya yanayotolewa kwenye kitabu hiki, na hapo hapo wanalazimika kutoa maelezo hayo mbadala yanayojitosheleza kuelezea matukio haya yanayotokana na *Qur'ani.*

Wale ambao wanaukana *Uislamu* na kudai kuwa wanamiliki Ukweli nawakaribisha na kuwapa uchochezi watumie huo Ukweli kuelezea jambo hili. Bila kujali kama hilo ni Taifa lenye msimamo wa kidunia usiokuwa wa kiroho unaomkana Mwenyezi Mungu linadai kuwa na huo Ukweli, au kama hiyo ni jumuiya ya kidini na kiroho kama ya Kiyahudi, Kikristo, Kihindu, Kijaini, Kibuddha, Kikonfushasi, Kitao, Kibahai, Kiahmadiya, au jumuiya yenye kusimamia misingi ya elimu na maadili ya utu na ubinaadamu usofungamana na imani za dini, au yenye kupendelea maendeleo na mabadiliko kwa upana wote bila vipingamizi vya aina yoyote, au wale wanaokana kuwapo kwa Mwenyezi Mungu kwa kutoamini au kukosa uhakika wa kumuona wazi mbele ya macho yao, basi madai yao ya kuumiliki Ukweli yangekubalika na kupata uzito na heshima inayostahili ikiwa wangeweza kutoa maelezo ya kina na yanayojitosheleza kuhusu suala hii. Hili linaonyesha kuwa ndilo jambo kubwa linalosimamia umuhimu wa kitabu hiki. Kinathibitisha madai ya dini ya Kiislamu kuwa ni ya, na inamiliki Ukweli!

Qur'ani imeweka wazi onyo kwa walimwengu kuwa dunia hivi sasa itashuhudia hesabu ya siku zilizobaki ikielekea Siku ya Mwisho:

وَٱقْتَرَبَ ٱلْوَعْدُ ٱلْحَقُّ فَإِذَا هِىَ شَٰخِصَةٌ أَبْصَٰرُ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟
يَٰوَيْلَنَا قَدْ كُنَّا فِى غَفْلَةٍ مِّنْ هَٰذَا بَلْ كُنَّا ظَٰلِمِينَ ﴿٩٧﴾

"*Na (onyo lililo kwenye) miadi ya haki (siku ya malipo) ikakaribia: Hapo ndipo yatapo kodoka macho ya walio kufuru (na watasema:) Ole wetu! Bila ya shaka tulikuwa tumeghafilika na haya, bali tulikuwa wenye kudhulumu*."

(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:98)

Wakati Ya'juj na Ma'juj watapoachiliwa huru 'watasongamana na kuteremka kutoka kwenye kila kilima' au 'watasambaa na kutawanyika kuelekea kila upande.' Hii inadhihirisha kuwa kutokana na kuwa na nguvu zisizokuwa na upinzani watachukua na kukamata miliki ya dunia nzima na hapo,

kwa mara ya kwanza kwenye historia ya binaadamu, jamii moja ya watu itatawala dunia nzima. **Hiki kwa hakika ni kipindi hususan katika historia ambacho dunia sasa hivi imekifikia.**

Mfumo wa dunia wa Ya'ajuj na Ma'ajuj utakuwa ni ule wenye *Fasad* (ikimaanisha ugandamizaji, uovu na dhulma). Sura ya al-Kahf imeelezea aina mbili ya tabia na silika za *Fasad* za mfumo huo wa Ya'juj na Ma'juj kuwa zitakuwa tofauti na kinyume ya tabia na silika za mfumo wa dunia wa *Dhul Qarnain*. Nazo ni kama ifuatavyo:

Dhul Qarnain alitumia nguvu (iliyojengwa kwa misingi ya imani ya Allah) kuadhibu mgandamizaji na, katika kufanya hivyo, alijenga uwiano wa moja kwa moja baina ya mfumo wa dunia wa hapa duniani ukaendana na mfumo wa mbinguni wa Mwenyezi Mungu (pakawa na upatanifu na uwiano wa moja kwa moja baina ya hali halisi ya mpito wa hapa duniani na hali halisi ya kiroho). Ya'juj na Ma'juj, kwa upande wa pili, watatumia nguvu zao zisizokuwa na mshindani (zilizojengwa kwa misingi ya kumkana Mwenyezi Mungu) kukandamiza, na kuadhibu wanyonge na wanaogandamizwa. Katika kufanya hivyo watakuwa wanajenga hapa duniani mfumo wa dunia ambao utakuwa unakingana katika kila hali na mfumo wa mbinguni. Pili, mfumo huu utakuwa ni ule ambao wakati wote utashuhudia kuongezeka kwa ugandamizaji.

Dhul Qarnain alitumia nguvu kuwazawadia wale ambao walikuwa na imani kwa Mwenyezi Mungu Mtakatifu ambao walikuwa na mwenendo wa kiadilifu. Ya'juj na Ma'juj watatumia nguvu kwa kufanya kinyume na hivyo. *Dhul Qarnain* alijizuia kutumia nguvu zake na hakufanya lolote alipokutana na watu wasiokuwa na maendeleo walioishi maisha duni hapa duniani. Alionyesha busara na huruma kwa kulinda hali yao na mfumo wao duni wa maisha kwa kuwaacha bila kuwaingilia kwenye maisha na mfumo wao. Ya'juj na Ma'juj, kwa upande wa pili, watatumia nguvu zao kuingilia na kuharibu mfumo wa maisha wa watu wote wenye maisha duni wanaoishi kwa misingi asilia waliyoirithi vizazi na vizazi vilivyopita hapa duniani. Pili, mfumo huo wa maisha utakuwa ni ule ambao daima utakuwa ukishuhudia mashambulizi yatakayoelekezwa kwenye mfumo huo wa maisha wa watu duni mpaka utafikia hatimaye kutoweka.

Ya'juj na Ma'juj watafikia kujenga na kusimamia mfumo wa dunia ambao hautoweza kuepuka kutambuliwa na wale watakaokuwa na muono wa kiroho (uliojengwa kwa imani, tabia, mwenendo na maadili mema) utakaowawezesha kuona uasilia wa, na kiini cha mambo, bila kudanganywa na muonekano wa gamba la nje lenye lengo la kupoteza na kudanganya walimwengu. Ikiwa Wayahudi wamewaruhusu watu hao kuwa mabingwa na wakombozi wao katika kuikomboa

Ardhi Takatifu kwa niaba yao, na hivyo kuwawezesha kurudi Jerusalem, hii itaashiria kuwa Wayahudi walikuwa vipofu wa kiroho.

Toka kipindi cha enzi za kati za Ukristo wa kizungu hadi kufikia enzi hizi za utamaduni wa kisasa wa kimagharibi, bara la Ulaya limekuwa likionyesha ishara zote za kuwa na silika za mfumo wa dunia wa Ya'juj na Ma'juj na pia limetimiza wito na matakwa yao ya kimsingi yanayotokana na silika zao. Bara la Ulaya limepotosha dunia nzima na Ulaya ndiyo iliyowarudisha Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu. Hivyo basi, haya yote ni ishara kubwa mno ya upofu wa muono wa kiroho wa jumuiya ya Kiyahudi ambayo, kwayo, wamruhusu kudanganywa na kuelekezwa kwenye barabara inayowapeleka kwenye angamizo la mwisho litakalofanywa na Ya'juj na Ma'juj.

Mtume (*rehma na amani juu yake*) ametupa kipimo ambacho, kwacho, tunaweza kupima na kufuatilia hesabu za muda uliobaki kuelekea kwenye adhabu ya mwisho kwa Wayahudi. Kwanza, adhabu hii haitotokea hadi pale ambapo Yesu, Masihi wa kweli, atakapomuua *Dajjal*, Masihi wa Uwongo na hadi Allah Mtukufu Mwenyewe atakapowaangamiza Ya'ajuj na Ma'ajuj kwa kutumia silaha za kivita za bayolojia. Kipindi hiki hakitafika na kutokea wakati bado patakuwa na maji yaliyobaki kwenye bahari ya Galilei. Tafakari *hadithi* ifuatayo:

"Amesimulia al-Nawwas ibn Sam'am: …Itakuwa kwenye hali kama hiyo ambapo Allah atambainishia Yesu (*rehma na amani juu yake*) maneno haya: Nimeumba miongoni mwa waja Wangu watu ambao dhidi yao hakuna atakayeweza kushindana na kupigana nao; wachukue watu hawa kwa usalama wapeleke Tur, kisha Allah atawatuma Ya'ajuj na Ma'ajuj na watasambaa na kuteremka kutoka kwenye kila kilima. Wa mwanzo kati yao watapita kwenye ziwa Tiberius (ikimaanisha Bahari ya Galilei) na watakunywa maji yake. Na wakati wa mwisho atakapopita, atasema: Hapa zamani palikuwa na maji. Yesu na washirika wake ndipo watazingirwa hapo Tur (na watabanwa kwa nguvu mno) kiasikichwa cha ng'ombe kitakuwa na thamani kubwa kuliko dinari mia moja…"

(Sahih Muslim)

Hivyo basi ni jambo la umuhimu wa hali ya juu kabisa kuwa tuelekeze uangalifu wetu kwenye kiwango cha maji katika Bahari ya Galilei. Kiambatanishi nambari 1 kinaonyesha hilo. (Kitabu chetu kinachoitwa: *Suratul Kahf na Zama za Kisasa* kitasahihisha, *Insha Allah*, na kujazia mapungufu yoyote yatakayojitokeza katika kulielezea somo la Ya'ajuj na Ma'ajuj katika ufupisho uliomo kwenye surah hii).

SURA YA 11

WAYAHUDI NA WAARABU



"*Hakika utawakuta (mara kwa mara) walio shadidi kuliko watu wote katika uadui kwa walio amini ni Mayahudi na washirikina. Na utawakuta walio karibu mno kwa mapenzi ni wale wanao sema: Sisi ni Manasara. Hayo ni kwa sababu wapo miongoni mwao makasisi na wamonaki, na kwa sababu wao hawafanyi kiburi."*

(*Qur'ani, al-Maida, 5:82*)

Kabla hatujarudi na kuanza kuangalia na kuchunguza moja ya bashira za kuogofya ambayo imekwishakamilika, ikimaanisha kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu atawarudisha Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu wakati ambapo hesabu ya muda wa tukio la adhabu waliyopangiwa itaanza, ni muhimu kwanza kuliangalia somo la 'Ismaili (*rehma na amani juu yake*), Waarabu na Ardhi Takatifu.' Somo hili ni muhimu kwa sababu Shirikisho la Wazayonisti limefanikisha kuundwa kwa Taifa la Israeli baada ya kulazimisha kufukuzwa kwa Waarabu kutoka kwenye Ardhi na nyumba walizokuwa wakimiliki. Wasingeweza kuthubutu kufanya hivyo bila ya kuwa na sababu zenye ushahidi wa andiko. Hata hivyo Ushahidi huo wa Andiko ambao ndiyo walioutumia ulikuwa ni uongo na uzushi uliofanywa kwa jina la Mungu wa Abraham (*rehma na amani juu yake*). Wazayonisti walijua kuwa huo ulikuwa ni uongo na uzushi walioutumia bila kikomo. Ni suala hili ambalo sasa hivi tunalizungumzia.

Mtazamo wa Kidini wa Wayahudi kuhusu Waarabu

Kiongozi wa kidini wa Chama cha Shas chenye hamasa kubwa na msimamo mkali cha Wayahudi wa Sephardi, amesikika akitamka wakati wa hutba yake ya Jumamosi tarehe 5 mwezi wa nane mwaka 2000 kuwa: *"Watu wa kizazi cha Ishmael (Waarabu) wote ni watendamaovu waliolaaniwa, na wote ni maadui wa Israeli. Mtukufu aliye Pekee, Abarikiwe, anajilaumu kwanini*

aliwaumba watu hawa (wa kizazi cha ishmaeli)" Ripoti hiyo ilifafanua jinsi Rabbai Ovadia Yosef alivyokuwa akikejeli jitihada za Serikali ya wakati huo ya Waziri Mkuu wa Israeli Ehud Barak za kutaka kufikia makubaliano na Chama cha Ukombozi cha Palestina kuhusu madai yao ya pamoja ya mji mtakatifu wa Jerusalem. "*Kwanini tuugawe Mji wa Kale?*" alihoji, *"ili wapate fursa nyingine ya kutuua? Kuna sababu gani ya sisi kutaka tuishi nao kama majirani?"* Akimuongelea Waziri Mkuu Barak, Rabbai aliongeza: "*Wewe unatuletea nyoka karibu yetu. Unawezaje kuwa na mkataba wa amani na nyoka?" "Barak"* akaongeza kwa kusema: *"anaenda hovyo kwa kuwafuata kizazi cha Ishmaeli… Atatuletea majoka yaje kuishi jirani nasi hapa Jerusalem. Hana busara."* Gazeti la Jerusalem Post liliripoti kuwa waliokusanyika kusikiliza hotuba ya Rabbai, waliyapokea matamshi yake kwa kumpigia makofi (tazama www.JerusalemPost.com – August 5, 2000).

Moja ya sababu zinazoelezea chuki ya Rabbai kwa wana wa wa Ismaili na kutopendezewa kwake kwa madai yao juu ya Jerusalem ni, kwa uhakika, ukweli kuwa Kitabu cha Mwanzo kinazungumzia kuwa Ishmaeli alikuwa:
"…mtu mkorofi kama punda, mkono wake kupingana na kila mtu, na mkono wa kila mtu kupingana naye."

*(*Mwanzo 16:12)

Hivyo basi, Rabbai na wafuasi wake wanapata fursa ya kudai kuwa ugandamizi unaozidi kuongezeka na usiokuwa na kikomo wanaofanyiwa Waarabu na Taifa la Israeli unapata sababu za kuuhalalisha kwa kutumia kinachodaiwa kuwa ni ujumbe wenye shari wa kiroho unaojumuisha matamko: *"mkono wa kila mmoja kupingana naye."* Vinginevyo, inawezekanaje kwa dunia nzima ya watu waliostaarabika kuelezea matendo ya kikatili na kinyama ya shambulio la Israeli kwenye kambi ya wakimbizi ya Jenin katika Ardhi Takatifu. Laiti kama Wayahudi wasingebadili na kuandika upya na hivyo kuuweka uongo huu dhidi ya Ismaili *(rehma na amani juu yake)*, mtoto wa Abraham *(rehma na amani juu yake)*, ingewawia rahisi kwao kugundua udanganyifu na mtego chini ya mpango wa kishetani wa Wazayonisti kuwanyang'anya Waislamu wa Kiarabu Ardhi Takatifu kwa lengo la kulirudisha Taifa la Israeli.

Maelezo kuhusu Ismaili *(rehma na amani juu yake)*, mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu yanayopatikana kwenye *Qur'ani*, hayabakishi hoja wala wasiwasi wowote kuwa maandiko haya yaliyomo kwenye Taurati ni ya kughushi na uongo dhidi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

وَٱذۡكُرۡ فِي ٱلۡكِتَٰبِ إِسۡمَٰعِيلَۚ إِنَّهُۥ كَانَ صَادِقَ ٱلۡوَعۡدِ وَكَانَ رَسُولٗا نَّبِيّٗا ٥٤

وَكَانَ يَأۡمُرُ أَهۡلَهُۥ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱلزَّكَوٰةِ وَكَانَ عِندَ رَبِّهِۦ مَرۡضِيّٗا ٥٥

"Na pia mtaje katika Kitabu (habari za) Ismaili. Bila ya shaka yeye alikuwa ni mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume (na) Nabii.
Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Sala na Zaka, na alikuwa mbele ya Mola wake Mlezi mwenye kuridhiwa."

(Qur'ani, Maryam,19:54-5)

وَإِسْمَٰعِيلَ وَإِدْرِيسَ وَذَا ٱلْكِفْلِ ۖ كُلٌّ مِّنَ ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿٨٥﴾

وَأَدْخَلْنَٰهُمْ فِى رَحْمَتِنَآ ۖ إِنَّهُم مِّنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ﴿٨٦﴾

Na (kumbuka) Ismaili, na Idris, na Dhul-Kifli - wote walikuwa miongoni mwa (watu) wenye uthabiti na wenye subira. Na tukawaingiza katika Rehema Yetu: Hakika wao walikuwa katika watu Wema.

(Qur'ani, al-Anbiya, 21:85-6)

وَاذْكُرْ إِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ وَذَا الْكِفْلِ وَكُلٌّ مِّنَ الْأَخْيَارِ هَٰذَا ذِكْرٌ وَإِنَّ لِلْمُتَّقِينَ لَحُسْنَ مَآبٍ جَنَّاتِ عَدْنٍ مُّفَتَّحَةً لَّهُمُ الْأَبْوَابُ مُتَّكِئِينَ فِيهَا يَدْعُونَ فِيهَا بِفَاكِهَةٍ كَثِيرَةٍ وَشَرَابٍ وَعِندَهُمْ قَاصِرَاتُ الطَّرْفِ أَتْرَابٌ هَٰذَا مَا تُوعَدُونَ لِيَوْمِ الْحِسَابِ إِنَّ هَٰذَا لَرِزْقُنَا مَا لَهُ مِن نَّفَادٍ

"Na mkumbuke Ismaili, Alyasaa na Dhul-Kifl, wote hao walikuwa katika bora. Huu ni (ujumbe wa) ukumbusho na hakika wachaMungu wana marejeo mema. Bustani za milele zitafunguliwa milango yake kwa ajili yao. Humo wataegemea matakia, wataagiza matunda mengi na vinywaji vizuri. Na pamoja nao wake zao wenye kutuliza macho, hirimu zao. Haya ndiyo mliyoahidiwa kwa Siku ya Hisabu. Hakika hii ndiyo riziki yetu (kwenu) isiyomalizika."

(Qur'ani, Sad, 38:48-54)

وَتِلْكَ حُجَّتُنَآ ءَاتَيْنَٰهَآ إِبْرَٰهِيمَ عَلَىٰ قَوْمِهِۦ ۚ نَرْفَعُ دَرَجَٰتٍ مَّن
نَّشَآءُ ۗ إِنَّ رَبَّكَ حَكِيمٌ عَلِيمٌ ﴿٨٣﴾
وَوَهَبْنَا لَهُۥٓ إِسْحَٰقَ وَيَعْقُوبَ ۚ كُلًّا هَدَيْنَا ۚ وَنُوحًا هَدَيْنَا
مِن قَبْلُ ۖ وَمِن ذُرِّيَّتِهِۦ دَاوُۥدَ وَسُلَيْمَٰنَ وَأَيُّوبَ وَيُوسُفَ
وَمُوسَىٰ وَهَٰرُونَ ۚ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿٨٤﴾
وَزَكَرِيَّا وَيَحْيَىٰ وَعِيسَىٰ وَإِلْيَاسَ ۖ كُلٌّ مِّنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ﴿٨٥﴾
وَإِسْمَٰعِيلَ وَٱلْيَسَعَ وَيُونُسَ وَلُوطًا ۚ وَكُلًّا فَضَّلْنَا عَلَى
ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٨٦﴾
وَمِنْ ءَابَآئِهِمْ وَذُرِّيَّٰتِهِمْ وَإِخْوَٰنِهِمْ ۖ وَٱجْتَبَيْنَٰهُمْ وَهَدَيْنَٰهُمْ إِلَىٰ صِرَٰطٍ
مُّسْتَقِيمٍ ﴿٨٧﴾
ذَٰلِكَ هُدَى ٱللَّهِ يَهْدِى بِهِۦ مَن يَشَآءُ مِنْ عِبَادِهِۦ ۚ وَلَوْ أَشْرَكُوا۟ لَحَبِطَ
عَنْهُم مَّا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿٨٨﴾
أُو۟لَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ ءَاتَيْنَٰهُمُ ٱلْكِتَٰبَ وَٱلْحُكْمَ وَٱلنُّبُوَّةَ ۚ فَإِن يَكْفُرْ بِهَا هَٰٓؤُلَآءِ
فَقَدْ وَكَّلْنَا بِهَا قَوْمًا لَّيْسُوا۟ بِهَا بِكَٰفِرِينَ ﴿٨٩﴾
أُو۟لَٰٓئِكَ ٱلَّذِينَ هَدَى ٱللَّهُ ۖ فَبِهُدَىٰهُمُ ٱقْتَدِهْ ۗ قُل لَّآ أَسْـَٔلُكُمْ
عَلَيْهِ أَجْرًا ۖ إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرَىٰ لِلْعَٰلَمِينَ ﴿٩٠﴾

وَمَا قَدَرُوا۟ ٱللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِۦٓ إِذْ قَالُوا۟ مَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ عَلَىٰ بَشَرٍ مِّن شَىْءٍ ۗ قُلْ مَنْ
أَنزَلَ ٱلْكِتَٰبَ ٱلَّذِى جَآءَ بِهِۦ مُوسَىٰ نُورًا وَهُدًى لِّلنَّاسِ ۖ تَجْعَلُونَهُۥ
قَرَاطِيسَ تُبْدُونَهَا وَتُخْفُونَ كَثِيرًا ۖ وَعُلِّمْتُم مَّا لَمْ تَعْلَمُوٓا۟ أَنتُمْ وَلَآ ءَابَآؤُكُمْ ۖ
قُلِ ٱللَّهُ ۙ ثُمَّ ذَرْهُمْ فِى خَوْضِهِمْ يَلْعَبُونَ ﴿٩١﴾
وَهَٰذَا كِتَٰبٌ أَنزَلْنَٰهُ مُبَارَكٌ مُّصَدِّقُ ٱلَّذِى بَيْنَ يَدَيْهِ وَلِتُنذِرَ أُمَّ ٱلْقُرَىٰ
وَمَنْ حَوْلَهَا ۚ وَٱلَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِٱلْءَاخِرَةِ يُؤْمِنُونَ بِهِۦ ۖ وَهُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ
يُحَافِظُونَ ﴿٩٢﴾

"Na hizo ndizo hoja zetu tulizo mpa Ibrahim (azitumie) kuhojiana na watu wake. Tunamnyanyua kwa vyeo tumtakaye hatua baada ya hatua. Hakika Mola Mlezi wako ni Mwenye hikima na Mwenye ujuzi. Na tukamtunukia (Ibrahim) Is-haq na Yaakub. (Na) Kila mmoja wao (kati yao hao watatu) tulimwongoa. Na Nuhu tulimwongoa kabla. Na katika kizazi chake tulimwongoa Daud na Suleiman na Ayyub na Yusuf na Musa na Harun. Na hivi ndivyo tunavyo walipa wafanyao wema."

"Na Zakaria na Yahya na Isa na Ilyas. Wote walikuwa miongoni mwa watu wema. Na Al Yasaa, na Yunus, na Lut'. Na wote tuliwafadhilisha juu ya walimwengu wote:

"Na kutokana na baba zao, na vizazi vyao na ndugu zao: Na tukawateuwa. Na tukawaongoa kwenye Njia iliyo nyooka. Hiyo ni hidaya ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo humhidi amtakaye katika waja wake. Na lau wangeli mshirikisha yangeli waharibikia yote waliyo kuwa wakiyatenda.

"Hao ndio tulio wapa Vitabu na hukumu na Unabii: Ikiwa hawa (wanaotokana nao) watayakataa hayo, basi tumekwisha yawakilisha kwa watu wasio yakataa.
Hao (mitume) ndio ambao Mwenyezi Mungu amewahidi. Basi fuata hidaya yao. Sema: Mimi sikuombeni ujira. Haya hayakuwa ila ni mawaidha kwa walimwengu wote.

"Na hawakumkadiria Mwenyezi Mungu kwa haki ya kadri yake, walipo sema: Mwenyezi Mungu hakumteremshia mwanaadamu chochote (kwa wahyi). Sema: Nani aliyo teremsha Kitabu alicho kuja nacho Musa, chenye nuru na uwongofu kwa watu? Mlicho kifanya kurasa (tofauti na) kurasa (nyingine) mkizionyesha, na mengi mkiyaficha. Na mkafunzwa mlio kuwa hamyajui nyinyi wala baba zenu? Sema: Mwenyezi Mungu. Kisha waache wacheze katika porojo lao.

"Na hiki ni Kitabu (Qur'ani) tulicho kiteremsha, kilicho barikiwa, chenye kuhakikisha yaliyo tangulia, na ili uuwonye Mama wa Miji na walio pembezoni mwake. Na wenye kuamini Akhera wanakiamini hichi (Kitabu), nao wanazihifadhi Sala zao."

(Qur'ani, al-An'am, 6:83-92)

Rabbai anapaswa agundue kuwa hili ni onyo kali linalotolewa katika Qur'ani kwa wale wote ambao wanamuhusisha Mwenyezi Mungu Mtukufu na uwongo walioutengeneza wao, ikiwemo uwongo unaohusiana na Ismaili (*rehma na amani juu yake*) na kizazi chake:


وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ ٱفْتَرَىٰ عَلَى ٱللَّهِ كَذِبًا أَوْ قَالَ أُوحِيَ إِلَيَّ وَلَمْ يُوحَ إِلَيْهِ شَيْءٌ
وَمَن قَالَ سَأُنزِلُ مِثْلَ مَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ ۗ وَلَوْ تَرَىٰٓ إِذِ ٱلظَّٰلِمُونَ فِي غَمَرَٰتِ
ٱلْمَوْتِ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ بَاسِطُوٓا۟ أَيْدِيهِمْ أَخْرِجُوٓا۟ أَنفُسَكُمُ ۖ ٱلْيَوْمَ
تُجْزَوْنَ عَذَابَ ٱلْهُونِ بِمَا كُنتُمْ تَقُولُونَ عَلَى ٱللَّهِ غَيْرَ ٱلْحَقِّ وَكُنتُمْ
عَنْ ءَايَٰتِهِۦ تَسْتَكْبِرُونَ ﴿٩٣﴾

"Nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye mzuliya uwongo Mwenyezi Mungu, au anaye sema: Mimi nimeletewa wahyi; na hali hakuletewa wahyi wowote, au (pia) na yule anaye sema: Nitateremsha kama alivyo teremsha Mwenyezi Mungu? Na lau ungeli waona madhaalimu wanavyo kuwa katika mahangaiko ya mauti, na Malaika wamewanyooshea mikono wakiwambia: Zitoeni roho zenu! Leo mtalipwa adhabu ya fedheha kwa sababu ya mliyokuwa mkiyasema juu ya Mwenyezi Mungu yasiyo ya haki, na mlivyo kuwa mkizifanyia kiburi Ishara zake."

(Qur'ani, al-An'am, 6:93)

Rabbai, pamoja na wale wote ambao imani zao zinatokana na aya za kughushi zilizomo kwenye Taurati, wanaishi kwenye ulimwengu wa kusadikika. Utambuzi na ufahamu wao wa hali halisi au kile wanachodhani ni ukweli hauna mashiko na ni mpotofu. Uharibifu uliotokea ni kuwa pametengenezwa, na inaendelea kushikiliwa na kuaminika kuwa, ubaya wa imani potofu inayomhusu Ismaili (*rehma na amani juu yake*). Na hakuna sehemu yoyote ambayo Taurati inatoa Ushahidi wa ubaya wa tabia, mwenendo au upinzani unaoonyeshwa na Ismaili ambao ungeonyesha kuthibitisha maneno makali ya lawama na ubaya wa tabia zake kama unavyoonyeshwa na hizo zinazodaiwa kuwa aya zilizopokelewa kwa wahyi kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Badala yake, wana wa Ismaili ambao Rabbai kwa chuki na dharau anawaita 'nyoka' ndiyo waliowakarimu na kuwasitiri Wayahudi kwa

kuwapa ruksa na haki ya kuishi miongoni mwao kwa miaka elfu mbili. Waliweza kuishi kwa amani, usalama wa mali zao na pia waliruhusiwa kuendesha maisha yao ya kila siku ikiwemo ibada zao kwa mujibu wa imani yao kama Wayahudi.

Wale ambao waliunga mkono, na wanaoendelea kuunga mkono kuundwa kwa Taifa la Kitapeli la Israeli (nchi yenye msimamo, sera na mwelekeo wa kidunia, siasa kali za kizalendo na kiujumla yenye msimamo usioshikamana na kanuni za sheria za Mwenyezi Mungu) lenye misingi ya uonevu, ugandamizaji, ni watu ambao hawana na wanakosa kabisa muono wa kina wa kiroho. Upofu huo huo wa kiroho, ambao unawasababishia kutoona Utapeli wa Taifa hilo, ambalo kila kukicha linawaelekeza kwenye mteremko wa mto kwenda bondeni ambako hakuna marejeo, ndio uliowafanya wadai kuwa Maryam amefanya zinaa, na Yesu (Masihi) alikuwa mtoto wa nje ya ndoa na madai yake kuwa ni Masihi ni ya uongo. Ndiyo uliowafanya watende tendo la aibu na kikatili kuliko yote katika historia, tendo la kujaribu kumsulubu Yesu (*rehma na amani juu yake*), na kisha kujisifu kuwa wamefanikiwa kumuua. Upofu huo wa kiroho pia umewasababishia kumkana na kumkataa Mtume wa mwisho aliyeletwa kwa binaadamu wote na Mungu wa Abraham, Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*). Imewasababishia kuikataa *Qur'ani*, kuwa ni neno la Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tabia zao za kibaguzi, mwenendo wao kuhusiana na masuala ya fedha, uchumi yote yanachukiza na yanaonekana wazi kabisa kuwa hayana uhusiano wowote na makatazo yaliyomo kwenye misingi ya imani za kidini.

Walipomtukana nabii Musa (*rehma na amani juu yake*), muda mrefu uliopita, kwa kumwambia kuwa yeye na Mungu wake wanapaswa wakapigane wenyewe (kuikomboa Ardhi Takatifu), wakati wao wangebaki pale pale walipokuwa, Mwenyezi Mungu Mtukufu alijibu kebehi na utovu wao wa imani na nidhamu kwa kuifanya Ardhi Takatifu kuwa *Haram* (iliyokatazwa) kwao kwa miaka 40, kwa kuwafanya wazurure hovyo wakipita sehemu mbalimbali ardhini. Baadaye Mwenyezi Mungu Mtukufu alizungumza na Nabii Musa (*rehma na amani juu yake*) na kumwambia: "*Usisononeshwe na watu hawa waliojaa madhambi*." Hakuna nafasi ya huruma kwenye maneno hayo. Hata kama dunia isingekuwa imeshushiwa *Qur'ani* inayoonyesha wazi kuwa baadhi ya aya kwenye Taurati ni za kughushi, muono wa kiroho ungewatosheleza wafuasi wa Taurati na Biblia kuhisi na kugundua kuwa pana mgogoro miongoni mwa aya kama hizo zinazohusiana na Ismaili.

Hivyo basi hawakustahili kuonewa huruma wakati ule, na hakika kwa sababu hizo hizo hawastahili kuonewa huruma hivi sasa. Muda wao umetimia. Hatma yao imeshaamuliwa na kufungwa. Wamedanganywa na kuingizwa kwenye upotofu ulio mkubwa kuliko mapotofu yote

ambayo dunia na historia imeshawahi kushuhudia, wamedanganywa kwa kuacha makazi walimokuwa wakiishi kwa amani, utulivu na uhuru wa kuabudu kwa mujibu wa imani yao ya kiyahudi miongoni mwa vizazi vya Ismaili kwa miaka elfu mbili (huko Yemeni, Moroko, Egypt, Irani, Iraq, Syria, n.k.) na kurejea kwenye Ardhi Takatifu bila kugundua kuwa wanajiingiza kwenye kuunga mkono uonevu na ugandamizaji. Na kama kawaida ya nuksi ilivyo, uonevu na ugandamizaji huo unaongezeka siku hadi siku. Hawakuhadaiwa na Waislamu. Pia, hawakualikwa na Waislamu warejee. Qur'ani inasema wazi kuwa ni Mungu wa Abraham ndiye aliyeamuru. Mungu huyo huyo, Mtukufu, ambaye tayari mara mbili alikwishaliteketeza Sinagogi (*Masjid*) lililojengwa na Nabii Suleyman (*rehma na amani juu yake*) ndiye atakayehakikisha kuteketezwa kwa Taifa la Kitapeli la Israeli. Lengo la kitabu hiki ni kumuelekeza msomaji kwenye mtazamo wa *Qur'ani* pale inapozungumzia Jerusalem na kuteketezwa kwa Taifa la Israeli. Siku tukio hilo litakapotokea, na hakuna kipingamizi kuwa litatokea, adhabu kubwa kuliko adhabu zote za Mwenyezi Mungu juu ya binaadamu katika historia yote itakuwa imejidhihirisha mbele ya macho yao yatakayokuwa yamejawa na mshtusho, woga na mshangao mkubwa. Rabbai, pokea onyo!

Upotofu huo huo wa utambuzi wa hali halisi ambao unaonekana wazi kwenye matamshi ya Rabbai pia unaonyeshwa na pande mbili zilizojikita kwenye majadiliano, yasiyokuwa na tija, kuhusu hatma ya Jerusalem na Ardhi Takatifu, ikimaanisha chama cha Ukombozi wa Wapalestina (PLO) na Taifa la Israeli. Kwa upande wao, wote kwa pamoja, wanadhihirisha kutofahamu kabisa, au kutojali hata kidogo, miongozo inayopatikana kwenye *Qur'ani* na Taurati kama vyanzo vya maelekezo kuhusiana na suala hilo. Wanaonyesha kuwa na alama nyingi zinazoshabihiana baina yao, kuliko vile ambavyo kila mmoja ana uhusiano na dini ya *Kiislamu* au Kiyahudi. Wote ni ushirika wa kitaifa wenye mwelekeo na msimamo wa kidunia na unatumia dini kama kisingizio katika kufuatilia na kutekeleza malengo ya kitaifa na kidunia yasiyokuwa na lengo la kumuweka Mwenyezi Mungu na sheria zake kama msingi wa msimamo wao mkuu na wa awali. Msimamo wa kidunia hauna mahitaji ya kutafuta Ukweli Halisi. Mungu wanayemuabudu ni yule mungu ambaye wao wenyewe wanayemuumba na kumtengeneza upya, kila mara panapohitajika. Na maadili yao, yanayotokana na mahitaji ya kipindi husika, yanatengenezwa upya kila mara kutegemeana na mabadiliko ya mahitaji na malengo yao kidunia ya wakati husika.

Huenda pakapatikana suluhisho lenye werevu mkubwa ndani yake litakalotimiza matakwa ya Wapalestina ya kupewa na kutawala Mashariki ya mji wa Jerusalem pakiwa kama Makao Makuu ya Tiafa lao la Palestina. Lakini ikiwa, na hapo hilo litakapotokea, Taifa hilo la Kipalestina litakuwa ni kama nakala halisi ya Taifa la Israeli la kidunia lisilomtambua na linalomkana Mwenyezi Mungu.

Ardhi Takatifu hapo itakuwa imedhihirisha kuwa ni sehemu ya mfumo mpya wa dunia ya *shirk* inayotokana na utamaduni wa kimagharibi. *Shirk* inajitokeza na kufanyika pale ambapo Taifa, au sehemu nyingine yoyote, badala ya Mwenyezi Mungu, inajipachika yenyewe mamlaka ya juu kabisa ya kutunga na kusimamia sheria za Nchi au Taifa na kuzipa nguvu na mamlaka ya kuwa sheria kuu zinazofuatwa na kutekelezwa!

Onyesho kubwa kuliko yote la *Shirk* lililokosa kabisa hata chembe ya aibu ni pale ambapo Serikali ya Marekani ilipotoa pendekezo la kusuluhisha mgogoro wa misimamo inayopingana baina ya Serikali ya Israeli na Chama cha Ukombozi wa Palestina (PLO) kuhusu eneo ambapo upo msikiti *Masjid* uliojengwa na Nabii Suleyman, kwa sasa ukijulikana miongoni mwa Waislamu kama *al-Haram al-Sharzf*, na miongoni mwa Waisraeli ukijulikana kama Hekalu la Mlimani (Temple Mount). Pendekezo la Marekani lingewapa haki Serikali ya Israeli ya kuwa na 'uhuru' juu ya ukuta wa Magharibi (au 'Ukuta wa Kilio'). Wayahudi wanautambua huu ukuta kama mabaki ya hekalu la awali (*Masjid)* lililojengwa na Nabii Suleyman Upande wa pili, Taifa la Kipalestina lingepatiwa uhuru juu ya mamlaka ya *Masjid Al-Aqsa* na *msikiti wa Umar* (pia linalojulikana kama 'Kuba juu ya Jiwe' – Dome over the Rock). Na Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) angelazimika kuridhika na 'uhuru' juu ya sehemu zilizobaki za *al-Haram al Sharzf* (au eneo lililozungukwa na ukuta kwa wale ambao katika kulitamka jina la Kiarabu kunawanyima raha). Nadhani shetani mwenyewe binafsi alikuwa mshauri kwenye hiki kikao wakati pendekezo hili linatayarishwa.

Shirk inajitokeza na kutendwa pale ambapobTaifa linajipa mamlaka ya kupanga na kutangaza kuwa Halal kile ambacho Mwenyezi Mungu ameamrisha na kukataza kuwa *Haram* na kinyume cha hapo, yaani kugeuza na kufanya *Haram* kile ambacho Allah Mtukufu ameamrisha kuwa *Halal*. Ina uhakikakama vile jua linavyoangaza kuwa Serikali inayokusudiwa ya Wapalestina ingeruhusu kamari na bahati nasibu nap engine hata kuanzisha na kufadhili mchezo wa bahati nasibu kitaifa. Ingeruhusu *Riba,* ikimaanisha kukopesha na kukopa pesa kwa faida inayotokana na *Riba*. (*Tazama kitabu chetu kinachohusu Riba, kwa maelezo ya kina kuhusu somo hili)*. Pia ingeruhusu matumizi na unywaji wa pombe. Kwa maneno mengine, Serikali ya Wapalestina ingekumbatia *Shirk* sawa sawa na Taifa la Israeli na dunia nzima ilivyokumbatia hivi sasa (yakiwemo mataifa mengi ya Kiislamu), kitu ambacho tayari kimekwishatokea na tunakishuhudia. Taifa la Wapalestina chini ya uongozi wa PLO pia lingesimamia kushuka kwa maadili ya jamii yake yote, kama vile inavyotokea kwenye Taifa la Israeli lenye mwelekeo na msimamo wa kidunia jambo ambalo limesambaa pia kote duniani.

Waislamu hawawezi, na hawapaswi, kuunga mkono makubaliano ya aina yoyote kama vile Pendekezo la Saudia, ambalo lina lengo la kuhalalisha Taifa la Israeli lenye muundo wa kidunia na kukubali miaka yake hamsini ya ugandamizaji wa haki za watu wa Palestina, wakiwemo Wakristo na Waislamu. Pia Waislamu wasikubali kuundwa Taifa la Kipalestina lenye kushabihiana na Taifa la Kiyahudi kwenye Ardhi Takatifu. Katika kutoa sababu za ziada kuhusu msimamo wetu huu tumeandika makala kuhusu suala hili la Jerusalem na hatma yake, likiangaliwa kwa mtazamo wa *Qur'ani*. Maelezo ya kina Zaidi yanapatikana kwenye kitabu chetu: *"Dini ya Abraham una Taifa la Israeli – Mtazamo wa Qur'ani"*

Kitabu hiki pia kina lengo la kutoa maelezo kuhusu hali halisi ambapo Wayahudi bila kufanya udadisi wa kina wa kidini na kiroho na kutumia maarifa, hekima na busara, wameikubali Israeli yenye msimamo wa kidunia unaomkana na usiomtambua Mungu kuwa ndiyo sawa na lile Taifa tukufu la Israeli lililoanzishwa na Nabii Daud (*rehma na amani juu yake*) na Nabii Suleyman (*rehma na amani juu yake*). Taifa hili la Israeli ni la kilaghai na limewadanganya Waisraeli. Dr. Ismail Raji al-Faruqi, mwanazuoni wa Kiislamu mwenye asili ya Palestina ambaye alikuwa akiishutumu sana Israeli, ambaye aliuawa katika mazingira ya sintofahamu, aliielezea Israeli kuwa ni "shirikisho la kikoloni", "lililozaliwa kwa dhambi", "lililoanzishwa kwa misingi na malengo na mfumo wa utaifa uliopitwa na wakati" na "mgandamizaji wa kijeshi wa jamii asilia." (Tazama kitabu chake kizuri na maarufu: '*Uislamu na Tatizo la Israeli'*. Wakazi na wenyeji asilia wa Kiarabu ambao waliondolewa toka kwenye majumba yao, au ambao walilazimika kukimbia kwa hofu, walikuwa ni watu ambao wanamuabudu Mungu wa Abrahamu. Lakini, hata baada ya Waisraeli kujihakikishia utawala na mamlaka ya Ardhi takatifu, bado wanakataa kuwakaribisha au pia kuwaruhusu wakimbizi hao warudi majumbani mwao. Hadi leo hii, Zaidi ya miaka hamsini baadaye, Taifa la Kiisraeli linakataa kabisa kuruhusu wkimbizi kwenye makazi yao wakati huo huo linaendelea kuweka mualiko ulio wazi kwa Wayahudi, kutoka popote walipo duniani, waje kuishi kwenye Ardhi Takatifu. Huu siyo mwenendo wala tabia nzuri. Ni mwenendo na tabia ya Kishetani!

Utabiri wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) unaashiria kuwa Taifa la Kizayonisti la Israeli hatimaye litawasaliti Banu Israel na kuwatupa mbele ya watu hao hao ambao wamekuwa wakionewa na kugandamizwa bila kuficha na Waisraeli katika namna na hali inayokosa kabisa hisia za aina yoyote za kuona aibu zilizojaa chuki.

Yassir Arafat naye anajipachika na pia hawawakilishi wale ambao wamenyang'anywa nyumba na makazi yao, na ambao wamekuwa wakinyanyaswa kwa Zaidi ya miaka hamsini. Hao ni

Wapalestina ambao wameondolewa bila haki kutoka Palestina. Wameishi kwenye kambi za wakimbizi nchini Lebanon na sehemu nyingine kwa Zaidi ya miaka hamsini. Arafat atawasaliti kama vile ambavyo Israeli imeshaanza kuwasaliti Wayahudi. Wale ambao watakuwa wamesalitiwa na Arafat hatimaye wataishia kuwa chini ya mamlaka ya jeshi la Kiislamu ambalo litawakabili na kuwapa adhabu Wayahudi wakazi wa Ardhi Takatifu pale ambapo Taifa la Israeli litakapowakimbia. Jeshi hilo la Kiislamu tayari limeshaonyesha nguvu zake za mapambano kusini mwa Lebanon. Na kujiondoa kutoka Kusini mwa Lebanon kwa jeshi la Israeli ambako kumeliacha jeshi lake la kambo la Kikristo katika eneo hilo (baada ya jeshi hilo kupigana kwa niaba ya Israeli) ni mwanzo tu wa matukio yenye hamasa kubwa yatakayojitokeza.

Ubaguzi wa kimbari wa kizazi cha Ismaili unaofanywa na Taifa la kidunia la Israeli umeongezeka kwa kasi kubwa na kuzidi kudidimiza hali ya ugandamizaji wa kidini, kisiasa na kiuchumi kwenye Ardhi Takatifu. Ugandamizaji huo unazidi kuongezeka siku hadi siku. Ni katika hali na misingi hii ndipo tunaweza kuelewa vizuri utabiri mchungu wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ambaye alitamka:

"Kwa hakika mtapigana na Wayahudi, na hakika mtawaua. (Na hali hiyo itaendelea) hadi (hata) mawe yataongea (na kusema): Enyi Waislamu! Kuna Myahudi amejificha nyuma yangu hivyo njoo na umuue.:

(Sahih Bukhari)

Sura ya 12

MAELEZO YA QUR'ANI KUHUSU KUREJEA KWA WAYAHUDI KWENYE ARDHI TAKATIFU

وَقُلِ ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ سَيُرِيكُمْ ءَايَٰتِهِۦ فَتَعْرِفُونَهَا ۚ وَمَا رَبُّكَ بِغَٰفِلٍ عَمَّا تَعْمَلُونَ ﴿٩٣﴾

"Na sema: Alhamdu Lillahi, Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu. Yeye atakuonyesheni Ishara zake, na mtazijua. Na Mola wako Mlezi si mwenye kughafilika na yote yale myatendayo."

(Qur'an, al-Naml, 27:93)

Tunaishi kwenye kipindi ambacho Wayahudi wamerejea Jerusalem na *kujirudishia* Ardhi Takatifu baada ya ukimbizi kwa amri ya Mwenyezi Mungu uliowaondoa hapo kwa karibu miaka elfu mbili (2000). Leo hii Jerusalem inashamiri. Ina uwezo na nguvu zinazoiwezesha kuathiri matukio kweny eneo lote la jirani ambapo Ardhi Takatifu ipo. Taifa la Israeli limefanikisha na kuigia mikataba ya 'amani' na nchi-wateja wan chi za kimagharibi zisizomtambua Mungu kama vile Egypt na Jordan. Israeli pia imetiliana saini mikataba kadhaa ya nyongeza na Chama cha Ukombozi wa Palestina (PLO) ambayo imepelekea kufifilika kwa upinzani wake dhidi ya uundwaji wa Taifa la Israeli katika Ardhi Takatifu. Na hata pia Saudi Arabia imeingia kwenye hilo hilo kumbatio la Israeli lakini ilifanya hivyo kwa siri kubwa hadi ilipojitokeza kwenye pendekezo lake la 'Mpango wa Saudi' ambao unajumuisha *kulitambua* Taifa la Kiyahudi.

Wakati huo huo mji wa Madina umerudi nyuma katika kila uwanja, na unakosa umuhimu wowote wa kuweza kuathiri maendeleo katika ghuba, mashariki ya kati au duniani. Mbaya zaidi kwa Madina, ni kuwa Taifa la Saudia ambalo ndilo lenye mamlaka juu yake, taifa lililoibuka baada ya kuteketea kwa Khalifa, liliundwa kwa lengo la kuwa taifa-mteja la Uingereza. Wakati Marekani ilipoipiku Uingereza na kuchukua nafasi yake kama *Taifa Tawala* la dunia, Taifa la Saudia likawa taifa-mteja wa Marekani. Saudi Arabia, kama ilivyo Israeli, tangu mwanzo wa kuwapo kwake, limekuwa likitegemea kwanza Uingereza na baadaye Marekani ili kuweza kuendelea kuwapo.

Ushirika wa *Wahhabi wa Saudia* ambao ndiyo unaoshikilia madaraka na mamlaka kwenye siasa na dini nchini Saudi Arabia umefanikiwa kuilinda hiyo hali ya taifa-mteja tangu mwaka 1916 wakati Abd al-Aziz ibn Saud alipokubali pendekezo na ahadi ya Waingereza ya paundi 5000 kila mwezi ikiwa ni ujira wa kuwa mshirika ambamo ungeiwezesha Uingereza kutekeleza lengo lake la kuichomoa na kuchukua mamlaka juu ya Hejaz kutoka kwenye utawala wa Khalifa wa Kiislamu wa Ottoman. Umoja wa kidini wa *Wahhabi* uliweza kuhimili hali hii ya kuwa taifa-mteja na mataifa ya Kikristo na Kiyahudi ya magharibi kwa sababu umoja huo siku zote ulikuwa na imani kuwa Wayahudi na Wakristo wako karibu nao zaidi kuliko umma uliobaki wa Waislamu. *Wahhabi* wanawaona Waislamu wasiokuwa wa *ki-Wahhabi* kuwa si waumini kwa kuwa wanawashutumu kwa kutenda *Shirk* (Tazama kitabu chetu: '*Khalifa, Hejaz na Taifa la Wahhabi wa Saudia.*')

Taifa la Israeli lilizaliwa katika mazingira sawa sawa kabisa na hayo, likiwa kama taifa-mteja wa mataifa ya magharibi. Hata hivyo, kuna tofauti ya kimsingi baina ya mataifa-mteja haya mawili, Israeli na Saudi Arabia. Taifa la Israeli linaelekea kwenye kujing'oa kutoka kwenye uhusiano wa taifa-mteja na (kwanza) Uingereza na baadaye Marekani, na pia hatimaye kujitokeza kama *Taifa Tawala* la dunia. Hilo litakapotokea, Saudi Arabia itakuwa taifa-mteja wa Israeli. Wakati huo, Jerusalem itakuwa ikishamiri na Madina itakuwa kama gofu (ikimaanisha kuwa itakuwa chini ya mamlaka na uongozi wa Taifa la Israeli).

Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alikwisha bashiri kuwa hili litatokea siku moja. Isipokuwa utabiri huu unaambatana na ahadi ya onyo kwa Israeli:

"Amesimulia Mu'adh ibn Jabal: Mtume (*rehma na amani juu yake*) alisema: Wakati Jerusalem itakapokuwa na hali ya kushamiri, mji wa Yathrib (ambayo ndiyo Madina ya leo hii katika Saudi Arabia) itakuwa imefifia, na hali ya kuangamia kwa Yathrib na kuwa kama gofu itatokea itakapojizi vita kuu, na matokeo ya vita kuu itakuwa wakati wa kuiteka Konstantinopol na kutekwa kwa Konstantinopol kutatokea wakati wa kujitokeza Dajjal (Mtume wa Uongo). Yeye (mtume) aliligusa paja au bega lake kwa mkono na kusema: Huu ni ukweli kama vile ambavyo wewe upo hapa au umekaa hapa (akimaanisha Mu'adh ibn Jabal)

(Sunnah Abu Daud)

Kung'ara kwa mji wa Jerusalem leo hii ambako kunaifunika na kutawala miji yote katika eneo hilo la Mashariki ya kati kwa kifupi kunauthibitisha utabiri huu. Tayari Israeli imekwisha kaidi azimio la Umoja wa Mataifa na pia kumkaidi Raisi wa marekani ambapo wote walidai Israeli iondoe majeshi yake kutoka maeneo ya Wapalestina ya Ukanda wa Magharibi. Hii ilikuwa baada ya Israeli

kujibu mashambulizi ya mfululizo wa Wapalestina waliokuwa wakijivisha mabomu na kujiripua (ambao ni *shuhada* na hawapaswi kuitwa walioamua kujiua kwa mabomu). Lakini haya yataongezeka wakati Israeli itakapoanzisha na kupigana kwenye vita kubwa kuliko zote, vita ambayo inatarajiwa kutokea na pande zote (isipokuwa, labda, Raisi wa Marekani). Vita hiyo itawawezesha Waisraeli kutanua himaya yake na kumiliki ardhi kwa eneo kubwa kuliko ilivyo sasa. Utabiri huu wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ndipo utakapokuwa umeeleweka kikamilifu.

Kuanguka kwa uchumi wa Marekani, ambako kuna ishara zote kuwa kutatokea, na kufanikishwa kwa ukaidi wa amri yake kwa Israeli kutaka kurudisha ardhi iliyoiteka katika vita kutakamilisha kabisa utabiri huu. Hivyo hivyo hali ya Yathrib (ikimaanisha Madina) kuwa imeathirika na kubaki kama gofu tayari kumeshatokea kwani kwa jinsi ilivyo hivi sasa kuwa na uhusiano unaoiweka kuwa kama ni nchi-mteja wa Marekani, nchi ambayo haina msimamo wa kumuweka Mungu mbele, ni jambo lisiloyumkinika ukitilia maanani kuwa Madina iko katikati ya eneo ambalo ni chimbuko la *Uislamu.* Pindi Israeli itakapochukua nafasi ya Mtawala wa Dunia na Taifa la Saudi litakpokuwa tifa-mteja wa Israeli, utabiri huu utakuwa umetimia kikamilifu. Tokeo la kukamilika kwa utabiri huu wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) unaopatikana kwenye hadithi hii ni kuwa Waislamu sasa watakuwa wanakabiliwa na vita kuu ambayo Israeli, huenda, wakaianzisha pamoja na majeshi ya Uturuki ya Kemal. Mtume (*rehma na amani juu yake*) pia ametabiri vita ya Waislamu na uturuki ambayo majeshi yake wakati huo yatakuwa yakitumika kama chombo cha Waisraeli:

"Amesimulia Abu Hurairah:
Mtume alisema: Saa haitotimia hadi kwanza mpigane na taifa linalovaa viatu vyenye manyoya, na hadi mpigane na Waturuki, ambao watakuwa na macho madogo, nyuso nyekundu na pua zilizo bapa, na nyuso zao zitakuwa kama ngao bapa. Na mtagundua kuwa watu bora zaidi ni wale ambao hawapendi kabisa majukumu ya kutawala hadi wanapochaguliwa wawe watawala. Na watu wako wa aina tofauti: Waliokuwa bora zaidi wakati wa zama za kabla ya kuja Uislamu ndiyo hao hao watakuwa bora zaidi kwenye Uislamu. Utafika muda ambapo yoyote kati yenu atapenda zaidi anione mimi kuliko kuwa na familia yake au kuongeza mali zake maradufu."

(Sahih, Bukhari)

Vita hiyo huenda ikaanza kwa mashambulizi ya Uturuki dhidi ya Syria ambayo yangetumika na Israeli kama chanzo cha kuteketeza eneo kubwa katika Mashariki ya kati. Lakini mwisho wa yote Taifa la Israeli litaibuka kama taifa tawala la dunia. Ni katika kipindi hicho ndipo ambapo *Dajjal* naye ataibuka *katika siku ambayo itakuwa sawa na siku yetu*, ikimaanisha kuwa atajitokeza katika masijala

na bayana yetu au katika muda na uhalisi huu wa dunia yetu hii kama tuijuavyo sisi. Wakati *Dajjal*, masishi wa Uongo atakapojitokeza ndipo pia utakuwa wakati ambapo Masihi wa Kweli, mwana wa Maryam, atakaporejea. Naye atamuua *Dajjal*, na ndipo jeshi la Kiislamu litaliteketeza Taifa la Israeli.

Qur'ani imetabiri kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu na pia imeelezea matokeo yake. Pia kuna aya nyingi za *Qur'ani* na tabiri nyingine nyingi ikiwemo misemo ya Mtume (*rehma na amani juu yake*) ambayo inaashiria vipi Jerusalem itaishia kuwa. Je, ni aya zipi hizo za *Qur'ani* zinazosema hayo? Na ni hadithi zipi za Mtume (*rehma na amani juu yake*) zinabashiri matukio na hatma ya Jerusalem kwa muda ujao? Msomaji anapaswa aelekeze akili, fikra na umakini wake kwenye misemo kumi ifuatayo kwani inajumuisha kiini cha yale ambayo *Qur'ani* inayasema kuhusu hatma ya Jerusalem:

Qur'ani na *Ahadith* zote zinathibitisha kuwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) siku moja atarudi duniani. Na wakati wa marejeo yake, Wayahudi hawatokuwa na jinsi nyingine zaidi ya kumuamini kuwa yeye ni Masihi. Kisha ndipo watakapoteketezwa, isipokuwa kifo chao kitakuwa cha taabu kubwa, ikimaanisha watakufa wakiwa na uhakika kuwa walikuwa wamedanganywa na 'ukweli' ambao walikuwa wameung'ang'ania na kuukumbatia kwa ukaidi na maringo mengi kumbe ulikuwa ni 'uongo' wakati ujumbe wa Yesu (*rehma na amani juu yake*) na ule wa Muhammad (*rehma na amani juu yake*) walioukataa kuwa ni 'uongo' na kumbe ndiyo 'ukweli." Hivyo basi watakuwa wanakufa na huku wanajua fika kuwa makazi yao ni moto wa Jehannamu.

Baada ya kujigamba kuwa wamemsulubu Yesu (*rehma na amani juu yake*), Allah aliwafukuza kutoka katika Ardhi Takatifu. Wakati huu, hata hivyo, kufukuzwa kwao kulitofautiana na kufukuzwa kulikowatokea kabla yake wakai walipopelekwa Babylon kama watumwa. Kipindi hiki jamii zao zilikuwa zikivunjwavunjwa katika vipande na vikundi vidogo vidogo na kusambazwa dunia nzima miongoni mwa wakazi wa dunia. *Qur'ani* ndipo ikaendelea na kufunua hatma ya Jerusalem kwa kusema na kuweka wazi kama ifuatavyo:

- Mtawanyiko wa Wayahudi kwa vikundi vikundi kujikuta wamesambaa dunia nzima,
- Wayahudi kupigwa marufuku (kuzuiwa) kurejea kwenye Ardhi Takatifu,
- Uwezekano wa Wayahudi kusamehewa na Allah, Mwingi wa Rehma, ikiwa watamuamini Mtume (*rehma na amani juu yake*) ambaye atakuwa 'Ummi' (asiyejua kusoma na mgeni asiye na asili ya Kiyahudi),
- Kurejea kwao kwenye Ardhi Takatifu kwa amri ya Mungu wakati wa kipindi cha 'Nyakati za Mwisho' (awamu ya mwisho ya Zama za mwisho au Kipindi cha Mwisho)

- Ya'juj na Ma'juj ndiyo wahusika watakaowrudisha Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu,
- Onyo kwa Wayahudi kuwa adhabu ya Mwenyezi Mungu kwao inaweza kurudiwa,
- Onyo kwa Wayahudi kuwa adhabu itakuwa kali kuliko adhabu yoyote iliyokwishawahi kutolewa,
- Upofu wa (mtazamo wa) kiroho wakati muda wa adhabu ya mwisho utakapotimia,
- Mwili wa Fir'auni (wa Kutoka) utapatikana ukiwa haujaharibika na utadhihirisha kuwa Wayahudi watatokewa na jambo hilo hilo lililomtokea Fir'auni,
- Wayahudi hawatokuwa na jinsi wala uchaguzi mbadala zaidi ya kumuamini Yesu (*rehma na amani juu yake*) kuwa ni Masihi pale atakaporejea isipokuwaitakuwa tayari wamekwishachelewa kuweza kupata uokozi kutoka kwenye adhabu kali ya moto.

1. **Mtawanyiko wa Wayahudi vikundi vikundi kusambaa dunia nzima**.

Wakati Mwenyezi Mungu Mtukufu alipowaondoa Wayahudi kutoka katika Ardhi Takatifu baada ya kumkataa Masihi na kufanya jaribio la kutaka kumuua, Alitoa tamko lililoonyesha kuwa jamii hii mpya iliyotawanyika duniani itakuwa tofauti na ile jamii ya zamani (iliyokuwa Babilonia). Wakati ule, Wayahudi walikuwa ni jamii ya aina moja wakiishi kwenye eneo moja la kijiografia (Babylonia). Lakini wakati wa kuondolewa kwao kwa mara ya pili kutoka kwenye Ardhi Takatifu, Mwenyezi Mungu Mtakatifu Alisema kuwa mara hii watakuwa ni jamii tofauti baada ya tukio hilo la kusambaratishwa:

"Na Tuliwasambaza wao kama jamii kwenye makundi tofauti duniani…"

(Qur'ani, al-Araf, 7:168)

Tamko hili la *Qur'ani* lilitimia kwa ukamilifu wake wote wakati, baada ya miaka elfu mbili, Wayahudi walibaki wametawanyika duniani kote. Waliishi katika kipindi hiki kirefu Yemen, Moroko, Iraq, Iran, Egypt, Jordan, Libya, Ethiopia, Arabia, Syria, Turkey n.k.

Kutawanyika huku kwa kiajabu kwa vikundi vikundi vya Wayahudi duniani kwa miaka elfu mbili kulitakiwa kueleweke kuwa ni ishara kwa Wayahudi ya hasira ya kiroho na adhabu kwao, na Wayahudi wengi waliutambua mtawanyiko huo kuwa ndiyo maana yake.

2. Wayahudi kuzuiwa kurejea kwenye Ardhi Takatifu na kuichukua kuwa iwe mali yao

Baada ya kuwaondoa Wayahudi kutoka kwenye Ardhi Takatifu, Mwenyezi Mungu aliweka kizuizi juu yao cha kuwazuia wasiweze kurudi kwenye Ardhi hiyo. (Waliweza kuja kama watalii lakini hawakuweza kurudi na kuichukua au kudai kuwa Ardhi hiyo ni ya kwao). Kizuizi hicho kimetokea kuwa ukweli wa kihistoria na kimeendelea kuwapo wazi kwa miaka elfu mbili kiasi kila kila mtu amepata fursa ya kushuhudia. Na jambo hili pia ni uthibitisho wa kishindo kikubwa wa tamko la *Qur'ani* lililomo kwenye *Surah al-Anbiyah*:

"*Tumepiga marufuku / Tumeweka kizuizi kwenye 'Mji' ambao Tuliuteketeza, ili wao (watu wa mji huo) wasiweze kurejea (kwenye mji huo na kuuchukua uwe wao).*

(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:95)

(Angalia chini: 'Ya'juj na Ma'juj wakihusishwa na kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu' na pia angalia sura ya 10 yenye kichwa cha habari '*Ya'juj na Ma'juj kwenye Qur'ani na hadithi'* ambamo tumeonyesha kwa Ushahidi kuwa 'Mji' huo ni Jerusalem.)

Zuio hilo la kiroho juu ya Wayahudi kuwazuia wao kurejea Jerusalem (na kwenye Ardhi Takatifu) na kuichukua kuwa mali yao lilikuwa na lengo la kuwapa ishara Wayahudi kuwa pana hasira ya kiroho na kwao ni adhabu inayotokana na mwenendo wao. Pia zuio hilo lilikuwa na lengo la kuwapa ishara na taarifa isiyokuwa na kificho, kuwa wao siyo tena 'taifa teule.'

3. Uwezekano wa Wayahudi kusamehewa na Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma, ikiwa watamuamini na kumfuata Mtume ambaye atakuwa 'Ummi' (asyesoma na Asyekuwa Myahudi / Mgeni)

Hata baada ya kuondolewa kwenye Ardhi Takatifu na Mwenyezi Mungu Mtakatifu kutoka kwenye Ardhi Takatifu baada ya jaribio lao la kumsulubu Yesu (miongoni mwa madhambi mengi mengine), na baada ya kufungiwa uwezekano wao wa kurejea Jerusalem (na kuudai na kuuchukua mji kuwa wao), *Qur'ani* ilitamka kuwa bado palikuwa na uwezekano kwa wao kupata msamaha wa Mwenyezi Mungu, Aliye Mwingi wa Misamaha:

"Huenda ikawa Mola wenu akawapa msamaha juu yenu." (Qur'ani, Banu Israel, 17:8)

Mwenyezi Mungu Mtakatifu aliwapa kipindi cha muda ambamo ndani yake Alikuwa tayari kuwasamehe ikiwa wangeamua kubadili mwenendo wao, kuomba msamaha Wake, na kurudi kwenye dini ya Abrahamu *(rehma na amani juu yake).* Lakini palikuwa na mlango mmoja tu ambapo msamaha huo ungepatikana. *Qur'ani* iliwazungumzia na kuwapa taarifa *Banu Israil* ambao tayari walikuwa wamekwishapewa taurati na Injili (Injili ya Yesu), hivyo basi ni *Banu Israil* ambao walikwishafanya jaribio la kumsulubu Yesu, na iliwapa maelekezo ya jinsi gani wangeweza kuyafuata kufikia msamaha huo, kwa maneno yafuatayo:

ٱلَّذِينَ يَتَّبِعُونَ ٱلرَّسُولَ ٱلنَّبِيَّ ٱلْأُمِّيَّ ٱلَّذِي يَجِدُونَهُۥ مَكْتُوبًا
عِندَهُمْ فِي ٱلتَّوْرَىٰةِ وَٱلْإِنجِيلِ يَأْمُرُهُم بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَىٰهُمْ
عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ
ٱلْخَبَٰٓئِثَ وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَٱلْأَغْلَٰلَ ٱلَّتِي كَانَتْ عَلَيْهِمْ ۚ
فَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ بِهِۦ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ وَٱتَّبَعُوا۟ ٱلنُّورَ ٱلَّذِيٓ أُنزِلَ
مَعَهُۥٓ ۙ أُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ ﴿١٥٧﴾

"Ambao kwamba wanamfuata huyo Mtume, Nabii (Mgeni – asiye Myahudi), asiye soma wala kuandika, wanaye mkuta kaandikwa kwenye vitabu vyao - Taurati na Injili, anaye waamrisha mema na anawakanya maovu, na anawahalalishia vizuri, na ana waharimishia viovu, na anawaondolea mizigo yao na minyororo iliyo kuwa juu yao. Basi wale walio muamini yeye, na wakamhishimu, na wakamsaidia, na wakaifuata Nuru iliyo teremshwa pamoja naye - hao ndio wenye kufanikiwa."

(Qur'ani, al-Araf, 7:157)

Hivyo basi, katika kumkubali, kumuamini na kumfuata Mtume wa Mwisho, Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake)* msamaha ungeweza kupatikana.

Palitokea ishara kadhaa zilizodhihirisha kuwa muda waliopewa *Banu Israil*, muda ambamo wangeweza kuutafuta na kujipatia msamaha, kuwa sasa umekwishapita. Miongoni mwa ishara hizo ni pamoja na kuachiwa huru kwa *Dajjal* na pia kuachiwa huru kwa Ya'juj na Ma'juj waingie duniani. **Matukio haya yote mawili yalitokea wakati wa uhai wa Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake)*.** Nayo yalitokea baada ya Mtume *(rehma na amani juu yake)* kuishi Madina na Wayahudi kwa muda wa miezi kumi na saba na katika kipindi hicho ilijitokeza wazi kuwa Wayahudi wamemkataa, ikiwa pamoja na kuikataa *Qur'ani* na walikuwa wakipanga njama za kuuteketeza Uislamu. Hapo ndipo kikafikia kipindi ambamo Mwenyezi Mungu Mtukufu alipoteremsha aya iliyotoa amri ya kukirudisha *Qiblah* kuelekea *Ka'aba*. Amri hii ya kubadilisha Qiblah kutoka

Jerusalem na kuelekea Makkah kuliweka wazi kuwa fursa moja na pekee waliyopewa Wayahudi kuupata Msamaha wa Kiroho na Baraka za Mwenyezi Mungu, kuwa sasa fursa hiyo haipo tena na imefungwa. Zama za mwisho sasa zimeanza na adhabu isiyozuilika kwa Wayahudi tangu hapo imekuwa haizuiliki. Likawa ni jambo ambalo amri na maagizo yake yakawa yameshapitishwa.

Ingawa Zama za Mwisho zilikuwa zimeshaanza, na mlango wa fursa ya Msamaha wa Kiroho ukawa umeshafungwa, Wayahudi walilazimika kusubiri kwa kipindi Fulani kabla adhabu yao ya mwisho haijatekelezwa. Kwa hakika adhabu hiyo itajitokeza kwa ubora wa hali ya juu wa adhabu kali na itatekelezwa kwa 'mwendo wa mnyato.' Katika kipindi kirefu kabla ya kutokea kwa adhabu hiyo ya mwisho kujitokeza, Wayahudi watajikuta wanapata faraja yak inga miongoni mwa Waislamu:

ضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ ٱلذِّلَّةُ أَيْنَ مَا ثُقِفُوٓاْ إِلَّا بِحَبْلٍ مِّنَ ٱللَّهِ وَحَبْلٍ مِّنَ ٱلنَّاسِ
وَبَآءُو بِغَضَبٍ مِّنَ ٱللَّهِ وَضُرِبَتْ عَلَيْهِمُ ٱلْمَسْكَنَةُ ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ
كَانُواْ يَكْفُرُونَ بِـَٔايَٰتِ ٱللَّهِ وَيَقْتُلُونَ ٱلْأَنۢبِيَآءَ بِغَيْرِ حَقٍّ ۚ ذَٰلِكَ بِمَا
عَصَواْ وَّكَانُواْ يَعْتَدُونَ ﴿١١٢﴾

Wamepigwa na kufunikwa na udhalili (mithili ya turubali juu yao) popote wanapopatikana (walipo), isipokuwa wakiwa chini ya ahadi (ya kinga) ya Mwenyezi Mungu na ya watu. Na wakastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na wamefunikwa (kwa turubali la) unyonge. Hayo ni kwa sababu walikuwa wakizikataa Ishara za Mwenyezi Mungu, na wakiwauwa Manabii kwa kiburi pasi na haki; hayo ni kwa sababu waliasi na walikuwa wakivuka mipaka.

(Qur'ani, Ale-Imran, 3:112)

Kisha kipindi cha kuanza kuhesabu 'muda uliobaki' kuelekea kwenye adhabu iliyokusudiwa, pia patapatikana ishara kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtakatifu. Miongoni mwa ishara hizo, noja itakayokuwa yenye kuonekana zaidi ni ile ya kupatikana kwa mwili wa Fir'auni ambaye alizama wakati akimfuatilia na kumkimbiza Nabii Musa (*rehma na amani juu yake*) pamoja na wana wa Israili. Bahati mbaya kwa Wayahudi, mwili wa Fir'auni (Rameses II) umekwishapatikana na hivi sasa wamekwishachelewa kuweza kutubu (ikimaanisha kufanya *Taubah*), kuupokea ukweli ulioletwa na Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) uliopo kwenye *Qur'ani*, na kuamini kuwa

Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ni Mjumbe wa Mwisho wa Allah, Mtukufu, na pia wamekwishachelewa kujiepusha na adhabu kali kuliko zote itokayo kwa Mwenyezi Mungu:

"Je, wanangoja ili wawafikie Malaika, au awafikie (Mwenyewe) Mola wako Mlezi, au zifike baadhi ya 'Ishara' za Mola wako Mlezi? Siku zitakapo fika baadhi ya Ishara za Mola wako Mlezi (k.v. Dajjal, ya'ajuj na Ma'ajuj, kupatikana kwa mwili wa Fir'auni, n.k.), kuamini hapo hakutomfaa mtu kitu, ikiwa hakuwa ameamini kabla yake, au amefanya kheri katika Imani yake. Sema: Ngojeni, Nasi pia tunangoja."

(Qur'ani, al-An'am, 6:158)

4. Kurejea kwao kwenye Ardhi Takatifu kwa amri ya Mungu wakati wa kipindi cha 'Nyakati za Mwisho' (awamu ya mwisho ya Zama za mwisho au Kipindi cha Mwisho)

Qur'ani imeendelea na kutamka kuwa Allah Mtukufu Mwenyewe atawarudisha Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu katika 'Zama za Mwisho.' Wayahudi watadanganyika na kuamini kuwa kurudi kwao kwenye Ardhi Takatifu na kuichukua kuwa chini ya himaya ya kunamaanisha na kunathibitisha kuwa wao ndiyo wenye kumiliki Ukweli. Utabiri huu unaohusiana na kurejea kwao kwenye Ardhi Takatifu nao umekwishatimia, hususan katika hali ya kustaajibisha, kupitia kuanzishwa kwa Taifa la Israeli la kilaghai lenye msimamo na mwenendo wa kidunia usiomtambua Mungu ukilinganisha na lile Taifa la awali la Israeli lililoanzishwa na Nabii Daud (*rehma na amani juu yake*):

"*Na tukawaambia baada yake Wana wa Israili: Kaeni katika (Ardhi Takatifu) nchi (kwa sharti kuwa mtaendelea kuwa watii kwa Allah na kuwa na mwenendo wa kiadilifu). (Lakini kaeni mkijua kuwa) itapo kuja ahadi ya Akhera (ikimaanisha kuwa pindi muda wa Zama za Mwisho utakapofika) tutakuleteni nyote pamoja kwenye kundi lililochanganyika (ikimaanisha kuwa wote mtarudishwa kwenye Ardhi Takatifu pamoja na mchanganyiko wenu wote uliopatikana kutokana na miaka mimgi ya kuishi vikundi vikundi duniani kote)."*

(Qur'ani, Banu Israil, 17:104)

Utabiri huu uliomo kwenye *Qur'ani* unasema kuwa Zama za Mwisho zitashuhudia kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu ambamo mchanganyiko na tofauti zitajitokeza baina yao zinazotokana na athari ya kuishi vikundi vikundi na kutawanyika dunia nzima zitaonekana wazi. Neno *lafif* linamaanisha kundi la watu ambao siyo wa aina moja. Na hivi ndivyo hasa ilivyo jamii ya Wayahudi wanaoishi Israeli leo hii. Ni kundi la Wayahudi lililochanganyika wakitokea sehemu

mbalimbali za dunia, ikiwemo sehemu tofauti za nchi za Kiarabu na Kiislamu, wanaoongea lugha tofauti tofauti, nyingine zikihitilafiana aidha kwenye baadhi ya maneno, au wenye lafdhi zinazotofautiana, wanaovaa mavazi tofauti, wenye kula vyakula tofauti, na hata wanaoabudu tofauti kwenye masinagogi tofauti tofauti, n.k. Hata hivyo, tofauti iliyo kubwa kuliko zote ni ile tofauti ya kiambari, na hapo ndipo utabiri wa *Qur'ani* unapata uthibitisho mkubwa na wa kutisha. Israeli mpya ya kisasa ina Wayahudi wakazi wengi zaidi ambao ni wazungu wenye asili ya bara la Ulaya wenye macho ya bluu na nywele zenye rangi ya kimanjano. Kuna Ushahidi wa kinasaba / jenetiki unaojitokeza unaoonyesha kuwa Wayahudi wa Ulaya (ikim. Wayahudi wa ki-Ashkenazi) wanatofautiana kijenetiki na watu wote waishio duniani.
Umoja wa kiambari wa watu ambao walipaswa wote watokane na kizazi cha Abrahamu (*rehma na amani juu yake*), kupitia kwa Is'haka na Yakubu (*rehma na amani juu yake*), hivi sasa umepotea.

Je, kukamilika huku kwa utabiri wa *Qur'ani* kunakohusiana na kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu kuna maana gani na kunaleta athari zipi kwenye kipindi hiki cha Zama za Mwisho?

5. Ya'ajuj na Ma'ajuj ndiyo wahusika watakaowrudisha Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu

Kuna aya zisizopungua tatu kwenye *Qur'ani* ambazo zinaelekea kuonyesha adhabu kali ya kiroho kwa Wayahudi wakati watakaporudishwa kwenye Ardhi Takatifu. Tatizo la wale ambao huwa wanaiangalia *Qur'ani* kwa kutumia 'jicho moja' ni kuwa uelewa wao wa hali halisi hususan inapohusiana na Zama za Mwisho huwa haupatikani isipokuwa pale ambapo patatumika 'mtazamo wa ndani wa kiroho' (ikim. Jicho la ndani) linapoungana na 'mtazamo wa nje.' Zifuatazo ni aya mbili kati ya hizo tatu zilizozungumziwa hapo juu:

"*Tumepiga marufuku / Tumeweka kizuizi kwenye 'Mji' ambao Tuliuteketeza, ili wao (watu wa mji huo) wasiweze kurejea (kwenye mji huo na kuuchukua uwe wao) mpaka watapo funguliwa Ya'ajuj na Ma'ajuj (kutoka kwenye kizuizi chao) wakawa wanateremka kutoka kila mlima (au kusambaa kuelekea kila upande).*

(Qur'ani, al-Anbiyah, 21:95-96)

Wakati jina la 'mji' husika halikutajwa moja kwa moja, ni wazi kabisa kwamba haiwezekani ikawa ayah ii inauhusisha 'mji' mwingine zaidi ya Jerusalem. Pana kitambulisho kisichokuwa cha moja kwa moja kinachopatikana kwenye *Qur'ani*, nacho ni kama ifuatavyo: Marabbai wa Madina (wakati huo

ukijulikana kwa jina la Yathrib) walijibu maombi ya watu wa kabila la *Quraish*, kabila la Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*), ya jinsi gani wafanye ili kugundua kama Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ni mtume wa kweli na kama ujumbe wake ni sahihi. Jibu la ombi hilo, Marabbai waliwataka wamuulize maswali matatu, na kusema ikiwa atayajibu kwa usahihi, basi huyo atakuwa kweli ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu alichukua hatua ya kujibu maswali yote matatu kwenye *Qur'ani* kama kawaida kwa wahyi. Majibu ya maswali mawili ya kwanza, ikim., vijana waliokimbia na kujificha kwenye pango na la pili la 'msafiri mkubwa mashuhuri' ambaye alitembelea pande mbili za dunia yanapatikana au yaliwekwa kwenye *Surah al-Kahf*. (*tazama al-Kahf, 18:9-26 na 18:83-98*), lakini jibu la swali la tatu linalohusu *ruh* (roho) liliwekwa kwenye *Surah Banu Israil, 17:85*. Kinachofuatia kutokana na kuwekwa huku kusikokuwa kwa kawaida kwenye *Surah* tofauti kwa majibu ya maswali ambayo yanatoka kwa kundi moja la watu, ni kuwapo kwa uhusiano wa kimsingi unaoziunganisha hizi *Surah* mbili za *Qur'ani* kama ilivyoelezwa na Dr. Israr Ahmad, mwanazuoni maarufu wa *Qur'ani*, ambaye ameweka wazi Ushahidi wa kutosha unaothibitisha muungano huo wa *Surah* hizi.

Hivyo basi, ili kupata ufunguo wa kitendawili cha utambulisho kuwajua vijana waliokimbilia na kujificha kwenye pango, na kumjua *Dhul Qarnain, Ya'juj na Ma'juj na Qaryah* (mji), tunalazimika kuikabili *Surah Banu Israil* ili kupata msaada huo wa maelezo. Na tunapofanya hivyo tunagundua kuwa Surah hiyo inajihusisha na *Qaryah* 'mji' mmoja tu nao ni Jerusalem.

Ahadith za Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) kwa upande wa pili, moja kwa moja zinauunganisha utambuzi huo kuwa ni mji wa Jerusalem. Si tu kuwa Jerusalem unatajwa moja kwa moja kwa jina kwenye *Ahadith* kuhusiana na *Ya'juj na Ma'juj* bali pia hakuna mji mwingine wowote uliovunjwa na Allah Mtkatatifu unaotajwa zaidi yake. Hadith ifuatayo ambayo inazungumzia tukio la kurejea kwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) inatosheleza kuthibitisha kiungo baina ya *Ya'ajuj na Ma'ajuj* na Ardhi Takatifu, ikiwemo Jerusalem, na hivyo basi kuutambua kuwa *Qaryah* 'mji' si mwingine bali ni Jerusalem:

"Amesimulia al-Nawwas ibn Sam'an: … Basi itakuwa kwenye mazingira kama hayo ambapo Allah atambainishia Yesu (*rehma na amani juu yake*) maneno haya: Nimejaalia miongoni mwa Waja Wangu aina ya watu ambao hakuna atakayeweza kupigana nao, wachukue watu hawa kwa usalama hadi Tur, na ndipo Allah atawatuma *Ya'ajuj na Ma'ajuj* na watasambaa kushuka chini kutoka kwenye kila kilima. Wa mwanzo miongoni mwao watapita pembeni ya ziwa Tiberius (ikim. Bahari ya Galilei) na watakunywa maji yake. Na wakati wa mwisho atakapokuwa akipita, atasema: Hapa zamani palikuwa na maji. Kisha Yesu (*rehma na amani juu*

yake) na maswahaba wake watazingirwa hapo Tur (na watabanwa sana) kiasi kichwa cha ng'ombe kitakuwa na thamani kubwa sana kwao kupita dinari mia moja…"

(Sahih Muslim)

Bahari ya Galilei iko kwenye Ardhi Takatifu. Pili, mlima Tur unaotajwa kwenye *Hadith* ni mlima uliopo Jerusalem. Haya yote yanatajwa tena kwenye *Hadith* inayopatikana kutokana na mnyororo huo huo uliothibitisha (Sahih) wa wasimulizi uliotajwa hapo juu:

"*Ya'juj na Ma'juj* watatembea hadi wafike kwenye mlima al-Khamur, n ani mlima wa *Bait al-Maqdis* (ikim. Jerusalem) na kisha watasema: Tumewaua watu wote waliokuwa duniani. Acha sasa tuwaue wale ambao wako mbinguni. Watarusha mishale yao mbinguni na mishale hiyo itarudi kwao ikiwa imetapakaa damu."

(Sahih Muslim)

Hadi hapo, tunakuwa tumefikia mahali ambapo tunagundua kuwa kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu kwenye 'Zama za Mwisho' kama 'Ishara' iliyobashiriwa kwenye *Qur'ani*, ambayo siyo tu kuwa inathibitisha kuachiwa kwa *Ya'juj na Ma'juj* bali pia inadhihirisha na kuweka wazi kuwa hivi sasa wao ndiyo wanaoitawala dunia kwa nguvu ambazo haziwezi kuangamizwa na kitu au mtu yeyote. (tazama sura ya 10 kwa maelezo ya ziada kuhusu *Ya'juj na Ma'juj*). Hao *Ya'juj na Ma'juj* ni maajenti wa *fasad*. (tazama *Qur'ani,* al-Kahf, 18:94). Neno fasad linamaanisha "uharibifu, utumiaji mbaya, ufujaji, ugombanishaji, hujuma, fitina, saliti, kuvuruga, ukosefu wa maadili, mwenendo wa tabia za kiajabu, n.k." Wakati Ya'juj na Ma'juj wakishashibana na watu, basi mwelekeo wa watu hao unakuwa ni kwenye moto wa jahannamu. Hadithi inafumbua na kututambulisha kuwa mchakato mzima wa mtandao wa kidunia unaounganisha kila mji na kila Kijiji katika kila nchi kwenye sekta zote za kimaisha duniani kote, kwenye zama za Ya'juj na Ma'juj, utaishia kwenye kila watu 999 katika watu 1000 kuingia kwenye moto wa jehannamu:

"Amesimulia Abu Said Al Khudri: Mtume alisema: Siku ya Kiyama Allah atasema: Ewe Adam! Adam atajibu: Labbaik Mtukufu, na Sa'daik. Kisha patakuwa na sauti kali ikiita na kusikika ikisema: Allah anakuamuru uchukue kutoka miongoni mwa kizazi chako kuingia kwenye Moto (wa Jehannamu). Adam atasema: Ewe Mtukufu, ni wangapi hao wanaoingia kwenye Moto (wa Jehanamu?) Allah atasema: Katika kila elfu moja, chukua 999. Wakati huo, kila mwanamke mwenye mimba atadondosha mzigo wake (mimba itatoka) na mtoto atakuwa na nywele za mvi.

"Na utawaona binaadamu wako kama vile wamelewa, japo hawajalewa, isipokuwa mateso ya mwenyezi Mungu yatakuwa makali mno." (*Qur'ani, al-Hajj, 22:2*)

(Baada ya Mtume (*rehma na amani juu yake*) kuyatamka haya mbele ya maswahaba wake) maswahaba walishikwa na huzuni na bumbuwazi kubwa (ikiwa na woga) na kubadilisha hali ya rangi za nyuso zao ndipo alipotamka: Hao watu 999 watatokana na watu wa Ya'juj na Ma'juj na huyo mmoja atatoka miongoni mwenu. Nyinyi Waislamu (ukilinganisha na kaumu kubwa ya watu waliobaki) mtakuwa kama unywele mweusi kwenye ubavu wa ng'ombe mweupe, au unyoya mweupe kwenye ubavu wa ng'ombe mweusi na nina matumaini kuwa mtakuwa robo ya watu wa Peponi. Alipotamka hayo tukasema: Mungu Mkubwa! Kisha akasema: Nina matumaini mtakuwa theluthi ya watu wa peponi. Tena tukasema: Mungu Mkubwa! Kisha akasema: (Nina matumaini kuwa mtakuwa) Nusu ya watu wote wa peponi. Nasi tukasema: Mungu Mkubwa!

Kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu na kuundwa upya kwa Taifa la Israeli, kumewezekana kwa kupitia kwa *Ya'juj na Ma'juj*, na pia kwa nguvu za Mtume wa Uongo (*al-Masih al-Dajjal*). Hivyo basi, kurejea huko kunawaweka kwenye hali hatarishi kuliko zote ambazo Wayahudi wamekwishawahi kuwa katika historia yao yote. Hakika, hatma yao hadi hivi imekwishafungwa na haina shaka. Lakini wao wenyewe hata habari hawana. Ni pale tu ambapo wangeuikubali *Qur'ani* kuwa ni Neno lililoteremshwa na Mwenyezi Mungu wa Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*) na mafundisho ya Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*), Mtume wa Mwisho, ndipo Wayahudi wangeweza kubaini hali halisi ambayo sasa hivi inawakabili. Vyanzo vya *Ahadith* na *Qur'ani* vilivyomo kwenye kitabu hiki vinapasa kutosheleza kuwasaidia waielewe hali hii inayowakabili.

6. **Onyo kwa Wayahudi kuwa adhabu ya Mwenyezi Mungu kwao inaweza kurudiwa**

Qur'ani iliwaonywa Wayahudi kuwa ikiwa wtarudia hulka zao mbaya Allah, Aliye Juu ya Kila Kitu, atarejea na adhabu Yake. Mwanzo aliwaadhibu kwa jeshi la Babilonia. Baadaye aliwaadhibu kwa jeshi la Kirumi. Mara ya mwisho, itakapotokea adhabu Yake, itakuwa kwa jeshi la Kiislamu:

"Huenda Mola wenu Mlezi akakuonyesheni (huko mbele) rehma zake, lakini ikiwa mtarudia (kwenye dhambi zenu) na Sisi tutarudia (kwa adhabu Yetu): Na tumeifanya Jahannamu kuwa ni gereza kwa ajili ya wanaopinga (imani zote)."

(Qur'ani, Banu Israili, 17:8)

7. **Onyo kwa Wayahudi kuwa adhabu itakuwa kali kuliko adhabu yoyote iliyokwishawahi kutolewa kwao**

Qur'ani imetoa onyo lililo wazi lenye kueleweka na kuweka kinagaubaga uwezekano kuwa siku moja Wayahudi (baada ya muda wa kuomba msamaha na kujirekebisha kupita) watakabiliwa na hali ambayo hivi sasa inawakabili, ikim. *Ya'ajuj na Ma'ajuj* pamoja na *Dajjal*, Mtume wa Uongo wataachiliwa waingie duniani. Wayahudi walikataa kuiamini *Qur'ani* kuwa ni neno linalotoka kwa Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) na pia walikataa kumuamini na kumfuata Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) kama Mtume wa Mwisho wa Mungu wa Ibrahimu. Matokeo ya hali hiyo ya kutoamini, wanakosa uwezo wa kugundua hali halisi ilivyo:

"Tazama! Na pale alipo tangaza Mola wako Mlezi kwamba hapana shaka kuwa atawaletea (ikim. Wayahudi) watu ambao watawaadhibu kwa adhabu mbaya mpaka Siku ya Kiyama. Hakika Mola wako Mlezi ni Mwepesi katika kuadhibu, na bila ya shaka ni Mwenye Maghfira, na Mwenye Kurehemu."

(Qur'ani, al-Araf, 7:167)

Hukumu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa mujibu wa sharia na busara Zake ni kuwa adhabu lazima iendane na kiwngo cha kosa lililotendwa. Na kwa kuwa Wayahudi wametenda kosa kubwa kuliko yote ya kujaribu kumsulubu Yesu (*rehma na amani juu yake*), kuandika na kufanya mabadiliko kwenye Taurati, n.k. wanastahili kupata adhabu kali zaidi iwezekanayo. Na adhabu hiyo itaanza kutekelezwa kabla ya Siku ya Kiama. Ukweli ni kuwa itaanza kujitokeza baada ya kuja Mtume wa Mwisho (Muhammad) duniani na kumkataa. Mtiririko wa matukio utafuatia kuanzia hapo ambao utapelekea kuishia kwa Wayahudi kuadhibiwa kwa adhabu kali. Allah atawainua na kuwatumia wale ambao watakuwa ndiyo watekelezaji wakuu wa mpangilio huo. Nao ni, bila ya shaka yoyote, *Ya'ajuj na Ma'ajuj, Dajjal*, Mtume wa Uongo. Tumeshaelezea tukio la kioja la *Dajjal*, Mtume wa Uongo kwenye Sura ya Nane ya Kitabu hiki.

8. Upofu wa (mtazamo/muono wa) kiroho wa Wayahudi wakati muda wa adhabu ya mwisho utakapotimia

Allah Mtukufu Alijihakikishia Mwenyewe kuwa Wayahudi pamoja na umma uliobaki usioamini hawatoweza kugundua:

سَأَصۡرِفُ عَنۡ ءَايَٰتِيَ ٱلَّذِينَ يَتَكَبَّرُونَ فِي ٱلۡأَرۡضِ بِغَيۡرِ ٱلۡحَقِّ وَإِن
يَرَوۡاْ كُلَّ ءَايَةٖ لَّا يُؤۡمِنُواْ بِهَا وَإِن يَرَوۡاْ سَبِيلَ ٱلرُّشۡدِ لَا
يَتَّخِذُوهُ سَبِيلٗا وَإِن يَرَوۡاْ سَبِيلَ ٱلۡغَيِّ يَتَّخِذُوهُ سَبِيلٗاۚ ذَٰلِكَ
بِأَنَّهُمۡ كَذَّبُواْ بِـَٔايَٰتِنَا وَكَانُواْ عَنۡهَا غَٰفِلِينَ ١٤٦

"Nitawatenga na Ishara zangu wale wanao fanya kiburi katika nchi bila ya haki. Na wao wakiona kila Ishara hawatoiamini. Wakiiona njia ya uwongofu hawaishiki kuwa ndiyo njia; lakini wakiiona njia ya upotofu wanaishika kuwa ndiyo njia. Hayo ni kwa sababu wamezikanusha Ishara zetu, na wameghafilika nazo."

(Qur'ani, al-Araf, 7:146)

Mtendaji mkuu ambaye atachukua nafasi kuu kwenye tamthilia ya kusisimua ya Zama za Mwisho, tamthilia ambayo inawarudisha na inawaweka binaadamu wote (ukiacha waumini) katika hali ya upofu wa (muono wa) kiroho – si mwingine bali ni yeye mwenyewe, Masihi wa Uongo, *Dajjal*. Ni muhimu kuwa chombo muhimu kuliko vyote ambacho Mwenyezi Mungu amemjaalia *Dajjal* (kwa lengo la kutimiza jukumu lake ni 'jicho lake moja.' *Dajjal* ni kipofu kwenye jicho lake la kulia, na hiyo inaashiria kuwa ni kipofu kwenye muono wake wa ndani wa kiroho. Wale wote watakaokuwa wamedanganywa naye nao watakuwa vipofu wa muono wa kiroho na hawatoweza kuona na kuzigundua Ishara za Allah kwenye Zama za Mwisho. Upofu huo wa kiroho utaendelea hadi pale atakaporejea Masihi wa Kweli, Yesu mwana wa Mariyamu.

9. Mwili wa Fir'auni (wa enzi za kitabu cha 'Kutoka') utapatikana ukiwa haujaharibika na utadhihirisha kuwa Wayahudi watatokewa na jambo hilo hilo lililomtokea Fir'auni

Qur'ani imetoa ishara nyingine tena ambayo wale wenye uwezo wa wajuzi wa kutambua wangeweza kugundua kuwa hesabu za kueleka mwisho wa *Banu Israil* kwenye Zama za mwisho kumeshajizi na adhabu kali kabisa kuliko zote kwa Wayahudi iliyokusudiwa na Allah Mtukufu sasa itaweza kujitokeza. Ishara hiyo ni kugunduliwa kwa mwili wa Fir'auni aliyeangamia kwa kuzamishwa kwenye bahari alipokuwa akijaribu kuivuka akiwa anamkimbiza Musa (*rehma na amani juu yake*). Mwenyezi Mungu Mtukufu aliitenganisha bahari ili kuwaokoa *Banu Israil*. Na baada ya

wao kuivuka na kutoka salama, alizishusha kuta za mawimbi ya maji juu ya Fir'auni na jeshi lake na wote wakateketea. *Qur'ani* iliyazungumzia haya kama ifuatavyo:

"Na kumbukeni kuwa Tuliipasua Bahari kwa ajili yenu na tuliwaokoa nyinyi na kumzamisha Fir'auni na watu wake mbele ya macho yenu"

(Qur'ani, al-Baqarah, 2:50)

Banu Israil hawakujua wakati huo, na pia hawajagundua hadi leo hii, kwamba wao wenyewe siku moja watateketea kama vile ambavyo Fir'auni aliteketezwa, na kuwa utawafikia umauti katika namna ile ile ambayo Fir'auni ilimfikia ikiwa watamsaliti Mwenyezi Mungu na kutenda madhambi fulani.

Je, ni jinsi gani Fir'auni alikufa? Msomaji mpole atapata mshtuko mkubwa pale atakaposoma maelezo ya *Qur'ani* kuhusiana na kifo cha Fir'auni:

۞ وَجَٰوَزۡنَا بِبَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ ٱلۡبَحۡرَ فَأَتۡبَعَهُمۡ فِرۡعَوۡنُ وَجُنُودُهُۥ بَغۡيًا
وَعَدۡوًاۖ حَتَّىٰٓ إِذَآ أَدۡرَكَهُ ٱلۡغَرَقُ قَالَ ءَامَنتُ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱلَّذِيٓ
ءَامَنَتۡ بِهِۦ بَنُوٓاْ إِسۡرَٰٓءِيلَ وَأَنَا۠ مِنَ ٱلۡمُسۡلِمِينَ ٩٠
ءَآلۡـَٰٔنَ وَقَدۡ عَصَيۡتَ قَبۡلُ وَكُنتَ مِنَ ٱلۡمُفۡسِدِينَ ٩١
فَٱلۡيَوۡمَ نُنَجِّيكَ بِبَدَنِكَ لِتَكُونَ لِمَنۡ خَلۡفَكَ ءَايَةٗۚ وَإِنَّ كَثِيرٗا مِّنَ
ٱلنَّاسِ عَنۡ ءَايَٰتِنَا لَغَٰفِلُونَ ٩٢

"Tukawavusha bahari Wana wa Israili: huku Firauni na askari wake wakawafuatia kwa hasira na jeuri iliyojaa kebehi. Hata Firauni alipo kuwa anataka kuzama akasema: Naamini kuwa hapana

mungu ila yule waliye muamini Wana wa Israili, na mimi ni miongoni mwa (wanaomuamini Allah katika Uislamu) walio nyenyekea!

"Ala! Sasa? Na hali kabla yake uliasi na ukawa miongoni mwa mafisadi (kwa ugandamizaji na ukatili!)

"Leo, basi, (Tumeamua kuwa) tutauhifadhi mwili wako, ili (ikim. Huo mwili utakapojitokeza tena kwenye historia) uwe Ishara kwa ajili ya wale watakaokuja (kizazi kijacho) baada yako. Na hakika watu wengi wameghafilika na Ishara zetu."

(Qur'ani, Yunus, 10:90-92)

فَلَمَّآ ءَاسَفُونَا ٱنتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَغْرَقْنَٰهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٥﴾

فَجَعَلْنَٰهُمْ سَلَفًا وَمَثَلًا لِّلْءَاخِرِينَ ﴿٥٦﴾

Na walipoendelea Kutukasirisha Tuliwakutanisha na adhabu yetu tukawazamisha wote! Kisha tukawafanya kuwa miongoni mwa waliopita, na mfano (wenye onyo) kwa wale (watakaokuja) baadaye.

(Qur'ani, al-Zukhruf 43:55-56)

Hivyo basi, *Qur'ani* imetoa utabiri wa kustaajabisha kuwa mwili wa Fir'auni anayetajwa katika kitabu cha 'Kutoka' siku moja utapatikana na utakuwa miongoni mwa Ishara ya kiroho yenye onyo kali. Kwa mastaajabu makubwa, mwili wa Fir'auni uligunduliwa takriban karibu na mwisho wa karne iliyopita. Ni ishara ya kutisha yenye kuonyesha maafa makubwa yaliyoufikia umma wa Kiislamu na wanazuoni wake ambao wote wameshindwa kusoma, kuelewa na kudodosoa maana yoyote kutokana na tukio hili la kustaajabisha (ikim. Kupatikana kwa mwili wa Fir'auni wa zama za 'Kutoka') zaidi ya kusema tu kuwa utabiri wa *Qur'ani* umekamilika. Hii ilikuwa ni ishara ya kutisha zaidi kwa Wayahudi kuwa Shirikisho la Wazayonisti lilianzishwa takriban katika muda huo huo ambapo mwili wa Fir'auni uligunduliwa. Ni wazi kuwa *Dajjal*, Mtume wa Uongo, alikuwa ndiye mwanzilishi wa kimawazo kwenye kuundwa kwa Shirikisho la Kizayonisti. Hivyo basi, na zama za *Ya'juj na Ma'juj* pia ni zama za *Dajjal.*

Maana ya matukio haya yote hapo juu ni kuwa Wayahudi sasa wanaongozwa na *Dajjal*, Mtume wa Uongo, na *Ya'juj na Ma'juj*, kupelekwa kwenye uchochoro ambao utawakutanisha na

adhabu kali ya kiroho itokayo kwa Mwenyezi Mungu na mbaya kuliko adhabu zote zilizokwishawakuta na itaishia kwa wao Wayahudi kuteketezwa. Lakini mwisho wao utakuwa kama vile mwisho wa Fir'auni. Upi huo utakuwa mwisho wao? Kugunduliwa kwa mwili wa Fir'auni kulikuwa ni Ishara kubwa yenye uzito mkubwa kabisa na umuhimu wa hali ya juu sana iliyotoka kwa Mwenyezi Mungu Mtakatifu inayoashiria kuwa kuanzia sasa dunia itashuhudia mithili ya tamthilia yenye matukio makubwa ambayo hayajawahi kutokea kwenye historia ya binaadamu. Muda sasa umewaishia Wayahudi hususan, na kwa binnadamu wote kiujumla. Wale walioishi kama Fir'auni sasa nao watakufa kwa namna ile ile ambayo Fir'auni alikufa.

10. Wayahudi hawatokuwa na jinsi wala uchaguzi mbadala zaidi ya kumuamini Yesu (*rehma na amani juu yake*) kuwa ni Masihi pale atakaporejea isipokuwa itakuwa tayari wamekwishachelewa kuweza kupata uokozi kutoka kwenye adhabu kali ya moto.

Baada ya *Qur'ani* kusimulia tukio ambamo Wayahudi walijaribu kumsulubu Yesu (*rehma na amani juu yake*) na kisha kutamba na kujisifu kuwa wametimiza lengo lao, Mwenyezi Mungu amefikisha ujumbe wenye onyo kali. Wayahudi ambao walimkataa Yesu (*rehma na amani juu yake*) kuwa ni Masihi (na Wakristo ambao wanamuabudu kuwa ni Mungu) wamepewa taarifa kuwa (watalazimika) kumkubali na kumuamini yeye (Yesu) kabla hajafikiwa na *Maut*, ikim. Baada ya kurejea na kabla hajafa. Hivyo basi Wayahudi watalazimika kumkubali na kumuamini kuwa ni Masihi na Wakristo watalazimika kuacha kumuabudu kama Mungu na kumtambua kuwa ni Mtume:

"Na hakutakuwa katika Watu wa Kitabu (ikim. hapatokuwa hata na Myahudi mmoja atakayemkataa Yesu kama Masihi na Mtume wa Allah, na hapatokuwa hata na Mkristo mmoja atakayedai kuwa Yesu inabidi aabudiwe kama Mungu na kama mtoto wa Mungu) na ila hakika watamuamini yeye (Yesu) kabla ya kufa kwake. Naye Siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu (dhidi) yao."

(Qur'ani, al-Nisa, 4:159)

Aya hiyo hapo juu inaonyesha kuwa wakati Yesu (*rehma na amani juu yake*) atakaporejea Wayahudi siyo tu watamkubali imani yao kuhusu yeye kuwa Masihi, bali pia, kutokana na hilo, watagundua na kuthibitisha imani yao juu ya Muhammad (*rehma na amani juu yake*) kuwa ni Mtume wa Mwisho aliyeletwa na Mungu wa Ibrahimu, na kuwa *Qur'ani* ni Neno la Mwisho la Mungu kushushwa duniani. Isipokuwa kukubali huku kwa imani kwa upande wa Wayahudi hakutowasaidia wala kuwapatia faida yoyote kama vile ambavyo kukubali kwa imani na kumuamini Mungu katika dakika ya mwisho hakukuweza kumpatia Fir'auni faida yoyote (aliendelea kulaaniwa na kuahidiwa

kuwaataingizwa kwenye moto wa Jahannamu). Huu ndiyo ujumbe mchungu kwa Wayahudi ambao unatokana na kupatikana kwa mwili wa Fir'auni!

Tokeo la ziada, muhimu sana ili kuweza kuuelewa mtiririko wa kihistoria kwa kadiri dunia inavyozidi kuelekea kwenye kilele kikuu cha mwisho, ni kuwa Wayahudi pamoja na makafiri watabaki wakiwa na uhakika kabisa wa kuwa wao wamo katika njia sahihi na iliyonyooka kuelekea kwenye ushindi hadi dakika za mwisho kabisa. Hivyo basi mkondo wa mwenendo wa kiroho wa Ukweli (ikim. *Uislamu*) duniani kwenye Zama za Mwisho ni ule ambamo utazamaji wa nje wa juu juu usiyoweza kupenya na kuona kwa kina, utaonyesha kuwa *Uislamu* umeshindwa na hauna mvuto wala hautegemei kupata ushindi. Na hiyo ndiyo hali sahihi na halisi leo hii duniani.

Sura ya 13

QUR'ANI NA HATMA YA JERUSALEM

"... lakini ikiwa mtarudia (kwenye dhambi zenu zinazotokana na kuvunja masharti ya kurithi Ardhi Takatifu) na Sisi tutarudia (kwa adhabu Yetu, ikim. mtafukuzwa na kuondolewa kutoka kwenye Ardhi Takatifu tena na tena..."

(Qur'ani, Banu Israili, 17:8)

Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake*) alisema: Utume utabaki miongoni mwenu kwa kadiri ambavyo Mwenyezi Mungu atataka ubaki, na kisha Allah atauinua. Baadaye patakuwa na Khilafah kwa mujibu wa njia za Utume kwa kadiri ambavyo Mwenyezi Mungu atataka ubaki, kisha Allah atauinua. Baadaye patakuwa na utawala wa kurithi (kwa makubaliano) na utabaki kwa kadiri Allah atakavyotaka, kisha Allah atauinua. Baada yah apo patakuwa na ugandamizaji mbaya wenye mateso makubwa na utabaki kwa kadiri Allah atakavyotaka ubaki, kisha atauinua. Kisha patakuwa na khilafah kwa mujibu wa njia za Utume na hapo Mtume *(rehma na amani juu yake*) akabaki kimya"

(Musnad, Ahmad bin Hanbal)

Baada ya kuwaondoa Wayahudi kutoka kwenye Ardhi Takatifu kwa mara ya pili, Allah Mtakatifu aliitamka nia Yake ya kuendelea kuwaadhibu (na kuwafukuza) ikiwa wataendelea kuichafua Ardhi Takatifu kwa kuvunja amri na masharti ya imani na mwenendo mwema:

عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَن يَرْحَمَكُمْ ۚ وَإِنْ عُدتُّمْ عُدْنَا ۘ وَجَعَلْنَا جَهَنَّمَ لِلْكَافِرِينَ حَصِيرًا ﴿٨﴾

"... lakini ikiwa mtarudia (kwenye dhambi zenu zinazotokana na kuvunja masharti ya kurithi Ardhi Takatifu) na Sisi tutarudia (kwa adhabu Yetu, ikim. mtafukuzwa na kuondolewa kutoka kwenye Ardhi Takatifu tena na tena..."

(Qur'ani, Banu Israili, 17:8)

Hatma ya Jerusalem imewekwa wazi kabisa kwenye onyo linalopatikana ndani ya aya hiyo hapo juu iliyo kwenye *Qur'ani*. Bila ya kujali makubaliano yaliyofikiwa kwenye Kambi ya David au sehemu nyingine yoyote baina ya wawakilishi wa Shirikisho lenye msimamo wa kidunia la Kitaifa la Wapalestina na Wayahudi Wazungu wenye msimamo mkali wa kitaifa ambao wamejinyakulia haki ya kuwawakilisha Wayahudi asilia 'mbegu' ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*), *Banu Israil*, hatma ya Jerusalem inaonekana wazi kwenye muktadha wa mwenendo mbaya na mchafu, usiojali maadili ya kiroho na amri za Mwenyezi Mungu, uozo wa maadili, na ugandamizaji wa haki ambao unaendelea hapo na kuichafua kabisa Ardhi Takatifu. Kitu cha kushangaza Zaidi kati ya vyote hivyo katika Taifa la Israeli ni hali ya kutomjali Mwenyezi Mungu na kuacha njia, misingi, miongozo na utaratibu mzima wa mwenendo wa maisha wa kidini. Makala ya mhariri ya muda mfupi uliopita ya toleo la Jerusalem Post ilikuwa na haya yafuatayo kwa kusema kufuatana na hali hiyo ya utekelezaji wa dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*) ndani ya nchi ya Israeli: *Kwa Wayahudi wengi, Uyahudi umegeuka kuwa tabia na mwenendo wa kizamani, wa kishenzi, na mfumo usiokuwa na uhusiano wowote ambao umo kwenye mashindano kugombania madaraka na kupata pesa, na kufikia hata kuwa ni chanzo cha kutia aibu kwa jamii ya kisasa yenye msimamo na mwelekeo wa maisha unaoegemea utumiaji wa akili na uwezo wake wa kufikiri kwenye njia zote za kuendesha maisha. (Jerusalem Post, mwezi wa Tisa, Mwaka 2000)*

Miongoni mwa 'Ishara' za kiroho za Mwenyezi Mungu ambazo alionyeshwa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) wakati wa safari yake ya kiajabu kuelekea Jerusalem, zilikuwamo zile ambazo zilimuonyesha hatma ya Jerusalem. Suala hili inaonyesha limempita Daniel Pipes pembeni na hakuliona. Hii haishangazi kwani, kama ilivyo kwa Wayahudi wengi, haonyeshi dalili za kuyasikia 'mawe' ya *intifada* ambayo tayari yaneshaanza kuongea kwenye Ardhi Takatifu. Lakini, Brigedia-Jenerali mstaafu wa Jeshi la Anga la Israeli Aphraim Eitam, ambaye alijiuzulu muda mfupi uliopita kutoka kwenye Jeshi la Ulinzi la Israeli – IDF anaonyesha kuamini kuwa ni kweli 'mawe' yanaongea kwenye Ardhi Takatifu. Amenukuliwa akisema: *"Israeli ni nchi ya hatari kuliko nchi zote duniani kwa Wayahudi…" Jerusalem Post, tarehe 20, mwezi wa Pili, Mwaka 2001).*

Qur'ani imeweka wazi hatma ya Jerusalem ambayo itashuhudia Waislamu kurudisha utawala wao Jerusalem – utawala ambao ulianza muda mfupi baada ya kifo cha Mtume (*rehma na amani juu yake*) na ambao uliendelea bila kusitishwa kwa karne kadhaa. Wakati wapiganaji wa Kikristo-Wazungu wa Krusedi walioivamia Jerusalem waliachiwa nafasi fupi ya kuitawala kwa takriban

miaka 80 kabla hatma ya Jerusalem haijachukua mkondo wake. Jeshi la Kiislamu liliwaangusha na kuwashinda wapiganaji wa krusedi na utawala wa Waislamu kwenye Ardhi Takatifu ukaanza tena upya. Kwa mara nyingine tena, ukaendelea bila kukatishwa kwa karne kadhaa hadi pale muda ulipofikia, ambapo kwa Mpango wa Mungu, Wayahudi walirudishwa kwenye Ardhi Takatifu. Haiyumkiniki kuwa utawala wa Kiyahudi, kama vile ambavyo utawala wa Krusedi wa Kizungu kabla yake, utaweza kubaki madarakani kwa zaidi ya miaka themanini, na Mwenyezi Mungu ndiye mjuzi zaidi. Jeshi la Kiislamu litawashinda Wayahudi, na utawala wa Kiislamu utarudishwa tena upya. Allah Mtukufu Amesema hivyo kwenye *Qur'ani*:


وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى
ٱلْأَرْضِ كَمَا ٱسْتَخْلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ
ٱلَّذِى ٱرْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِى لَا
يُشْرِكُونَ بِى شَيْـًٔا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ
ٱلْفَٰسِقُونَ ﴿٥٥﴾

"Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walio amini (katika Uislamu) miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba Atawafanya makhalifa katika ardhi (Ardhi Takatifu) kama alivyo Wafanya makhalifa wa kabla yao (ikim. Wayahudi), na kwa yakini atawasimamishia Dini yao (ikim. Uislamu) aliyo Wachagulia (tazama Qur'ani, al-Maidah, 5:3), na atawabadilishia (hali yao iwe ya) amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu Mimi, wala wasinishirikishe na chochote. Na watao kufuru baada ya hayo, basi hao ndio wapotovu."

(Qur'ani, an-Nur, 24:55)

Wakati *Qur'ani* inazungumzia hali ya khofu ambamo waumini wanaishi lazima inajumuisha hali isiyokuwa ya kawaida ambamo utumiaji mabavu na ugandamizaji unafanywa na Israeli leo hii kwenye Ardhi Takatifu. Aya ya *Qur'ani* ambayo inaweka wazi kuwa Waislamu pekee watakaopewa fursa ya kurithi Ardhi Takatifu kwenye kipindi kijacho ni wale tu ambao wanamuabudu Allah peke yake na hawafanyi *Shirk*. Chama cha PLO hakina nafasi kwenye jumuiya ya wale walio na wanaoendela kuwa watekelezaji wa amri za Allah, Mtukufu.

Ahadi hii ya Mwenyezi Mungu pia inapata uthibitisho kutoka kwa Mtume (*rehma na amani juu yake*) kwenye Hadith ifuatayo:

"Abu Huraira amesimulia kuwa Mtume (*rehma na amani juu yake*) alisema: Mabango meusi yataibuka kutokea Khorasan (eneo ambalo hivi sasa linajumuisha maeneo yaliyopo kwenye nchi za Afghanistani, Pakistani na kiasi kidogo kilichopo Iran na Asia ya Kati), na hakuna nguvu itakayoweza kuwazuia hadi watakapojiijngiza Aelia (Jerusalem)."

(Sunan Tirmidhi)

Qur'ani pia inatoa sababu za kuthibitisha uhalali wa hayo matumizi ya 'jitihada za kijeshi' ambazo zitaishia kwenye utekaji wa mji wa Jerusalem. Mwenyewe Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) Anasema kuwa Ameruhusu nguvu za kijeshi zitumike katika kujibu ugandamizaji ambao umepelekea dunia nzima kushuhudia watu kufukuzwa kutoka majumbani mwao na kunyang'anywa ardhi yao ambamo wameishi kwa vizazi na vizazi – kufukuzwa ambako hakuna sababu yoyote ya msingi iliyopelekea kuwa hivyo zaidi ya kuwa wao ni Waislamu:

أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقَٰتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظُلِمُوا۟ ۚ وَإِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ
لَقَدِيرٌ ﴿٣٩﴾
ٱلَّذِينَ أُخْرِجُوا۟ مِن دِيَٰرِهِم بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّآ أَن يَقُولُوا۟ رَبُّنَا ٱللَّهُ ۗ
وَلَوْلَا دَفْعُ ٱللَّهِ ٱلنَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَّهُدِّمَتْ صَوَٰمِعُ وَبِيَعٌ
وَصَلَوَٰتٌ وَمَسَٰجِدُ يُذْكَرُ فِيهَا ٱسْمُ ٱللَّهِ كَثِيرًا ۗ
وَلَيَنصُرَنَّ ٱللَّهُ مَن يَنصُرُهُۥٓ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَقَوِىٌّ عَزِيزٌ ﴿٤٠﴾

"Wameruhusiwa kupigana wale wanao pigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia -
(Haw ani) wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, basi tu kwa kuwa wanasema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! …"

(Qur'ani, al-Hajj, 22:39-40)

Hatma ya Jerusalem ni kuwa jeshi la Kiislamu litalishambulia Taifa la Israeli na Masihi (Yesu mwana wa Maryamu) ndipo atakapotwaa madaraka ya kutawala dunia kutokea Jerusalem akiwa kama Mtawala Mwadilifu. Yesu, Masihi (*rehma na amani juu yake*) 'atatawala' akiongoza Taifa la Kiislamu ambalo litaanzishwa kwenye Ardhi Takatifu na kuchukua nafasi ya Taifa la kilaghai la Wayahudi wa Kizayonisti wa Israeli.

Pia ni hatma ya Jerusalem kuwa kabla ya matukio tajwa hapo juu kuweza kutokea, Taifa la Wayahudi la Israeli lazima liwe 'Taifa Tawala' la dunia. Israeli itatawala dunia kwa kipindi cha urefu wa *siku ambayo itakuwa kama wiki moja*. Itakapofikia mwisho wa kipindi hicho cha ugandamizaji na uonevu uliokithiri, *Dajjal*, Mtume wa Uongo, binafsi atajitokeza katika *siku yake ikiwa kama siku yetu*. Wakati huo, maji katika Bahari ya Galilei yatakuwa yamekauka. *Dajjal* 'atatawala' dunia kutokea Jerusalem na hivyo basi kutimiza jukumu na lengo lake la kujifanya Masihi wa kweli. Wakati *Dajjal* atakapojitokeza kama binaadamu ndipo kipindi ambapo *Imam al-Mahdi* naye atajitokeza.

Mtume (*rehma na amani juu yake*) alilizungumzia tukio hili kwenye *Hadith* ifuatayo:

"Mtume Muhammad *(rehma na amani juu yake*) alisema: Utume utabaki miongoni mwenu kwa kadiri ambavyo Mwenyezi Mungu atataka ubaki, na kisha Allah atauinua. Baadaye patakuwa na Khilafah kwa mujibu wa njia za Utume kwa kadiri ambavyo Mwenyezi Mungu atataka ubaki, kisha Allah atauinua. Baadaye patakuwa na utawala wa kurithi (kwa makubaliano) na utabaki kwa kadiri Allah atakavyotaka, kisha Allah atauinua. Baada yah apo patakuwa na ugandamizaji mbaya wenye mateso makubwa na utabaki kwa kadiri Allah atakavyotaka ubaki, kisha atauinua. Kisha patakuwa na khilafah kwa mujibu wa njia za Utume na hapo Mtume *(rehma na amani juu yake*) akabaki kimya"

(Musnad, Ahmad bin Hanbal)

Dajjal atamshambulia *Imam* kwenye mji wa Damaskas, na Yesu Masihi wa kweli, ndipo atakaposhuka na kumuua *Dajjal*, Masihi wa Uongo. Baada ya kuuawa kwa *Dajjal*, ndipo utafika muda ambapo *Ya'juj* na *Ma'juj* wa mwisho wataachiwa na kupita kwenye Bahari ya Galilei na kusema: "*hapa zamani palikuwa na maji*." *Ya'juj* na *Ma'juj* watamfuatilia Yesu masihi hadi kwenye mlima uliopo Jerusalem na Allah atampa amri Yesu aupande mlima huo. *Ya'ajuj* na *Ma'ajuj* hapo watajisifu kuwa wameshawaua wale waliokuwa ardhini na sasa wataanza kuwaua wale ambao wako mbinguni. Watarusha mishale yao kuelekea juu kwenye mawingu na Allah atiwezesha kurudi ikiwa imetapakaa damu. (Natumai patajitokeza mtu atakayeweza kuichambua na kuielezea maana ya *Hadith* hii katika kipindi kifupi kijacho, *Insha Allah*). Yesu Masihi ndipo atakapomuomba Allah awateketeze Ya'ajuj na Ma'ajuj na Allah atawateketeza kwa wadudu watakaowashambulia nyuma ya shingo zao. Wote wataanguka chini na asubuhi itakayofuatia siku hiyo wote watakuwa wamekufa.

Wakati *Ya'juj* na *Ma'juj* watakaposhambuliwa na kuteketezwa, hali tawala ya 'mfumo wa watu weupe' duniani itaanguka na ulimwengu wa kisayansi na teknolojia utaanguka. Kitabu hiki

kinatarajia kuwa matukio haya yatajitokeza ndani ya miaka hamsini ijayo. Ni katika kipindi hicho ndipo jeshi la Kiislamu litajitokeza kutokea *Khorasan* na litawakabili Wayahudi kwenye uwanja tambarare wa vita. Mtume (*rehma na amani juu yake*) alisema kwenye *Hadith* ambayo inapatikana kwenye *Sahih Bukhari* na pia kwenye *Sahih Muslim* kuwa Waislamu watapigana vita na Wayahudi. Haya ni maneno yake:

"Kwa hakika mtapigana na Wayahudi, na hakika mtawaua. (Na hali hiyo itaendelea) hadi (hata) mawe yataongea (na kusema): Enyi Waislamu! Kuna Myahudi amejificha nyuma yangu hivyo njoo na umuue.:

(Sahih Bukhari)

"Amesimulia Abu Hurairah: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alisema: Saa ya Mwisho (Kiama) hakitotokea hadi kwanza Waislamu wapigane dhidi ya Wayahudi. Waislamu watawaua Wayahudi hadi wajificho nyuma ya mawe au nyuma ya mti, na hilo jiwe au huo mti utasema: Ewe Muislamu, au Ewe mja wa mwenyezi Mungu, kuna Myahudi kajificha nyuma yangu, njoo umuue, isipokuwa mti wa Gharqad hautosema (kitu kama hicho) kwani ni mti wa Wayahudi."

(Sahih Muslim)

Ni rahisi sana kuwaengua wale wanazuoni wa Kiislamu ambao hawana uwezo wa kutoa mwongozo na mawaidha yenye kuzingatia ukweli unaohusu zama hizi. Ni wanazuoni ambao daima, au kwa uchache mkubwa mno, hawawezi kuisimulia *Hadith* hii wazi wazi kwenye jumuiya.

Hatma ya Jerusalem ni ile ambayo inawapa Waislamu imani kubwa kuliko zote na matumaini kuwa Ukweli utaushinda uongo na ulaghai, ikiwemo ugandamizaji na uonevu kwa kutumia mabavu.

Kitabu hiki kimeandikwa hasa kwa ajili ya kutimiza lengo hilo – la kutoa maelezo kwa Waislamu na kufafanua dunia ya ajabu ambamo leo hii tunajikuta tunaishi. Ni dunia ambayo lengo la Uislamu linaonekana kuwa ni lengo lililopotea na kupoteza mwelekeo. Lakini baada ya kukisoma kitabu hiki, msomaji sasa atajua, ikiwe hadi hapo alikuwa hajui, kuwa hali halisi iko kinyume kabisa na hiyo. Na pindi wakijua kwa uhakika kuwa ni hatma ya Jerusalem kutoa na kuyapa uthibitisho madai ya Uislamu kuwa ndiyo dini ya Kweli na Haki, Waislamu wataweza kukusanya nguvu za kustahmili na kukinga mashambulizi yanayoendelea hivi sasa duniani ambapo dunia isiyomtambua Mwenyezi Mungu inajaribu kufanya majaribio mengi iwezekanavyo ili kuivunja imani yao kwa Allah, Mola Mlezi Mtukufu.

Sehemu ya Pili

Israeli

Sura ya Kwanza

ARDHI TAKATIFU NA SHIRK YA KISIASA YA TAIFA LA ISRAELI



"Na tukampa Musa Kitabu, na tukakifanya muongozo wenye uwongofu kwa Wana wa Israili. (Tukawapa amri humo kwa kuwaambia): Msiwe na mtegemewa yoyote mwingine isipokuwa Mimi (kama Mpangaji na Mjaliaji Mkuu) wa mambo (yenu) yote!"

(Qur'ani, Banu Israil, 17:2)

(Shirk ni kuabudu chochote au yoyote mwingine zaidi ya Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*). Uchafuaji wa aina yoyote ile wa ibada hiyo ya Mungu Mmoja nayo pia ni *Shirk*. *Kufr* ni kukataa na kuupinga Ukweli.)

Israeli ni nchi ya kisasa yenye mwelekeo na msimamo wenye misingi ya kidunia isiyomuweka Mwenyezi Mungu na amri zake mbele ambayo ipo kwenye Ardhi Takatifu. Je, Taifa hili la kisasa lina uhalali gani wa kidini plae linapoangaliwa na kuhukumiwa kwa mujibu wa dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*)? Na je, Taifa hilo la kisasa lenye misimamo ya kidunia, lililoanzishwa kwenye Ardhi Takatifu, linafuata, au linavunja, masharti na amri za Mwenyezi Mungu za kurithi Ardhi Takatifu? Surah ii inajaribu kujibu maswali hayo.

Mfumo wa kisasa wa dunia

Ni jambo la kushangaza kuwa leo hii duniani ambako bado kuna tamaduni kadhaa mashuhuri na maarufu, nyingine zikiwa zimedumu kwa maelfu ya miaka, hakuna hata moja ambayo inamiliki eneo fulani. Popote alipo duniani, binaadamu amekumbatiwa na kusimamiwa na mfumo wa utaifa

uliobuniwa na Wazungu wa Ulaya. Hiki ni kitu ambacho ni cha aina yake pekee ambacho hakijawahi kutokea kwenye historia yote ya binaadamu. Ni kitu ambacho pia ni cha ajabu na chenye utata. Mfumo huu wa utaifa wa maadili kidunia ya kujitungia wenyewe mwishowe ulizalisha shirikisho la umoja wa aina mpya wa kimataifa ambalo (mwanzoni) liliitwa Shirikisho la Mataifa na baadaye kufufuliwa kama Umoja wa Mataifa. Ndani ya jina lenyewe la 'Umoja wa Mataifa' palipachikwa na kutukuzwa lengo la Mfumo Mpya wa Dunia uliotungwa na bara la Ulaya. Lengo hilo lilikuwa ni kuunganisha dunia chini ya mfumo wa kisiasa na utashi wa bara la Ulaya ili kuweza kuikamata na kuitawala dunia kama serikali ya dunia nzima. Katika kipindi ambacho kitabu hiki kinaandikwa, bara la Ulaya liko kwenye ukingo wa kuweza kujinyakulia ushindi wa mkakati huo wa kisiasa. Tamaduni na mataifa yote yasiyokuwa na asili ya Ulaya yanaonyesha kukosa nguvu za kujikwamua kutoka kwenye mshiko huu wa kidunia usiomtambua Mungu ulioanzishwa kwenye bara la Ulaya.

Arnold Toynbee, mwanahistoria maarufu mwenye asili ya Uingereza, amependekeza maelezo ya tukio hili lisilokuwa la kawaida kwa kusema kuwa tamaduni zote zilizopita (ikim. kabla ya utamaduni mpya wa kimagharibi) aidha '*zimekufa*' au '*ziko mahututi*' na hivyo basi *inayumkinika kuwa utamaduni wa kimagharibi nao pia utakumbwa na kuporokoka na kuvunjika kama huko ambako kumezikumba tamaduni zilizopita (Toynbee: Civilization on Trial (Utamaduni kwenye Hukumu) Oxford University Press, London, 1957: ukurasa wa 38.)*Lengo la wakazi wa bara la Ulaya lilikuwa wazi kabisa, lakini la kiajabu na la shari, nalo lilikuwa lengo la kujenga utawala wa Wazungu kuweza kuitawala dunia nzima. Toynbee amedhihirsha hili kwa msemo wake ambao ni wa wazi unaojitokeza kwenye muktadha ndani ya kitabu chake hicho maarufu *(Civilization on Trial - Utamaduni kwenye Hukumu)"*:

"Utamaduni wa kimagharibi hauna lengo pungufu ya kujumuisha binaadamu wote kuwa jamii moja kubwa na kukamata madaraka ya kuongoza kila kitu ardhini, kwenye hewa, kwenye maji…"

(Katika kitabu: ukurasa wa 166)

Lengo kubwa na la mwisho la Wazungu, hata hivyo, lilikuwa ni kuwarudisha Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu na kuwakabidhi Wayahudi *utawala* wa dunia ili waweze *kuitawala* dunia kutokea Jerusalem. Kitabu hiki kinaelezea na kufafanuaukweli huo ambao umejificha na hauonekani kwa yeyote anayetupia jicho la haraka haraka bila kufanya uchambuzi wa kina!

Qur'ani (al-Anbiyah, 21:96) imesema wazi kuwa watakapoachiwa huru na Mwenyezi Mungu, *Ya'juj* na *Ma'juj "watasambaa kwenda kila upande."* Kutokana na hilo, wale watu ambao

waliondolewa kutoka kwenye ‘Mji’ ambao uliteketezwa na Allah Mtukufu, ambao walipigwa marufuku kurudi hapo kwenye huo mji, sasa hivi watarejea na kuuchukua upya ‘Mji’ huo. Kitabu hiki kimeweka wazi sababu za kuthibitisha kuwa ‘Mji’ huo ni Jerusalem! Wakati *Ya’juj* na *Ma’juj “wakisambaa kuelekea kila upande*” itakuwa vigumu kwa binaadamu waliobaki kuwamudu kwa mujibu wa kauli ya Mwenyezi Mungu:

“Nimewaleta kutoka miongoni mwa waja Wangu watu ambao dhidi yao hakuna atakayeweza kupambana nao; wachukue watu hawa kwa usalama uwapeleke Tur, kisha Allah atawatuma Ya’juj na Ma’juj na watasambaa kuelekea kwenye kila upande.”

(Sahih Muslim)

Ni wazi kutokana na hayo kuwa utamaduni wa bara la Ulaya (baada ya ujio wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*)) ni utamaduni wa *Ya’juj* na *Ma’juj*.

Kitabu hiki pia kinaelezea tukio la ajabu la *Dajjal*, Masihi wa Uongo. *Dajjal* na *Ya’juj* na *Ma’juj*, kwa pamoja wanawakilisha moja ya alama kuu za Zama za Mwisho. Kwa kuwa ni lengo lake kuchukua kilaghai nafasi ya Masihi ambaye lazima atawale dunia kutokea Jerusalem, inalazimika kuwa naye, pia, lazima atawale dunia kutokea Jerusalem. Kitabu hiki kimepatambuamahali ambapo mwanzo kabisa *Dajjal* alipoanzia jitihada zake kuwa ni kisiwa cha Uingereza. Hivyo basi lengo kubwa na la mwisho la Wazungu lilikuwa ni kuwarudisha Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu na kuwakabidhi Wayahudi *utawala* wa dunia ili waweze *kuitawala* dunia kutokea Jerusalem!

Taifa la Israeli ambalo limejengwa kwa misingi ya kidunia, isiyomuweka mbele Mwenyezi Mungu na amri zake kwenye sharia na haki za wananchi wake, linakuwa ni sehemu ya nyenzo muhimu ambayo kwa kupitia kwayo, bara la Ulaya linadhamiria kutimiza lengo hilo.

Chanzo cha Taifa la kisasa lenye misingi ya kidunia

Taifa la kisasa linalojengwa kwa misingi ya kidunia lilijitokeza kwa mara ya kwanza kwenye bara la Ulaya baada ya utamaduni wa Kikristo wa Ulaya baada ya mashambulizi ya ajabu ya ndani kwa ndani baina ya wahusika wenyewe na likashuhudia mabadiliko yenye hatari kufuatia mapinduzi hayo. Mapinduzi hayo yalisababisha mabadiliko ya utamaduni uliokuwa umeegemea kwenye misingi ya imani ya dini ya Kikristo na Kiyahudi (kwani dini ya Kikristo ilizaliwa kutokana na dini ya Kiyahudi na kubadilishwa kuwa utamaduni wenye nguvu kubwa mno, usiomtambua Mungu, wenye

uwezo mkubwa sana wa kulaghai na usiokuwa wala kujali maadili. Haya yalikuwa ni matokeo ya kipekee, yenye msukumo mkubwa mno ambayo hayajawahi kutokea kabla katika historia yote ya bara la Ulaya.

Ukosekanaji wa maadili na mwenendo wa kutomjali na kutomtambua Mungu kulikojitokeza kwenye utamaduni huu mpya wa kisasa wa bara la Ulaya na kuonekana wazi pale ambapo ulipokumbatia 'uyakinifu.' Matokea ya hili ilimaanisha kuwa bara la Ulaya halikutambua tena kuwapo kwa hali nyingine yoyote halisi Zaidi ya hali 'uyakinifu.' Ukumbatiaji huu wa uyakinifu ulikuwa ni mwendelezo kuelekea kwenye hitimisho la faradhi la mantiki ya elimu mpya ya ufahamu (*epistemolojia*) ya 'jicho moja' ambayo inang'ang'ania kiubishi kuwa elimu au ufahamu unatokana na chanzo kimoja tu, nacho ni aidha kwa kufanya uchunguzi au majaribio. 'Jicho' la pili, ikim, jicho la ndani la hisia za kiroho, lilikataliwa kuwa ni njia nyingine ambayo kwayo, elimu inaweza kupatikana.

Taifa jipya la kisasa lenye misingi ya kidunia kwenye bara la Ulaya limezaliwa kutokana na kufuata matumizi ya nadharia za kutomjali na kutomtambua Mungu kwenye falsafa za kisiasa na nadharia ya kisiasa. Lakini huu siyo mwisho wake pekee! Japo huko nyuma kwenye historia paliwahi kujitokeza taifa lililojengwa kwa misingi ya kidunia, ni katika kipindi hiki cha kisasa pekee ndipo pametokea upokeaji na ufuataji mfumo huu mpya takriban na binaadamu wote dunia nzima kiasi cha kuwapo kwa mfumo mpya wa dunia usiomjali Mungu. Na dunia mpya ya kisasa imeibuka hususan baada ya mapinduzi hayo ya Ulaya ya hatari na yaliyokuwa na msukumo mkubwa. Mapinduzi hayo ya bara la Ulaya yamewakumba binaadamu wote duniani na kuwa kitu kimoja kwenye kuukumbatia na kuushikilia msimamo wa kidunia na kuwa na mfumo wa aina moja usiomtambua na usiomjali Mungu, wa kidunia na unaokosa maadili mema. Hili lilikuwa ni tukio la kipekee kabisa katika historia yote ya binaadamu. Je, kuna uwezekano wa kupatikana maelezo kamili ya matokeo haya? Madai yetu ni kuwa *Qur'ani* pekee ndiyo yenye maelezo ya jambo hili!

Mapinduzi yalileta mfumo usiomtambua Mungu yaliyotokea kwenye bara la Ulaya yalikuwa ni tukio la kustaajabisha Zaidi kwani yaliambatana na mapinduzi ua kisayansi na teknolojia ambayo yalilipa Ulaya 'nguvu' zilizoonekana kutokuwa na upinzani, na pia kuwa na 'haiba' na 'mvuto' uliyokuwa mgumu kuukataa. Ugunduzi wa injini ya mvuke, treni, magari ya abiria na mizigo, vifaru na silaha za kijeshi, meli zinazoendeshwa kwa injini za mvuke na mafuta, ndege n.k., zilibadilisha kabisa namna ambazo watu duniani waliweza kusafiri, kupigana vita, na hiyo ikapelekea na kuathiri namna na jinsi ya watu walivyokuwa wakiendesha maisha yao ya kila siku. Ugunduzi wa simu na telegrafu ulirahisisha mawasiliano ya haraka kwenye masafa makubwa nayo pia ilibadilisha namna na

hali za maisha ya watu. Mwishowe, mapinduzi ya nadharia ya haki na usawa wa wanawake yakawapa wanawake uhuru wa kujichukulia majukumu ya wanaume kwenye jamii kinyume cha na bila kujali tofauti za majukumu yalivyopangwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu *(Qur'ani, al-Lail, 92:1-4)*. Hilo lilishangiliwa na kupitishwa kuwa kama ni ukombozi wa mwanamke! Lilileta moja ya mabadiliko makubwa na ya hatari yenye msukumo mkubwa kabisa katika namna na jinsi ambavyo binaadamu wote wanaishi.

Ulaya mpya ilielekeza mashambulizi kwa binaadamu kwa kutumia silaha ya mvuto wa hisia asilia za kibinaadamu za uroho na ashki. Mapinduzi ya kingono yaliashiria kuweka wazi na kuiweka ngono – asilia na isiyokuwa ya kiasilia – inapatikana kirahisi na kila mahali kama mwanga wa jua. Ndoa na maisha ya ndoa yakawa yanakoseshwa umuhimu wake na watu wakawa huru kuchagua kuishi pamoja bila ya ndoa na kukubalika kuwa wanaendesha maisha yao kiheshima. Jacqueline Kennedy, mke wa raisi wa zamani wa Marekani John F. Kennedy na ikoni wa Amerika wa enzi za Camelot, aliishi miaka ya mwisho wa maishayake nje ya mfungo wa ndoa. Na alipofariki, 'mwenza' wake wa maisha mwenye asili ya Kiyahudi alikuwa akitambulishwa kwenye dunia kama 'rafiki.'

Usenge, ubasha na usagaji ukawa unatetewa kuwa ni moja ya namna mbadala za mahusiano ya kijinsia na zikawa zimekubalika kwenye fikra za jamii kwa kiwango kikubwa kiasi kwamba mchungaji au Rabbai msenge, basha au msagaji anaweza kujitokeza na kujitangaza hadharani na bado akaendelea kuheshimika na kukubalika baada ya hapo. Zaidi, hata neno lenyewe la 'kujamiiana kwa jinsia moja' limepewa hadhi ya kidunia na kuondolewa ubaya na uchafu wake uliokuwa ukijumuishwa na kujamiiana kusikokuwa kwa asilia. Likabadilishwa na kupewa jina la 'gay' na jamii iliyokuwa imekosa shuku ikalikubali neno na jina hilo kuwa halina lengo wala athari yoyote mbaya.

Mapinduzi ya ununuzi na utumiaji yaliwapa binaadamu uchu, hamu na njaa isiyotoshelezeka ya kujipatia bidhaa zaidi na zaidi zinazopendezesha jicho. Mapinduzi haya ya bidhaa za matumizi yamejipenyeza na kuwakumba binaadamu kiasi hata majiko, mabafu na vyoo ya watu wote ukiacha wale tu walio masikini wa kukithiri, yamebadilishwa kwa kiwango kikubwa kabisa.

Ulaya mpya isiyojali maadili na kutomtambua Mungu iliendelea kutumia 'nguvu' kushambulia na kukamata dunia iliyobaki na kuwa makoloni yao, na kisha ikatumia 'haiba' na 'mvuto' kuirubuni dunia nzima kuiga na kufuata mfumo wao wa maisha usiokuwa na maadili mema, uliomilikiwa na utamaduni wa manunuzi na matumizi, usiomuweka Mungu mbele na kutambua sheria na amri zake. Utamaduni huu wa kidunia wa Ulaya ulishuhudia mabadiliko ya kisiasa baada ya

mapinduzi ya Marekani, Ufaransa na Bolshevik kwenye miaka 1776, 1787-1800, na 1917. Mabadiliko ya kiuchumi yalishuhudia kuibuka kwa mfumo wa uchumi uliojengwa kwa misingi ya Riba, na mfumo huu ulitengamana vyema kupitia mapinduzi ya Waprotestanti. Mwishowe mabadiliko ya kijinsia na kitamaduni yalipatikana pale yalipoibukamapinduzi ya kijinsia yaliyoambatana na juhudi za kuwakomboa wanawake na kuwapa haki sawa na wanaume. Mapinduzi haya yote yasingeweza kupatikana kama isingekuwa yameambatana na mapinduzi ya sayansi na teknolojia.

Shirk na _Kufr_ ya Taifa la kisasa lenye mfumo wa kidunia

Baada ya mapinduzi hayo ya Kikristo ya Ulaya, utamaduni wa bara la Ulaya ambao kabla ya hapo ulikuwa umeegemea kwenye imani ya Mungu na kwenye Ufalme Wake wa enzi ulio huru na pia ulikuwa umeegemea kwenye Mamlaka Yake ya juu ya kila kitu (kwa kupitia nadharia ya Haki ya Kiroho ya Wafalme iliyokuwa ikikabidhiwa kwa 'wawakilishi wa Mungu duniani' iliyokuwa ikitumika kwenye Kanisa la Kirumi), yote haya yalisitishwa na utamaduni mpya uliacha kumtambua Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) nahapo hapo ukaacha pia kuutambua Ufalme wake na Mamlaka Yake na kuacha kuzitambua Sheria Zake kama ndizo zenye mamlaka na hadhi ya juu kabisa kutekelezwa. Badala yake, 'taifa la kisasa la kidunia' ndilo likaanza kutambuliwa kuwa lina 'uhuru na mamlaka ya juu kabisa' na hii ni *Shirk! (Shirk ni kuabudu yeyote asiyekuwa Mungu wa Abrahamu (rehma na amani juu yake). Shirk pia ni uchafuzi wa ibada ya Mungu Mmoja. Kufr ni kupinga na kukataa Ukweli!)* Mamlaka na sheria za 'taifa la kidunia' sasa zinatambuliwa kuwa ndiyo 'mamlaka ya juu kabisa' na hii pia ni *Shirk!* Taifa lina mamlaka ya kujichagulia *Halal* (ikim. kuamua kuwa kitu au jambo fulani linaruhusiwa kisheria) kitu au jambo ambalo Mungu wa Arahamu (*rehma na amani juu yake*) alilikataza kwa kusema kuwa ni *Haram* (ikim. kuwa haliruhusiwi kwa sharia Zake) – na taifa likaendelea kutekeleza hayo – na hiyo ni *Shirk!*

Shirk ni dhambi kubwa sana. Kwa hakika ni dhambi kubwa kuliko dhambi zote. Ni dhambi moja ambayo Mungu wa Abrahamu, Mtukufu, ameitaja kuwa Hatoisamehe:

إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغۡفِرُ أَن يُشۡرَكَ بِهِۦ وَيَغۡفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَآءُۚ وَمَن يُشۡرِكۡ بِٱللَّهِ فَقَدِ ٱفۡتَرَىٰٓ إِثۡمًا عَظِيمًا ﴿٤٨﴾

"Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe (na hatosamehe) kushirikishwa (Shirk), na husamehe yaliyo duni ya hilo kwa amtakaye. Na anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu (Shirk) basi hakika amezua dhambi kubwa."

(Qur'ani, an-Nisa, 4:48)

Yeyote anayetenda *Shirk*, na akafa katika hali hiyo, hatoweza kuingia peponi:

لَقَدْ كَفَرَ ٱلَّذِينَ قَالُوٓا۟ إِنَّ ٱللَّهَ هُوَ ٱلْمَسِيحُ ٱبْنُ مَرْيَمَ ۖ وَقَالَ
ٱلْمَسِيحُ يَٰبَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ ٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ رَبِّى وَرَبَّكُمْ ۖ إِنَّهُۥ مَن يُشْرِكْ
بِٱللَّهِ فَقَدْ حَرَّمَ ٱللَّهُ عَلَيْهِ ٱلْجَنَّةَ وَمَأْوَىٰهُ ٱلنَّارُ ۖ وَمَا لِلظَّٰلِمِينَ مِنْ
أَنصَارٍ ﴿٧٢﴾

"...Kwani anaye mshirikisha Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu atamharimishia Pepo, na mahala pake ni Motoni..."

(Qur'ani, al-Maidah 5:72)

Kuabudu masanamu ni moja ya aina iliyo wazi zaidi na isiyokuwa na mjadala ya *Shirk*. Aina hii ya *Shirk* kwa kiasi kikubwa imetoweka duniani. Lakini ulimwengu wa Hindu, bado wameikumbatia *Shirk* hiyo. Hivyo basi, muumini wa dini ya Kiislamu hana sababu ya kushindwa kuitambua Shirk inayofanywa na jamii ya Hindu! *Qur'ani* imeonya wazi waumini kuwa watakuta mara kwa mara, Wayahudi na wale wanaotenda *Shirk* (kama wale wanaoabudu masanamu) watakuwa wakionyesha chuki na uadui wa hali ya juu kabisa:

۞ لَتَجِدَنَّ أَشَدَّ ٱلنَّاسِ عَدَٰوَةً لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱلْيَهُودَ وَٱلَّذِينَ
أَشْرَكُوا۟ ۖ وَلَتَجِدَنَّ أَقْرَبَهُم مَّوَدَّةً لِّلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱلَّذِينَ
قَالُوٓا۟ إِنَّا نَصَٰرَىٰ ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّ مِنْهُمْ قِسِّيسِينَ وَرُهْبَانًا
وَأَنَّهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ ﴿٨٢﴾

"Hakika utawakuta walio shadidi kuliko watu wote katika (chuki na) uadui (wa hali ya juu kabisa) kwa walio amini (ikim. Waislamu) ni Mayahudi na washirikina. Na utawakuta walio karibu mno kwa mapenzi ni wale wanao sema: Sisi ni Manasara. Hayo ni kwa sababu wapo miongoni mwao makasisi na wamonaki, na kwa sababu wao hawafanyi kiburi."

(Qur'ani, al-Maidah, 5:82)

Lakini zipo aina nyingine za *Shirk* ambazo zmetajwa kwenye *Qur'ani*. Fir'auni, kwa mfano, alimwambia Nabii Musa (*rehma na amani juu yake*): *"Mimi ni Mungu wako Mtukufu,"* na akawambia Machifu wa watu wake: *"Enyi Machifu! Simjui Mungu wenu isipokuwa mimi mwenyewe…"*Hii ilikuwa *Shirk!* Kumuabudu Fir'auni kulikofanywa na watu wa Egypt kuliwataka wao kumkubali yeye na mamlaka yake kuwa ni ya juu kuliko yote kwenye ardhi ya Egypt. Hiyo pia ilikuwa *Shirk!*

Qur'ani imerudia mara kwa mara na kuwaonya wale ambao, kama Fir'auni, wanaunda *Hukm* (ikim. wanatengeneza mfumo wa sheria na mahakama kwa misingi 'zaidi ya', au 'kinyume cha' Mamlaka na Sheria za Allah. Hata hivyo, wakati amri za Mungu zinapowafikia watu (kama vile Wayahudi, Wakristo, Waislamu) na wakakubali muongozo huo, hapo mustakbali unakuwa tofauti kabisa. Ikiwa watu hao watapata fursa ya kujinyakulia madaraka juu ya ardhi hiyo, kama vile ambavyo Waislamu wa India walivyofanya walipoanzisha Pakistan, na kisha wakashindwa kuisimamisha sharia kwa mujibu wa amri za mwenyezi Mungu, hapo *Qur'ani* kwa sauti moja inawashutumu na kuwakosoa kuwa wanatenda *Kufr* (wanakataa imani), *Dhulm* (uvunjaji sheria) na *Fisq* (udhalimu na dhambi kubwa):

"…Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri."

"…Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhaalimu."

"…Na wasio hukumu kwa yale aliyo yateremsha Mwenyezi Mungu basi hao ndio wapotofu."

(Qur'ani, al-Maidah, 5:44-47)

Kwa kuwa tamko la Fir'auni na matumizi yake kwenye ardhi ya Egypt lilikuwa ni tendo la *Shirk*, kwa mantiki hiyo hiyo, tamko kama hilo la taifa la kisasa lenye msimamo wa kidunia nalo pia ni *Shirk!* Na kwa kuwa Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) ametamka kuwa: *"…Na wasio hukumu kwa aliyo teremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri, madhaalimu na wapotofu"*na taifa la kisasa la kidunia imefanya hayo, hivyo basi mantiki inapelekea kuwa Wayahudi, Wakristo na Waislamu n.k. ambao wanaunda taifa la kisasa la kidunia baada ya kupokea Amri na

Sheria za Mwenyezi Mungu kwa kupitia Agano la Kale, Zaburi, Agano Jipya na *Qur'ani,* watakuwa na kosa la kufanya *Kufr, Dhulm na Fisq!*

Ikiwa Myahudi, Mkristo au Muislamu atapiga kura kwenye uchaguzi wa kitaifa kwenye taifa lenye msimamo wa kidunia, hiyo itamaanisha kuwa amekichagua hicho chama alichokipigia kura kuwa kinafaa kuwa na mamlaka na madaraka ya utawala juu yake. Na ikiwa kile chama kwenye serikali yake kikatenda *Shirk, Kufr, Dhulm* au *Fisq*, hapo maana yake ni kuwa huyo Myahudi, Mkristo au Muislamu, atakuwa amefuatana na kukubaliana na chama chake na serikali yake kwenye *Shirk, Kufr, Dhulm* na *Fisq!* (Hivyo hivyo pia utakuwa ukweli kwa wafuasi wa Hindu, Buddha n.k.). *Qur'an*i pia imelaani na kuita *Shirk* tendo lolote la kuifanya *Halal* chochote ambacho Allah amekifanya kuwa *Haram* (na pia kinyume cha hilo). Hivyo basi, amri ya Mungu imeshuka kutoka kwa Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) ambamo Amewakataza kutenda hasa dhambi hiyo iliyo kubwa mno:

اتَّخَذُوٓا۟ أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَٰنَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ ٱللَّهِ
وَٱلْمَسِيحَ ٱبْنَ مَرْيَمَ وَمَآ أُمِرُوٓا۟ إِلَّا لِيَعْبُدُوٓا۟
إِلَٰهًا وَٰحِدًا ۖ لَّآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۚ سُبْحَٰنَهُۥ عَمَّا
يُشْرِكُونَ ﴿٣١﴾

"Wamewafanya makuhani wao na wamonaki (wachungaji) wao kuwa ni Miungu na Mabwana watawala badala ya Mwenyezi Mungu, na pia (wamefanya hivyo hivyo kwa) Masihi bin Maryamu. Na wala hawakuamrishwa (hivyo) isipo kuwa (waliamrishwa) wamuabudu Mungu Mmoja, hapana mungu (mwingine) ila Yeye. Subhanahu, Ametakasika na hayo wanayo mshirikisha nayo."
(Qur'ani, al-Taubah, 9:31)

Baada ya ayah ii kuteremshwa, pana mtu alimfuata Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) na kumlalamikia kuwa Wayahudi na Wakristo hawawaabudu Marabbai (Makuhani) na Wachungaji wao. Inakuwaje, hapo Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) anawashutumu kwa kosa kama hilo? Mtume alilijibu swali hilo kwa swali lisilohitaji jibu: Je, hawakugeuza kuwa *Halal* yale ambayo Allah aliyafanya kuwa *Haram?* Hiyo alisema ilikuwa ndiyo *Shirk* yao! Kisha

akaongeza: Je, watu (ikim. Wayahudi na Wakristo) hawakuwafuata kwenye hayo? Hilo, akasema, ndiyo *Shirk*! Miongoni mwa mambo yaliyokuwa Haram na kufanywa kuwa *Halal* ilikuwa pamoja na kamari na bahati nasibu, kuuza na kunywa pombe, pamoja na kutumia *Riba* (asilimia za riba). Kwenye sehemu kadhaa Taurati yenyewe imebadilishwa ili kuruhusu *Riba* iwe *Halal* (tazama kitabu chetu*: Dini ya Abrahamu na Taifa la Israeli – Mtazamo wa Qur'ani*)

Pale ambapo Wayahudi walitenda mambo haya, Nabii Daud (*rehma na amani juu yake*) na Nabii Isa - Yesu (*rehma na amani juu yake*) waliwalaani:

لُعِنَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ مِنۢ بَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ عَلَىٰ لِسَانِ دَاوُۥدَ
وَعِيسَى ٱبْنِ مَرْيَمَ ۚ ذَٰلِكَ بِمَا عَصَوا۟ وَّكَانُوا۟ يَعْتَدُونَ ﴿٧٨﴾
كَانُوا۟ لَا يَتَنَاهَوْنَ عَن مُّنكَرٍ فَعَلُوهُ ۚ لَبِئْسَ مَا
كَانُوا۟ يَفْعَلُونَ ﴿٧٩﴾

"Walilaaniwa walio kufuru miongoni mwa Wana wa Israili kwa ulimi wa Daud na wa Isa mwana wa Maryamu. Hayo ni kwa sababu waliasi na wakawa wanapindukia (wanavuka) mipaka. Walikuwa hawakatazani maovu waliyo kuwa wakiyafanya. Hakika ni maovu yalioje mambo waliyo kuwa wakiyafanya!"

(Qur'ani, al-Maidah, 5:78-9)

Yeyote anayekufa akiwa ana laana ya Mtume juu yake mtu huyo hana nafasi yoyote ya kuukwepa moto wa Jahannamu! Kwa uhakika ni jambo la kinafiki kwa mtu yeyote kudai kuwa anamuabudu Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) na kisha kuendelea mbele baada ya hapo na kuhalalisha (kufanya *Halal*) kile ambacho Mungu ameamrisha kiwe *Haram* na kisha kuzuia kile ambacho kimeruhusiwa:

ٱلْمُنَٰفِقُونَ وَٱلْمُنَٰفِقَٰتُ بَعْضُهُم مِّنۢ بَعْضٍ ۘ يَأْمُرُونَ
بِٱلْمُنكَرِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمَعْرُوفِ وَيَقْبِضُونَ أَيْدِيَهُمْ ۚ
نَسُوا۟ ٱللَّهَ فَنَسِيَهُمْ ۗ إِنَّ ٱلْمُنَٰفِقِينَ هُمُ
ٱلْفَٰسِقُونَ ﴿٦٧﴾

"Wanaume wanaafiki na wanawake wanaafiki, wote ni hali moja. Huamrisha maovu na huyakataza mema, na huifumba mikono yao. Wamemsahau Mwenyezi Mungu, basi na Yeye pia amewasahau. Hakika wanaafiki ndio wapotofu."

(Qur'ani, al-Taubah, 9:67)

Kama ilikuwa *Shirk* kwa makuhani na wachungaji kuyafanya *Halal* yale ambayo Allah aliyafanya *Haram*, basi pia inakuwa ni *Shirk* ikiwa serikali itafanya jambo hilo hilo. Ikiwa hayo yalikuwa ni matendo ya kinafiki wakati ule, nayo itabaki kuwa hivyo hivyo hivi sasa. Na kama matendo hayo yalilaaniwa na Mitume kipindi kile, basi vile ile yangelaaniwa na Mitume kiindi hiki!

Kwa kawaida namna mojawapo ya kulichunguza somo hili kwa kina ni kupima 'faida' na 'hasara' za waumini kushiriki kwenye chaguzi za kisiasa kwenye taifa la kisasa la kidunia**.** Watetezi wa mfumo wa kidunia hutumia maneno matamu yaliyopangwa kwa ustadi mkubwa. Husema kuwa huu ni mfumo wa kisiasa uliopiga hatua kubwa sana kimaendeleo katika historia yote ya binaadamu. Wengine husema: "Ikiwa hatutoshiriki kwenye chaguzi za kisiasa, hatutokuwa na wawakilishi ambao wangepigania haki zetu." Na kwenye fikra za kina zaidi panapendekezwa na kutolewa hoja nzito zaidi: "Kushiriki kwenye chaguzi za kisiasa ni kiungo muhimu katika kuhakikisha kuwa tunafanikiwa kubadilisha mfumo wa kidunia usiomtambua Mungu" Suala la *Shirk* linachukuliwa kama kisingizio (ikim. namna au chombo cha mkakati): "Tutashiriki kwenye chaguzi lakini tutafanya hivyo kwa misingi ya wazi kuwa hatukubaliani na katiba ya kutungwa na watu bila kujali amri za Mungu na tunapinga taifa lenye mfumo wa kidunia ambayo katiba hiyo inalilinda. Kifungu hiki cha kujitoa kitatulinda na *Shirk*."

Jibu letu ni kupigilia mstari ukweli kuwa kushiriki kwenye uchaguzi wa kisiasa kwenye taifa lenye msimamo wa kidunia ipso facto kunatia mkazo kuukubali mfumo wa kidunia wa taifa husika. Taifa lenye msimamo wa kidunia usiomtambua Mungu unasema kile kile ambacho Fir'auni alimwambia Nabii Musa (*rehma na amani juu yake*). Na msemo huo ni kuwa: Taifa ni huru. Mamlaka yake hayana mpinzani wala kikomo. Sheria zake hali kadhalika, hazina mpinzani, kikomo na hazimtegemei yoyote, zikitungwa na kupitishwa lazima zifuatwe bila kujali kama zinapingana na sheria za Mungu. Hiyo ni *Shirk!* Watu wanapopiga kura kwenye uchaguzi kwenye nchi yenye msimamo wa kidunia, hapo maana yake ni kuwa wanakubali madai ya taifa hilo kuwa ni huru. Pia

wanakubali madai ya kuwa na mamlaka ya juu kabisa na kukubali kuwa sharia zake hazina mpinzani. Waumini wanapopiga kura kwenye nchi kama hiyo, hawawezi kujitenga na kosa la kutenda *Shirk!*

Pili, waumini wanapopiga kura kwenye taifa la namna hiyo wanalazimika kukipigia kura chama fulani. Ikiwa chama hicho, kikiwa kama serikali kikageuza kuwa *Halal* kile ambacho Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) alikifanya kuwa *Haram* au kupitisha sharia kama hizo, hapo serikali hiyo inakuwa imetenda *Shirk!* Duniani kote leo hii serikali na mabunge ya nchi zenye misimamo ya kidunia, zimeshageuza kuwa *Halal* karibu yale yote ambayo Allah aliyaamrisha yawe *Haram*. Wakati waumini wanapiga kura kuvipigia vyama vya siasa na serikali zilizokwishapitisha *Shirk* juu ya *Shirk*, kura hizo zitamaanisha kuwa watu hao wanafaa kuwatawala. Hiyo inamaanisha kuwa waumini watakuwa wanawafuata kwenye *Shirk, Kufr, Dhulm* na *Fisq!*

Tatu, utaratibu huu unaenda kinyume kabisa na unahitilafiana na *Sunnah* ya Mtume wa *Islam* (*rehma na amani juu yake*).

Vyama vya siasa na serikali zake duniani kote leo hii vina wanachama na viongozi wake ambao wamedumu kwenye kudharau na kuendelea kubadilisha kuwa *Halal* yale ambayo Allah amemarisha yawe *Haram*. Sura hii imewakilisha mifano kadhaa inayothibitisha madai hayo. Wakati waumini wanawapigia kura watu hao na vyama hivyo kwenye chaguzi za kisiasa na kuwaona kuwa wanafaa kuwatawala, waumini wanapaswa kukaa kitako kwanza na kutafakari nini maana ya wao kuwapigia kura na kuwapa ushirikiano wao. Watu wakiwa wanadumu kwenye Haram kwa dharau, watu hao wanakuwa wanapata hasara kubwa sana. Ni Dhahiri kuwa mataifa ya kidunia yanapata hasara kubwa sana. Ni hasara ipi hiyo?

فَلَمَّا عَتَوْا عَن مَّا نُهُوا عَنْهُ قُلْنَا لَهُمْ كُونُوا قِرَدَةً خَاسِئِينَ ﴿١٦٦﴾

"...Walipo jifakharisha (kwa dharau na kuendelea kutenda) katika waliyo kanywa tuliwaambia (ikim. Tuliamrisha): Kuweni (kama) manyani wa kudharauliwa!

(Qur'ani, al-Araf, 7:166)

Hii inamaanisha kuwa hivi sasa wataishi kama manyani, kwa kupoteza uwezo wote waliokuwa nao wa kujizuia na kujilinda na hisia kali za aina zote (ikiwemo hamaki, mapenzi, haiba, n.k.) kiasi itakapofikia kipindi cha 'Zama za Mwisho' watakuwa wamefikia kiwango cha kufanya tendo la ndoa hadharani kama wanyama: punda, nyani n.k.

Taifa lenye mfumo wa kidunia limehalalisha ukopeshaji wa pesa kwa *Riba*. Dunia nzima namba kubwa na inayoongezeka siku hadi siku ya nchi hizo imekwishahalalisha kamari na bahati nasibu, matumizi na uuzaji wa vilevi (mfano pombe) na nyama ya nguruwe, matumizi ya pesa za makaratasi ambayo daima zinapoteza thamani (na inapotokea hiyo, umma wote unaibiwa kilaghai na

kubaki wamefungwa kwenye jela ya ‘ajira za kitumwa’). Utoaji mimba, mahusiano ya kingono ya watu wa jinsia moja, uasherati, uzinzi yote hayo yanahalalishwa. Kuna makampuni marekani ambayo yanajitangaza kwa wale wanaotaka kuuza Watoto wao. Pia pana hata Huduma ya Kukuletea Kondom popote ulipo kwa wale ambao wangetaka kujinyakulia fursa iliyojitokeza bila kutarajia!

Duniani kote leo hii kwenye nchi nyingi za kisasa zenye mwelekeo wa kidunia hakuna tena nchi inayofuata sharia ya Mwenyezi Mungu kuwa mtoto wa kiume anapaswa arithi maradufu kuliko dada yake. Wanapitisha sheria zao kwa madai kuwa sheria hii inawabagua wanawake, na hiyo ya kwao inatoa haki zaidi kuliko sheria ya Allah. Kwa uhakika, sheria yao siyo sheria kabisa. Mtu anaweza kumuachia punda wake urithi wa mali zake zote na kumnyima kumwachia chochote mke wake na watoto wake mwenyewe! Taifa la kisasa linamkataza mwanaume kuoa wake zaidi ya mmoja kwa madai kuwa kufanya hivyo ni kuwabagua wanawake. Badala yake, wamelazimisha kwa mwanamume kuoa mke mmoja tu, muda wote, na hiyo, wanadai, inaondoa uonevu na unyimaji wa haki ambao umo kwenye Sheria ya Allah! Jambo hili limeishia kuleta mapinduzi ya kijinsia ambayo yanadhalilisha heshima na hadhi ya ndoa! Mwanamke hana tena wajibu, kisheria wala kimaadili, wa kumuheshimu mume wake kwani kufanya hivyo atakuwa anabaguliwa kutokana na usawa baina ya mwanamume na mwanamke. Jua halijawahi kuchomoza kwenye dunia yenye maajabu kuliko dunia hii ya kisasa, isiyomtambua Mungu iliyojaa mvuto na haiba, dunia-Ulaya, ambayo kwa hakika ni ishara mbaya!

Alama kuu ya utambuzi wa dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*) ni kuwa ndani yake hakuna kabisa nafasi yoyote ile kwa Kufr (kutoamini) na *Shirk* (uchafuzi wa, au kukana imani na ibada ya Mungu Mmoja wa Kweli). Wakati mfumo wa kidunia wa kisiasa wa utamaduni usiomtambua Mungu wa Kikristo wa Ulaya, sasa hivi unaojulikana kama utamaduni wa kisasa wa kimagharibi, umejengwa kwa misingi ya *Kufr* na *Shirk*. Umoja wa Mataifa ulianzishwa hususan kwa misingi hiyo hiyo ya *Shirk*. Katiba yake inasema kuwa Allah Mtukufu siyo tena *al-Akbar!* Kifungu cha 24 na cha 25 kinasema kuwa Baraza lake la Usalama lina mamlaka ya juu kabisa na ya mwisho duniani kwenye masuala yote yanayohusiana na usalama na amani kote duniani. Kwa maneno mengine, mamlaka ya Baraza la Usalama yako juu ya mamlaka ya Allah na Mjumbe wake Muhammad (*rehma na amani juu yake*). Hii ni *Shirk!*

Vipi basi tunaweza kuelezea kwa *Banu Israil* kuukubali mfumo wa taifa la kisasa la kidunia ndani ya Ardhi Takatifu (ikim. Taifa la Israeli)? Na pia vipi kwa Waislamu dunia nzima kuukubali mfumo huu wa taifa la kidunia (Jamhuri ya Uturuki, Ufalme wa Saudi Arabia, Jamhuri ya Pakistani,

Taifa la Malaysia, n.k.), yakiwa kama kiungo ama chombo mbadala wa Ukhalifa? Huenda ikawa huu ni muda muafaka wa kuelezea nini ilikuwa Khilafa na kisha kulinganisha na taifa la kisasa la kidunia. Ukosefu wa elimu leo hii duniani umefikia mahali ambapo hata Waislamu hawalijui somo hili.

Khilafa na taifa la kisasa lenye misingi ya kidunia

Mfumo wa Khilafa wa *Kiislamu* ulikuwa ni muundo wa taifa na mpangilio wa kisiasa ambao ulikuwa ukitambua Uhuru, Mamlaka na Utawala na Sheria za Allah kuwa ni za juu kabisa na za mwisho, na kutokana na hilo, Khalifa alihakikisha kuwa kwa mujibu wa amri za Mwenyezi Mungu Mtukufu *Haram* inatekelezwa kama *Haram*, na *Halal* kama *Halal*. Khilafa iliibuka kutokana na utekelezaji wa matakwa maalum yanayotokana na amri ya kumtii Allah, Mjumbe Wake na *'wale waliokuwa na mamlaka miongoni mwa Waislamu.'*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَطِيعُوا۟ ٱللَّهَ وَأَطِيعُوا۟ ٱلرَّسُولَ وَأُو۟لِى ٱلْأَمْرِ مِنكُمْ ۖ فَإِن
تَنَٰزَعْتُمْ فِى شَىْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى ٱللَّهِ وَٱلرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ
ٱلْءَاخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥٩﴾

"Enyi mlio amini! Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi. Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hayo ndiyo bora zaidi na ndiyo yenye mwisho mwema."
(Qur'ani, An-Nisa, 4:59)

Uislamu unakataa kuutambua mfumo na mpangilio wa mgao wa utiifu – kuwa mu atatii amri za Allah na wakati mwingine atatii amri za kitaifa. Dunia hizo mbili (dunia ya kisiasa na kidini) hazikupaswa kutenganishwa kwa sababu *Qur'ani* imesema: "*Allah ni wa Kwanza na wa Mwisho, aliye Dhahiri na Asiyeonekana." (Qur'ani, al Hadid, 57:3).* Utiifu mkubwa kabisa kuliko wote Muislamu anapaswa kuuelekeza kwa Allah, na siyo kwa taifa, kwa kuwa *Qur'ani* inawataka waumini waseme:

قُلْ إِنَّ صَلَاتِى وَنُسُكِى وَمَحْيَاىَ وَمَمَاتِى لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿١٦٢﴾

"Sema: Hakika Sala yangu, na ibada zangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote."

(Qur'ani, al-An'am, 6:162)

Wazungu wa Ulaya waliuharibu mfumo wa taifa la Kiislamu na utaratibu wa kisiasa wakati utawala wa Khalifa wa Ottoman ulipolengwa kwa mashambulizi na kuteketezwa. Watu hao wa Ulaya waliendelea mbele na kuweka mikakati inayohakikisha kuwa Ukhalifa hauwezi kurudishwa tena. Walifanya hivyo kwa kuhakikisha kuundwa kwa Taifa la Saudi Arabia ndani ya *Hejaz*, na kisha waliendelea kuhakikisha kuwapo kwa taifa hilo kwa kuwapa dhamana na usalama wake. (Tazama kitabu chetu: *Ukhalifa, Hejaz na Taifa la Wahhabi wa Saudia*). Khilafa haikuweza kurudishwa kwa sababu mbili. Kwanza, utawala wa *Wahhabi wa Saudi* uliokuwa na mamlaka juu ya *Haramain, Hejaz* na *Hajj* haukudai kutaka kuwapo kwa Khilafa. Pili, kwa muda wote ambao watakuwa wameshikilia *Haramain, Hejaz* na *Hajj* hakuna ambaye angeweza kudai kurudisha Ukhalifa bila ya kuwa na mamlaka ya hayo mambo tajwa hapo juu!

Kuna sababu kadhaa zinazoelezea kwanini bara la Ulaya lililenga kuharibu utawala wa Khalifa wa Kiislamu. Ya kwanza, bila ya shaka yoyote ilikuwa ni kuwawezesha kufanikisha lengo la kuikomboa Ardhi Takatifu na kuwarudisha Wayahudi kwenye Ardhi hiyo. Lakini sababu ya pili ndiyo iliyokuwa ya kuhakikisha kuwa dunia nzima inaukumbatia mfumo huu mpya wa *Shirk* ulioanzishwa wa tifa la kisasa la kidunia lisilofuata maadili na amri za Mwenyezi Mungu. Wakati Khilafa inavunjwa, mfumo wa kisasa wa Kitaifa la Uturuki ndiyo uliochukua moja kwa moja nafasi ya Khilafa. Baadaye iliibuka Taifa la kidunia la Iran, kwenye chimbuko la Uislamu wa *Kishia*, baadaye likaibuka Taifa la kidunia la Saudi Arabia kwenye chimbuko la Uislamu wa *Kisunni*. Mwishowe, Waislamu wa Kihindi nao wakadanganyika na kulikubali Taifa la kidunia la Pakistani. Tatu, Khilafa ilibidi ivunjwe kwa sababu ilikuwa ni kipingamizi katika utekelezaji wa lengo maalum la Ulaya isiyomtambua Mungu ambalo lilikuwa ndiyo ajenda yao. Ajenda hiyo ilikuwa ni kuundwa kwa Taifa la Israeli kama 'Taifa Tawala' la dunia nzima – litakaloitawala dunia tokea Jerusalem.

Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alitabiri kuwa Khilafa itapotea na kutoweka kabisa duniani. Aliyasema hayo kwenye *Hadith* ifuatayo:

"Mtakuwa kwenye hali gani pale ambapo mwana wa Maryamu atashuka na kuwa miongoni mwenu na Imamu wenu (ikim. Amirul Mu'uminiin au Khalifa) atakuwa anatokana miongoni mwenu (ikim. atakuwa Muislamu)?"

(Sahih, Bukhari)

Hadith hii inatufunulia mambo matatu:

Kwanza, inatufahamisha kuwa Khilafa itakuwapo duniani kwenye ‘Zama za Mwisho’ Hii inafikia utabiri kuwa Khilafa itapotea na kutoweka duniani lakini siku moja itarejeshwa. Pili, kabla Khilafa haijarejeshwa upya, Waislamu wataishi kwa kipindi fulani chini ya utawala na mamlaka ya wale ambao siyo Waislamu. Na hii ndiyo hakika hali halisi iliyopo duniani leo hii. Tatu, kurejea kwa Khilafa kutakuwa ni tendo au tukio la pamoja na kurejea kwa Yesu mwana wa Maryamu. Na kwa kuwa tunajua kuwa kurudi kwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) kutaambatana na kutawala dunia kama Mtawala Muadilifu atakayesimamia Sheria na Amri za Allah, faradhi ya mwisho wa mantiki hiyo ni kuwa Taifa la kidunia la Israeli la sasa hivi litanyang’anywa nafasi hiyo na badala yake nafasi hiyo itachukuliwa na Taifa halali la Kiislamu katika Ardhi Takatifu ambalo litakuwa huru na kuachana na *Shirk.*

Wale ambao wameng’ang’ania kutetea status quo ya mataifa ya Kiislamu yenye mfumo wa kidunia inawapasa wakae kitako na kutafakari juu ya utabiri wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) unaohusiana na kurejeshwa kwa khilafa. Kwa mujibu wa hisabu zetu, utabiri huu unawezekana ukatekelezeka ndani ya miaka hamsini ijayo.

Faida za taifa la kisasa lenye mfumo wa kidunia

Taifa la kisasa lenye mfumo wa kidunia lisingeweza kukubalika miongoni mwa Wazungu-Wakristo na Wazungu -Wayahudi au miongoni mwa Waislamu kama lisingeificha *Kufr* na *Shirk* zake kwa kutumia na kuonyesha baadhi ya faida zilizo wazi. Je, ni faida zipi hizo? Mfumo huu wa kidunia wa utaifa uliibuka kwenye bara la Ulaya ambapo ulikuwa ni majibu ya mfumo ulioshupaa wa kigandamizi wa kidini wa Kikristo wa Ulaya, ukawa unaupeleka changamoto ‘*ya muda mfupi*’ kwa nguvu za Kanisa la Ulaya la Kikristo. Ulilipinga Kanisa lilipotangaza ‘mtazamo mpya’ wa kusisimua ulioruhusu uhuru kamili wa kutumia akili na mantiki bila kipingamizi kwenye masuala ya kidini na imani ikiwemo haki za binaadamu kwa wote, uhuru wa kuabudu kwa wote. Pia iliashiria kanuni za kisiasa ambazo zingelinda uhusiano wa amani baina ya makundi tofauti ya kidini kwenye eneo moja. Hivyo basi ulifanikiwa kusitisha vita vya kidini na umwagaji damu ambao ulilikumba bara la Ulaya kwa karne kadhaa.

Pia kwa ustadi mkubwa mfumo huu wa kidunia ‘ulijilipia rushwa’ na kuilaghai dunia na kujiingiza mioyoni mwa binaadamu takriban wote kwa kutumia mbinu nzuri sana za ubunifu. Uligundua au ulitengeneza mengi kati ya yale ambayo binaadamu waliyakumbatia kwa furaha, bila kujali imani za kidini, kama ni utatuzi muhimu wa mfumo wa maisha ya kisasa, mfano umeme, radio,

simu, na simu za mkononi, runinga, kompyuta, ndege, magari, machine za nukushi, teknolojia ya fotokopi, n.k. Popote pale ambapo mtu aliukumbatia mfumo mpya wa maisha wa kisasa pamoja na vibwagizo vyake vyote vya kustaajabisha vyenye misingi yake iliyojengwa kwenye teknolojia, mtu huyo alijikuta ameukumbatia mfumo huo mpya wa taifa lenye misingi ya kidunia na utaratibu wake mzima wa maisha. Huo ulikuwa ni ushindi mkubwa mno kupita kiasi!

Uhalisia wa taifa la kisasa lenye misingi ya kidunia

Hata hivyo pamoja na hizi faida zilizo wazi za mfumo wa taifa la kidunia (ambazo baadhi yake pia zilipatikana kwenye mji-Taifa wa Madina ulioanzishwa na Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*), mfumo huo haukubadilisha misingi halisi ya *Kufr* na *Shirk*. Uhakika ulipatikana punde baada ya taifa la kidunia lilipoanza taratibu kupiga vita mwenendo wa maisha ya kidini. Kadiri jumuiya ilivyokuwa ikiukubali mfumo dunia, watu waliokuwa wakienda kusali makanisani wakawa wanapungua na kuzidi kuwa wachache, hadi kufikia mahali ambapo makanisa na masinagogi yaliyobaki matupu kwa kukosekana waumini yakaanza kuuzwa na kugeuzwa kuwa maholi ya michezo ya 'bingo' na bahati nasibu. Kwa hakika dini ikaendelea kupungua nguvu kwenye dunia yenye mfumo usiomtambua Mungu.

Demokrasia ya taifa la kidunia imebainika kuwa ni kidonge kilichobandikwa gamba la sukari ilhali ndani yake ni sumu. 'Siasa' za kidemokrasia zilifanya kazi kuhakikisha kuwa zinasimamisha mfumo wa ugandamizaji wa kiuchumi na unyonyaji wa wengi (kwa kuwa uchumi umeegemea kwenye *Riba*). Ugandamizaji huu wa kiuchumi mara nyingi uliambatana na ubaguzi wa rangi na kikabila. Umma wa masikini walio wengi haukuweza kupokonya madaraka kutoka kwa matajiri wachache, na hivyo hawakuweza kuwa na nguvu za kupigana na kuumaliza ugandamizaji wa kiuchumi. Hii ni kwa sababu aghlabu ni utajiri wa wale wanyonyaji wachache ndiyo uliokuwa ukitumika kusababisha aidha ushindi au kushindwa kwenye kampeni za uchaguzi zinazohitaji matumizi ya pesa nyingi. Injili mpya ya taifa la kidunia ikawa *matajiri ndiyo watakuwa warithi wa nchi*. Na hiki ndicho hasa kilichotokea.

Ulaya mpya ikaendelea kutumia nguvu zake zisizokuwa na mpinzani za kivita pamoja uwezo wake mkubwa mno wa kulaghai na kughilibu mataifa yote yasiyokuwa yenye asili ya bara la Ulaya. Mfumo mpya wa falsafa isiyomtambua Mungu, pamoja na wazo la taifa huria, mfumo wa kigandamizi wa kiuchumi na utamaduni wa uchafuzi, mwishowe uliirubuni dunia nzima. Huo nao ulikuwa ushindi mkubwa mno!

Utawala wa kikoloni wa nchi za magharibi sasa ukawa umelazimishwa kukubalika na binaadamu wote, wakiwemo Waislamu na kwa kupitia njia hii mpangilio mpya wa kisiasa, ulioegemea kwenye *Kufr* na *Shirk*, ukaingizwa kinyemela. Khilafa ya *Kiislamu* ya Ottoman, ilivunjwa na kwenye gofu lake liliibuka Taifa la kisasa la Uturuki. *Dar al Islam* ambayo ilianzishwa na mwenyewe Mtume (*rehma na amani juu yake*) kwenye ghuba ya Arabia nayo ilivunjwa na nafasi yake ikachukuliwa na Taifa la kidunia la Saudi Arabia (likiwa kamilifu pamoja na mapambo yake kama vile uhuru wa eneo husika, uraia na haki zake, n.k.) ikiwa kama nchi-mteja wa mataifa ya magharibi yasiyomtambua Mungu. Hivyo basi utabiri wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ukawa umekamilika! Alitabiri kuwa umma wake (wa Waislamu) utawaiga na kuwafuata Wayahudi na Wakristo kiasi kwamba hata hao (Wayahudi na Wakristo) wangeishia kuingia kwenye shimo la kenge, basi umma wake nao pia ungefanya hivyo hivyo kwa kuwafuata humo!

Matokeo ya haya yote ni kuwa umma wa Wayahudi, Wakristo na Waislamu kwa pamoja umeingia kwenye majaribu makubwa kuliko jaribu lolote lililowahi kutokea huko nyuma kwenye historia ya binaadamu (*fitnah*) na wote wameshindwa na kuanguka kwa kishindo kikubwa katika kufuata amri za Mungu Mtukufu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*), pale alipoamrisha:

اتَّبِعُوا مَا أُنزِلَ إِلَيْكُم مِّن رَّبِّكُمْ وَلَا تَتَّبِعُوا مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ ۗ قَلِيلًا مَّا تَذَكَّرُونَ ﴿٣﴾

“Fuateni mliyo teremshiwa kutoka kwa Mola Mlezi wenu, wala msifuate rafiki au walinzi wengine badala yake. Ni machache mnayo yakumbuka.”

(Qur’ani, al-Araf, 7:3)

Taifa jipya la kidunia likabuni mfumo wa chaguzi za kisiasa kwa lengo la kujenga uwakilishi wa Bunge na Serikali na wakati mwingine kuchagua Majaji. Wananchi wa taifa la kidunia, bila kujali dini zao, walipiga kura kwenye chaguzi za kidemokrasia. Hata kama serikali ingeundwa na wale ambao wanamuabudu Shetani mwenyewe kama Bwana na Mfalme wao, misingi ya chaguzi za kidemokrasia ziliwataka Wakristo, Wayahudi, Waislamu (n.k.) ambao wamepiga kura kwenye chaguzi hizo, kukubali kuwa serikali inayotokana na matokeo ya chaguzi hizo kuwa halali, yenye mamlaka ya kuwatawala. Walilazimika pia kukubali mamlaka yake na kufuata amri zake. Hata kama matokeo yangewaletea serikali iliyotawaliwa na Wahindi wanaoabudu sanamu ambao hata kama wazi

kabisa wangekuwa na uadui na wale wanaomuabudu Mungu wa Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*) au hata serikali hiyo ingetamka kuwa *Halal* (inaruhusiwa) vyote vile ambavyo Allah amevikataza na kusema kuwa ni *Haram* (imekatazwa) basi kwa misingi ya chaguzi za kidemokrasia Wayahudi, Wakristo, Waislamu, n.k. ambao ni raia wa nchi hiyo ya kidunia walilazimika kisheria kuitambua serikali hiyo kama ni yao na kukubali mamlaka yake juu yao, na kutii amri zake.

Hakuna amri yoyote kwenye maandiko (Taurati, Injili na *Qur'ani*) au kwenye *Sunnah* (mfano au mfumo wa maisha ya Mtume) ambao ungeweza kutumika kuthibitisha uhalali wa Wayahudi, Wakristo na Waislamu kushiriki kwenye chaguzi ambamo wanakuwa huru kuchagua serikali halali ya kuwatawala. Kwa upande wa pili kuna shutuma zilizo wazi kuhusiana na mwenendo huo! Halafu mwanasheria maarufu wa Kiislamu, Dr. Taha Jabir al-Alwani ameweza kutoa Fatwa (ushauri wa kisheria) (ambao umepokelewa kwa kukumbatiwa na Waislamu wenye kuona kwa jicho-moja) na kusema kuwa ni *Wajib* (inalazimika) kwa Waislamu kupiga kura kwenye uchaguzi wa Raisi wa Marekani wa mwezi wa kumi na moja mwaka 2000. Wengi wao walimpigia kura George Bush na sasa wameishia kujikuta na matope usoni. Laiti wangempigia kura mpinzani wake Al Gore, hali isingekuwa tofauti na hiyo ya mwanzo! Walimpigia kura George Bush na sasa wanawalilia Waislamu wa Ardhi Takatifu ambao wanazidi kugandamizwa na Serikali ya Israeli, ambayo matendo yake ya kigandamizi na kikatili yanapata msaada na kuungwa mkono na utawala wa Bush! Pia wanawalilia Waislamu wa Afghanistani ambao wameuawa kikatili na huo huo utawala wa Bush bila huruma. (Tazama Kiambatanishi na. 2: "Majibu ya Waislamu kwenye Shambulizi kwa Amerika.")

Suluhisho mbadala kwa waumini kwenye chaguzi za kisiasa kwenye taifa la kisasa la kidunia

Msomaji muumini wa dini ya Kiyahudi, Kikristo au Kiislamu an weza kuuliza swali: Je, kuna suluhisho (kwa waumini) mbadala kwenye chaguzi za kisiasa kwenye nchi zenye mfumo wa kidunia? Jibu ni kuwa: Ndiyo! Lipo. Suluhisho mbadala ni kupigania kurudisha Utawala na Mamlaka ya Mungu Mtukufu wa Abrahamu, kwenye mfumo wa kisiasa – na kupigania kutambulika kwa Mamlaka yake kuwa ni Mamlaka ya Ju una ya Mwisho na kupigania Sheria Yake kuwa ni Sheria Kuu. Haya ni mapambano matakatifu kuliko mapambano ya aina zote, ambayo mtu yeyote akijikita katika kupambana kwa niaba yake, basi atalazimika kuyaendeleza hadi mwisho wa muda wake. Kufanikiwa au kutokufanikiwa kwa mapambano haya hakuna uhusiano na mahitaji ya kuwapo kwake. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amethibitisha kuwa muda hautafikia mwisho wake kabla mapambano haya hayajapata na kuyafikia mafanikio yake.

Mbadala kwa waumini ni kushikilia chochote ambacho Allah amekifanya Halal kibaki Halal na chochote ambacho Allah ameamuru kiwe *Haram* kibaki *Haram*, bila ya kujali gharama watakayolazimika kulipa. Pia, wakati watu wakifanya *Shirk*, *Kufr*, *Dhulm* na *Fisq*, hapo waumini wanapaswa waushutumu mwenendo huo, waupinge na wapambane nao na wamgeukie Allah na kumuomba Yeye awatenganishe na watu wa aina hiyo:

"...Basi tutenge na hawa watu (watenda dhambi, wapinzani) na wapotovu."

(Qur'ani, al-Maidah, 5:25)

Qur'ani inazungumzia jukumu hili la waumini kama *"amr bil ma'aruf"* (kujiunga kupigania mema) na "*nahi 'an al-munkar*" (kupinga maovu). Ikiwa jitihada za kurudisha Mamlaka ya Allah Mtukufu na Utawala wa Sheria Zake (kwenye eneo lolote) kutambulika kuwa Sheria Kuu kushinda, hivyo basi eneo hilo linakuwa *Dar al-islam*. Waislamu wangetawala eneo hilo. Lakini pana mfumo mbadala wa mseto ambapo Waislamu wangetawala na wangejumuisha wasiokuwa Waislamu kwenye kutawala kwa misingi ya usawa wa kisiasa kwa kupitia kwenye makubaliano ya kikatiba ambayo ingewaruhusu Waislamu kuutambua Uhuru, Utawala, Mamlaka ya Allah na Sheria Zake juu 'yao.' Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alianzisha modeli ya utawala juu ya eneo, na juu ya taifa, kwa misingi ya usawa wa kisiasa.

Binaadamu wana uhuru wa kuikubali au kuikataa dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*). Hata hivyo, mara baada ya kuikubali dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*), waumini hawana tena uhuru wa kuchagua baina ya serikali ya waumini au serikali ya wasiokuwa waumini. Ilhali waumini wana uhuru wa kuchagua, wanalazimika kuchagua waumini wenzao kuwatawala. Pale wanaponyimwa uhuru huo kwenye eneo lolote lile wanalazimika kutafuta mahali ambapo uhuru huo unapatikana na baadaye kuweza kuhamia kwenye eneo hilo! Hapo Mungu wa Ibrahimu, ameamrisha waumini:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ وَأُوْلِي ٱلۡأَمۡرِ مِنكُمۡۖ فَإِن
تَنَٰزَعۡتُمۡ فِي شَيۡءٖ فَرُدُّوهُ إِلَى ٱللَّهِ وَٱلرَّسُولِ إِن كُنتُمۡ تُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ
ٱلۡأٓخِرِۚ ذَٰلِكَ خَيۡرٞ وَأَحۡسَنُ تَأۡوِيلًا ٥٩

"Enyi mlio amini! Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume na (pia wale) wenye madaraka kutoka miongoni mwenu..."

(Qur'ani, an-Nisa, 4:59)

Pale ambapo wanakuwa hawana uhuru wa kuunda serikali yao wenyewe popote pale, na ikawalazimu kuishi chini ya utawala wa wasiokuwa waumini, waumini wa dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*), watautii utawala wa wasiokuwa waumini hadi muda ambapo watapata fursa ya kuwachagua waumini wenzao kuwatala. Isipokuwa kukubali kutii na kutawaliwa na utawala usiokuwa wa waumini hakuwezi kuambatana na kushiriki kwenye kuunda hiyo serikali ya wasiokuwa waumini. Waumini watautii utawala huo chini ya makubaliano yatakayowahakikishia uhuru wao wa kuabudu, ikim. hakuna watakacholazimishwa kufanya kitakachokuwa kinaenda kinyume na Sheria na Amri za Mungu wa Ibrahimu, kwa mfano jukumu la kupigania (*al-Qital*) na hivyo basi kupata mafunzo ya kijeshi. Ni jambo lisilowezekana hivi sasa kwa Muislamu kuishi Marekani na kuitunza imani yake. Na hii ndiyo sababu mwandishi huyu hivi sasa anatafuta nyumba mpya ya kuishi). Wakati serikali kama hiyo haitokuwa serikali 'yao' wanaweza kuipa ushauri kwa mambo yote ambayo yatakuwa ya kweli, mazuri na yenye wema, na kuonya, kupinga na kutojihusisha kwa yote yale ambayo ni ya uongo, mabaya na yenye matokeo mabaya.

Ni miongoni mwa hulka za taifa la kisasa la kidunia daima kutoruhusu uchaguzi utumike kulibadilisha na kuwa taifa la aina nyingine – kwa mfano taifa ambalo lingeutambua Uhuru, Mamlaka ya Mwenyezi Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) na Ufalme wa Amri na Sheria Zake. Mfumo wa uchaguzi wa kisiasa umeandaliwa ili kulitumikia na kulilea taifa la kidunia lisilomtambua Mungu.

Mtume (*rehma na amani juu yake*) alisema kuwa dunia ya *Kufr* inaundwa na umoja wa aina yake (*al-kufru millatun wahidah*). Na hiki ndicho hasa kitu kilichojitokeza leo hii duniani. Myahudi na Mkristo wanapaswa watafakari juu ya ukweli kuwa wakati Waislamu wa Algeria walipotumia 'uchaguzi wa kisiasa' kutaka kubadilisha mfumo wa kitaifa na kurudisha dini ya Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) nchini mwao Algeria, na kushinda uchaguzi huo kwa asilimia 85 kwenye uchaguzi wa kitaifa, dunia isiyomtambua Mungu yote iliungana kwa pamoja na kuwapa adhabu hao asilimia 85 waliothubutu kubadilisha mfumo usiomtambua Mungu. Mashambulizi hayo yanayofanywa na mataifa ya kidunia yanaendelea hadi hivi leo kwa ukatili unaokosa aibu tangu kipindi baada ya kwisha uchaguzi huo.

Hivyo basi badala ya kupiga kura na kuhalalisha mfumo wa kidunia unaoegemea kwenye *Shirk*, Waislamu wanatakiwa wajilinde na hiyo *Shirk* kwa kujiondoa kwenye taifa la kidunia. Pia wanapaswa watoe majibu na maelezo kuwa mfumo wa taifa mesto lililoanzishwa na Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ni mfumo ulio bora Zaidi ukilinganisha na mfumo wa Taifa wa kidunia usiomtambua Mungu.

Maelezo ya Qur'ani juu ya kuenea kwa Shirk kwenye Taifa la kidunia lisilomtambua Mungu

Maoni yetu ni kwamba *Qur'ani* peke yake ndiyo yenye uwezo wa kuelezea, na imeelezea tukio hili lenye msukumo mkubwa la mabadiliko ya kisiasa ambayo yameukumba na kuipita dunia ya

Ukristo wa Ulaya na Uyahudi wa Ulaya**,** kuwakumba na kuwapita binaadamu wa sehemu zote zilizobaki duniani. Je, ni maelezo yapi hayo?

Qur'ani imefundisha kuwa mlolongo wa historia siku moja utafikia kikomo na utakwisha pale ambapo Allah Mtukufu atakapoamuru 'Siku ya Mwisho' iwakute binaadamu. Kabla ya 'Siku ya Mwisho' kutokea, hata hivyo, patajitokeza Zama za Mwisho ambazo zitajaa Alama kutoka kwa Allah ili kutoa ishara kuwa Zama za Mwisho zinatukabili. Miongoni mwa matukio yatakayojitokeza katika Zama za Mwisho mojawapo itakuwa ni kuachiwa huru na kuingia duniani kwa *Dajjal* – Mtume wa Uongo na *Ya'juj* na *Ma'juj*. Watakapofunguliwa na kuingia duniani wataishia kuwa watendaji wakuu wa mlolongo wa historia, na wao ndiyo watakaokuwa wahusika wakuu kwenye mkakati mzima wa kuibadilisha dunia na umma wote wa binaadamu kote duniani. Mtume (*rehma na amani juu yake*) alisema kuwa enzi za *Dajjal*, Mtume wa Uongo, zitashuhudia kuenea kwa *Riba* ikiambatana na ugandamizaji mkubwa wa kiuchumi. Pia zitakuwa ni zama za *Kufr* kwani *Dajjal* atakuwa na neno '*Kafir*' limeandikwa baina ya macho yake na pia zitakuwa zama za *Shirk* kwa kuwa *Dajjal* atajichukulia fursa ya kujifanya kuwa yeye ni mungu na atawghilibu binaadamu wamfuate na kumkubali kuwa yeye ndiye. Ni wazi kabisa kama mwanga wa jua kwa mwandishi huyu kuwa *Dajjal* ndiye mpangaji mkuu nyuma ya kuundwa kwa taifa la kidunia lisilomtambua Mungu na mfumo wake mzima wa chaguzi za kisiasa.

Mwandishi huyu amesimamisha hoja zake kutokana na Ushahidi wa *Qur'ani* na *Hadith* ambao unathibitisha kuwa kushiriki kwenye chaguzi za kisiasa kwenye mataifa ya kidunia yenye msimamo usiomtambua Mungu nit endo la *Shirk* na *Kufr*. Ikiwa watajitokeza wanazuoni wenye kupinga mtazamo huu basi wanawajibika kutoa maelezo yao yatakayotokana na Ushahidi wa *Qur'ani* na *Sunnah* ya Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*). Watalazimika kuelezea mazingira husika ambamo itakuwa ni *Halal* kwa waumini kupiga kura kwenye chaguzi za kitaifa. Kwa mfano, je muumini anaweza kumpigia kura muumini wa dini ya Kihindu ambaye anaabudu sanamu, au kwa mtu ambaye ni adui wa wazi wa Uislamu, muongo, mlevi, mwizi, mzinzi, mkopeshaji kwa *Riba* anayemiliki hisa za benki au meneja wa benki n.k.? Je, anaweza kupiga kura kwa misingi ya ujamaa na umoja wa kiambari, au kwa misingi ya ahadi: "tutakupigia kura kwa masharti kuwa utatupa kitu kadhaa wa kadhaa toka kwako?" Je, anaweza kukipigia kura chama ambacho kimejikita kwenye kuliunga mkono Taifa la Kizayonisti la Israeli kwenye uvamizi wake endelevu, na kuwakandamiza Wapalestina kwenye Ardhi Takatifu na *Masjid al-Aqsa?* Je, anaweza kukipigia kura chama cha kisiasa ambacho kinaunga mkono kuhalalisha ndoa na mahusiano ya watu wa jinsia moja au utoaji wa mimba?

Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alisema: *Kilicho Halal (kinachoruhusiwa) kinaeleweka (kiko wazi), na kilicho Haram (kilichokatazwa) kinaeleweka (kiko wazi), jitenge kutoka kwa chochote ambacho hakina uhakika (kilichokuwa hakieleweki kwa uhakika).* Imebaki kwa wanazuoni, ambao ni viongozi wa waumini, kusema wazi kama ni *Halal* kushiriki kwenye chaguzi za kisiasa kwenye taifa la kisasa llililojengwa kwa msimamo na misingi ya kidunia. Ili kuwasilisha jibu la uhakika linalojitosheleza wanazuoni mwanzo kabisa lazima waonyeshe kuwa siyo *Haram* kufanya hivyo, na kisha siyo jambo 'lisilokuwa na utata' kufanya hivyo. Na wanalazimika kuegemeza ushahidi wao kwenye misingi ya *Qur'ani* na *Hadith sahih*.

Taifa lenye misingi ya kidunia la Israeli lililopo katika Ardhi Takatifu

Hivi sasa inawezekana kwa sisi kufikia hitimisho kuhusu uhalali wa Taifa la kidunia la Israeli lililorudishwa kwenye Ardhi Takatifu. Je, kufanikisha kwa Ushirika wa Wazayonisti kulirudisha Taifa la Israeli kwenye Ardhi Takatifu ni uthibitisho wa madai ya Wayahudi kuhodhi Ukweli? Je, hilo lilikuwa ni tendo la kuwajaalia rehema na neema za Mungu lililosimamiwa kwa nguvu na ridhaa ya Mungu?

Taifa la kidunia la Israeli, kama mataifa mengine ya aina hiyo, ni tukio linalochukiza kwa kuwa limeanzishwa kwa misingi ya *Shirk!* Moja ya alama muhimu za dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*) ni kuwa dini hiyo haina uhusiano wowote na *Shirk!* Taifa hilo la Israeli, linalosimamishwa kwa misingi ya kidunia, bila ya shaka, linapingana na masharti ya urithi wa Ardhi Takatifu. Litavunjwa. Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alielezea kuwa jeshi la Kiislamu litatokea Khorasan na litaliteketeza Taifa la Israeli. Jeshi hilo litaibuka baada ya Imam al-Mahdi kujitokeza na ujio wake utafuatana na kurudishwa kwa Khilafa:

"Abu Hurairah alisema kuwa Mtume (rehma na amani juu yake) alisema: Bendera nyeusi zitatokea Khorasan (ikim. eneo ambalo hivi sasa linajumuisha nchi za Afghanistani, Pakistani, na maeneo ya Irani na Asia ya Kati) na hakuna jeshi wala nguvu itakayoweza kuwazuia hadi watakapoingia Aelia (Jerusalem)."

(Sunnah Tirmidhi)

Kurudishwa kwa Khilafa ya Kiislamu kutapelekea kuvunjwa kwa Israeli. Hii itakuwa ni mara ya tatu kutokea tukio kama hilo. Mara ya kwanza jeshi la Babilonia lilitumika kuvamia na kuiteketeza Israeli. Mara ya pili lilikuwa ni jeshi la Kirumi. Na sasa kwa mara ya mwisho litakuwa ni jeshi la Kiislamu.

Pia, zipo sababu nyingi nyingine za kisiasa ambazo zinatoa sababu za kujitosheleza kuvunja madai ya Taifa la Israeli kuwa kurejeshwa kwa Taifa hilo ndani ya Ardhi Takatifu ni uthibitisho wa Wayahudi kuhodhi Ukweli. Kwanza, ingekuwa ni kukanusha kwa kimsingi kuwa bara la Ulaya lisilomtambua Mungu, linalokosa maadili na mwenendo mwema unaofuata amri za Mungu, linalokandamiza mataifa mengine, liwe ndilo ambalo linatumika kufikisha ridhaa, rehema na neema za Mungu kwa Wayahudi ambao kupitia kwao Ukweli unathibitishwa. 'Nyenzo' lazima ziende sambamba na 'matokeo'.

Pili, utaratibu ambao umetumika kuirudisha Israeli imejumuisha kufukuzwa, kutoka kwenye Ardhi Takatifu, kwa watu wanaomuabudu Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*). Walifukuzwa bila ya sababu yoyote ya msingi zaidi ya kuwa wao hawakuwa Wayahudi. Kwa zaidi ya miaka hamsini baada ya kufukuzwa toka kwenye nyumba na ardhi zao, wamekuwa wakiishi kwenye kambi za wakimbizi. Huu ni ugandamizaji na uonevu mkubwa. Zaidi, tangu Israeli ilipoundwa upya, ugandamizaji wa Waarabu, Waislamu pamoja na Wakristo, ambao wanaishi ndani ya na kuizunguka Ardhi Takatifu, umekuwa ukiongezeka zaidi na zaidi. Tendo la rehema na neema za Mwenyezi Mungu linalofanywa kwa ridhaa Yake haliwezi kuambatana na uonevu huu!

Tatu, wakati Taifa la Israeli linaundwa ilikuwa wazi kuwa hakuna heshima wala kujali utukufu kwenye fikra za wale waliokuwa wakiliunda taifa hilo. Kukosa kumjali Mungu, ukosefu wa maadili na uadilifu kwenye nyanja mbali mbali za maisha ikiwemo kujamiiana, ibada, n.k. kwa Israeli hakuna tofauti yoyote na ukosefu wa maadili na uadilifu unaoendana na kukosa kumtambua Mungu kunakopatikana kwenye utamaduni wa bara la Ulaya. Tukio hili haliwezi kueleweka na kukubalika kama ni tukio la rehema na neema za Mwenyezi Mungu. Kwa hakika, Taifa hili lenye mfumo wa kidunia la Israeli limeleta kwenye Ardhi Takatifu uchafuzi, kushuka na kufifia kwa maadili, ambako hakujawahi kutokea katika kipindi chote cha historia ya Ardhi hiyo, na hivi sasa imefikia hata kiwango cha kuwapo na kushamiri utumwa wa ngono ndani ya Ardhi Takatifu. Hiki ni kinyume cha mwenendo mwema. Hakika, hivi sasa tuna jumuiya ya wapagani ambao ndiyo wanaishi kwenye Ardhi Takatifu!

Taifa la Kipagani ndani ya Ardhi Takatifu

Taifa la Kiyahudi la Israeli ni, kwa ufupi, taifa la kipagani ambalo lina dalili zote za kuwa na desturi na maadili ya upagani. Myahudi yoyote ambaye anaamini kuwa tukio la Wayahudi kurejea kwenye Ardhi Takatifu na 'kuundwa upya' kwa Taifa la Israeli ni maendeleo yanayowapeleka kwenye njia ya uhakika ya kurudisha zama za dhahabu na kuthibitisha kuwa dini ya Kiyahudi (*Judaizm*) ndiyo sahihi nay a Ukweli atashitushwa sana na kushikwa na mtetemeko akikutana na taarifa za muda si mrefu uliopita zilizotolewa kwenye Makala ya gazeti la Jerusalem Post ambazo zinathibitisha kushamiri kwa mfumo na mwenendo wa maisha wa kipagani ndani ya Ardhi Takatifu:

"Kulingana na takwimu za polisi, kuna zaidi ya madanguro 200, klabu za ngono 200 na idadi isiyojulikana ya ofisi zinazotoa huduma za malaya (wanaotoa huduma kwa wateja baada ya kuwasiliana kwa simu) zilizosambaa nchi nzima. Yael Dayan, mwenyekiti wa Kamati ya Bunge (Knesset) ya Hali za Wanawake, anakadiria kuwa pana wateja takriban milioni moja kila mwezi wanaokutana na malaya wa aina zote mbili, wale walio kwenye madanguro, na pia wale wanaojitembeza mitaani wakiwemo wale ambao wanatoa huduma za klasi ya juu ya escort. Kuna takriban 'klabu za afya' 50 hadi 60 zinazotoa huduma kwenye magorofa ya flati zilizo kwenye mji wa Tel Aviv karibu na Kituo cha Kati cha Mabasi peke yake, huku idadi kubwa ya klabu hizo ikipatikana kwenye miji ya Haifa, Jerusalem, Netanya, Beersheba, Ashkelon, Ashdod, na Eilat. Kurasa za nyuma za magazeti yote maeneo ya miji tofauti yamejaa matangazo ya huduma za ngono, yakiwemo pia matangazo ya kichinichini ya 'msaada unahitajika' ambapo kwa siri wanajaribu kushawishi na kuajiri wanawake na kuwaingiza kwenye biashara ya ngono."

(Jerusalem Post, tarehe 28, Mwezi wa Nane, 2000)

"Wapelelezi wa Polisi walivamia danguro la Bat Yam usiku wa Jumatatu wakati mmiliki wake alipojaribu kuwauza wanawake wanne wa kigeni kwa meneja wa danguro jingine, msemaji wa Polisi wa Wilaya ya Tel Aviv amesema. Mfanyakazi wa danguro la Bat Yam anatuhumiwa kumsaidia muajiri wake kufanya mawasiliano na kundi la kihalifu lililopo nchini Moldovia ambalo limejikita kwenye shughuli za usafirishaji haramu wa wanawake na kuwaingiza Israeli ili kufanya kazi kama malaya. Polisi waliwakamata wote watatu, pamoja na wanawake saba ambao walikuwa ndani ya eneo la danguro. Kati ya hao saba, si chini ya wanne ni raia wa Moldovia, ambao wamekuwa wakifanya kazi nchini Israeli kinyume cha sheria, waliachiwa baada ya kuhojiwa na Polisi. Wengine walipelekwa kwenye Mahakama ya Tel Aviv jana asubuhi kwa kusikilizwa kesi ya rumande… Inasemekana walililipa kundi la kijambazi dola za kimarekani 7,000 ili kuwaletea hao wanawake wanne, ambao walipanga kuwauzia makuwadi wa hapa kwa bei ya kati ya dola za kimarekani 5,000 hadi 10,000 kwa kila malaya mmoja." (Jerusalem Post, Tarehe 14, Mwezi wa Pili, 2001)

"Kwenye hii miezi ya mwisho, vyombo vya habari vimejaa taarifa za 'utumwa mweupe' ndani ya Israeli. Wanawake wanauzwa kama 'mali inayohamishika' kutoka kwa kuwadi mmoja kwenda kwa wa pili. Takriban kuna mapatano na/au malipo 25,000 (elfu ishirini na tano) kila siku nchini Israeli. Hali hii ikiambatana na kupatikana na makosa ya shambulio hatari la kingonokwa Waziri wa Ulinzi Yitzhak Mordechai na baadaye kusamehewa makossa hayo, matukio haya yameibua majadiliano yenye msukumo mkubwa kuhusu thamani ya mwili wa mwanamke kwenye jamii ya Israeli ya sasa. Ingawa jamii ya Waisraeli ilichelewa pale mwanzo wa mapinduzi ya kingono, leo hii mahusiano ya kingono ya Waisraeli, ukiachilia mbali wale wanaoshikilia dini, hayana tofauti kabisa na mwenendo wa raia wengine wa nchi za kimagharibi. Kukosekana kwa makubaliano kunafanya matendo ya Mordechai na wale wanaouza na kununua wanawake kwenye minada, wanastahili zaidi kushutumiwa kimaadili na kisheria kuliko wale ambao wanatumia fursa za kila siku kufanya ngono bila mpangilio. Lakini matendo yao yanadhihirisha mtazamo wa kawaida wa kuona hatia za wengine pekee."

(Jerusalem Post, Tarehe 10, Mwezi wa Tano, 2001)

Ripoti nyingine ya raia wa Israeli ambaye ana nafasi ya juu kwenye jamii hiyo inadhihirisha mengi zaidi kuhusu hali ya ugandamizaji ndani ya Taifa la Kiyahudi:

"…kwenye maelezo aliyoyatoa hadharani yaliyoishangaza Israeli nzima, kiongozi wa zamani wa Huduma za Usalama wa Ndani wa Israeli amezishutumu sera za Serikali kuwa zimesababisha kuibua machafuko ya Wapalestina.

"Ami Ayalon, kiongozi mstaafu wa Shin Bet (Usalama wa Taifa, Israeli), amesema Israeli inahusika na inabeba dhambi za sera za 'kibaguzi' zinazopingana na mwenendo wa kiroho wa dini ya Kiyahudi. Amesema kuwa Wapalestina wamefuata mantiki katika kuchagua kutumia nguvu na machafuko, na amezungumzia kuhusu kuguswa kwake kwa udhalilishaji wa hali ya juu sana unaofanywa na Israeli dhidi ya wafanyakazi wa Kipalestina na wengine ambao hutaka kuingia Israeli. Maneno kama hayo husikika sana kutoka kwa Wapalestina, lakini ni nadra sana kusikika yakitoka kinywani mwa Muisraeli aliyewahi kushika nafasi kubwa kabisa kwenye chombo cha usalama."

(Jerusalem Post, 4 Mwezi wa Kumi na Mbili, 2000)

Hata raisi wa Israeli bila kutarajia amethibitisha ugandamizaji wanaofanyiwa Wapalestina ambao wanapinga Taifa la Kiyahudi kwa *Intifada:*

"Ikiwa wanazo hisia zozote za kimantiki, Wapalestina watafungua macho yao na kugundua wapi udhalimu huu umewafikisha: mamia waliopoteza maisha yao, maelfu waliojeruhiwa japo tumejitahidi kujizuia kutumia nguvu,

umasikini na unyimaji, kukosekana ajira, uharibifu usiotenguka wa uchumi, kuanguka kwa mtandao wa utawala, na nyongeza kwa yote hayo, hawajaweza kusogea mbele kisiasa."

(Raisi wa Israeli Katsav, Jerusalem Post, 16 Mwezi wa Pili, 2001)

Raisi alidhihirisha bila kukusudia dharau yake kwa Waarabu kwa njia iliyozoeleka inayotumiwa takriban mara zote na wale wasiomtambua Mungu:

"Ni majirani zetu hapa, lakini inaonekana kama vile kwenye umbali wa mita mia kadhaa toka hapa, ni watu ambao hawatoki kwenye bara letu, wala kwenye dunia yetu, ila hakika wnatoka kwenye galaksi tofauti kabisa na hii ya kwetu."

(Raisi wa Israeli Moshe Katsav, Jerusalem Post, 11 Mwezi wa Tano, 2001)

Dan Jacobson, profesa katika Chuo Kikuu cha Tel Aviv, alisema haya kuhusu haki Israeli:

"Kwa miaka 52 wakazi wa Kiarabu ambao ni wachache wamekuwa kwa aibu kubwa wakibaguliwa. Kunyang'anywa ardhi ni moja ya njia kali za udhahirishaji wa ubaguzi huo. Kunyimwa kazi kwenye utumishi wa serikali, makampuni makubwa ya serikali, na makampuni ya umma; rasilimali chache kupangiwa kwenye sekta za elimu na afya zinazowahudumia Waarabu, na sehemu ndogo isiyokuwa na uwiano wa kitakwimu na ya kuhuzunisha, inayotia aibu ya bajeti zinazopewa halmashauri za Kiarabu, ni maelezo na uthibitisho wa ziada wa kuwaona na kuwafanya raia wa Israeli wenye asili ya Kiarabu kuwa ni raia wa hali ya 'daraja la pili.' Ukweli huu umekuwa ukitambuliwa tena na tena na serikali kadhaa, zikiwemo zile zenye msimamo wa bawa la kulia, lakini machache sana yamefanywa ili kubadilisha hali hiyo na kulitatua tatizo hili katika miaka hii hamsini."

(Jerusalem Post, 3 Mwezi wa Nne, 2001)

Haya yote hapo juu yanathibitisha kuwa sasa tunashuhudia kutimia kwa onyo la *Qur'ani* kwamba Jahannamu itawatokea mbele ya macho yao:

وَعَرَضْنَا جَهَنَّمَ يَوْمَئِذٍ لِّلْكَٰفِرِينَ عَرْضًا ﴿١٠٠﴾

ٱلَّذِينَ كَانَتْ أَعْيُنُهُمْ فِى غِطَآءٍ عَن ذِكْرِى وَكَانُوا۟ لَا يَسْتَطِيعُونَ سَمْعًا ﴿١٠١﴾

"Na siku hiyo tutawadhihirishia wazi Jahannamu makafiri (Kuffar) waione. Wale (makafiri) ambao kwamba macho yao yalikuwa paziani (ili kuweza kukubali na kukumbatia Mwongozo Wangu) hayanikumbuki, na wakawa hawawezi (hata) kusikia."

(Qur'ani, al-Kahf, 18:100-101)

Hebu sasa tuharakishe na tugundue kuwa Mpangilio Mpya wa Dunia umeibuka ikiwa ni matokeo ya kushikilia utawala wa dunia kwa utamaduni wa kidunia wa kimagharibi ambao unaambatana na kutomtambua Mungu, ugandamizaji wa kiambari, kiuchumi, kidini, ukosefu wa maadili, na utumwa wa kingono sasa hivi umesambaa duniani kote, ikiwemo nchi za Kiislamu. Lakini Ardhi Takatifu ni ardhi maalum. Na *Qur'ani* inasisitiza msemo wake kuwa ni wale tu ambao wana imani (kwa Mungu wa Abrahamu) na wanaoonyesha mwenendo mwema, ndiyo watakaoruhusiwa kuirithi Ardhi Takatifu (*Tazama Qur'ani, al-Anbiyah, 21:105*). Israeli ya kisasa, au hata Chama cha Ukombozi wa Palestina, havina nafasi hata ndogo kabisa ya kutimiza masharti haya. Mtazamo wa *Qur'ani* wa hatma ya Jerusalem kuhusiana na kushikilia na kutawala Ardhi Takatifu ni ule ambao si chama cha Ukombozi wa Palestina cha Yasser Arafat na wala si Taifa la kidunia la Israeli litaishi na kuiona. Ndege wa bawa la aina moja, wote watatokomea!

Hoja zilizowakilishwa hapo juu zinaonyesha wazi kuwa madai ya kisiasa ya Taifa la Israeli hayana mashiko na hayathibiki kuashiria haki ya kuirithi Ardhi Takatifu. Jambo hili halipaswi kuwa gumu sana kiasi muumini wa dini ya Kikristo au Kiyahudi akashindwa kuligundua na kulikubali.

Sura ya Pili

ARDHI TAKATIFU NA UCHUMI WENYE MISINGI YA RIBA WA ISRAELI


فَبِظُلْمٍ مِّنَ ٱلَّذِينَ هَادُوا۟ حَرَّمْنَا عَلَيْهِمْ طَيِّبَٰتٍ أُحِلَّتْ لَهُمْ
وَبِصَدِّهِمْ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ كَثِيرًا ﴿١٦٠﴾
وَأَخْذِهِمُ ٱلرِّبَوٰا۟ وَقَدْ نُهُوا۟ عَنْهُ وَأَكْلِهِمْ أَمْوَٰلَ ٱلنَّاسِ بِٱلْبَٰطِلِ ۚ وَأَعْتَدْنَا
لِلْكَٰفِرِينَ مِنْهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٦١﴾

"Basi kwa dhulma yao Mayahudi tuliwaharimishia vitu (vyakula) vizuri walivyo halalishiwa. Na (tumefanya hivyo pia) kwa sababu ya kuwazuilia kwao watu wengi (kufuata) Njia ya Mwenyezi Mungu. Na (kwa sababu ya) kuchukua kwao riba, japo wamekatazwa (kufanya hivyo), na kula kwao mali ya watu kwa dhulma. Basi (kwa sababu ya matendo haya maovu) tumewaandalia makafiri katika wao adhabu yenye uchungu."

(Qur'ani, an-Nisa, 4:160-1)

Utangulizi

Israeli ni Taifa la kisasa lenye mfumo wa kidunia ambalo lipo kwenye Ardhi Takatifu. Kama yalivyo mataifa mengine ya kidunia leo hii, uchumi wake umeegemea kwenye mfumo wa *Riba*. *Riba* kawaida hutafsiriwa kuwa ni asilimia za faida inayotozwa kwa kukopa au kukopesha pesa. Lakini fasili ya *Riba* kwenye Uislamu inajumuisha pia tendo la kununua au kuuza kibiashara kwa bidhaa au huduma kulikoegemea kwenye udanganyifu ambamo upande unaodanganya unafaidika kwa faida kubwa sana kuliko ambavyo ungepaswa kupata kihalali. (*Tazama kitabu chetu kinachoitwa: Kukatazwa kwa Riba kwenye Qur'ani na Sunnah*). Kwenye msamiati wa Kimarekani tendo hilo huitwa 'utapeli' Kama maamuzi yangebidi yafanywe kwa mujibu wa dini ya Ibrahimu (*rehma na amani juu yake*), basi tunauliza swali: Je, upi utakuwa uhalali wa kidini wa Israeli ambayo ipo kwenye Ardhi Takatifu ambayo uchumi wake umeegemea kwenye *Riba?* Je, inaendana na, au

inapingana na masharti ya Mungu yaliyowekwa kwa urithi wa Ardhi Takatifu? Surah hii inajaribu kujibu swali hilo.

Uchumi wa kisasa wa Dunia ulivyo

Alama ya msingi ya uchumi wa kisasa kote duniani ni kuwa utajiri umeacha kuzunguka kwenye sehemu na wahusika wake mbalimbali. Badala yake, utajiri hivi sasa unazunguka miongoni mwa matajiri peke yake. Matokeo ya hili ni kuwa duniani kote matajiri sasa hivi wanaendelea kubaki kuwa matajiri na masikini wanaendelea kubaki kwenye jela ya ufukara. Pili, matajiri wanaendelea kuwa matajiri zaidi kwani wananyonya damu ya umma, wakati masikini wanadondokea kwenye ufukara ambao unaleta upotevu wa amani, fujo, na mateso makubwa ikiwemo kuporomoka kwa imani na maadili. Fikiria kuwa binaadamu wote kama vile wangekuwa wako kwenye meli. Wachache ambao wanaendelea kubaki matajiri na kuwa matajiri zaidi wanasafiri wakiwa kwenye daraja la kwanza, kwenye usalama na anasa za juu kabisa. Wao wana tiketi za kudumu za daraja la kwanza. Matajiri wanaitawala meli. Wanatumia utajiri wao kujipa madaraka ya kuamua yote yanayohusu siasa. Demokrasia ndani ya meli hiyo inakuwa utawala wa matajiri kwa ajili ya matajiri kwenye hali ambayo inalingana na umalaya wa kifedha. Isipokuwa matajiri hawashiki madaraka hayo wao wenyewe moja kwa moja. Badala yake wanatawala kwa kupitia ‘wakala’ na ulaghai kupitia njia ya kuunga mkono wanasiasa au vyama vya siasa ambavyo wana uwezo wa kuvisimamia kwa siri bila kuonekana wazi. Haya ndiyo maelezo ya uhakika wa jinsi ya hali ilivyo kwenye uwanja wa siasa za kiuchumi duniani. Na ni Wayahudi wa Kizungu wa Uingereza na Marekani ambao wamefuzu kujenga mipango kabambe ya kuweza kujinyakulia mamlaka ya dola na kutawala watu popote wanapotaka. Sifa anastahili Henry Ford kwa kuweza kugundua mipango hii ya kishetani kwenye historia ya binaadamu.

Wengi katika mabilioni ya watu waliobaki duniani wamefungwa kwenye umasikini uliokithiri na wanasafiri kwa tiketi za daraja la chini uvunguni mwa meli huku mazingira yao yakizidi kuwa mabaya, uchafu mkubwa na mateso ya kila aina. Wanalazimika kufanya kazi kwa ujira wa kitumwa ili wengine wavune jasho la kazi zao na matajiri waishi maisha ya anasa. Pia wanaishi kwenye hali za wasiwasi wakitishiwa na wizi, ujambazi, kuuawa na ubakaji wa wanawake kwenye maeneo yaliyojaa madawa ya kulevya na makundi ya kikatili yanayojihusisha nayo.

Wale wanaosafiri kwenye ‘daraja la kwanza’ wanapata maji safi ya kunywa, huduma bora za afya ambazo za kulipia kwa pesa za kutisha. Na ulimwengu wa madawa kila kukicha unabuni njia

mpya za utibabu na maajabu ‘yanayowarudishia uhai wale waliokufa.’ Wale walio daraja la chini la meli, wanalazimika kunywa maji machafu yaliyojaa bakteria. Wanalazimika kula chakula na kunywa maziwa yaliyojazwa kemikali na homoni. Panaongezeka pia ulazima wa kula vyakula vilivyobadilishiwa vinasaba. Wakiugua hawamudu gharama za matibabu. Wanaishi maisha ya dhiki na kufa vifo vya shida. Kwa hakika, uchumi wa dunia kwa sasa ni njia mpya ya utumwa wa kiuchumi iliyoandaliwa kwa ustadi mkubwa. Na inatumika na kufanya kazi kwa ghilba ya hali ya juu.

Kabla ya yote, japo wale wote ambao wanauwezo na mamlaka ya kuusimamia uchumi duniani, ambao wanahubiri injili ya ‘soko huria na la haki sawa kwa wote’ wao wenyewe wanavunja misingi hiyo kwa kulazimisha majukumu ya kisheria kwa watu na serikali kutumia ulaghai wa pesa za makaratasi kama njia halali ya malipo. Wakati pesa za makaratasi daima zinapoteza thamani! Kadiri umasikini unavyoongezeka na hali kudidimia, wanalazimisha upangaji wa bei za bidhaa muhimu kwa maisha kama vile vyakula n.k., ikiwemo mishahara ya kima cha chini kwenye soko la nguvukazi. Wanafanya hivyo ili kuzuia uwezekano wa umma ulio na njaa kuweza kuzigomea serikali zao pamoja na matajiri wanyonyaji wachache. Pia wanafanya hivyo kujilinda ili umma usiwagundue hila zao za kuwaingiza kwenye utumwa mpya.

Ulaghai unavuka hayo ya hapo juu. Wengi kati ya masikini wanawaangalia wale wanaosafiri kwenye daraja la kwanza na kuamini kuwa watu hao na maisha yao yawakilisha pepo kamili. Na wanatamani kuingia kwenye pepo hiyo. Wanashindwa kuelewa jinsi ya mfumo wa ugandamizaji unavyofanya kazi. Wengine miongoni mwa masikini kutokana na kugandamizwa wanaamua kufanya fujo na kuzielekeza kwa wale ambao wana mali kiasi fulani na walio kwenye mamlaka. Masikini wote wanaamini kuwa wanaishi motoni na wanaiga maisha ya wanaosafiri daraja la kwanza wakiamini kuwa inawapa fursa ya kuonja pepo. Meli ya aina hii inapaswa kuangamizwa kwa kuzamishwa yote pamoja na abiria wake wote!

Raisi wa zamani wa Cuba, Fidel Castro, kama Ivan Illich (‘Energy and Equity’) aliuzungumzia uchumi wa dunia kwenye lugha inayofanana na hiyo:

“Haijawahi kutokea kwamba binaadamu wamekuwa na uwezo mkubwa kupita kiasi wa kisayansi na teknolojia, njia za kuzalisha mali na utajiri, lakini tofauti baina ya hali za watu na upendeleo miongoni mwao ni mkubwa kiasi haujawahi kutokea kabla kwenye historia nzima ya binaadamu duniani.”

Na alijibu kwa hoja na pendekezo lake la: “kufuta ugandamizaji huu wa kiuchumi kwa kuita wito wa Nuremberg nyingine ya kiuchumi” (Hotuba ya Raisi, Mkutano wa kundi la 77, Havana, Mwezi wa Tisa, 2000)

Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) aliipa dunia mpangilio wa kiuchumi ambao uko huru na usiokuwa na uonevu wala ugandamizaji wa kiuchumi. Hakuna aliyekuwa akifanya kazi kwa ujira wa kitumwa. Utajiri haukuzunguka miongoni mwa matajiri peke yake, bali kwenye uchumi mzima. Matajiri hawakubaki matajiri daima na masikini hawakubaki masikini daima. Hivyo basi, hapakuwa na haja ya kupanga kima cha chini cha mishahara kwa sheria maalum. Soko lilikuwa huria na haki. Hakuna aliyeruhusiwa ‘kuvuna’ bila ya ‘kupanda’. Pesa zilikuwa na thamani yake ndani ya fedha yenyewe na haikuwezekana kubadilishwa kilaghai na mabenki wala matajiri wachache ili kushusha thamani yake. Matokeo yake, soko hilo na uchumi huo haukuwa na tatizo la ‘mfumuko wa bei.’ Hapakuwa na upangaji wa bei, ikiwemo ujira kwa wafanyakazi. Huduma za jamii zilipatikana kwa malipo ya kodi ya utajiri iliyotumika kuwasaidia wale ambao walikosa kabisa mahitaji muhimu ya maisha. Lakini mfumo mzima wa thamani ya kijamii ulihakikisha kuwa jitihada zinafanywa, na wale wote wenye uwezo huo, kujikwamua kutoka kwenye hali hiyo tegemezi.

Mtume (*rehma na amani juu yake*) alifanikiwa pale ambapo kila serikali leo hii duniani imeshindwa. Alifanikiwa kwa sababu alitimiza sheria ya Mungu ya kuzuia *Riba*, hapakuwa na makampuni ya bima, na alifanikiwa kusimamia kutoshuka kwa thamani ya pesa kwa kutumia pesa halisi badala ya pesa za kilaghai (pesa za makaratasi, plastiki au za kidigitali). Pia alitumia sheria za makosa ambazo zilitoa adhabu kali zilizokuwa kizuio kwa wale waliopatikana na makosa ya wizi. Lakini, dunia ilimkataa, na Waislamu wameziacha *Sunnah* zake za kiuchumi. Hivyo basi dunia inalazimika kuishi na *Dhulm* na *Fasad*, ikim. uchafuzi na uharibifu wa soko huria na la haki, na hivyo basi uharibifu wa *Ba'i* (biashara).

Duniani kote hivi sasa, ugandamizaji huo wa kiuchumi unaendelea siku hadi siku, matajiri wanaendelea kuwa matajiri zaidi na masikini wanaendelea kuwa masikini zaidi. Kwa mfano watu weusi wa Marekani wana hali mbaya sana na daima masikini, wakati watu weupe wa Kimarekani siku zote wanabaki matajiri. Ugandamizaji unaongezeka kwa kuwa tofauti baina ya watu weusi na weupe, masikini na matajiri inazidi kuongezeka! Uchumi wa Marekani unaisisimua dunia ya wale wasiokuwa weupe, huku watu weupe wakiwa na hali nzuri sana ya kimaisha haijawahi kutokea kabla. Lakini kwenye nchi hii utajiri unazunguka miongoni mwa matajiri tu, wakati idadi ya masikini wanaoishi

kwa misaada ya serikali na ya watu binafsi inazidi kuongezeka. Utamaduni wa watu weupe wa kimagharibi ungependa tuamine kuwa mfumo wao wa maisha ya kiuchumi ni bora kuliko mifumo yote iliyowahi kubuniwa duniani na binaadamu wamebahatika kujikuta wameishi kwenye mfumo huo! Na hapo hapo Waislamu 'waigaji' wenye 'jicho moja' waliotiwa kasumba wanajishughulisha kwa nguvu zote kuhakikisha kuwa dunia ya *Islam* nayo inauiga utamaduni mfumo huu wa kimagharibi. Ukweli ni kuwa, mfumo huu wa kinyonyaji wa Kimarekani na wa watu weupe wa kimagharibi, pamoja na ndoto zake, unatiwa mbolea kwa damu za umma wote duniani, pamoja na utajiri unaokunwa kutoka sehemu zote za dunia, huku masikini wenyewe hawana taarifa nini kinaendelea. Lengo letu ni kutoa maelezo jinsi gani haya yanafanywa! Utamaduni wa watu weupe wa kimagharibi pamoja na umma wa wasiokuwa weupe unaotolewa jasho kwa kazi nzito kwa malipo ya kitumwa, wakiwemo Wayahudi asilia (wasiokuwa na asili ya Ulaya) wanaweza kufaidika ikiwa watayajali na kuyasikiliza maelezo haya na kuikubali *Qur'ani* kuwa ni Neno la Allah na Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ni mjumbe wake kabla haijawawia kuwa wamechelewa.

Tasnifu yetu ni kuwa watu wale wale ambao waliutengeneza mpango wa mabadiliko ya kisiasa ya utamaduni wa bara la Ulaya na, kwa kupitia maigizo, mabadiliko ya sehemu zote zilizobaki za dunia, na kuzifanya kuwa na mfumo wa kidunia unaoegemea kutomtambua Mungu, ni watu wale wale waliowarubuni Wayahudi Asilia kuwaunga mkono kwenye jitihada za kulirudisha Taifa la Israeli. Ni watu ambao wanaendelea kuushika utajiri wa dunia kupitia njia zao zenye ustadi mkubwa wa kilaghai na kitapeli kupitia mashirika na mifumo ya kimataifak.v. mfumo wa shirikisho la kimataifa la fedha na mfumo wa mabenki ulioegemea kwenye *Riba* na pia mfumo wa bima duniani kote. Hawa wameshawapita hata wale Wayahudi Asilia (ikim. watu waliojaribu kumsulubu Yesu (*rehma na amani juu yake*)) kwenye mchezo wao wenyewe walioutengeneza wa *Riba!* Mtazamo wetu ni kuwa mtu stadi mwenye kipaji kikubwa aliye kazini hapa ni mtu yule yule ambaye mzungu wa ajabu ambaye kwanza alijigeuza na kuwa Myahudi na baadaye aliendelea na kuiteka nyara dini ya Kiyahudi.

Qur'ani Tukufu si tu inaelezea jinsi dunia ilivyo hivi sasa bali pia inafafanua jinsi gani ugandamizaji wa kiuchumi unatokea. *Qur'ani*, ambacho ni kitabu cha 'busara' (nahii inajumuisha busara za kiuchumi), imeweka misingi ya sheria inayohakikisha kuwa utajiri hauzunguki na kubaki mikononi mwa matajiri peke yake:

مَّا أَفَاءَ اللَّهُ عَلَىٰ رَسُولِهِ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ فَلِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ كَيْ لَا يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الْأَغْنِيَاءِ مِنكُمْ ۚ وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۖ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ

"Mali aliyo leta Mwenyezi Mungu kwa Mtume wake kutoka kwa watu wa hivi vijiji ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na kwa ajili ya Mtume, na jamaa, na mayatima, na masikini, na msafiri, ili yasiwe yakizunguka baina ya matajiri tu miongoni mwenu. Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anacho kukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu."

(Qur'ani, al-Hashr, 59:7)

Waislamu wameziacha amri za *Qur'ani* na matokeo yake sasa hivi wanakutwa na majanga makubwa kwa kosa la kuisaliti *Qur'ani*. Mfumo mpya wa kilaghai wa uchumi unawakumba na unawapeleka kwenye utumwa, wao pamoja na umma usiokuwa na asili ya bara la Ulaya. Jambo la aibu na lililo wazi ni pale tunapokumbuka kuwa moja ya malengo ya *Uislamu* duniani ni kuwakomboa wanyonge wanaogandamizwa.

Je, nini ni chanzo cha ugandamizaji huu wa kiuchumi duniani? Jibu: ni *Riba!* Jamii ya kinyonyaji, iliyojisimika kwenye mfumo wa kimagharibi wa mabenki, yenye asili ya Kiyahudi, ambao pia wanapatikana dunia nzima, muda wote wanafyonza utajiri na damu ya umma na kuwafanya wazidi kuwa masikini kwa kupitia nyenzo ya *Riba*. Mgandamizaji anatayarisha mifumo ya kisiasa, kisheria, kiutawala na vyombo vya habari, kwa ghilba kubwa na anahakikisha kuwa vyote vinalenga kuutetea na kuusimamia hiyo mifumo iliyotayarishwa ya ugandamizaji wa kiuchumi. Burudani kama vile runinga, filamu, mtandao wa intaneti, muziki wa kisasa, nguo za dizaina n.k vyote vinatumika kuliwaza na kughilibu umma kwenda kwenye 'nchi ya kusadikika' ili wabaki kwenye hali ya kuduwaa wakati *Riba* inatumika kuwakamata na kuwatawala wakiwa kama watumwa. Lengo lao la mwisho la mwanzilishi wa mkakati mzima, *Dajjal*, Mtume wa Uongo, ni kuwafanya wote wawe watumwa, na kupitia umasikini na shida, na pia utajiri uliokusanywa kinyemela kwa utapeli, kuwapa wenye imani ya Allah na mfumo mzima wa maisha ya kidini mtihani mkubwa. Ushahidi unaopatikana hivi sasa tayari unaonyesha kuwa wengi kati ya Waislamu, wanyonyaji matajiri na pia masikini wa kukithiri, wote wanajikuta mtihani huu wa imani unawashinda. Lengo la pili la *Dajjal* ni kuwaghilibu Wayahudi na kuwapeleka kwenye adhabu yao ya kuteketezwa. Tathmini

ya malengo na dunia ya kisasa ilipofikia, na hususan Ardhi Takatifu, lazima ifikie hitimisho kuwa malengo hayo kwa kifupi yamekwishatimia. *Dajjal* tayari yumo mbioni kukamilisha jukumu lake la kuwakabidhi Wayahudi utawala wa dunia. Israeli itakapokuwa '*Taifa Tawala*' na kukamilisha muda wake wa siku moja itakayokuwa kama wiki, *Dajjal* mwenyewe atajitokeza na kutawala dunia akitokea Jerusalem. Hapo ndipo atakapokamilisha lengo lake la kujipachika utume akijifanya yeye kuwa ni Mtume wa Kweli.

Hii inapaswa kuwa ni chanzo cha wasiwasi mkubwa, ikiwa si hofu kubwa, kwamba dunia nzima ambayo ina jumuiya zinazotokana na tamaduni nyingi tofauti, nyingine zikiwa tayari zimeshatimiza miaka elfu moja, zote kwa pamoja ziwe zimekumbatia siyo tu mfumo wa aina moja wa kitaifa wa kidunia wa *Shirk*, usiomtambua Mungu, bali pia zimeshikilia mfumo wa aina moja wa uchumi unaoegemea kwenye *Riba*. Silaha ya kiuchumi ya *Riba* inajazia pamoja na silaha ya kisiasa ya taifa la kisasa la kidunia zikijumuishwa na Umoja wa Mataifa ambapo *Dajjal* kwa mafanikio ameweza kutimiza lengo lake la kuishikilia na kuitawala dunia nzima.

Utaratibu wetu ni kuwa kwanza tutaelezea umuhimu wa somo, na kisha, tutaendelea kuelezea aya za *Qur'ani* ambazo zinahusiana na somo la *Riba*, na *Hadith* za Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ambamo mwongozo wa *Qur'ani* unapata kuonyesha matumizi halisi. Mwishowe, tutajaribu kuelezea *Riba* ikiwa kazini kwenye uchumi wa kisasa. Baada yahapo, ndipo tutakapoweza kujaribu kuchunguza uhalali wa Taifa la Israeli katika Ardhi takatifu, Israeli ambayo uchumi wake umeegemea kwenye *Riba*.

Riba ni nini?

Riba inafahamika kuwa ni kukopesha pesa kwa kudai kiwango kikubwa cha asilimia za faida. Lakini ubadilishaji huu wa fasili ya neno hili uliotokea kwenye bara la Ulaya umefanywa ili kumuwezesha 'mkopeshaji wa pesa' (sasa hivi anaitwa 'benki') kulipiga chenga kanisa la Kikristo na msimamo wake wa kuikataa aina zote za *Riba*. R.W. Tawney aliandika kitabu maarufu mwaka 1935 chenye jina: "*Dini na Kuibuka kwa Ubepari*" ambamo ndani yake ameelezea upinzani wa muda mrefu wa kanisa na Wakristo wa Ulaya kuhusu *Riba*. William Shakespeare pia alifanya hivyo hivyo kwenye mchezo wake maarufu wenye jina "*mfanyabiashara wa Venisi*."

Riba kwenye Uislamu (kama vile kwenye Ukristo wa kipindi cha enzi za kati) ni kukopesha pesa kwa faida, bila kujali kiwango cha asilimia. Wakati 'mkopeshaji wa pesa' anakopesha pesa kwa

faida, hapo pesa anazokopesha, zinatenganishwa na uhusiano wowote na aidha kazi yoyote inayotarajiwa kufanywa, au nguvu na jitihada zitakazoelekezwa humo, au kubeba na kukubali hatari yoyote inayoweza kuhusiana na kupungua au kupotea kwa pesa zenyewe kama mtaji, bali ni lazima ziongezeke kadiri muda unavyopita. Je, uongezekaji huu unatokea vipi? Ongezeko linapatikana kwa ghilba kupitia kuwanyonya aidha wafanyakazi, au bidhaa na mali. Hii inaonekana wazi pale ambapo tutatazama kwa kina yale ambayo Allah bila mzunguko amesema kwenye *Qur'ani*:

وَأَن لَّيْسَ لِلْإِنسَٰنِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ﴿٣٩﴾

"...Na ya kwamba mtu hatapata kitu isipokuwa (yale) aliyo yafanya mwenyewe?"

(Qur'ani, al-Najm, 53:39)

Hivyo basi *Qur'ani* inakataa madai kuwa 'muda' unaweza kulinganishwa au kugeuzwa ukawa ni 'pesa' au kuwa pesa zinaweza kuongezeka kadiri muda unavyopita!

Moja ya njia mbazo hutumika kuwanyonya watu ni kupunguza thamani ya mishahara, au bidhaa na mali katika muda fulani, kitu ambacho Allah moja kwa moja amekipiga marufuku kwenye aya kadhaa za *Qur'ani.* Mtume *Shu'aib* (ambae hata jina lake limepotea kutoka kwenye Biblia) mara kwa mara alikuwa akiwaonya watu wake kuhusu udhalimu wa maisha yao ya kiuchumi. Alisema:

وَيَٰقَوْمِ أَوْفُوا۟ ٱلْمِكْيَالَ وَٱلْمِيزَانَ بِٱلْقِسْطِ ۖ وَلَا تَبْخَسُوا۟
ٱلنَّاسَ أَشْيَآءَهُمْ وَلَا تَعْثَوْا۟ فِى ٱلْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٨٥﴾

"...Na wala msiwakhini watu vitu (ambavyo kwa haki ni) vyao; ... kwa kupunguza thamani ya vitu vyao...wala msieneze uovu katika nchi mkafanya uharibifu."

(Qur'ani, al-Araf, 7:85; Hud, 11:85; al-Shu'ara, 26:183)

Innawezekana kuwa mabingwa wa kidunia wa nguvukazi, ambao wanaidharau *Qur'ani* kama kitabu chenye mwongozo, sasa wataanza kuelewa sababu kwanini nguvukazi au rasilimali watu siku zote

wanabadilishwa kuwa punda wa mizigo ambao hutoka jasho kwa niaba ya matajiri, na mabenki ambayo yanawamiliki.

Waislamu wanapaswa waelewe, ingawa inaonekana ni vigumu kwa baadhi yao kuelewa, kuwa Riba inakuwa kazini pale ambapo utajiri unafyonzwa kutoka kwa umma kupitia mfumo wa kitapeli uliohalalishwa wa matumizi ya pesa za makaratasi. Pesa hii imechukua nafasi ya pesa halisi ambayo ilikuwa ni pesa ya *Sunnah* ya kila Mtume wa Mwenyezi Mungu, ikim. dhahabu na fedha ikiwemo vyuma vingine vya thamani. Karatasi la kutengeneza, au plastiki na pesa za digitali (pesa zilizobuniwa na mfumo wa kidunia) hazina thamani ya ndani. Badala yake, thamani ya pesa hizo inachaguliwa na kubandikwa na kusababisha kushuka kwake, *kadiri muda unavyopita, kwani mfumo huo umetayarishwa ili iwe hivyo!* Mabenki ndiyo watendaji wakuu katika kulazimisha kushuka kwa thamani ya pesa, na mabenki ndiyo yanayopata faida kubwa hilo linapotokea. Wakati pesa inashuka thamani, thamani ya kila kitu pia inashuka. Bei zinapanda na mishahara inapoteza thamani. Wafanyakazi hapo wanakuwa wamefungwa kwenye jela ya utumwa.

Aya ya *Qur'ani* Iliyokuwa ya Mwisho Kushushwa

Katika aya ya mwisho ya *Qur'ani* kuteremshwa, Allah Mukufu na Mwingi wa Hekima na Busara, Aliamua kurudia somo ambalo tayari lilikwishazungumziwa kabla kwenye vitabu vilivyotangulia – akalirudia tena kwenye *Qur'ani*, kwenye Taurati, Zaburi na Injili – nalo ni somo la kukataza Riba. Kwa mujibu wa *Ahadith* zilizopokelewa na wote wawili, Ibn Abbas (*radhi za Mwenyezi Mungu juu yake*) na Umar (*radhi za Mwenyezi Mungu juu yake*), tunajua kuwa aya ya mwisho kupokewa na Mtume (*rehma na amani juu yake*) muda mfupi kabla ya kifo chake, ilikuwa ni kipande kinachopatikana kwenye *Surah al-Baqarah* (2:279-281) ambacho kilizungumzia *Riba*:

"Umar ibn Khattab alisema: Aya ya mwisho kushushwa ilikuwa inahusu *Riba*, lakini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*), alitutoka kabla hajaifafanua kwetu, hivyo basi achene siyo tu *Riba* peke yake, bali pia *Reebah* (ikim. chochote kinacholeta utata kwenye akili kuhusiana na uhalali wake)."

(Sunnah, ibn majah; Darimi)

"Ibn Abbas alisema: Enyi mlioamini, mwogopeni Allah na achene kile kinachobakia (mnachopaswa kupata) kinachotokana na Riba (kuanzia sasa kuelekea siku zijazo) ikiwa nyinyi kweli ni waumini… Na pasiwe na mmoja wenu ambaye atanyimwa haki yake. (*al-Baqarah, 2: 279 – 281*). Ibn Abbas alisema: Hii ilikuwa aya ya mwisho kushushiwa Mtume (*rehma na amani juu yake*)."

(Sahih Bukhari)

Hiyo aya ya mwisho ilithibitisha tendo la Mtume (*rehma na amani juu yake*) la kupitisha amri kabla ya kuzuia Riba kwenye *khutbah alwida'a* (Hotuba ya Kuaga) aliyoitoa akiwa '*Arafat*'. Aya ya mwisho inapatikana katika kipande hiki kifuatacho cha *Qur'ani*. Tunakiweka kipande chote pamoja na maelezo yetu binafsi kwenye maandishi madogo:

ٱلَّذِينَ يُنفِقُونَ أَمۡوَٰلَهُم بِٱلَّيۡلِ وَٱلنَّهَارِ سِرّٗا وَعَلَانِيَةٗ
فَلَهُمۡ أَجۡرُهُمۡ عِندَ رَبِّهِمۡ وَلَا خَوۡفٌ عَلَيۡهِمۡ وَلَا هُمۡ
يَحۡزَنُونَ ٢٧٤
ٱلَّذِينَ يَأۡكُلُونَ ٱلرِّبَوٰاْ لَا يَقُومُونَ إِلَّا كَمَا يَقُومُ ٱلَّذِي يَتَخَبَّطُهُ
ٱلشَّيۡطَٰنُ مِنَ ٱلۡمَسِّۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمۡ قَالُوٓاْ إِنَّمَا ٱلۡبَيۡعُ مِثۡلُ ٱلرِّبَوٰاْۗ وَأَحَلَّ
ٱللَّهُ ٱلۡبَيۡعَ وَحَرَّمَ ٱلرِّبَوٰاْۚ فَمَن جَآءَهُۥ مَوۡعِظَةٞ مِّن رَّبِّهِۦ فَٱنتَهَىٰ فَلَهُۥ مَا
سَلَفَ وَأَمۡرُهُۥٓ إِلَى ٱللَّهِۖ وَمَنۡ عَادَ فَأُوْلَٰٓئِكَ أَصۡحَٰبُ ٱلنَّارِۖ هُمۡ فِيهَا
خَٰلِدُونَ ٢٧٥
يَمۡحَقُ ٱللَّهُ ٱلرِّبَوٰاْ وَيُرۡبِي ٱلصَّدَقَٰتِۗ وَٱللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ كَفَّارٍ أَثِيمٍ ٢٧٦

إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ وَأَقَامُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُاْ
ٱلزَّكَوٰةَ لَهُمۡ أَجۡرُهُمۡ عِندَ رَبِّهِمۡ وَلَا خَوۡفٌ عَلَيۡهِمۡ وَلَا هُمۡ
يَحۡزَنُونَ ﴿٢٧٧﴾
يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَذَرُواْ مَا بَقِيَ مِنَ ٱلرِّبَوٰٓاْ إِن كُنتُم
مُّؤۡمِنِينَ ﴿٢٧٨﴾
فَإِن لَّمۡ تَفۡعَلُواْ فَأۡذَنُواْ بِحَرۡبٖ مِّنَ ٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦۖ وَإِن تُبۡتُمۡ فَلَكُمۡ
رُءُوسُ أَمۡوَٰلِكُمۡ لَا تَظۡلِمُونَ وَلَا تُظۡلَمُونَ ﴿٢٧٩﴾
وَإِن كَانَ ذُو عُسۡرَةٖ فَنَظِرَةٌ إِلَىٰ مَيۡسَرَةٖۚ وَأَن تَصَدَّقُواْ خَيۡرٞ
لَّكُمۡۖ إِن كُنتُمۡ تَعۡلَمُونَ ﴿٢٨٠﴾
وَٱتَّقُواْ يَوۡمٗا تُرۡجَعُونَ فِيهِ إِلَى ٱللَّهِۖ ثُمَّ تُوَفَّىٰ كُلُّ نَفۡسٖ مَّا
كَسَبَتۡ وَهُمۡ لَا يُظۡلَمُونَ ﴿٢٨١﴾

"Wale wanao toa mali zao usiku na mchana, kwa siri na dhaahiri, wana ujira wao kwa Mola wao Mlezi; wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika." (Ikiwa mali zao zitatumika kwa mpangilio ulio *Halal*, matumizi ya namna hiyo yatausisimua uchumi ukue na kuweka mali au utajiri kwenye mzunguko).

"Wale (upande wa pili) walao riba hawasimami (mbele ya Allah Siku ya Mwisho) ila kama anavyo simama aliye zugwa na Shet'ani kwa kumgusa. (Hii ni kwa sababu Riba ni kama kinyume cha 'kutumia' – kwenye *Riba* mali au utajiri unafyonzwa kutoka kwenye uchumi hadi kusababisha umma wote unarudishwa kwenye umasikini na ufukara). *Hayo ni kwa kuwa wamesema: Biashara ni kama Riba.* (Wanadai kuwa 'kukopesha pesa kwa faida za asilimia' ni aina ya biashara iliyo halali).

Lakini Mwenyezi Mungu ameihalalisha biashara na ameiharimisha Riba. (Madai yao na hoja zao si kweli. Allah ameifanya biashara kuwa ni *Halal*, na ameitamka *Riba* kuwa ni *Haram*. Hivyo basi *Riba* siyo aina ya biashara. Hii ni kwa sababu kiini hasa cha tendo lolote la kibiashara, ni lazima liambatane

na uwezekano wa aidha kupata faida au kupata hasara itokanayo na matokeo ya mwisho ya tendo hilo. Pesa inapokopeshwa kwa asilimia kadhaa za faida *(Riba)* uwezekano wa kupata hasara unashishwa chini mno kiasi hata unafikia kuwa haupo kabisa! Hivyo basi kukopesha pesa kwa faida hakupati ridhaa ya kukubalika kuwa ni tendo la kibiashara).

Basi aliye fikiwa na mawaidha (haya) kutoka kwa Mola wake Mlezi, kisha akajizuia (na Riba), basi yake ni yaliyo kwisha pita (ikim. Riba aliyokwishapokea siku za nyuma ni mali yake), na mambo yake yako kwa Mwenyezi Mungu. (ikim. Ni juu ya Allah kumhukumu – hatolazimishwa na utawala wa Taifa la Kiislamu kuirudisha *Riba* aliyokwishaichukua huko nyuma).

Na (wale) wenye kurudia (ikim. kuendelea kubaki kwenye matumizi ya *Riba,* yaani kukopesha pesa kwa faida ya asilimia, kwa mfano, baada ya ayahii ya *Qur'ani* kushushwa) *basi hao ndio watu wa Motoni, humo watadumu milele!"*

"(Na kwa hii) Mwenyezi Mungu huiondolea baraka riba, (wakati huo huo) huzibariki sadaka. "(kwa sababu kiini cha *Riba* ni 'kuchukua' bila ya 'kutoa' chochote kile baada ya kuchukua, wakati kiini cha sadaka ni 'kutoa' kitu bila 'kuchukua' chochote badala yake.)"

Na Mwenyezi Mungu hampendi asiyekuwa na shukurani na mwenye kubakikatika dhambi."(hususan mwenye kubaki kwa ubishi kwenye dhambi ya kula *Riba*)

"Hakika wale walio amini na wakatenda mema na wakashika Sala na wakatoa Zaka, wao watapata ujira wao kwa Mola wao Mlezi, wala haitakuwa khofu juu yao, wala hawatahuzunika."

"Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na acheni Riba zilizo bakia (ambazo bado mnadai kuwa mnapaswa mlipwe), ikiwa nyinyi ni Waumini."

"Basi msipofanya (hivyo) (ikim. ikiwa mtaendelea kukopesha pesa kwa kudai malipo ya *Riba* baada ya kuukubali Uislamu) *(basi)jitangazieni vita na Mwenyezi Mungu na Mtume wake* (ikim. kuwa jitayarisheni kwa vita ambayo Waislamu ambao watakuwa wameikubali amri ya kuachana na *Riba* watakapokuja kupigana vita nanyi mliobaki mnaendelea na tabia hii ya kupokea *Riba,* kwa lengo la kuwakomboa wale wanaogandamizwa kwa *Riba*)*."*

"Na mkitubu (ikim. mkiachana na Riba), basi haki yenu ni mtaji wenu (ambao mlikopesha kwa misingi ya *Riba*, ikim. unaruhusiwa kudai mtaji ulioanza nao (uliokopesha) – na siyo mtaji ukajumlishwa na asilimia za faida za *Riba*, au mtaji pamoja na gharama ya huduma)."

Msidhulumu wala msidhulumiwe." (Hii huenda ikabidi itafsiriwe vyema zaidi kwa namna ifuatayo: Katika kukubali kurudishiwa mtaji peke yake ambao ndiyo pesa uliyomkopesha mtu, utakuwa unajikinga na dhambi ya kudhulumu na kutowatendea haki wengine, na katika kuacha kudai asilimia za faida inayotokana na kukopesha (*Riba*), wewe mwenyewe hutokuwa umejifungua kupokea au kupatwa/kuguswa na aina yoyote ile ya ukosefu wa haki / dhulma.)

"Na akiwa (mdaiwa) ana shida, basi (mdai) angoje (na kumpa muda) mpaka afarijike (hali yake itakapokuwa nzuri kuweza kulipa). Na mkilifanya deni kuwa ni sadaka (mkalifuta deni), basi ni bora kwenu, ikiwa mnajua."

"Na iogopeni Siku ambayo mtarudishwa (ikim. binaadamu wote wakiwemo wale ambao wanakula Riba) kwa Mwenyezi Mungu, kisha kila nafsi italipwa ilicho chuma. Nao hawatadhulumiwa."
(Qur'ani, al-Baqarah, 2:274 – 281)

Kwanini Allah, Mwingi wa Hekima, aliamua kushusha aya hii muda mfupi tu kabla ya kifo cha Mtume (*rehma na amani juu yake*)? Kwanini alichagua muda ambao ulionekana kuwa ni muda wa mwisho kabisa uliokuwa bado unawezekana kutuma ujumbe huu? Kwanini Alifanya hivyo baada ya kutuma aya ambamo Alisema kuwa Ameshaikamilisha dini na Kukamilisha neema zake kwa waumini? Na mwisho kwanini Alichagua, Alipfanya hivyo, Kulirudia somo la kukataza *Riba*, somo ambalo Alishalizungumzia kwenye *Qur'ani?*

Kwa hakika lazima pana majibu muhimu sana ya maswali haya yote. Inaonyesha kwetu kuwa ujumbe huu wa mwisho ungeweza tu kutumiwa vizuri sana kusisitiza jambo ambalo limekaa katikati ya moyo wa mwongozo wa kiroho. Nyongeza, ungeweza kutumika kuelekeza uangalifu wa waumini kwenye eneo la mafunzo na maonyo mahali ambako imani za waumini zitarajie mashambulizi makali (mama wa mashambulizi yote) yanayokuja muda ujao yakatayozifanya zinyong'onyee ikiwa zitakosa uangalifu, matarajio na msimamo imara. Mwisho, huenda imekuja mwishoni kabisa kwa sababu itachukua nafasi muhimu kimkakati kwenye Zama za Mwisho. Allah pekee ndiye Mjuzi wa hakika!

Chaguo la somo la *Riba* kuwa ni wahyi wa mwisho linaonekana kuwa ni onyo kali kuliko yote kwamba *Riba* inaweza kuwa ni tishio kubwa na la hatari kubwa kuliko matishio yote yatakayoelekezwa kwenye imani, uhuru na nguvu za waumini. Suala hili ni la umuhimu mkubwa na wa hali ya juu kabisa kwani ndani yake kunapatikana hatari kubwa na mbaya kabisa inayoweza kuvunja na kuteketeza imani za waumini, misimamo yao ya uadilifu na nguvu za *Ummah* wa Mtume (*rehma na amani juu yake*). Hili ndilo jibu letu, na kwa mara nyingine tena, Allah pekee ndiye Mjuzi wa hakika!

Mtume Anathibitisha Kuwa Hatari Kubwa Zaidi ni Riba

Huu mtazamo wetu unaonekana kuwa umepata uthibitisho unaotokana na ukweli kuwa Mtume (*rehma na amani juu yake*) mwenyewe, kwenye *Hadith* iliyopokelewa na Abu Hurairah (*radhi za Mwenyezi Mungu juu yake*), kufanikiwa kwa mashambulizi ya aina hiyo yatakayofanywa kupitia uchochoro wa *Riba*. Yatakuwa ni mashambulizi ambayo bila ya shaka yatafanywa na maadui wa *Uislamu*, lakini yatawakumba binaadamu wote, wakiwemo wafuasi wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*):

"Kitafika kipindi" alisema Mtume, "ambamo hutoweza kumpata mtu hata mmoja miongoni mwa binaadamu wote ambaye hatokuwa akila *Riba*. Na ikiwa mtu yoyote atadai kuwa hatumii *Riba* basi kwa hakika mvuke wa Riba utamfikia." Kwa mujibu wa mapokezi mengine "vumbi la Riba litamfikia."

(Sunan Abu Daud)

Mtume (*rehma na amani juu yake*) hapo ameweka wazi kabisa kuwa hatari kubwa kuliko zote kwenye uadilifu wa *Ummah* na *Iman* ya waumini itakuja kutoka kwenye *Riba*. Hii inathibitisha onyo la Mwenyezi Mungu Mwenyewe ambalo limeshuhudia uchaguzi wa somo la *Riba* kuwa ni somo la mwisho kwenye kushushwa.

Utabiri wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) kuhusu kutapakaa kwa *Riba* duniani kote kuwagusa binaadamu wote leo hii umetimia. Na kwa uhakika, utabiri huo umetimia kwenye kipindi cha umri wetu wenyewe! Hususan umetimia katika kipindi ambacho kimepita tangu ulipoangushwa utawala wa Khilafa wa Kiislamu wa Ottoman uliovunjwa mnamo mwaka 1924. Hadi mwaka 1924, mfumo wa kibepari wa uchumi uliobuniwa kwenye bara la Ulaya ulioegemea kwenye *Riba* usingeweza kujipenyeza na kuingia kwenye uchumi na soko la dunia ya Kiislamu. Lakini Wazungu wa Ulaya walifanikiwa kuzivutia serikali zilizokuwa zikisimamia na kutawala kwenye dunia ya Kiislamu kuingia kwenye mfumo wa *Riba*. Khalifa wa Ottoman, kwa mfano, alikopa idadi kubwa ya pesa kutoka Ulaya, kwa *Riba*. Matatizo yake ya kiuchumi na pesa, yalikuwa makubwa kiasi kwamba yalifikia kiwango cha kuteteresha na kuleta hofu za kuweza kuuangusha Ufalme, na akalazimishwa kuomba kuingia kwenye mfumo wa Mataifa ya kidunia. Alifanikisha hili kwenye Mapatano ya Amani ya Paris yamwaka 1856. Lakini gharama iliyomkuta aliyotakiwa kuilipa kwa vitisho vya Wayahudi wa Ulaya waliomiliki mfumo wa kipesa ilikuwa kukubali kufuta *Jizyah* na *Ahl al-Dhimmah* katika maeneo yote ya Ufalme wa Ottoman. Hii pia ilikuwa ni malipizo (*quid pro quo*) ya deni na malipo ya *Riba* aliyokuwa akidaiwa. Kwa kufanya hivyo Khalifa alikuwa amemsaliti Allah Mtukufu ambaye Mwenyewe aliyaamrisha malipo ya kodi ya Jizyah katika *Qur'ani (al-Tauba, 9:29).* Ukweli ni kuwa *Jizyah* itafutwa pale Yesu (*rehma na amani juu yake*) atakaporejea:

"Abu Hurairah amesikika akisema kuwa Mtume (*rehma na amani juu yake*) alisema: Baina yake (Yesu) na mimi hakuna mtume. Atashuka (ardhini). Mtakapomuona mtamfahamu, mtu wa urefu wa kati, na nywele zinazoelekea wekundu, amevaa vazi jepesi lililo kwenye sehemu/vipande viwili vya rangi ya njano isiyokoza (na) ataonekana kama vile matone yanadondoka toka kichwani kwake japo hakitokuwa kimerowa. Atapigana na watu kupigania Uislamu. Atauvunja msalaba, atamuua nguruwe na ataivunja kodi ya *jizyah*. Allah atazivunja dini zote isipokuwa *Uislamu*. Naye (Yesu) atamteketeza *Dajjal* na ataishi duniani kwa miaka arobaini na kisha atakufa. Waislamu watamsalia."

(Sunan Abu Daud)

Ushindi wa wamiliki mabenki wa Kiyahudi wenye asili ya Kizungu dhidi ya Khalifa wa Ottoman ni mfano maarufu wa ubeberu wa kifedha ambao unawezekana kupitia *Riba*. Henry Kissinger alikuwa ni mwanzilishi wa mkakati wa namna hiyo hiyo ambao hatimaye uliweza kuliangusha taifa kubwa kabisa katika nyakati hizi za kisasa, ikim. Umoja wa Mataifa ya Kisoshalisti ya Urusi (USSR). Tukio hilo lilipaswa kuyafungua macho ya *Ulama wa Kiislamu*. Halikuweza!

Matokeo yake mkakati huo huo unaendelea kutumika na Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia, na wengine wengi, wakikamilisha hayo kwa urahisi na wepesi mkubwa. Siyo tu kuwa uchumi wa Israeli umeegemea kwenye *Riba* lakini Israeli pia inaikumbatia chama cha Arafat cha Ukombozi wa Palestina cha PLO pamoja na serikali nyingine za nchi za Kiarabu kwa kutumia mkakati huo huo wa hatari wa kiuchumi ambao unawapeleka kwenye umasikini, ufukara na utumwa wa kiuchumi. Ushindi wa vitisho vya kifedha vya kundi la Kiyahudi wa Ulaya vimeshuhudia mwanzo wa kuvunjika kwa mfumo mtakatifu wa kitaifa wa jumuiya ya *Kiislamu* (*Dar al-Islam*), na kubadilishwa huku mahala pake pakachukuliwa na modeli ya kizungu. Katika modeli hiyo ya utaifa, haki ya 'Ufalme' ikanyakuliwa toka kwa Allah Mtukufu na kupachikwa kwenye Taifa. Hilo nitendo la *Shirk!*

Kwa uhakika, tangu mwaka 1924 *Riba* imejipenyeza kwenye maisha yote ya kiuchumi ya Muislamu duniani kote. Ubeberu wa kifedha ambao unapatikana ndani ya *Riba* umeipeleka shingo ya Ummah wote wa *Kiislamu* kwenye kisu kikali kilicho mikononi mwa maadui. Hakika binaadamu wote wamenasa kwenye mtego wa *Riba* na *Shirk*. Siyo tu kuwa utabiri wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) umekamilika kwa ushindi mkamilifu wa mfumo wa kibenki ulioegemea kwenye *Riba* duniani kote, na pia kupitia kwenye *Riba* ambayo inapatikana kwenye pesa za bandia (mfano za pesa za makaratasi) zisizokuwa na thamani huru ya kukomboleka, ikiwemo pesa za plastiki na za kidigitali, bali pia utabiri huo umekamilika kwa uchafuzi kamilifu wa soko huria na la haki. Soko la kisasa linaloitwa huria, kwa ufupi ni 'pango la wezi' ambamo wenye nguvu wachache wanawanyonya wanyonge walio wengi, kitu ambacho kilitarajiwa na Ali ibn Abi Talib (*radhi za Mwenyezi Mungu juu yake*), ambaye alisema:

"Hakika muda utafika ambapo binaadamu watakuwa wakiumana wao kwa wao…" (Sunan, Abu Daud)

Mwishowe, Mtume (*rehma na amani juu yake*) mwenyewe aliashiria uzito mkubwa na onyo kali sana kwenye aya za *Qur'ani* kwa kutumia lugha kali na nzito kabisa kuhusiana na *Riba*:

"Abu Hurairah amesikika akisema kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*) alisema: Riba ina sehemu sabini tofauti, na iliyokuwa na hatari ndogo kuliko zote ubaya wake ni sawa na mtu kumuoa (ikim. kuwa na uhusiano wa kingono na) mama yake mzazi."

(Sunan, ibn Majah; Baihaqi)

"Abdullah ibn Hanzala (*radhi za Mwenyezi Mungu juu yake*) amesikika akisema kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*) alisema: *Dirham* moja (sarafu ya fedha) ya *Riba* ambayo mtu anaipokea huku akijua fika kuwa inatokana na *Riba*, ni mbaya kuliko kutenda dhambi ya zinaa mara thelathini na sita. (Ahmad). Baihaqi amesikika akisema, kwa mujibu wa ibn Abbas (*radhi za Mwenyezi Mungu juu yake*), akiongeza kuwa Mtume (*radhi za Mwenyezi Mungu juu yake*) aliendelea kusema: Jahannam inamfaa zaidi yule ambaye mwili wake unajengwa kwa vile vilivyo *Haram*."

"Abu Hurairah amesikika akisema kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*) alisema: Kwenye usiku ambamo nilichukuliwa kwenda mbinguni, niliwakuta watu ambao matumbo yao yalikuwa kama

nyumba zilizokuwa na nyoka ambao walikuwa wanaweza kuonekana kutoka nje ya matumbo yao. Nikamuuliza Jibril (*alaihi as-slaam*) hawa ni nani na akaniambia kuwa hao ni watu waliokuwa wakila *Riba*."

(Musnad, Ahmad; Sunan, ibn Majah)

"Abu Hurairah amesikika akisema kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*) alisema: Mwenyezi Mungu atakuwa ana haki kuwakatalia watu wanne kuingia peponi au kuonja baraka zake: yule ambaye ana hulka ya kunywa (ikim. kunywa pombe) yule ambaye anapokea *Riba*, yule ambaye anadhulumu na kuchukua mali ya yatima bila haki, na yule ambaye hawajali wazazi wake."

(Mustadrak, al-Hakim, 'Kitab al-Buyu')

"Samura ibn Jundab (*radhi za Allah juu yake*) amesikika akisema kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*) alisema: Usiku huu nimeota kuwa watu wawili wamekuja na kunichukua kwenda kwenye ardhi takatifu ambako tuliendelea hadi kufikia sehemu yenye mto wa damu, ambapo palikuwa na mtu aliyesimama, na ukingoni mwake pakawa na mtu mwingine aliyekuwa amesimama huku mikononi mwake akiwa ameshika mawe. Yule mtu aliyekuwa katikati yam to alijaribu kutoka humo, lakini yule wa pili akamtupia jiwe mdomoni mwake na kumlazimisha kurudi pale mwanzo alipokuwapo. Kila alipojaribu kutoka, yule mtu wa pili alimrushia jiwe mdomoni na kumlazimisha kurudi alipokuwa. Nikauliza, 'Huyu nani?' Nikaambiwa: yule mtu aliyekuwa kwenye mto ni mtu aliyekuwa akila *Riba*."

(Sahih, Bukhari)

Mtume (*rehma na amani juu yake*) pia alithibitisha tamko la vita toka kwa Allah na Mjumbe wake kuhusiana na kukataza *Riba* kwenye *Hadith* ifuatayo:

"Jabir ibn Abdullah (radhi za Allah juu yake) amesema: nimemsikika Mtume (*rehma na amani juu yake*) akisema: Ikiwa yoyote kati yenu hatoacha mukhabara basi lazima agundue kuwa pana vita kutoka kwa Allah na Mjumbe Wake. Zaid ibn Thabit alisema: Nikamuuliza: Ni nini mukhabarah? Akasema: Kuwa unakuwa na ardhi ya kulima kwa nusu, theluthi, au robo (ya mazao yake)." (Hatari hapa ni kuwa hii kwa ulaghai inapelekea kwenye kuwapo kwa nguvukazi za kitumwa.)

(Sunan, Abu Daud)

Hadi kufikia hapa, baada ya kuwasilisha ushahidi ulioonyeshwa hapo juu, inakuwa wazi kabisa kuwa kuanzishwa kwa uchumi ulioegemea kwenye *Riba* ni dhambi iliyo kubwa mno. Karibu kila dhambi nyingine isiyokuwa *Shirk* inapotea kwenye umuhimu wake ikilinganishwa na hiyo. Matokeo yake ni kuwa kwa uhakika inavunja amri za Allah za kupata ridhaa Yake kwenye kurithi Ardhi Takatifu.

Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) na Kuanguka kwa Pesa za Makaratasi

Ni jambo lenye umuhimu wa hali ya juu kabisa kuwa Waislamu wanapaswa wausome kwa uangalifu mkubwa sana utabiri wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) ambamo ameashiria kuanguka kwa mfumo wa pesa za kidunia za bandia (ikim. pesa za makaratasi, plastiki na digitali, n.k.):

"Abu Bakr ibn Abi Maryam (radhi za Allah juu yake) amesimulia kuwa alimsikia Mjumbe wa Allah akisema: Kwa hakika muda unakuja juu ya binaadamu ambamo hakutokuwa na chochote (kitakachobaki) chenye manufaa ukiacha dinari na dirhamu (sarafu ya dhahabu na fedha)."

(Musnad, Ahmad)

Utabiri huu wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) uko karibu sana kufikia kukamilika kwake. Mfumo wa kisasa wa kifedha unatumia 'karatasi' kutengeneza 'pesa.' Huu ni udanganyifu ulio wazi! Pesa za bandia ni tofauti kabisa na pesa halisi. Pesa halisi zina thamani huru inayokomboleka ambayo daima hubaki ndani ya hiyo pesa, wakati pesa ya karatasi hainayo. Thamani pekee ya pesa bandia ni ile ambayo hupachikwa kwa uamuzi wa nguvu za kisoko. Thamani yake ya soko itabaki hivyo kwa kadiri, na hadi pale ambapo, patakuwa na imani ya jamii juu yake na pia patakuwa na mahitaji yake kwenye soko hilo. Mahitaji peke yake yanategemea imani, na imani ni kitu ambacho kinaweza kuathirika kwa kuchezewa kwa werevu 9kama vile ambavyo Waziri Mkuu wa Malaysia sasa hivi amegundua, na pia kama vile ambavyo Indonesia imegundua, lakini wamekwishachelewa). Kadiri ambavyo serikali zinadhibiti kile kinachoitwa masoko huria ya sarafu, zingeweza kuingilia kati na kulinda na kuokoa imani ya jamii. Isipokuwa soko la sarafu sasa hivi linadhibitiwa na nguvu hatari kati ya zote, nguvu za kilanguzi zinazochochewa na uroho bila kujali utiifu wala uwajibikaji na hakuna uzalendo. Chochote kitakachochafua na kuharibu imani kwenye soko kwa kiasi kikubwa kitasababisha mkurupuko wa nguvu za kilanguzi ambazo zitapelekea utabiri wa Mtume (*rehma na amani juu yake*) kutimia.

Kuanguka kwa pesa kwenye kile kinachoweza kuitwa 'kuyeyuka kwa pesa' kutashuhudia ushindi wa mwisho wa Wazungu (waliojibadili na kuwa Wayahudi) kwenye jitihada zao zilizoanza takriban miaka zaidi ya elfu moja kwa kutaka Wayahudi waitawale dunia nzima. Wale ambao wanazo pesa halisi wataweza kumudu huo myeyuko wa pesa, wakati wale walanguzi watakaoweza kujipanga vizuri kuutumia huo myeyuko, watapata pesa na faida kubwa sana. Umma uliobaki utapoteza mali zao na kubaki kwenye utumwa. Watajikuta wamebaki na makaratasi mikononi yasiyokuwa na thamani yanayojifanya kuwa ni pesa! Hayo ni maangamizi ya kifedha ambayo tuna uhakika yatatokea.

Wapo wengine pia ukiacha Mtume (*rehma na amani juu yake*) ambao sasa wanatabiri kutokea kwa 'myeyuko' huo wa kipesa. Judy Shelton, kwa mfano, anatumia maneno hay ohayo kama jina la kitabu chake maarufu: *"Myeyuko wa Pesa: Kurudisha Utulivu Kwenye Mfumo wa Dunia wa Sarafu."* (New York, The Free Press, 1994). Hatupaswi kusahau, na pia hatupaswi kuiwacha dunia isahau, tukio lisilokuwa la kawaida, la kuanguka kwa dola ya Kimarekani Mwezi wa Kwanza, Mwaka 1980 wakati thamani ya dola kwa dhahabu ilifikia takriban dola 850 kwa aunsi moja! (Mwaka 1917 ilikuwa dola 35 kwa aunsi moja. Sasa hivi thamani yake ambayo 'inabebwa' inawekwa takriban kati ya dola 280 – 300 kwa aunsi moja.) Kuanguka huku kwa dola kulitokea mara baada ya kufanikiwa kwa mapinduzi ya Kiislamu la dhidi mfumo wa kimagharibi ya Taifa la Irani ambalo liliipa serikali kiislamu iliyokuwa ikipinga mfumo uliopo uwezo wa kudhibiti visima vyenye mafuta mengi. Kwanini mapinduzi ya Kiislamu ya Iran yatishie kuanguka kwa mfumo wa kidunia wa kifedha? Wataalamu wa mfumo wa kimataifa wa uchumi wa kifedha wamebaki kimya.

Anguko kama hilo la sarafu ya dola ya Kimarekani liliyokea mwaka 1973 mara tu baada ya vita kati ya Waarabu na Israeli na kuwekwa kwa vikwazo vya kuiuzia Marekani mafuta. Dola ilishuka thamani kwa 400% kutoka kiwango cha dola 40 kwa aunsi moja ya dhahabu hadi kufikia dola 160.

Kuanguka kwa mfumo mzima wa Kimataifa wa Kifedha utatokea pale ambapo Wayahudi wataona kuwa ni muafaka kwao kuiangusha dola. Wataweza kufanya hivyo wakati wowote kwani dola ya Kimarekani inayotengenezwa kwa karatasi ni bandia na kiujumla haina thamani. Dola itakapoangushwa itazibeba na kuziangusha pesa nyingine zilizobaki za karatasi duniani. Mnufaikaji mkubwa wa hilo litakuwa Taifa la Israeli, kwa kuwa ni wale ambao hivi sasa wanadhibiti mabenki ndyo sasa watadhibiti pesa. Serikali hazitoweza tena kuwa na uwezo wa kuchapisha na kutoa pesa. Badala yake mabenki (yanayodhibitiwa na Wayahudi) ndizo zitakazokuwa zikitoa pesa za plastiki ikim. pesa za digitali! Huo myeyuko wa pesa, huenda ukatokea pale Israeli itakapoamua kufanya mashambulizi makubwa kuliko yote dhidi ya nchi za Kiarabu na kuweza kutojali malalamiko na shutuma za nchi za dunia nzima dhidi ya kitendo hicho. Onyesho hilo la nguvu za kijeshi na kisiasa likiambatana na udhibiti wa mfumo mpya wa kifedha baada ya kuanguka kwa pesa za karatasi kutaipa Israeli hadhi ya kuwa *Taifa Tawala* la dunia. Mwandishi huyu anaamini kuwa tukio kama hili lina uwezekano wa kutokea ndani ya miaka mitano hadi kumi ijayo, na pengine hata kabla ya hapo. Israeli tayari imeshaweza kuukataa ushauri wa Raisi wa marekani ambaye aliitaka iondoe majeshi yake kutoka miji ya Wapalestina aliyoichukua baada ya wimbi la wanaobeba mabomu kwa kujitoa mhanga kuleta maafa makubwa kwa maisha ya Wayahudi. Na hivi tunavyoandika Israeli inaonekana imefanikiwa kuukataa wito wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa ambalo liliitaka Israeli iruhusu ujumbe wake kuja kuchunguza yaliyojizi kwenye kambi ya wakimbizi ya Jenin kwenye eneo la Ufuko wa Magharibi na kufuatilia tuhuma za makossa ya jinai ya kivita ya Israeli.

Nini Hasa ni Hali Halisi ya Shambulizi la Riba?

Nguvu zile zile zilizoibuka kwenye historia nzima ya kipindi hiki na kusababisha kuwezekana kwa kufufuliwa kwa Taifa la Israeli, pia zimeweza kujipenyeza kwa binaadamu wote na kuwafikishia *Riba. Qur'ani* imezitambua nguvu hizo kuwa ni watu wa *Ya'juj* (Gog) na *Ma'juj* (Magog) na Mtume (*rehma na amani juu yake*) alimzungumzia *Dajjal*, Mtume wa Uongo, kwa kirefu. Alisema kuwa zama za *Dajjal* zitakuwa ni zama za kushamiri kwa *Riba*. Mwanazuoni maarufu wa Kiislamu na mtu mwenye hekima nyingi, Dr. Muhammad Iqbal, aliushitua ulimwengu wa Kiislamu, mnamo mwaka 1917, aliposema kuwa, kuachiwa huru kwa *Ya'juj* na *Ma'juj* kunakozungumziwa kwenye *Qur'ani*, tayari kumekwishatokea. Ni wazi kabisa kuwa kuingiliwa kwa *Ummah* na nguvu zinazowakilisha *Riba*, kunawakilisha shambulizi linalofanywa na Viumbe Waovu ambao wameumbwa na Allah Mwenyewe. Lengo la washambuliaji haw ani kuwaweka watu wote, wakiwemo Waislamu, kwenye jaribu kubwa kuliko majaribu yote yaliyowahi kutokea tangu kuumbwa kwa Adam (*rehma na amani juu yake*) hadi Siku ya Mwisho. Lengo la washambuliaji ni kuwaghilibu Wayahudi na kuwafikisha kwenye teketezo lao la mwisho. Na katikati ya teketezo hilo ni jaribio la *Riba!* Hivi sasa tunaishi kwenye ulimwengu unaoguswa moja kwa moja na jaribu hilo. Huu ndiyo uhalisi wa shambulio la *Riba*. Na Ushahidi hadi hivi sasa ni kuwa ulimwengu wa Wayahudi ambao ni vipofu wa kiroho,

wanashindwa vibaya sana na mtihani wa majaribu haya. Ulimwengu wa *Kiislamu* nao unaonekana kuwa vipofu, kama ule wa Wayahudi.

Allah Mtukufu Anaongoza Vita Dhidi ya Israeli

Mwenyezi Mungu Mtukufu Amezungumza kwa lugha kali sana kuhusu dhambi ya *Riba*, kuwa ni dhambi kubwa sana (baada ya *Shirk*) ambayo ipo kwenye uwanja wa imani na mwenendo. Hasira za Allah dhidi ya mgandamizaji (unaotokana na ugandamizaji wa *Riba*) ni kubwa sana kiasi watasimama mbele yake baada ya kufufuliwa kama watu ambao wataonekana kama vile wanaendeshwa kuwa wendawazimu kwa kuguswa na shetani. Wakati Taifa la Israeli limejiingiza kwenye mfumo wa *Riba*, ni kwamba Allah hatowapa adhabu watu hao kwenye siku ya kiama, bali pia, Yeye na Mjumbe Wake (*rehma na amani juu yake*) pia watawapiga vita wakiwa bado kwenye dunia hii.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱتَّقُواْ ٱللَّهَ وَذَرُواْ مَا بَقِيَ مِنَ ٱلرِّبَوٰٓاْ إِن كُنتُم
مُّؤۡمِنِينَ ٢٧٨

فَإِن لَّمۡ تَفۡعَلُواْ فَأۡذَنُواْ بِحَرۡبٖ مِّنَ ٱللَّهِ وَرَسُولِهِۦۖ وَإِن تُبۡتُمۡ فَلَكُمۡ
رُءُوسُ أَمۡوَٰلِكُمۡ لَا تَظۡلِمُونَ وَلَا تُظۡلَمُونَ ٢٧٩

"Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na acheni Riba zilizo bakia (ambazo bado mnadai kuwa mnapaswa mlipwe), ikiwa nyinyi ni Waumini.Basi msipofanya (hivyo) (basi)jitangazieni vita na Mwenyezi Mungu na Mtume wake: Na mkitubu (ikim. mkiachana na Riba), basi haki yenu ni mtaji wenu. Msidhulumu wala msidhulumiwe."

(Qur'ani, al-Baqarah, 2:278-9)

Kitabu hiki kinalenga kusisitiza ukweli kwamba Wayahudi wanadhibiti mfumo wa kibenki duniani kote kwenye dunia ya kisasa. Wakati aya hizi za *Qur'ani* hapo juu zinasisitiza umuhimu wa hali juu kabisa ambao Allah Ameuweka kwenye kukataza *Riba*. Kwenye historia yote ya mafundisho ya kiroho, kwa mujibu wa uelewa wangu, Mwenyezi Mungu Mtukufu hajatumia lugha kali kiasi hicho katika kulizungumzia saula lolote jingine zaidi ya *Riba*. Kama pangekuwa na wasiwasi wowote kwenye akili ya mtu yeyote kuhusu suala hili, sasa anapaswa ajihakikishie kuuondoa wasiwasi huo. Allah, kwa hakika, amewapa Ushahidi mkubwa kabisa *Banu Israil*, ya Uwezo Wake Kupigana vita juu ya *Riba*. Na katika kufanya hivyo, Amefundisha somo ambalo hususan Pakistani inapaswa ijikumbushe kwa woga na hofu kubwa!

Baada ya kifo cha Nabii Suleyman (*rehma na amani juu yake*) Wayahudi waliichafua Taurati kwa kujiandikia upya mara kadhaa na kufanya matoleo kadhaa tofauti. Mwanazuoni wa Kimarekani wa Biblia aliyesomea Harvard, Richard Friedman, ameonyesha pasi na shaka kwenye kazi yake muhimu yenye kichwa cha habari: "*Nani Aliandika Biblia?*" (New York: Harper and Row, 1989). Wayahudi waliondoa vifungu vyote vya maneno kwenye Taurati vilivyohusiana na hekalu (au *masjid*) lililojengwa na Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) na Ishmael (*rehma na amani juu yake*) Arabia. *Ka'aba* na *Hajj* hayako tena kwenye Taurati. Pia walibadilisha maneno yote yalimuhusisha Ishmael (*rehma na amani juu yake*) kuwa ni mtoto aliyehusika kwenye kafara na kuweka jina la kaka yake Ishaq (*rehma na amani juu yake*), japokuwa Ishaq (*rehma na amani juu yake*) alikuwa hata bado hajazaliwa wakati wa jaribio la kutoa kafara lilipotokea. Zaidi, mtoto muhusika kwenye kafara hiyo alielezwa na Allah kwenye *Qur'ani* kuwa alikuwa *Haleem* (mtulivu, mvumilivu, msikivu) (*Qur'ani, Surat Saffat, 37:101*), wakati mtoto aliyezaliwa na Sarah alizungumziwa kuwa ni Aleem (mwenye busara) (*Qur'ani, al-Hijr, 15:53*). Walibadilisha Arabia na kuweka Palestina kuwa ndiyo ilikuwa mahali pa tendo hilo la kafara. *Zam Zam*, ambayo ni chemchemu ya kustaajabisha ambayo iliibuka ghafla jangwani wakati Jibril (*rehma na amani juu yake*) aliposugua kisigino chake kwenye mchanga, sasa pamebadilishwa na kufanywa ni kisima kilichopo Palestina. Wakamchafua Ishmael (*rehma na amani juu yake*) kwenye Taurati na kumwita "*mtu mshenzi kama punda mwitu*" na kumuondoa kwenye mkataba na Mungu ili wajiwachie wazi nafasi ya madai kuwa wao peke yao ndiyo 'taifa teule' kwa Mwenyezi Mungu. La hatari kuliko yote, hata hivyo, lilikuwa ni kuchafua, na kubadili kwa makusudi amri ya Mungu ya kukataza *Riba*. Walibadilisha Taurati ili kuifanya ikubali kuruhusu kukopesha pesa kwa faida kwa wasioamini wakati wakaiacha ikataze *Riba* kwenye mahusiano ya kibiashara baina ya Wayahudi (Kumbukumbu ya Taurati, 23:20-21)

Allah Mtukufu Alijibu makosa haya ya kiburi kikubwa kwa kuwapeleka miongoni mwa viumbe Wake ambao walikuwa na uwezo na nguvu kubwa za kupigana vita. Mfalme wa Babilonia, Nebuchadnezzar, aliiteka Palestina, akawashinda Wayahudi, akawachukua utumwani wote aliowateka, akaliteketeza Taifa la Israeli na *Masjid al-Aqsa* (uliojengwa na Solomon – Suleyman) na kuwasafirisha Wayahudi kama watumwa kwenda Babilonia (*Qur'ani, al-Isra, 17:4 -5*). Hii kwa hakika ilikuwa ni mfano hai wa uwezo wa Allah kupigana vita.

Palikuwa na tukio la pili la onyesho la nguvu za Allah wakati Mfalme wa Kirumi, Titus, alipoisambaratisha Jerusalem, na kulivunja hekalu (au *masjid*) kwa mara ya pili (*Qur'ani, al-Isra, 17:7, 104*). Hii pia ilihusiana na *Riba*. Allah aliwapeleka mitume watatu Zakariah (*rehma na amani juu yake*), Yohanna (*rehma na amani juu yake*) na Yesu (*rehma na amani juu yake*) kwa Wayahudi. Sehemu ile ya Wayahudi waliowakataa mitume hawa wanajulikana kama Wayahudi (*al Yahood*). Wayahudi walimuua Zakariah (*rehma na amani juu yake*) ndani ya Masjid al-Aqsa (*Matayo, 24:35, 36; Luka, 11:51*). Yohanna alikatwa kichwa katika mazingira ya udanganyifu. Na mwisho, Wayahudi walijigamba kwa jinsi gani wamemuua yesu (*rehma na amani juu yake*). Katika matukio haya yote matatu, Mitume ya Mungu iliwashutumu na kuwashambulia kwa maneno kwa vitendo vyao viovu. Hii ilijumuisha pia shutuma kwa Wayahudi za kubadilisha Andiko (Taurati) na kutumia *Riba*. Yesu (*rehma na amani juu yake*), kwa mfano aliingia kwenye *Masjid al Aqsa* na kuwakuta

wakijishughulisha na vitendo vya *Riba*. Aliwalaani, akazipindua meza zao na kuwafukuza watoke kwenye hekalu (masjid) na kusema: "*Mmeichukua nyumba ya Allah na kuifanya kuwa pango la wezi*." Hivyo basi ni kwa sababu Mitume ya Mwenyezi Mungu waliziweka wazi dhambi zao za kutumia *Riba*, ikiwa ni mojawapo ya madhambi mengine, wakaamua wawaue (isipokuwa Yesu, ambaye Allah alimuokoa kimaajabu). Allah Mtukufu alijibu ukosefu wao wa kutii amri Zake kwa kulipeleka jeshi la Kirumi kwenye Taifa la Israeli kwa mara ya pili. (Israeli itashambuliwa na kuteketezwa kwa mara ya tatuna jeshi la Kiislamu likiongozwa na *Imam al-Mahdi*)

Onyo la Allah kwa vita itakayotokana na kula *Riba*, linapata umuhimu mkubwa zaidi pale tunapokumbuka ukweli kuwa Allah Mtukufu aliingilia kati kuulinda *Masjid*ya (msikiti wa) kwanza (*ikim. Ka'aba*) wakati Abraha alipokuja na jeshi lake la tembo kwa lengo la kuuteketeza (*Qur'ani, al-Fil, 105:1-5*). Hata pale ambapo *Ka'aba* ilikuwa imejaa masanamu, Allah Mtukufu aliingilia kati na kuuokoa kutoka kwenye hatari ya kuteketezwa. Halafu, japokuwa hapakuwa na masanamu yoyote kwenye *Masjid* ya (msikiti wa) pili, (*ikim. Masjid al-Aqsa*) Allah Mtukufu aliyapeleka majeshi mara mbili kuuteketeza. Huu ndiyo ukweli kuhusu hali ya Hasira za Mungu kuhusiana na ugandamizaji wa *Riba*.

Onyo kali mno kwa Wayahudi ni kuwa *Shirk* ya Taifa la Israeli la kisasa lenye mfumo wa kidunia lisiloegemeza sheria zake kufuata amri za Mwenyezi Mungu, lililokubuhu kwenye uchumi ulioegemea kwenye misingi ya *Riba*, yote haya yanaweka wazi uvunjaji wake wa masharti ya urithi wa Ardhi Takatifu. Matokeo ya uvunjaji huo wa amri Zake, ni kwa Allah kujibu kwa kuwapa adhabu.

HITIMISHO

وَلَوْ جَعَلْنَاهُ قُرْآنًا أَعْجَمِيًّا لَّقَالُوا لَوْلَا فُصِّلَتْ آيَاتُهُ أَأَعْجَمِيٌّ وَعَرَبِيٌّ قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ آمَنُوا هُدًى وَشِفَاءٌ وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي آذَانِهِمْ وَقْرٌ وَهُوَ عَلَيْهِمْ عَمًى أُولَٰئِكَ يُنَادَوْنَ مِن مَّكَانٍ بَعِيدٍ

"Na lau tungeli ifanya Qur'ani kwa lugha ya kigeni wangeli sema: Kwanini Aya zake haziku pambanuliwa (katika lugha ambayo tunaweza kuielwa)? Yawaje lugha ya kigeni na Mtume Mwaarabu? Sema: Hii Qur'ani ni uwongofu na poza kwa wenye kuamini. Na wasio amini umo uziwi katika masikio yao, na pia upofu (kwenye macho yao) hawaioni. Hao wanaitwa nao wako pahala mbali.

(Qur'ani, Fussilat, 44:41)

Umefika wakati ambapo tunahitimisha kwa kutoa kwa muhtasari mambo muhimu ambayo kitabu hiki kimelenga kuyafikisha kwa msomaji. Nayo ni kama ifuatavyo: Mapinduzi ya kiajabu ambayo yalilibadilisha bara la Ulaya kutoka kwenye upagani na kuingia kiujumla kwenye Ukristo, lakini likiwa na kundi dogo la Kiyahudi lenye uwezo mkubwa wa kuweza kuathiri matukio, baadaye lilijikuta limeshikwa na mapinduzi ya kiajabu zaidi ambayo yaliwapelekea watu hao hao wa bara la Ulaya sasa kuwa hawana imani tena na Mungu. Katika mlolongo wa kugeuka na kuwa Mkristo na Myahudi, mtu huyo Mzungu Mweupe ambaye kiujumla hana imani na Mungu amezihujumu dini zote mbili za Kikiristo na Kiyahudi na kuharibu yale yote matakatifu yaliyotoka kwa Mungu yaliyobakia kwenye dini hizi.

Mtu huyo wa kisasa Mzungu Mweupe akishirikiana na watu-kasuku wenziwe wenye ngozi za kahawia, njano na nyeusi hivi sasa wanajaribu kuufanyia Uislamu yale yale ambayo huko nyuma walizifanyia dini za Kikristo na Kiyahudi. Haya ni maelezo ya kimsingi yanayoweka wazi sababu za vita ya miaka elfu moja inayoelekezwa dhidi ya Uislamu ambayo ilianzishwa kwa hasira kubwa baada ya tukio la tarehe 11 mwezi wa Tisa. Waislamu sasa hivi wanajikuta wanaelemewa na juhudi zenye changamano pana zinazoelekezwa kwao zikiwa na lengo la kuubadillisha Uislamu uweze kushabihiana na matakwa na mwenendo wa jumuiya ya kimataifa isiyomtambua Mungu. Uislamu mpya uliojipodoa unatafutwa ujitokeze ambao utawakubali Wayahudi kama watawala wa dunia na kulikubali Taifa la Israeli kama *Taifa Tawala* la dunia. Ili hili litokee inalazimu Uislamu huo uyaachilie mbali majukumu yote ya *Jihadi.*

Waislamu wanaambiwa kuwa thamani na maadili ya jumuiya mpya ya kimataifa ni yale yale yanayoendana na Uislamu halisi. Lakini jumuiya mpya ya kimataifa pamoja na tabaka lake la juu la mchanganyiko wa watu watokanao na jamii tofauti duniani, ni matokeo ya utamaduni wa kimagharibi

usiomtambua Mungu na mtazamo wao wa maisha ni sawa na ule wa utamaduni usiomtambua Mungu. Miongoni mwa maadili yao ni *Shirk* ya kisiasa ambayo sasa hivi imewakumbatia kwa hatari kubwa binaadamu wote, na mfumo wa uchumi wa *Riba* ambao pia umewakumbatia binaadamu umewaletea aina mpya ya uchumi wa kitumwa.

Utamaduni wa kimagharibi usiomtambua Mungu ndiyo uliyowezesha kufufuliwa kwa Taifa la Israeli, na kuanzishwa kwa Taifa la *Wahhabi wa Saudi* la Saudi Arabia, nani utamaduni huo huo ndiyo uliohakikisha kuwa mataifa yote mawili, Israeli na Saudi Arabia yanaendelea kuwapo kuanzia yalipozaliwa hadi leo hii. (Tazama kitabu chetu kinachoitwa: '*Khilafa, Hejaz na Taifa la Wahhabi wa Saudia.*') Huu ndiyo ufunguo ambao Waislamu wanaweza kupata fursa ya kuielewa dunia ya leo. Hakuna kinachoweza kuyaelezea matukio haya mawili yasiyokuwa ya kawaida bila kuitumia *Qur'ani*. Maelezo ya *Qur'ani* yaliyojitokeza na kuwa kama ni kiini cha kitabu hiki ni kwamba dunia sasa hivi iko chini ya udhibiti wa *Ya'juj* na *Ma'juj* pamoja na *Dajjal*, Mtume wa Uongo.

Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alielezea lengo la Mpango wa Mungu ambamo Wayahudi (ikim. Wayahudi asilia) waliondolewa kutoka kwenye Ardhi Takatifu baada ya kumkataa masihi, mtoto wa Bikira Maria, na jaribio lao la kumsulubu. Allah, Mwingi wa Huruma, akawapa kipindi maalum ambamo walipewa fursa ya kutafuta msamaha Wake *(Huenda ikawa Mola Wenu akawarehemu) Qur'ani, Banu Israil, 17:8)* na Aliwaachia mlango mmoja pekee wazi ambao wangeweza kupata msamaha. Mlango huo wa msamaha ulikuwa ni Mtume ambaye alikuwa anatarajiwa kuja. Alikuwa Muhammad (*rehma na amani juu yake*), Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wayahudi wanapaswa kumuamini na kumfuata, kumuheshimu, na kumsaidia ili kupata msamaha wa Mungu (*Qur'ani, al-Araf, 7:157*).

Ikiwa Wayahudi asilia watamkataa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*), matokeo yake ni kuwa huo mlango wa fursa ya msamaha utafungwa, na muda wa hesabu kuelekea kwenye Zama za Mwisho utakapofika, Allah Mtukufu atawarudisha kwenye eneo ambalo walitenda madhambi makubwa kabisa kuliko yote, ikim. Ardhi Takatifu *(Qur'ani, Banu Israil, 17:104).*Kurudi kwao kwenye Ardhi Takatifu kungemaanisha kuwa mwanzo wa adhabu yao ya mwisho umeshaanza. Kitabu hiki kinataarifu kuwa muda huo umeshafika! Kipindi cha miezi kumi na saba kilichoanzia pale ambapo Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) alipowasili Madina kilikuwa ni kipindi muhimu kuliko vipindi vyote vya historia ya Wayahudi. Mlango wa fursa ya msamaha wa Mungu kwao ulifunguliwa. Pale ilipodhihirika kuwa Wayahudi siyo tu wamemkataa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*), bali pia walianza kupanga kwa siri njama za kuuangusha Uislamu, Allah Mtukufu aliamrisha kubadili *Qiblah* na hiyo amri ilimaanisha kuwa mlango wa Msamaha wa Mungu umefungwa kwa Wayahudi. Haitatokea tena milele kwa wao kuweza kupata ridhaa ya urithi wa Ardhi Takatifu. Badala yake ni Waislamu ndiyo waliopewa nafasi hiyo ya urithi:

وَهُوَ ٱلَّذِى جَعَلَكُمْ خَلَٰٓئِفَ ٱلْأَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ بَعْضٍ
دَرَجَٰتٍ لِّيَبْلُوَكُمْ فِى مَآ ءَاتَىٰكُمْ ۗ إِنَّ رَبَّكَ سَرِيعُ ٱلْعِقَابِ وَإِنَّهُۥ لَغَفُورٌ
رَّحِيمٌ ﴿١٦٥﴾

"Naye ndiye aliye kufanyeni (Waislamu) makhalifa wa Ardhi (Takatifu) (baada ya Wayahudi), na amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa kubwa, ili akujaribuni kwa hayo aliyo kupeni (Banu Israil walipewa zaidi kuliko watu wengine). Hakika Mola Mlezi wako ni Mwepesi wa kuadhibu, na hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu."

(Qur'ani, al-An'am, 6:165)

Ilikuwa katika kipindi hiki, ikim. baada ya kubadili *Qiblah* na kabla ya kifo cha Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ndipo kuwa kuachiwa huru kwa *Dajjal* na *Ya'ajuj* na *Ma'ajuj* kulitokea. Ni Waislamu wenye jicho moja peke yao ndiyo watakaojumuika kushiriki kwenye ghafla za 'pamoja za jumuiya za dini tofauti' na vikao vya sala za pamoja. Hii ni kwa sababu Wayahudi hivi sasa wamerudishwa kwenye Ardhi Takatifu ili kukabiliana na matunda ya matendo yao maovu, ikiwemo uovu ambao hivi sasa wanaendelea kuutenda. Juu kabisa ya orodha hiyo ya matendo maovu ni usaliti wao wa kuvunja agano baina yao na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Wayahudi tayari wamegundua kuwa Allah Mtakatifu amewaadhibu wao mara kadhaa huko nyuma. Kitabu hiki kimeelezea mtazamo wa *Kiislamu* kuwa historia haiwezi kufikia mwisho wake kabla Wayahudi hawajapata adhabu ya mwisho. Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) ametuachia habari muhimu mno juu ya suala hili, nayo ni kuwa jeshi la *Kiislamu* litavamia na kuiteka Jerusalem, litaivunja na kuliteketeza Taifa la kitapeli la Israeli na kuwapa adhabu Wayahudi. Wafuasi wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) hapo wataikomboa Ardhi Takatifu. Hapa kwa mara nyingine tena, ni utabiri wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) unaosema:

"Abu Hurairah amesikika akisema kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*) alisema: Bendera nyeusi zitaibuka kutokea Khorasan (ikim. eneo ambalo hivi sasa linajumuisha Afghanistani, Pakistani na sehemu ndogo ya Irani na Asia ya Kati) na hakuna jeshi litakaloweza kuwasimamisha hadi watakapoingia Aelia (Jerusalem)."

(Sunan, Tirmidhi)

"Amesema Auf bin Malik: Nilienda kwa Mtume wakati wa Ghazwa wa Tabuk wakati akiwa amekaa kwenye hema la ngozi. Akasema: Hesabu mambo sita ambayo yataashiria kuwa 'Saa' imekaribia: kifo change, kushambuliwa kwa Jerusalem, ugonjwa hatari ambao utawashambulia (na kuwaua kwa wingi sana) kama ugonjwa unaowaathiri kondoo, kuongezeka kwa utajiri kiasi kwamba hata mtu akipewa dinari mia moja, hatoridhika, kisha mateso ambayo hakuna nyumba ya mwarabu itakosa kuyapata, na amani baina yenu na bani al-Asfar (ikim. Ufalme wa Kirumi) ambao watawashambulia chini ya bendera themanini. Na kila chini ya bendera moja kutakuwa na askari elfu kumi na mbili.

(Sahih Bukhari)

"Amesema Abdallah ibn Umar: Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*) alisema: "Nyinyi (ikim. Waislamu) mtapigana na Wayahudi hadi baadhi yao watajificha nyuma ya mawe. Mawe yataongea (na kuwasaliti) yakisema: 'Abdullah (ikim. mtumwa wa Allah!) Hapa kuna Myahudi amejificha nyuma yangu, hivyo muue."

(Sahih Bukhari)

"Abu Hurairah amesikika akisema kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (*rehma na amani juu yake*) alisema: 'Saa ya Mwisho' haitotokea isipokuwa kabla yake Waislamu watapigana na Wayahudi. Waislamu watawaua hadi Wayahudi watajificha nyuma ya jiwe au mti, na jiwe au mti litasema: Ewe Muislamu, au mja wa Mwenyezi Mungu, kuna Myahudi kajificha nyuma yangu, njoo umuue, lakini mti wa Gharqad hautosema (kitu kama hicho) kwa kuwa ni mti wa Wayahudi."

(Sahih Muslim)

Huenda kwa mara ya kwanza vita inapiganwa kwa 'mawe.' Maasi ya Waislamu wa Palestina '*intifada*' yanaendelea kupambana na ugandamizi wa Israeli kwa kutumia 'mawe.' Hii kwa kweli ni alama ya kutisha kwa Israeli. Zaidi, Israeli imejikita kwenye kuharibu 'miti' kwenye Ardhi Takatifu. Maelfu ya miti ya zaituni imekwishaharibiwa na Israeli kwenye jitihada zake za kishetani za kuongeza ugumu wa maisha ya kiuchumi ya Wapalestina, wote wa Kiislamu na Kikristo. Hasira dhidi ya matendo haya ya *Fasad* ni kuwa '*miti na mawe iliyopo kwenye Ardhi Takatifu sasa hivi imeanza 'kuongea*' katika kutimiza utabiri wa Mtume (*rehma na amani juu yake*). Ni Dhahiri kuwa miti na mawe hayawezi kusikika na sikio la nje. Badala yake, ni kwa kutumia uwezo wa ndani wa moyo wa kusikia kwa wale ambao wana iman, hao ndiyo wanaoweza kuisikia 'miti' na 'mawe' wakati inaongea! Hilo, huenda ndilo linaloelezea kwanini serikali za Saudi Arabia, Egypt, Uturuki, Jordan, na Pakistani zikiwemo serikali nyingi nyingine duniani, zinaonekana kuwa haziwezi kuyasikia mawe yakiongea kwenye Ardhi Takatifu!

Mtazamo wetu ni kwamba utabiri huo hapo juu wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) tayari unatimia leo hii kwenye jitihada za intifada za Wapalestina. Kadiri muda unavyopita mawe yataendelea kuongea kwa sauti kubwa zaidi na zaidi. Ni wale tu walio viziwi na vipofu wa kiroho ndiyo watakaokuwa wanashindwa kuyasikia yakiongea. Ikiwa mawe yenyewe sasa hivi yanawalilia Waislamu popote walipo duniani kuikomboa Ardhi Takatifu kutokana na kuchukuliwa na kushikiliwa kwa mabavu na Wayahudi, kinachotarajiwa ni kuwa Waislamu wanapaswa kujizatiti na kujipanga kuelekeza nguvu na mali zao kwenye juhudi hizo badala ya kupoteza nguvu kwenye masuala yasiyo na uzito wa kutosha kama vile kupandisha kiwango cha maisha ya watu ambao tayari wanaishi maisha mazuri. Inafuata mkondo wa mantiki kuwa Waislamu hawapaswi kuishi kwenye maeneo ambayo vita dhidi ya Uislamu na kuunga mkono Taifa la Israeli kunaonekana kwa kiwango cha juu zaidi. Nchi hizo ni Marekani, Uingereza, n.k. Waislamu wanapaswa kuhama kutoka kwenye nchi kama hizo na kwenda kuishi kwenye maeneo ambayo wataweza kulinda imani zao vyema zaidi na kuunga mkono jitihada za kuikomboa Ardhi Takatifu. Dunia inazidi kugundua kuwa ugandamizi

ulioanzishwa na unaoendelea kusimamiwa na Israeli, ugandamizaji ambao utaendela kuongezeka hadi, kwa mujibu wa utabiri wa Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*):

"… mtu atapita pembeni ya kaburi na tajigalagaza juu yake na kusema: Natamani mimi ndiye ningekuwa ndani ya kaburi (badala ya aliyezikwa humo), na siyo kwa sababu za kidini, bali ni kwa sababu ya ugandamizaji."

(Sahih, Muslim)

Huenda, onyo kali kuliko yote ambalo kitabu hiki kinaweka wazi ni kuwa kila siku ijayo hivi sasa itashuhudia kukandamizwa kwa Waislamu ambao watabaki wanaushikilia Uislamu. Kuanzia tarehe 11 mwezi wa Tisa, ugandamizaji wa Waislamu wa aina hiyo umeongezeka kwa kiasi kikubwa duniani kote. Waislamu sasa hivi wanaishi kwenye 'mama wa majaribu yote.' 'Taifa Tawala' la dunia sasa hivi (Marekani) inaongoza juhudi za kuifanya dunia iwe salama kwa 'Taifa Tawala' lijalo (Israeli!)

Mwongozo ambao *Qur'ani* inatupa kwenye *Surah al-Kahf* ni mwongozo pekee ambao Waislamu wanaweza kutarajia kuyashinda mawimbi hatari yanayowakabili. Mwongozaji pekee ambaye anaweza kuwaongoza Waislamu kwa ufanisi kwenda kwenye ushindi ni yule mwongozaji ambaye anazielewa zama hizi tunazoishi hivi sasa na ambaye uelewa wake unatokana na *Qur'ani* na *Ahadith* za Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*). Kiongozi huyo ataielewa Shirk kwenye taifa la kisasa la kidunia na mfumo wake wa chaguzi za kisiasa na atawashauri Waislamu kutoshiriki kwenye chaguzi hizo zenye *Shirk* kwa kutotoa ridhaa yake kwenye katiba za kidunia zizizotambua kuwapo kwa Mungu na kushiriki kwenye chaguzi za nchi zaenye mfumo wa kisasa. Pia ataelewa *Riba* ya mfumo wa uchumi wa kisasa na atawashauri Waislamu kuacha kushikamana na aina zote za *Riba* kwa kiasi kikubwa watakavyoweza. Atagundua kuwa 'pesa za makaratasi' ni *Haram* na atachukua hatua kuwahamasisha Waislamu kurudi kwenye matumizi ya sarafu za dhahabu na fedha kama pesa ambazo zinaweza kutumika kwenye soko kama chombo cha malipo halali. (Ni kitu kigumu kutokea kwa Myahudi wa kimataifa ataweza daima kuiruhusu serikali ya Malaysia kuanzisha matumizi ya sarafu za Dhahabu na Fedha kama 'malipo halali' kwenye soko.)

Mwongozaji atagundua na kuwaonya watu wake kuhusu *Riba* ya 'mlango wa uani' ambayo sasa hivi inatumiwa na Mabenki ya Kiislamu, Vyama vya Ushirika na taasisi mbalimbali za kifedha. Kiongozi kama huyo atakitaja kipindi hiki kuwa ni zama za *Ya'juj* na *Ma'juj* na *za Dajjal*, Mtume wa Uongo. Waliobaki si lolote zaidi ya kuwa ni 'wapiga miruzi kwenye upepo.'

Kitabu change kinachoitwa *Surah al-Kahf* na Zama za Kisasa, ambacho sasa hivi ninakiandika, insha Allah kitajaribu kuelezea mwongozo ambao *Surah* hii ya *Qur'ani* inautoa. Na katikati ya moyo wa mwongozo huo ni umuhimu wa kujiondoa kwenye miji mikubwa na kwenda vijijini na nje ya miji ambako ardhi ni ya bei nafuu na ambapo maji yanapatikana. Vijiji vya *Kiislamu* vinaweza kuanzishwa kwenye maeneo hayo na juhudi zinaweza kufanywa kufufua na kuanzisha *Uislamu* kama njia na mfumo wa maisha vijijini humo. Sehemu 2 za kitabu cha mwalimu wangu, Maulana Dr. Fadlur Rahman Ansari, kinachoitwa '*Misingi ya Qur'ani na Muundo wa Jamii ya Kiislamu*' ni mpango makini wa kutosheleza kuleta uponaji wa imani kwa kuwa inatoa miongozo maalum inayotokana na *Qur'ani* ambayo lazima itekelezwe ili kuanzisha Uislamu wa kweli ndani ya vijiji hivyo. Mwandishi wa kitabu hiki amefafanua zaidi kuhusu suala hili kwenye Utangulizi watoleo

la hivi karibuni la kitabu cha Dr. Ansari, ambacho tunakipendekeza kwa msisitizo mkubwa kwa wasomaji wetu.

Ni kutokana na Watoto wataolelewa kwenye vijiji vya Kiislamu ambavyo vimejitenga na dunia isiyomjali na kumtambua Mungu ndimo watakapotoka jeshi la baadaye la Kiislamu litakaloikomboa Ardhi Takatifu.

Viambatanishi

Kiambatanishi cha kwanza

Bahari ya Galileo

(Pia inajulikana kama Ziwa Kinneret au Ziwa Tiberius)

Bahari ya Galileo ni chanzo cha mwanzo, kikubwa Zaidi na muhimu kuliko vyote kwa upatikanaji wa maji ya kunywa kwenye eneo lote la Ardhi Takatifu. Waisraeli, Wapalestina na Wajordani wanategemea sana chanzo hicho kwa mahitaji yao ya maji. Ikiwa Bahari ya Galileo itakauka (kama ilivyotabiriwa kwenye Hadith ya Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) Waisraeli wataweza mara moja kuanza kutumia teknolojia ya kuchuja maji ya chumvi ya bahari ili kupata maji ya kunywa na kuumaliza upungufu wa maji ya kunywa utakaojitokeza. Lakini Wapalestina na Wajordani hawatoweza kufanya hivyo, watakosa suluhisho hilo mbadala. Watajikuta wamekuwa mateka ambao wanalazimika kununua maji kutoka kwa Waisraeli ili waweze kuendelea na maisha yao kama kawaida. Hawatoweza kumudu gharama za maji hayo kwani matumizi ya silaha ya kiuchumi ya Kiyahudi ya *Riba* imekwishawapeleka kwenye umasikini na ufukara. Matokeo yake ni kuwa watalazimika kujiweka chini na kujisalimisha kisiasa kwa Israeli ili wapate maji. Wasipofanya hivyo watapoteza maisha.

Kiwango cha maji kwenye Bahari ya Galileo sasa hivi kiko chini sana kiasi kuwa hautopita muda mrefu kabla ya Israeli kuweza kuitumia hiyo karata yake mbaya ya maji.

Uri Saguy ni Mwenyekiti wa Mekorot, Bodi ya Shirika la Taifa la Maji la Israeli. Katika mkutano wa hivi karibuni wa Bodi (mwanzoni mwa mwezi wa Kumi na Mbili, 2000) alitoa maelezo haya: “Rasilimali maji ya Taifa yako kwenye ukingo wa maafa na serikali haifanyi jitihada za kutosha kuweza kujikinga na hali hiyo ya hatari” Aliyakataa mapendekezo ya kuagiza maji ya kunywa kutoka Uturuki ili kutatua tatizo hilo la maji kuwa hayatekelezeki, tatizo ambalo limejitokeza kutokana na upungufu mkubwa wa maji kwenye Ziwa Kinneret na kwenye mabwawa ya chini ya ardhi ya akiba za kitaifa, ikiwemo pia vyanzo vya Pwani na Milimani vya maji. Kiwango cha maji kwenye Ziwa Kinneret kiko chini kuliko kipindi chochote kilichopita kwenye historia, na vyanzo vingine viko katika hali hiyo hiyo. Kiwango hicho kwenye ziwa hilo kiko chini sana kiasi hautopita muda mrefu kabla Mekorot hawajalazimika kuacha kuvuta maji kutoka humo ili kuyaingiza kwenye mabomba ya maji kwa matumizi ya wateja nchi nzima. Pampu za maji zilishawekewa kipimo kuwa kiwango cha maji kikifikia hapo basi hazitoweza kufanya kazi.

Kiambatanishi cha pili

MAJIBU YA WAISLAMU KUHUSIANA NA SHAMBULIZI LA 9/11 LILILOFANYIKA AMERIKA

Mwandishi: Imran N. Hosein

Tafsiri: Abdul Hamisi Akida

فَلَا تَهِنُوا وَتَدْعُوا إِلَى السَّلْمِ وَأَنتُمُ الْأَعْلَوْنَ وَاللَّـهُ مَعَكُمْ وَلَن يَتِرَكُمْ أَعْمَالَكُم

Je, kiwango cha maji kimefikia wapi? Yitzhak Gal, mfanyakazi wa siku nyingi wa Mamlaka ya Ziwa Kinneret aliwahi kusema: *"Kutokana na utafiti tulioufanya, hiki ni kiwango cha chini kabisa kwa muda wa miaka 150 iliyopita. Pia tumetazama nyaraka za elimukale (ekiolojia) kurudi nyuma hadi enzi za Warumi na inaonekana kuwa ziwa hili halijawahi kuwa na maji kidogo kama ilivyo hivi sasa."*

Saguy alionya: "Ikiwa hapatokuwa na mabadiliko ya kimsingi [kwenye sera za serikali] katika muda mfupi ujao, hapatokuwa na maji mwaka ujao ya kutosha kukidhi mahitaji ya watumiaji." Na akaongeza: *"mwakani patakuwa na maafa."* Maafa hayo yatakuwa na athari za kimataifa kwa sababu Israeli ina jukumu la kuwapatia maji Wajordani na Wapalestina kutoka kwenye vyanzo ambavyo vinakauka kwa haraka sana.

Mwenyekiti wa Mamalaka ya Ziwa Kinneret Zvi Orenberg ameizungumzia hali ya maji kwenye ziwa hilo kuwa ni "ya kutisha" na akaendelea kusema: "*Tutakabiliwa na maafa makubwa ikiwa hatutopata mvua za kutosha ambazo kila mtu amekuwa akiweka matumaini kuwa zitanyesha pamoja na kufanya sala za maombi katika kipindi hiki cha masika."* Tayari hali ya uchumvi chumvi inapanda kiwango na mwani na mchipwi inashamiri.

(Makala kadhaa zimechapishwa kuhusu suala hili katika gazeti la Jerusalem Post na David Rudge. Miongoni mwao ni hizi zifuatazo:

"Serikali inapuuza umuhimi wa upungufu wa maji." Tarehe 5, mwezi wa Kumi na Mbili, 2000 na "Maafa ya ukosefu wa maji yanakuja kwa mabomba" tarehe 19, mwezi wa Kumi na Mbili, 2000. Makala za hivi karibuni zinaonyesha hali kuwa ni mbaya zaidi. Sababu za kifedha zinatuzuia kuchapisha Makala hizo kwenye kiambatanishi hiki.)

Kiambatanishi cha pili

MAJIBU YA WAISLAMU KUHUSIANA NA SHAMBULIZI LA 9/11 LILILOFANYIKA AMERIKA

Mwandishi: Imran N. Hosein

Tafsiri: Abdul Hamisi Akida

فَلَا تَهِنُوا وَتَدْعُوا إِلَى السَّلْمِ وَأَنتُمُ الْأَعْلَوْنَ وَاللَّـهُ مَعَكُمْ وَلَن يَتِرَكُمْ أَعْمَالَكُم

"Basi msiregee na kutaka suluhu, maana nyinyi ndio mtakaoshinda. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja nanyi, wala hatakunyimeni malipo ya vitendo vyenu."

(Qur'ani, Muhammad, 47:35)



"Na mwenye kuhama katika Njia ya Mwenyezi Mungu atapata pengi duniani pa kukimbilia, na atapata wasaa. Na anaye toka nyumbani kwake kuhama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kisha yakamfika mauti njiani basi umethibiti ujira wake kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye maghfira na Mwenye kurehemu"

(Qur'ani, an-Nisa, 4:100)

Utangulizi

Nilifuatilia mashambulizi ya Marekani dhidi ya Waislamu wa Afghanistani yaliyokosa hata chembe ya ushujaa basi tu kwa sababu walisimamia *Uislamu* na ambao hawakuhusika kabisa na shambulio la Marekani la 9/11, huku nikiwa na uchungu mkubwa usioelezeka. Yamekosa ushujaa kwa sababu adui anaogopa kabisa kukabiliana na Muislamu wakiwa kwenye uwanja ulio sawa. Vita vyao wanapigana wakiwa kwenye usalama wa ndege za kivita na kutumia makombora yanayoelekezwa, wakiwa mbali kabisa na uwanja wa vita na juu ya mawingu. Lakini, Allah, atatuletea siku hiyo, *Insha Allah* ambayo tutaweza kukutana nao ana kwa ana kwenye uwanja wa mapambano. *Amin!* Hadi siku hiyo itakapofika, hatuna budi kuendelea na jitihada zetu kujilinda na huku tukionyesha subira kubwa.

Watalibani walikuwa kwenye hali inayolingana na ya yule kijana wa miaka 12 wa Kipalestina aliyekuwa akipigana kwa jiwe mkononi mwake dhidi ya kifaru kilichotengenezwa Marekani cha jeshi

la ulinzi la Israeli. Watalibani hawakushindwa na Wamarekani na wala hawakusindwa pia na mkusanyiko wa ma-Yankee wa Ushirika wa Kaskazini ambao Irani bado wanajisikia kuwa na ridhaa nao. Na vijana wadogo wanaopigana kwa mawe kwenye Ardhi takatifu hawatoshindwa. Badala yake, Watalibani walirudi kwenye milima ambako mabomu na ndege za Marekani hazikuweza kuwafikia. Hivyo basi hawa askari wa Allah, wamepona na watakuwa tayari kujiunga tena kwenye mapambano yajayo. Tunawapa hongera zetu! Hakika vita hii haitoisha hadi jeshi la Kiislamu liibuke kutokea Khorasan na liendelee hadi Jerusalem. Wale wote ambao watasoma kitabu hiki, walio Waislamu, wanapaswa wawe na hamu na fukuto ndani ya nyoyo zao ili kuwa sehemu ya jeshi hilo.

Kitabu hiki kinatoa hongera na salamu za rambirambi kwa kumbukumbu ya kila Muislamu aliyekufa ikiwa ni matokeo ya ugaidi usiokuwa na chembe ya ushujaa wa Waingereza, Wamarekani na Israeli. Damu na machozi ya vijana wetu mashujaa ambao waliuawa Afghanistani, na ambao sasa watauawa kwingineko duniani, au ambao watafungwa kwenye jela zilizomo kwenye nchi zenye mfumo usiomtambua Mungu, hayatopotea bure. Badala yake yatatia mbolea kwenye juhudi na jitihada zisizokuwa na kikomo za mamilioni ya Waislamu (hasa vijana wa Kiislamu) sehemu zilizobaki ambao sasa wataamua kfuatia kitendo hiki cha aibu isyofichika, kujikita wao wenyewe na watoto wao na wajukuu wao kwenye juhudi za kijeshi la Kiislamu ambalo llitaishia kuikomboa Ardhi Takatifu. Huu '*usiku wa giza'* hakika hauwezi kubaki hivyo kwa miaka mingine hamsini kabla mwanga wa jua haujarejea, *insha Allah*, na Ukweli uushinde uongo kwa mara ya mwisho, *Uislamu* utawale dunia kutokea Jerusalem. Kitabu hiki '*Jerusalem katika Qur'ani'* kimeandikwa ili kuwapa motisha vijana wa Kiislamu. Ninamuomba Allah, Mtukufu, aniletee wale ambao watakitafsiri kitabu hiki kwenda kwenye kila lugha inayoongewa na Waislamu ili iwafikie vijana hao wa Kiislamu. *Amin!*

Shambulio la kigaidi la 9/11 lililotokea Marekani, limetufikisha mahali penye umuhimu wa kihistoria ambapo patatokea mabadiliko kama vile ilivyotokea mnamo mwaka 1914, wakati shambulio jingine la kigaidi lilitokea na kusababisha kuanzisha Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia. Ninaamini kuwa wale ambao kwa hali na mali wameng'ang'ania kujihakikishia kuwa mwishowe *wanaitawala dunia nzima* wanahusika na mashambulizi yote mawili, na kuwa shirika la kijasusi la Israeli, Mossad na washirika wake wamehusika kwenye kupanga na kutekeleza shambulio hilo la mwezi wa Tisa. Tukio hilo, pamoja na matokeo yake ya vita dhidi ya 'ugaidi' ambayo liliisababisha, yalipangwa ili kuifanya dunia iwe salama zaidi kwa Wayahudi na Taifa la Israeli. Magaidi husika waliofanya shambulizi hilo, wenyewe wanajijua kuwa wao ni nani, na Allah Mtukufu pia Anawajua wao ni nani. Tunamuomba Allah, Mtukufu, awaumbue kwa kuwaweka wazi wajulikane, na kisha Awaadhibu. *Amin!*

Mfumo wa kidunia wa Waingereza / Wamarekani / Wayahudi unaotawala duniasasa hivi umejifungua na kuupiga vita Uislamu kwa wazi zaidi kuliko kipindi kingine chochote kilichopita kabla ya hapa. Hii ni kwa sababu wanakaribia kilele cha vita wanayopigana kwa zaidi ya miaka elfu moja sasa. Kitabu hiki, *Jerusalem katika Qur'ani*, kimefanya jitihada ya kuielezea vita hii dhidi ya Uislamu, na kutafakari nini kinakuja kwenye mfumo huo wa dunia baada ya hapa, kwenye mpangilio wa matukio duniani, kwa Waislamu na Taifa la Israeli.

Viumbe wa hatari na wenye kutia aibu kuliko wote kwenye mgongo wa dunia leo hii (au tuseme watu wabaya kuliko wote chini ya mawingu) ni wale wanazuoni wa *Kiislamu* au viongozi mbalimbali ambao ni Waislamu ambao walipotoshwa na kudanganywa kabisa na tukio hilo la kigaidi la 9/11 ambao walihamaki na kuwalaani Waarabu na Waislamu kwa shambulio hilo na kunyoosha mikono kuwaunga mkono Uingereza/Amerika/Israeli kwenye vita yao dhidi ya Waislamu wa Afghanistani. Mtazamo wangu ni kwamba Usama bin Laden na utawala wa Talibani hawakuhusika kabisa na tukio hilo la kigaidi la 9/11. Vita dhidi yao ni ya dhulma na haiwatendei haki kabisa. Wanazuoni na viongozi wa aina hiyo wa Kiislamu wanapaswa kupingwa hadharani na watakiwe kutoa sababu zao za kuthibitisha wanayoyasema.

Siku chache baadaye niiliitikia shambulio hilo la tarehe 11 mwezi wa Tisa kwa sala na maombi kwa Allah Mtukufu kwenye Kituo cha Kiislamu cha Queens, New York, awape adhabu kali kuliko adhabu zote wote waliohusika, na adhabu iendelee hadi Siku ya Mwisho. Wote waliokuwa kwenye *Masjid*, walijiunga nami kwenye maombi hayo. Baada ya kufanya hivyo, hivi sasa nawakaribisha Wayahudi nao wafanye maombi kama hayo.

Nani Kafaidika na Shambulio la 9/11?

Haiyumkiniki kuwa Mzungu Myahudi aliye Uingereza, au Amerika au kwenye Ardhi Takatifu atataka kukisoma kitabu hiki. Isitoshe, ana mambo mengi muhimu zaidi ya kuyafuatilia – kama vile kuendelea na jitihada za kila siku zitakazoishia yeye *kuitawala dunia* kutokea Jerusalem. Ili aweze kufanikiwa kufanya hivyo, analazimika kuwafanya watumwa binaadamu wote duniani (ikim. wale wote ambao si Wayahudi) wawe kwenye umasikini mkubwa mno wa kisiasa na kiuchumi. Na anafuatilia lengo hili bila 'kujali hali' kwa sababu hawawachukulii wale wasiokuwa Wayahudi kuwa ni watu ambao wanastahili kupewa heshima na haki na maadili kama vile ambavyo anastahili Myahudi (pale wanapokuwa na mahusiano na Wayahudi wenzao).

Qur'ani inazungumzia tabia hii ya undumilakuwili wa kimaadili ya Wayahudi, na dharau kwa wale waiokuwa Wayahudi, kwenye aya ifuatayo:


۞ وَمِنْ أَهْلِ ٱلْكِتَٰبِ مَنْ إِن تَأْمَنْهُ بِقِنطَارٍ يُؤَدِّهِۦٓ إِلَيْكَ وَمِنْهُم مَّنْ
إِن تَأْمَنْهُ بِدِينَارٍ لَّا يُؤَدِّهِۦٓ إِلَيْكَ إِلَّا مَا دُمْتَ عَلَيْهِ قَآئِمًا ۗ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ
قَالُوا۟ لَيْسَ عَلَيْنَا فِى ٱلْأُمِّيِّـۧنَ سَبِيلٌ وَيَقُولُونَ عَلَى ٱللَّهِ ٱلْكَذِبَ وَهُمْ
يَعْلَمُونَ ٧٥

"Na miongoni mwa Watu wa Kitabu yupo ambaye ukimpa amana ya 'kantar' (mali iliyo nyingi) atakurudishia, na miongoni mwao yupo ambaye ukimpa amana ya dinari moja hakurudishii isipo kuwa ukimsimamia kumdai (muda wote ili akurudishie). Haya ni kwa kuwa wakisema: Hatuna lawama (ya amana ya kutenda haki) kwa ajili ya hawa wasiokuwa (Wayahudi) wasiojua kitu. Na wanamzulia uwongo Mwenyezi Mungu, hali nao wanajua."

(Qur'ani, ale-Imran, 3:75)

Tunanukuu *Qur'ani* kwa kuwa Allah Mtukufu Ametuamrisha tupigane vita kali dhidi ya wasioamini kwa kuitumia *Qur'ani*:


فَلَا تُطِعِ ٱلْكَٰفِرِينَ وَجَٰهِدْهُم بِهِۦ جِهَادًا كَبِيرًا ٥٢

"Basi usiwat'ii makafiri. Na badala yake (kwa kutumia Qur'ani) pambana nao kwa Jihadi kubwa dhidi yao."

(Qur'ani, al-Furqan, 25:52)

Myahudi wa Kizungu yuko karibu sana kufanikisha lengo lake la kisiasa na kiuchumi la kuwafanya binaadamu kuwa watumwa. Pale atakapokuwa ametimiza lengo lake, na hakuna dalili za kuonyesha kuwa hatofanikiwa, itaonekana kwake kuwa hiyo inathibitisha madai yake ya Kiyahudi ya kuhodhi ukweli. Ni jambo, bila ya shaka, lilsilohusiana kabisa na hilo kuwa 'ugaidi', ugandamizaji na udanganyifu hayana uhusiano kabisa na maadili ya kweli ambayo ndiyo yanajenga misingi ya dini ya Abrahamu (*rehma na amani juu yake*). Lakini upofu wa kiroho wa Myahudi ambaye alimkataa Masihi na Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) imemfanya asiwe na uwezo wa kuutambua ukweli huu wa awali wa kimsingi. Matokeo ya upofu huo wa hisia za ndani za kiroho, unamfanya Myahudi akongojwe, bila kujitambua, kuelekea kwenye moto wa Jahannamu. *Qur'ani* inathibitisha

kiungo baina ya hayo mawili (fasiri na maoni yangu naambatanisha kwa kusherehesha kwa maandishi yaliyopigiwa mistari chini yake):


وَلَقَدْ ذَرَأْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيرًا مِّنَ ٱلْجِنِّ وَٱلْإِنسِ ۖ لَهُمْ قُلُوبٌ لَّا
يَفْقَهُونَ بِهَا وَلَهُمْ أَعْيُنٌ لَّا يُبْصِرُونَ بِهَا وَلَهُمْ ءَاذَانٌ لَّا يَسْمَعُونَ بِهَآ ۚ
أُو۟لَٰٓئِكَ كَٱلْأَنْعَٰمِ بَلْ هُمْ أَضَلُّ ۚ أُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْغَٰفِلُونَ ﴿١٧٩﴾

"Na tumeiumbia Jahannamu majini wengi na watu. (kwanini?) *Wana nyoyo, lakini hawafahamu kwazo* (kwa kuwa nyoyo zao zimekufa). *Na* (pia) *wana macho, lakini hawaoni kwayo* (kwa kuwa ni vipofu wa ndani). *Na wana masikio, lakini hawasikii kwayo* (kwa kuwa ni viziwi kwa ndani). *Hao ni kama ng'ombe (mnyama wa kufugwa), bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walio ghafilika (na Alama za Mwenyezi Mungu)."*

(Qur'ani, al-Araf, 7:179)

Myahudi atashangaa sana atakapogundua kuwa wale wanaoisoma *Qur'ani* pamoja na *Ahadith* za Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) wanaijua fika siyo tu mipango yake na malengo yake ya siri, bali pia njama zake anazozitumia katika juhudi zake zisizokuwa na simile kutaka kuyatimiza malengo yake. Hali halisi ni kuwa japokuwa hivi sasa hali ya Waislamu ni mbaya, kipindi kijacho ni cha *Uislamu*, na kama msemo maarufu wa Kiingereza unavyosema: *Anayecheka mwishoni, ndiye mwenye kicheko bora zaidi!*' Humo ndimo mnamopatikana tofauti kati ya *muonekano* na *hali halisi*.

Ukweli haukuwapitia pembeni Waislamu kwamba upande pekee uliofaidika na shambulio la kigaidi dhidi ya Amerika la 9/11 ni Taifa la Israeli. Kitabu hiki, kwa hakika, 'hakikurupuki na kurukia kuhitimisha' hivyo, pale inapolitambua shirika la kijasusi la Mossad na makundi mengine ya Kiyahudi (kwa mfano Wayahudi wanaofanya kazi kwenye serikali ya Amerika) kama ni washukiwa wakuu kwenye upangaji na utekelezaji wa tukio hilo. Mwanasiasa wa Kimarekani, Lyndon La Rouche, anadai na kutoa hoja kwamba shambulio kama hilo la 9/11 lingehitaji ujuzi wa habari, mambo na taarifa nyingi kutoka ndani kabisa mwa vyombo na taasisi za serikali ili kuweza kupanga na kutekeleza shambulizi hilo (tazama *tovuti ya La Rouche*). Kitabu hiki kimefikia hitimisho kama hilo kwa kuangalia, pasi na hamaki, faida ambazo Israeli, na *Israeli peke yake*, imezipata kutokana na shambulio hilo. Je, ni faida zipi hizo?

Faida ya Kwanza: Fanikio Kubwa la Mahusiano ya Kijamii

Kwanza, Ariel Sharon alifanya uchokozi uliopimwa kwa ustadi mkubwa kwa kuutembela *Masjid al-Aqsa* Jerusalem mwezi wa Tisa mwaka 2000 ambao uliamsha na kufungua sura mpya ya upinzani wa Waarabu uliofuatiwa na umwagaji damu na ugandamizaji uliofanywa na Israeli. Kipindi chote hadi kufikia muda wa shambulizi la 9/11 mwaka uliofuata, dunia ilishuhudia juhudi za Israeli za kuwasha moto wa vita na huku ikifanya njama za kuonyesha kuwa Israeli ndiye mhujumiwa. Dunia nzima iliugundua ugandamizaji na uonevu wa Israeli ambayo ilipata pigo kubwa la mahusiano ya kijamii pale ambapo dunia yote iliungana kwa pamoja na kuilaani Israeli kwenye Mkutano wa Dunia wa Durban, Afrika ya Kusini uliohusu ubaguzi wa Rangi mnamo mwezi wa Nane/Tisa mwaka 2001.

Shambulio la kigaidi la 9/11 dhidi ya Amerika liliibadilisha hali hiyo kwa ghafla na kishindo kikubwa, kuwa kinyume chake na kuwaletea Waarabu maafa ya mahusiano ya kijamii mabaya Zaidi kuliko yale ambayo yaliikuta Israeli. Runinga, hakika ilipata kukamilika na kufikia umri wa utu uzima kuanzia hapo, ikim. tarehe 11 mwezi wa Tisa, kwani vituo vyote vya matangazo ya TV, vilijiunga kwenye 'Krusedi ya vyombo vya habari' na kutumia kifungu cha maneno *Vita dhidi ya Ugaidi* kama tasifida ya *Vita dhidi ya Uislamu*. Ukweli kwamba Waarabu na Waislamu hawakuhusika kabisa kwenye shambulio hilo dhidi ya Amerika ulikuwa ni kuongezea 'kupaka chumvi kwenye vidonda vyao.'

Faida ya Pili: Kuchonga Njia ya Vita Kubwa ya Kuthibitisha Ukweli wa Uzayonisti wa Kiisraeli

Pili, mabadiliko ya maafa ya mahusiano ya kijamii yaliiweesha Israeli, baada ya kuachiwa kutka 'kwenye ndoano' kuendelea kufuatilia sera zake za uchokozi wa makusudi na kuongeza ugomvi uliosbabisha umwagaji damu dhidi ya Waarabu na Waislamu bila kipingamizi chochote, hata kutoka kwenye serikali ya Amerika. Huu siyo ushindi mdogo.

Mkakati wa Israeli katika vita yake dhidi ya *Uislamu, Qur'ani*, na Mtume Mwarabu ambaye ni wa mwisho (Mtume Muhammad, (*rehma na amani juu yake*) ni kutekeleza onyesho la nguvu litakalothibitisha kile *kitakachoonekana* kuwa kinathibitisha 'ukweli' wa Taurati (na Biblia) na hivyo basi, uongo wa *Qur'ani*. Onyesho hilo siyo tu litawakatisha tamaa Waislamu wajinga wasioifahamu dini yao vizuri, bali pia litawathibitishia Wayahudi kuwa wao bado wanabaki kuwa 'taifa teule.' Wataamini kuwa kurudi upya kwa 'zama za dhahabu' za Judaizmu wakati Masihi atatawala dunia kutoka kwenye kiti cha enzi cha Daud (*rehma na amani juu yake*) kutatokea punde tu. Kitabu hiki, kwa uhakika kinaelezea jambo hilo. Uthibitisho wa namna hiyo wa ukweli wa 'Taurati' utapatikana kupitia shambulio la ghafla na la kubumbuwaza la vita ya Israeli dhidi ya maeneo yote yanayoizunguka Ardhi Takatifu. Hili ndilo lilikuwa lengo la uchokozi wa kimkakati uliofanywa na

Ariel Sharon ukiwa kama kisingizio maarufu. Vita hiyo, ambayo kwa hakika imo kwenye matayarisho hata hivi tunavyoandika kitabu hiki, itaishiakwa kuongeza ukubwa wa ardhi ambayo Israeli itakuwa inamiliki na kuthibitisha madai ya Taurati (na Biblia) kuwa mipaka ya Ardhi Takatifu (hivyo Israeli) *inatoka kuanzia "kwenye mto wa Egypt (mamlaka juu ya Mfereji wa Suez) hadi kwenye mto Yufretis* (*ikim. mamlaka juu ya mafuta ya Ghuba – Saudi, Iraqi, Kuwaiti, n.k., isipokuwa mafuta ya Irani)*. Idadi ya watu ndani ya Israeli ambao wanaamini kuwa uongezaji huo wa eneo la Taifa la Israeli ukiwa kama ni 'matokeo ya wazi yanayotarajiwa yaliyokwishapangwa yasiyokuwa na mushkeli kwenye kutoka kwake' walikuwa 15% mwaka 1960, na wanaonekana kuzidi kuongezeka.

Hivi sasa inakuwa wazi kabisa kuwa lengo la Vita ya Ghuba ya mwaka 1991 ilikuwa ni kuiangusha Iraqi na hii itaiwezesha Israeli kuimeza bila shida yoyote ndani ya miaka kumi ijayo. Lengo, bila ya shaka limefanikiwa. Iraqi iko tayari kuchumwa na kumezwa. Pia inaonekana wazi kuwa lengo la shambulizi dhidi ya Amerika la 9/11 linaloonekana kuwa lilipangwa na Mossad lilikuwa ni kuichokoza Amerika icharukie vita ya shaghalabaghala, dhidi ya mataifa kadhaa ya eneo hilo ambalo lingeiwezesha Israeli kupigana vita yake kubwa yenye lengo la utanuzi wa ardhi yake. Vita hii ya Amerika pia ilipaswa kuwapa Israeli fursa ya kuzitangua silaha za nyuklia za Pakistani ikiwemo uwezo wa silaha za mizinga wa Irani, kuwapo kwa hayo yote kukiwa ni kikwazo muhimu kinachoweza kuizuia Israeli kufanya mashambulizi yake katika vita ya utanuzi wa eneo lake.

Lengo hilo bado halijatimia kwani ndege 'iliyotekwa nyara' ambayo ilipaswa ikaangukie kwenye Ikulu ya Marekani (kugongana na ndege maalum ya Raisi wa Marekani), na kumuua raisi, na Amerika kulazimika kuingia kwenye vita kubwa, badala yake iliangukia Pennsylvania. Mossad na washirika wake, huenda, hawakujiandaa kwa baadhi ya abiria ndani ya ndege hiyo kupigiwa simu kwenye simu zao za mikononi na kupewa taarifa kama zilivyokuwa zikitokea kwenye vyombo vya habari. Kama hii ni kweli, huenda mawasiliano hayo yalileta hitilafu kwenye mfumo wa mawasiliano wa ndege hiyo, (bila kujali kama ilikuwa ikiendeshwa na rubani au ikiendeshwa kutoka mbali) na kuweza kusababisha kuanguka. Vyovyote ilivyokuwa, hakika ni kuwa hakuna dalili kama kilichotokea kwa ndege hii moja ulikuwa mpango uliokusudiwa.

Israeli bado inaweza kufaidika, hata hivyo, kwanza kwa mabadiliko ya utawala wa ngazi ya juu kabisa ambao ulitokea Pakistani (ikim. kabla ya tarehe 11/9), mabadiliko ambayo utawala wa kiraia ulibadilishwa na utawala wa kijeshi. Ni utawalawa kijeshi peke yake (na hakika siyo wa kiraia) ndiyo ungeweza kutoa ridhaa ya kuunga mkono Amerika kwenye vita yake dhidi ya Afghanistani ya Kiislamu. Hivyo basi ilikuwa muhimu kwanza kuuweka madarakani utawala wa kijeshi Pakistani kabla ya shambulio hilo. Jeshi la Pakistani lilijichukulia madaraka kutoka kwa Waziri Mkuu *Nawaaz Sharif* katika mazingira yanayoonekana kuwa ni ya njama, na serikali hiyo haikuwa na jinsi isipokuwa kukubali kuunga mkono madai ya Amerika kuipiga vita serikali ya *Talibani* ya Afghanistani. Kukataa kufanya hivyo kungehatarisha kutolewa kwa siri ya njama iliyowawezesha kushika madaraka. Baada ya serikali ya Pakistani kukubali kuunga mkono Amerika kwenye vita hiyo dhidi ya serikali ya

Talibani, mtego ukawa umekamilika na tayari kunasa. Saddam Hussein alijiingiza kwenye mtego kama huo miaka 10 iliyopita. Jeshi la Pakistani limejikuta limeingia kwenye mtego kama huo, miaka 10 baadaye.

Kitabu hiki kinatarajia kuwa ushirika unaoongozwa na Uingereza/Marekani utapigana vita kali Afghanistani na kwingineko kwa sababu watakazozitaja, miongoni mwa mambo mengine, huku wakiwa na lengo la kuibua vita ya wenyewe kwa wenyewe ndani ya Pakistani. Ikiwa patatokea baadhi ya wanajeshi wa Pakistani kuishia kupinga na kujiunga na wananchi wanaopiga msimamo wa sera za serikali wa kuunga mkono vita ya Amerika dhidi ya Waislamu wa *Talibani* wa Afhanistani, na vita ya wenyewe kwa wenyewe ikaibuka Pakistani, hiyo itakuwa ni ishara na kisingizio kwa Amerika kuongoza washirika wake kuishambulia Pakistani na kuvunja viwanda vyake vinavyohusiana na utengenezaji wa silaha za nyuklia. Ikiwa hili halitofanikiwa, bado wanazo njia kadhaa mbadala za kuwafikisha hapo ili kutimiza lengo hili. Amerika na washirika wake wanaweza kabisa kuendelea mbele na kuibadilisha Pakistani ikawa kama Uturuki au Iraqi, au kusimamia kuvunjika (zaidi) na kuitenganisha Pakistani. Israeli na India huenda wai au wakashiriki moja kwa moja kwenye shambulio la Pakistani, lakini Israeli hakika watashiriki kwenye upangaji wa mkakati huo.

Kama akili ya kuzaliwa ingeambatana na muono wa jicho la ndani la hisia za kiroho hata kwa uchache (kitu ambacho kinakosekana kwa kiasi kikubwa mno kwenye utamaduni wa kimagharibi ambao hivi sasa unatawala dunia) ingemuwezesha kila mtu kugundua kuwa shirika la kijasusi la Mossad la Israeli na washirika wake ndiyo washukiwa wakuu kwenye upangaji na utekelezaji wa shambulio hilo la kigaidi na la kishetani dhidi ya Amerika lililofanywa kwa ustadi mkubwa. Ikiwa *Usama bin Ladin* na kikundi chake kidogo cha wapiganaji cha *al-Qaidah* wangeweza kupanga na kutekeleza shambulio hilo, basi pia ni lazima iwezekane kwa *ng'ombe kuuruka mwezi na kutua upande wa pili!*

Waislamu wanapaswa pia kujali onyo linalotolewa kwenye *Qur'ani la kutokukubali taarifa tunazokutana nazo hususan zinazotoka kwenye vyanzo vilivyo wazi vya wale wasiomtambua Mungu bila ya kuchunguza ukweli wake na kusababisha uharibifu ambao baadaye tutakuja kuujutia*:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن جَاءَكُمْ فَاسِقٌ بِنَبَإٍ فَتَبَيَّنُوا أَن تُصِيبُوا قَوْمًا بِجَهَالَةٍ فَتُصْبِحُوا عَلَىٰ مَا فَعَلْتُمْ نَادِمِين

"Enyi mlio amini! Akikujieni mpotovu na khabari yoyote, ichunguzeni, msije mkawasibu watu kwa kuto jua, na mkawa tena wenye kujuta kwa mliyo yatenda."

(Qur'ani, al-Hujurat, 49:6)

Utamaduni wa kimagharibi na wale wote wanaojikomba kwa kutaka kufanana nao duniani kote ambao wanamshutumu *Usama bin Ladin* kwa kuhusika na shambulizi la kigaidi dhidi ya Amerika la 9/11, na ambao hawatoi Ushahidi wowote ulio wazi kwa jamii wa tuhuma hizo (ikim. Ushahidi ambao ungeweza kutumika kwenye mahakama ya kisheria kutoa hukumu ya kosa hilo), hawawezi kujitoa kwenye tuhuma za kuwa na dhambi za ukosefu wa ushahidi wa tuhuma hizo. Kwa upande wa pili, Usama bin Ladin, ambaye anamuabudu Mungu wa Abrahamu (*rehma na amani juu yake*) amekataa kabisa kuhusika na shambulizi hilo. Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) amemtaja Muislamu kuwa ni *"yule ambaye kutoka kwenye ulimi na mkono wake Waislamu wengine wako salama"* Ni jukumu la Waislamu wote kuukubali ukweli wa *Usama bin Ladin* kukataa kuhusika na shambulio hadi na pale ambapo patapatikana Ushahidi utakaothibitisha kuwa hasemi ukweli.

Faida ya tatu: Kutengeneza Njia ya Israeli kuwa Taifa Tawala la dunia

Baada ya kufanya uchambuzi wa kina wa *Qur'ani* na *Ahadith* za Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*) tulioufanya kwenye kitabu hiki, *Jerusalem katika Qur'ani*, inakuwa wazi kabisa kuwa lengo kuu la Israeli ambalo ndilo lilikuwa lengo kuu la shambulizi la kigaidi la 9/11 dhidi ya Amerika, lilikuwa ni kuchonga njia ya kuiwezesha Israeli kuchukua nafasi ya Amerika kama '*Taifa Tawala'* duniani. Masihi 'wa kweli' anatarajiwa kutawala dunia kutoka kwenye kiti cha enzi cha Daud (ikim. Israeli na Jerusalem). Ili Masihi 'wa uongo' (*ikim. Dajjal*) aweze kuwafanya Wayahudi wamuamini ukweli na uhalali wake (kama Masihi) atalazimika:

- Kuikomboa Ardhi Takatifu kutoka kwenye utawala wa wasiokuwa Wayahudi,
- Kuwarudisha Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu na kuichukua upya kuwa mali yao kwa niaba ya Judaizmu,
- Kuliunda Taifa la Israeli na kuwaaminisha Wayahudi kuwa ni Israeli kama ile ya Daud (*rehma na amani juu yake*) na Suleyman (*rehma na amani juu yake*),
- Kusababisha Israeli iwe *Taifa Tawala* duniani,
- Ajitokeze mwenyewe binafsi ili aweze kutawala dunia kutoka Jerusalem.

Kitabu hiki kina lengo la kuelekeza na kutilia mkazo kwa msomaji kwenye ukweli kwamba pointi nambari (i hadi iii) zilizotajwa hapo juu tayari zimekwishakamilika, wakati pointi nambari (iv) iko karibu kukamilika na nambari (v) itachukua muda mrefu zaidi.

Dunia hivi sasa imefikia mahali ambapo ilikuwa imefikia wakati wa kipindi cha kiangazi cha mwaka 1914 wakati tukio jingine la kigaidi lililokuwa limepangwa kwa ustadi mkubwa (mauaji ya Mwana wa Mfalme Frank Ferdinand wa Austria-Hungary) lililopelekea kuanza kwa vita ambayo iliiangusha Uingereza iliyokuwa '*Taifa Tawala'* duniani la kipindi hicho. Vita hiyo pia iliwahakikishia Wayahudi *Tamko la Balfour*, ambalo kwalo, kurejea kwa Wayahudi kwenye Ardhi Takatifu na kuanzishwa upya kwa Taifa la Israeli. Utamaduni wa kimagharibi usiomtambua Mungu

ulikuwa na upofu mkubwa mno wa kiroho kiasi kwamba haukuweza kugundua kuwa unavutwa kwa kamba za pua kuelekezwa kwenye vita ambamo Wazungu wengi kwa mamilioni waliuawa. Utamaduni huo, ambao haukuweza kuwatambua wale ambao walihusika na tukio hilo la mauaji ya kigaidi la mwaka 1914, pia hivyo hivyo leo hii hawana uwezo wa kuwatambua watu wale wale ambao wamekuwa wakipanga na kutekeleza shambulio la mwezi wa Tisa, tarehe 11.

Ni wazi kabisa kuwa Amerika, *Taifa Tawala*, haliwezi kuangushwa kwa njia nyingine Zaidi kwa kupitia kuanguka kwa uchumi wake na pia kuanguka kwa thamani ya sarafu ya dola. Hayo ndiyo hasa yangekuwa matokeo laity kama Raisi Bush angeuawa. Tishio kwa Amerika, ambalo bado lipo hata wakati tunaandika kitabu hiki, baada ya dunia nzima kujikusanya kuupiga vita *Uislamu, Qur'ani*, na Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*), n ahata baada ya vita ya Amerika dhidi ya Usama bin Ladin na wapiganaji wake, inaonyesha kuwa juhudi za Wayahudi kuuangusha uchumi na sarafu ya dola ya Kimarekani bado zinaendelea.

Henry Ford, mwanamapinduzi maarufu wa Kimarekani katika sekta ya uzalishaji wa viwanda, ambaye alikuwa mtu wa kwanza kuanzisha uzalishaji wa wingi wa magari kwa kutumia machine, aliionya Amerika kuhusu hatari hii mnamo miaka ya 1919-1920. Baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, aligundua fujo zinazosababishwa na matajiri wa kimataifa wa Kiyahudi. Aliteua kamati ya wachunguzi wenye ujuzi na uzoefu wa kina wafanye uchunguzi wa Wayahudi wa kimataifa na walichapisha matokeo yao mwaka 1919-1920 kwenye 'Dearborn Independent' likiwa kama chombo maalum cha Kampuni ya Magari ya Ford. Baadaye kilichapishwa kama kitabu kwa jina la '*Myahudi wa Kimataifa.*'Kitabu kizima (chenye sehemu nne kwa pamoja) kimechapishwa upya nchini Malaysia muda si mrefu uliopita na 'Kampuni ya Uchapishaji ya Others' na kinapatikana kwa urahisi kwenye maduka ya vitabu.

Uchumi wa Amerika bado haujaanguka lakini maandishi yanaonekana ukutani kuwa uko chini ya mashambulizi ya maadui ambao wamo ndani ya mfumo wan chi yenyewe.

Ikiwa, na pale uchumi huo utakapoanguka, na ikiwa na pale ambapo Israeli pia itakapofanikiwa kujenga udhibiti wake wa kimataifa wa kijeshi na kusimamia eneo lote na kuweza kuongeza eneo lake huku ikipuuzia shutuma za mataifa yote duniani, Israeli itachukua nafasi ya Amerika kama '*Taifa Tawala'* duniani. Hilo litakapotokea, dunia itashangazwa sana, lakini wafuasi wa kweli wa Mtume Mwarabu (*rehma na amani juu yake*) hawatoshangazwa kabisa.

Ni Uislamu ndiyo unaouelezea mwisho na hatma inayoisubiri Jerusalem, mwisho ambao hatimaye utaushuhudia Uislamu ukiibuka tena kama '*Taifa Tawala*' duniani. Kipindi hicho cha ushindi wa Uislamu utakuja baada ya jeshi la Kiislamu kutokea Khorasan, na katika mlolongo wa kuikomboa Ardhi Takatifu, Taifa la Israeli litavunjwa na Ardhi hiyo kukombolewa:

"Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume (*rehma na amani juu yake*) alisema: Bendera nyeusi zitaibuka kutokea Khorasan (ikim. eneo ambalo sasa hivi linajumuisha Afghanistani, Pakistani Kaskazini Magharibi, Kaskazini Mashariki ya Irani, Asia ya Kati, na Asia Kaskazini ya Afghanistani, n.k) na hakuna nguvu / jeshi litakaloweza kuwazuia hadi waingie Aelia (Jerusalem)."

(Sunan Tirmidhi)

Hakika Mtume (*rehma na amani juu yake*) aliendelea na kuwataka Waislamu kujiunga na jeshi hilo "*hata kama watalazimika kutambaa kwenye barafu"* (ikim. hata kama itawabidi wavunje amri za serikali za kisasa zisizomjua Mungu ambazo leo hii zinatawala dunia na ambazo zitakuwa zikipinga na kulenga kuwazuia wakazi wao Waislamu wasiweze kufuata amri ya Mtume (*rehma na amani juu yake*).

Hadith hii ya Mtume (*rehma na amani juu yake*) inaweka wazi kabisa kuwa Jerusalem itakombolewa kupitia *jitihada za kijeshi la Kiislamu*.

Majibu ya Kiislamu kuhusu Vita dhidi ya Uislamu

Jibu la mwisho la *Kiislamu* kuhusiana na 'shambulizi la Amerika' shambulizi ambalo limetumiwa kinyemela kujaribu kuuvuruga Uislamu pamoja na Waislamu wakati wanajificha nyuma ya pazia la 'ugaidi' ni kujizatiti upya na kuweza kubaki wenye imani na kuendelea kubaki waaminifu kwa Allah Mtukufu na Mjumbe wake *bila ya kujali tafrani zitakazowakuta kwa kufanya hivyo!* Watafanya hivyo ikiwa wataazimia kuelekeza maisha yao kwenye kujitayarisha *kushiriki kwenye mapigano* ili kuimboa Ardhi Takatifu kupitia *(Jihad)* na Uislamu kuibuka tena kama dini mshindi duniani. Hakuna mahitaji ya kuitangaza rasmi *Jihad* hiyo kwani tayari imekwishaanza. Pia, hakuna nguvu wala jeshi duniani litakaloweza kuisimamisha hiyo *Jihad* hadi itakapoikomboa Ardhi Takatifu. Alama ya usaliti ambayo Waislamu wataweza kuitumia kupima na kuzigundua serikali za nchi zisizomtambua Mungu zinazotawala dunia hivi sasa ni kuwa hazitokuwa tayari kuwaruhusu Waislamu wajiunge kwenye jitihada za kuikomboa Ardhi Takatifu.

Haya ni machache ambayo *Qur'ani* imeyasema kuhusu jitihada hizo za kivita:

Ilikuwa ni tarehe mbili ya mwezi wa *Shaaban* kwenye mji wa Madina wakati Allah *Subhanahu wa T'alah* aliposhusha wahyi na aya kuhusu *Qital* (kupigana). Waziri Mkuu wa Uingereza, Raisi wa marekani na Waziri Mkuu wa Israeli wanaweza kujisikia vibaya wakijaribu kuzielewa aya hizi za *Qur'ani*. Lakini ukichukulia maanani mwenendo wa Uingereza /Amerika / Israeli kuhusiana na mashambulio yao kuelekea kwa Waislamu, tunalazimika kuelekeza macho ya Waislamu wote kwenye yale ambayo Allah Mtukufu ameyasema kuhusu kupigana.

Kwanza, Amelifanya hilo kuwa ni *Fardh*. Hivyo basi ni *Shirk* kwa serikali, au Umoja wa Mataifa, kuyakataza yale ambayo Allah ameamrisha. Pia ni *Shirk* kwa yeyote kukubali kuwa hairuhusiwi kufanya au kutenda kile ambacho Allah ameamrisha kifanyike kwa mujibu wa aya ifuatayo (na maelezo / ufafanuzi wangu wa nyongeza uko kwa maandishi madogo zaidi na nimepigia mstari chini yake):

كُتِبَ عَلَيْكُمُ ٱلْقِتَالُ وَهُوَ كُرْهٌ لَّكُمْ ۖ وَعَسَىٰٓ أَن تَكْرَهُوا۟ شَيْـًٔا
وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۖ وَعَسَىٰٓ أَن تُحِبُّوا۟ شَيْـًٔا وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ ۗ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ
وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٢١٦﴾

"Mmeandikiwa kupigana vita (kuwa ni fardh), japo inachukiza kwenu. Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu (kutopenda kupigana) nacho (kikawa) ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu (na wala siyo Wayahudi na Wakristo wa Ulaya wasiomtambua Mungu ambao sasa hivi wanadhibiti mamlaka ya dunia) *anajua na nyinyi hamjui."*

(Qur'ani, al-Baqarah, 2:216)

Mwongozo wa *Qur'ani* uko wazi kabisa kuwa Allah, na wala siyo Wayahudi na Wakristo wa Ulaya wasiomtambua Mungu ambao sasa hivi wanadhibiti mamlaka ya dunia, ndiye Anayejua kipi ni kheri kwa Waislamu na kipi ni shari kwa Waislamu.

Pili, *Qur'ani* inawaamrisha Waislamu kupigana katika kujilinda wao wenyewe pale wanaposhambuliwa (na maelezo / ufafanuzi wangu wa nyongeza uko kwa maandishi madogo zaidi na nimepigia mstari chini yake):

"Piganeni kwa ajili ya Allah na wale wanaokupigeni vita nyinyi (na Wayahudi na Wakristo wa Ulaya wasiomtambua Mungu ambao sasa hivi wanadhibiti mamlaka ya dunia ndicho hasa wanachokifanya*) lakini msivuke mipaka kwani Allah hawapendi wale wanaovuka mipaka."*

Qur'ani pia inaweka wazi kabisa kuwa Waislamu lazima wachukue hatua kwa wale ambao 'bila sababu ya haki' wanawatoa majumbani mwao na kuwanyang'anya ardhi walimokuwa wakiishi. Wanafukuzwa basi tu kwa kuwa ni Waislamu. *Qur'ani* inawataka hapo Waislamu kuingia kwenye vita kupigania kujikomboa kutokana na uonevu huo. Na hii ndiyo hasa hali halisi ilivyo kwenye Ardhi

Takatifu. Lakini wale ambao leo hii wanawatawala Waislamu wamekuwa vipofu kiasi hata hawawezi kuugundua uhalalishaji wa *Qur'ani* kuhusu kupigana kwa lengo la kuikomboa Ardhi takatifu. Badala yake wanajiunga na Serikali ya Marekani inayoongozwa na chama cha Republican kwenye vita yake dhidi ya ugaidi nah apo kujikuta, kwa kujua au kutokujua, wanawashutumu na kuwalaani wale ambao wanapigana kwa mujibu wa amri zilizomo kwenye *Qur'ani* kuwa ni magaidi. Huu ni uhalali unaopatikana kwenye *Qur'ani* kuhusu kupigania haki hiyo:


أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقَٰتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظُلِمُوا۟ ۚ وَإِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ
لَقَدِيرٌ ﴿٣٩﴾
ٱلَّذِينَ أُخْرِجُوا۟ مِن دِيَٰرِهِم بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّآ أَن يَقُولُوا۟ رَبُّنَا ٱللَّهُ ۗ
وَلَوْلَا دَفْعُ ٱللَّهِ ٱلنَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَّهُدِّمَتْ صَوَٰمِعُ وَبِيَعٌ
وَصَلَوَٰتٌ وَمَسَٰجِدُ يُذْكَرُ فِيهَا ٱسْمُ ٱللَّهِ كَثِيرًا ۗ
وَلَيَنصُرَنَّ ٱللَّهُ مَن يَنصُرُهُۥٓ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَقَوِىٌّ عَزِيزٌ ﴿٤٠﴾

"Wameruhusiwa kupigana (ruksa ya Mwenyezi Mungu) wale wanao pigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa – na (watakapopigana) kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Muweza wa kuwasaidia; (hawa ni) wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki, ila kwa kuwa wanasema: Mola wetu Mlezi ni Mwenyezi Mungu! Na lau kuwa (isingekuwa kwa amri hii ya Mungu kutoa ruksa kupigana vita ambapo) Mwenyezi Mungu huliangalia kundi moja la watu kupitia kwa kundi jingine la watu, basi hapana shaka zingeli vunjwa nymba za wat'awa, na makanisa, na masinagogi, na misikiti, ambamo ndani yake jina la Mwenyezi Mungu linatajwa kwa wingi. Na bila ya shaka Mwenyezi Mungu humsaidia yule anaye msaidia Yeye (kutekeleza Yake). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu Mtukufu."

(Qur'ani, al-Hajj, 22:39-40)

Tatu, kupigana kunapelekea amani kupatika na kusimama kitu kinacholeta na kujenga dunia yenye haki na huru kutokana na ugandamizaji, na hilo linawezekana pale tu ambapo Din ya Mwenyezi Mungu inapokuwa imehimili duniani:

وَقَٰتِلُوهُمْ حَتَّىٰ لَا تَكُونَ فِتْنَةٌ وَيَكُونَ ٱلدِّينُ لِلَّهِ ۖ فَإِنِ ٱنتَهَوْا۟ فَلَا عُدْوَٰنَ إِلَّا
عَلَى ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿١٩٣﴾

"Na piganeni nao mpaka pasiwepo fitina, na Dini iwe ya Mwenyezi Mungu tu. Na kama wakiacha (kupigana) basi usiweko uadui ila kwa (wale) wenye kudhulumu."

(Qur'ani, al-Baqarah, 2:193)

Nne, Allah amefanya kuwa ni *Wajib* kwa Waislamu kupigana kuokoa wale ambao wanadhulumiwa ambao wao wenyewe wanaomba msaada na kukombolewa kutokana na ugandamizaji na uonevu:

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَٰتِلُونَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱلْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ ٱلرِّجَالِ وَٱلنِّسَآءِ
وَٱلْوِلْدَٰنِ ٱلَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَآ أَخْرِجْنَا مِنْ هَٰذِهِ ٱلْقَرْيَةِ ٱلظَّالِمِ أَهْلُهَا
وَٱجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ وَلِيًّا وَٱجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ نَصِيرًا ﴿٧٥﴾

"Na kwa nini msipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanao onewa, wanaume na wanawake na watoto, ambao husema: Mola Mlezi wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhaalimu, na tujaalie tuwe na mlinzi anaye toka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anaye toka kwako."

(Qur'ani, al-Nisa, 4:75)

Mwenyezi Mungu ameendelea na kuutaja ukaidi wa Wayahudi kukataa kupigana. Kisha anaonya kuhusu ukaidi huo wa kukataa amri ya kupigana:


أَلَمْ تَرَ إِلَى ٱلَّذِينَ قِيلَ لَهُمْ كُفُّوٓا۟ أَيْدِيَكُمْ وَأَقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُوا۟ ٱلزَّكَوٰةَ فَلَمَّا
كُتِبَ عَلَيْهِمُ ٱلْقِتَالُ إِذَا فَرِيقٌ مِّنْهُمْ يَخْشَوْنَ ٱلنَّاسَ كَخَشْيَةِ ٱللَّهِ أَوْ أَشَدَّ
خَشْيَةً ۚ وَقَالُوا۟ رَبَّنَا لِمَ كَتَبْتَ عَلَيْنَا ٱلْقِتَالَ لَوْلَآ أَخَّرْتَنَآ إِلَىٰٓ أَجَلٍ قَرِيبٍ ۗ
قُلْ مَتَٰعُ ٱلدُّنْيَا قَلِيلٌ وَٱلْءَاخِرَةُ خَيْرٌ لِّمَنِ ٱتَّقَىٰ وَلَا تُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٧٧﴾

“Je, huwaoni wale walio ambiwa: Izuieni mikono yenu (kupigana), na mshike Sala na mtoe Zaka? Na (baada ya muda mrefu) walipo amrishwa kupigana, mara kundi moja kati yao liliwaogopa watu kama kumwogopa Mwenyezi Mungu, au kwa khofu kubwa zaidi. Na wakasema: Mola Mlezi wetu! Kwa nini umetuamrisha kupigana? Laiti unge tuakhirishia kiasi ya muda kidogo hivi! Sema: Starehe ya dunia ni ndogo, na Akhera ni bora zaidi kwa mwenye kumcha Mungu. Wala hamtadhulumiwa hata uzi wa kokwa ya tende.”

(Qur’ani, al-Nisa, 4:77)

Muislamu haruhusiwi kupigana chini ya mamlaka na uongozi wa kamanda asiyekuwa Muislamu na vinginevyo isipokuwa chini ya amri za Mwenyezi Mungu kuhusiana na kupigana. Wale ambao wanapigana chini ya amri na kamanda nyingine yoyote, wanapigana chini ya amri mbaya isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu:


ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ يُقَٰتِلُونَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ ۖ وَٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ يُقَٰتِلُونَ فِى سَبِيلِ
ٱلطَّٰغُوتِ فَقَٰتِلُوٓا۟ أَوْلِيَآءَ ٱلشَّيْطَٰنِ ۖ إِنَّ كَيْدَ ٱلشَّيْطَٰنِ كَانَ ضَعِيفًا ﴿٧٦﴾

“Walio amini wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na walio kufuru wanapiana katika njia ya upotofu. Basi piganeni na marafiki wa Shet'ani. Hakika hila za Shet'ani ni dhaifu.”

(Qur’ani, al-Nisa, 4:76)

Na Mwislamu asiogope asilani na kujitoa kwenye kupigana kwa khofu au kukhofia chochote:

أَيْنَمَا تَكُونُوا۟ يُدْرِككُّمُ ٱلْمَوْتُ وَلَوْ كُنتُمْ فِى بُرُوجٍ مُّشَيَّدَةٍ ۗ وَإِن تُصِبْهُمْ
حَسَنَةٌ يَقُولُوا۟ هَٰذِهِۦ مِنْ عِندِ ٱللَّهِ ۖ وَإِن تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ يَقُولُوا۟ هَٰذِهِۦ مِنْ
عِندِكَ ۚ قُلْ كُلٌّ مِّنْ عِندِ ٱللَّهِ ۖ فَمَالِ هَٰٓؤُلَآءِ ٱلْقَوْمِ لَا يَكَادُونَ يَفْقَهُونَ
حَدِيثًا ﴿٧٨﴾

"Popote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome zilizo na nguvu zilizo juu! Na likiwafikilia jema wanasema: Hili limetoka kwa Mwenyezi Mungu. Na likiwafikilia ovu wanasema: Hili limetoka kwako wewe (Mtume). Sema: Yote yanatokana na Mwenyezi Mungu. Basi wana nini watu hawa hata hawakaribii kufahamu maneno?"

(Qur'ani, an-Nisa, 4:78)

Makafiri watapigana na waumini kwa hasira kali na udhalimu mkubwa. Nafuu itatoka kwa Allah ikiwa waumini watajiinua wenyewe na kuchukua hatua za kupambana na makafiri:

فَقَٰتِلْ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ لَا تُكَلَّفُ إِلَّا نَفْسَكَ ۚ وَحَرِّضِ ٱلْمُؤْمِنِينَ ۖ عَسَى ٱللَّهُ
أَن يَكُفَّ بَأْسَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ ۚ وَٱللَّهُ أَشَدُّ بَأْسًا وَأَشَدُّ
تَنكِيلًا ﴿٨٤﴾

"Basi pigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu. Hukalifishwi ila nafsi yako tu. Na wahimize Waumini. Huenda Mwenyezi Mungu akayazuia mashambulio ya walio kufuru. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mkali zaidi wa kushambulia na Mkali zaidi wa kuadhibu."

(Qur'ani, an-Nisa, 4:84)

Waislamu walio bora zaidi ni wale ambao wanachukua hatua za kufuata amri za Allah kupigana kwa Njia Zake mara moja kila panapotokea mahitaji ya kufanya hivyo. Hawa ni bora zaidi kuliko wale 'wanaokaa nyumbani':

لَّا يَسْتَوِي ٱلْقَٰعِدُونَ مِنَ ٱلْمُؤْمِنِينَ غَيْرُ أُو۟لِى ٱلضَّرَرِ وَٱلْمُجَٰهِدُونَ فِى سَبِيلِ
ٱللَّهِ بِأَمْوَٰلِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ ۚ فَضَّلَ ٱللَّهُ ٱلْمُجَٰهِدِينَ بِأَمْوَٰلِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ عَلَى
ٱلْقَٰعِدِينَ دَرَجَةً ۚ وَكُلًّا وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلْحُسْنَىٰ ۚ وَفَضَّلَ ٱللَّهُ ٱلْمُجَٰهِدِينَ عَلَى
ٱلْقَٰعِدِينَ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٩٥﴾

"Hawawi sawa Waumini wanao kaa (nyumbani) tu wala hawanadharura, na wale wanao pigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Mwenyezi Mungu amewatukuza cheo (cha juu zaidi) wale wanao pigana kwa mali yao na nafsi zao kuliko wale wanao kaa tu (nyumbani). Ingawa Mwenyezi Mungu amewaahidi wote mashukio mema, lakini Mwenyezi Mungu amewafadhili wanao pigana kwa ujira (maalum) mkubwa kuliko wanao kaa tu."

(Qur'ani, an-Nisa, 4:95)

Watajitokeza wachache ambao watatoa sababu zao zilizowafanya washindwe kushiriki kwenye kupigana kwa kusema hawakuwa na uwezo. Kwa mfano wanaweza kusema kuwa waliishi chini ya utawala wa serikali mabazo hazikuwaruhusu kupigana kwa Njia ya Allah. Lakini hoja hizo hazitowaokoa Waislamu hao kuingizwa kwenye moto wa Jahannamu kwani wataulizwa:

'*Je, ardhi ya Allah haikuwa pana vya kutosha kuweza kuhamia sehemu nyingine ambapo wangepata uhuru mkubwa zaidi?*'

إِنَّ ٱلَّذِينَ تَوَفَّىٰهُمُ ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ ظَالِمِىٓ أَنفُسِهِمْ قَالُوا۟ فِيمَ كُنتُمْ ۖ قَالُوا۟ كُنَّا
مُسْتَضْعَفِينَ فِى ٱلْأَرْضِ ۚ قَالُوٓا۟ أَلَمْ تَكُنْ أَرْضُ ٱللَّهِ وَٰسِعَةً فَتُهَاجِرُوا۟ فِيهَا ۚ
فَأُو۟لَٰٓئِكَ مَأْوَىٰهُمْ جَهَنَّمُ ۖ وَسَآءَتْ مَصِيرًا ﴿٩٧﴾

إِلَّا ٱلْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ ٱلرِّجَالِ وَٱلنِّسَآءِ وَٱلْوِلْدَٰنِ لَا يَسْتَطِيعُونَ حِيلَةً
وَلَا يَهْتَدُونَ سَبِيلًا ﴿٩٨﴾

فَأُولَٰئِكَ عَسَى اللَّهُ أَن يَعْفُوَ عَنْهُمْ ۚ وَكَانَ اللَّهُ عَفُوًّا غَفُورًا ﴿٩٩﴾

۞ وَمَن يُهَاجِرْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يَجِدْ فِي الْأَرْضِ مُرَاغَمًا كَثِيرًا وَسَعَةً ۚ وَمَن يَخْرُجْ مِن بَيْتِهِ مُهَاجِرًا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ يُدْرِكْهُ الْمَوْتُ فَقَدْ وَقَعَ أَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿١٠٠﴾

"Hakika Malaika (wakati wanatoa roho za wale waliotenda dhambi) watawaambia wale ambao waliojidhulumu nafsi zao: Mlikuwa vipi? Watasema: Tulikuwa dhaifu na tunaonewa. Watawaambia: Kwani ardhi ya Mwenyezi Mungu haikuwa na wasaa wa (pana vya kutosha kuweza) kuhamia humo? Basi hao makaazi yao ni Jahannamu, nayo ni marejeo mabaya kabisa!

Isipo kuwa wale walio kuwa wanyonge miongoni mwa wanaume na wanawake na watoto wasio na uweza wa hila ya kuongoza njia ya kuhama.

Basi hao huenda Mwenyezi Mungu akawasamehe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa maghfira.

Na mwenye kuhama (toka nyumbani kwake) katika Njia ya Mwenyezi Mungu atapata pengi duniani pa kukimbilia, na atapata wasaa. Na anaye toka nyumbani kwake kuhama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake, kisha yakamfika mauti njiani basi umethibiti ujira wake kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye maghfira na Mwenye kurehemu."

(Qur'ani, an-Nisa, 4:97-100)

Kiambatanishi cha Tatu

IBN KHALDUN – IQBAL – NA JERUSALEM KATIKA QUR'ANI

Kitabu hiki pia kimejaribu kuwakaribisha wale ambao wamekubaliana na maandishi ya Dr. Muhammad Iqbal (*Ujengaji Upya wa Fikra za Kidini katika Uislamu – Reconstruction of Religious Thought in Islam*) nay ale ya Ibn Khaldun (*Muqaddamah*) ambao wote walikataa imani ya ujio wa *Imam al-Mahdi*. Katika kukataa imani hiyo wanazuoni hawa waliobobea wa Kiislamu wamefanya

kosa kubwa sana kama mlima. Kwa Dr. Iqbal, inaonyesha hilo limemfanya pia asiamini kurejea kwa Khilafa, kwa *Dajjal*, Mtume wa Uongo na pia kurejea kwa Masihi, Yesu, mwana wa maryamu. Hata hivyo, alipendezwa na msimamo wa kidunia wa Kituruki wa *ijtihad* kuwa mfumo wa kisasa wa bunge ulikuwa ni suluhisho halali linalokubalika badala ya Khilafa. Haya ndiyo yale ambayo Iqbal aliyasema kuhusu *Imam al-Mahdi*:

"(Kanuni ya kufikia mwisho wa utume) inaweza ikaangaliwa kama ni uponyaji wa kisaikolojia kwa mtazamo wa Kimajian (wazee werevu watatu) wa kubaki daima kwenye mtarajio kitu ambacho kinaelemea kujenga mtazamo usiokuwa sahihi wa kihistoria. Ibn Khaldun, baada ya kuona kiini cha mtazamo wake, amekikosoa kwa nguvu zote na, ninaamini, mwishowe amefikia kuivunja ile imani inayodhaniwa kuwa na misingi ya upokezi wa kiroho kwenye Uislamu wa wazo sawa na hilo, kwenye misingi yake ya kisaikolojia, na wazo la awali la Kimajian ambalo lilijitokeza upya kwenye Uislamu kwa kusababishwa na msukuko wa fikra za Kimajian)."

(Iqbal, Dr. Muhammad: (*Ujengaji Upya wa Fikra za Kidini katika Uislamu – Reconstruction of Religious Thought in Islam*), ed. by M. Saeed Sheikh, Lahore: Institute of Islamic Culture, 1986, ukurasa wa 115.

Tazama pia barua ya Iqbal aliyomtumia Muhammad Ihsan ambamo anakataa imani juu ya kile anachokiita *masihiyat*. *Iqbalnama*, Toleo la II, ukurasa 231, kutoka M. Saeed Sheikh, *"Utangulizi wa Mhariri"* kwenye kitabu cha Iqbal kama hapo juu.

Ibn Khaldun na Iqbal wote ni wanazuoni mahiri kabisa kiasi kwamba ninajikuta nalazimika kutafakari tena na tena kabla ya kutoa maoni yangu ambayo yanakosoa maoni yao. Lakini kama wangeelewa vyema muundo wa mlolongo wa kihistoria unaohusiana na ujio wa Masihi, hilo lingewaokoa kwenye kufanya makossa ambayo kwa bahati mbaya wameyafanya. Je, upi ni muundo wa mlolongo wa kihistoria? Ni ule ambao linapatikana swali la utambuzi wa uhakika wa Masihi (pale atakapojitokeza) linapopatiwa jibu na Allah kwa kujaalia kuwapo kwa mtu maalum, atakayekuwa na jukumu la kumtambua Masihi kwa uhakika wote. John Mbatizaji (*rehma na amani juu yake*) hakuwa tu akirudiarudia kuwaambia watu kuwa Yesu (*rehma na amani juu yake*) anakuja, ila, ziada ilikuwa ni mbele ya John Mbatizaji (*rehma na amani juu yake*) ndipo Yesu (*rehma na amani juu yake*) alijitokeza aliporudi kwenye Ardhi Takatifu akiwa kama mtu mzima. John ndipo alipotamka kwa kaumu: "Huyu ndiye mtu mliyekuwa mkimsubiri, huyu ndiye Masihi!" Huu ndiyo mpangilio wa Mungu wa 'utambuzi wa uhakika' wa Masihi!

Hivyo hivyo, wakati Masihi atakaporejea, Allah atajaalia mtu mwingine ambaye jukumu lake litakuwa kama lile la John Mbatizaji. Mlolongo wa kihistoria hapo unabaki kuwa na msimamo thabiti. Jukumu la Imam al Mahdi ni kama lile la John Mbatizaji.

Wakati Imam atakapoibuka na kutangaza wazi kuwa yeye ni *Mahdi*, hii itakuwa ni Alama kuwa kurejea kwa Masihi kumekaribia sana. Na wakati Yesu (*rehma na amani juu yake*) atakaporejea, atateremka mbele ya Imam ambaye atatamka maneno: "Huyu ndiye mwana wa Maryam!" (*Tazama Sahih Muslim*). Hivyo basi utambuzi wa uhakika utakuwa umekamilika kwa

nyakati zote mbili (atakapojitokeza duniani) na utakuwa umefanyika kwa mfumo ule ule, kwa hekima na busara za Allah, na kufanywa na mtu aliyejaaliwa na Mwenyezi Mungu kuja kufanya jambo hilo maalum. Uelewa mzuri wa jukumu muhimu la John Mbatizaji (*rehma na amani juu yake*) kuhusiana na Yesu Masihi (*rehma na amani juu yake*) kungemuokoa Ibn Khaldun kutokana na kutenda kosa kubwa na la hatari la kuzikataa *Ahadith* zote zinazohusiana na *Imam al Mahdi* na lingemuokoa Iqbal kutokana na kurudia na kujazia kwenye kosa hilo la awali la Ibn Khaldun.

Ni vyema pia tukaweka wazi kuwa imani kuhusiana na *Imam al Mahdi* ambaye kuibuka kwake kutatokea katika wakati ule ule wa kurejea kwa Masihi, mwana wa Maryamu, inaonyesha kuwa sawa na imani za kiyahudi kuwa watatokea watu wawili kwenye Zama za Mwisho, wa kwanza anatajwa kama Masihi 'wa kifalme' na wa pili kama Masihi 'wa kikasisi.' Haim Zafrani ametoa tamko muhimu kuhusiana na Nyaraka za kukunja za Dead Sea:

"Kutoka kwenye baadhi ya ibara kwenye maandishi ya Qumran, inaonyesha wazi na kwa uhakika kuwa jumuiya hii, ambayo ilikuwa kimsingi ni ya kikasisi, ilimtarajia kasisi mkuu maalum wa upako ('Masihi wa Aaron') na pia mtawala maalum wa upako ('Masihi wa Israeli). Inapaswa ijulikane kuwa Hati ya Kairo Damaskas – Cairo Damascus Document (CD 7:20) Masihi wa kifalme haitwi 'mfalme' isipokuwa 'mtoto wa mfalme' (nasi, kufuatana na Ezek. 34:24; 37:25; n.k.) Wazo la Masihi wawili, mmoja wa kifalme na wa pili wa kikasisi, huenda linarudi nyuma hadi kwa Zechariah 4:14 'Hawa ni wale wawili waliopakwa mafuta (upako) ambao wanasimama pembeni ya Mungu wa dunia yote'."

(Encyclopedia Judaica – Eschatology – Messianism)

Nyongeza ya hayo hapo juu, palikuwa na mtu wa tatu ambaye asingeweza kuwa mwingine zaidi ya Mtume Muhammad (*rehma na amani juu yake*):

"Utawala ambao wao (ikim. jamii ya kikasisi ya Qumran) waliupata kutoka kwake (ikim. mwalimu wao) ulikuwa uwe ndiyo mfumo wao wa maisha 'hadi atakapokuja Mtume na wale wa upako wa Aaron na Israeli',"

(1 Nyaraka za kukunja za Qumran 9:11)

(Encyclopedia Judaica – yahad – Eschatological Hope)

Faharisi

FAHARISI

Aaron,

Abd al-Aziz ibn Saud,

Abdullah ibn Hanzala

Abdullah ibn Umar,

Abraham,

Abu Bakr ibn Abi Maryam,

Abu Daud,

Abu Hurairah,

Abu Said Al Khudri,

Adam,

Afghanistan,

Ahl al-Dhimmah

Ahmad bin Hanbal,

Ahmadiyyah (Umoja wa)

Allenby

Al-Dajjal,

Al-Naml,

Al-Nisa

Al-Qaidah,

Al-Zukhruf,

al-Araf,

al-An'am,

al-An'am,

al-Anbiyah

al-Baqarah,

Albert Gore,

Ale-Imran,

Aleem,

al-Fatir,

al-Hazad,

al-Hajj,

al-Hakim,

al-Haram,

al-Hijr,

Ali ibn Abi Talib,

al Jasasah,

al-Kahf,

al-Maidah,

al-Najm,

al-Nawwas ibn Sam'an,

al-Nur,

al-Shu'ara,

al-Zumar,

Anthony Eden,
Arafat,
Ariel Sharon,
Arnold Toynbee,
Austria-Hungary,
Ayoub,
Bahari ya Galilei,
Babilonia,
Baihaqi,
Balfour (Tamko la Balfour),
Bait al-Maqdis,
Banu Israil,
Baysan,
Benki Kuu ya Uingereza,
Biblia,
Bretton Woods,
Byzantium (Warumi),
Chama cha Ukombozi wa Palestina,
Chama cha Shas,
Chechnya,
China,
D'abatul ardh,
Dajjal,
Damaskas,
Daniel Pipes,
Darimi,
Daud,
David Rudge,
David Ben Gurion,
Dhul Qarnain,
Dhul Kifl,
Dola ya Kimarekani,
Dukhan
Durban,
Dwight Eisenhower,
Elias,
Elisha,
Ethiopia,
Encyclopedia,
Ezra,
Fadlur Rahman Ansari,
Fatima bint Qays,
Franz Ferdinand,
Fidel Castro,
Hatma ya Jerusalem,
Fir'auni,
Fitan,
Fitnah,
Fussilat,
Gamal Abdel Nasser,

Gharqad,
George Bush,
Hadith al-Qudsi,
Hal Lindsey,
Halal
Hati / Nyaraka za Dead Sea,
Hejaz,
Henry Ford,
Hijrah,
Hindu,
Hud
Hudhayfah
Hukm,
Imani,
Ibn Kathir,
Ibn Khaldun,
Ibn Majah,
Ibn Sayyad,
Ibn Umar,
Intifada,
Isaiah,
Isma'il Raji Faruqi,
Ishmael
Ishaq,
Islamu,
Israeli Mossad,
Israeli,
Israr Ahmad,
Jabir bun Abdullah,
Jacqueline Kennedy,
Jeshi la Ulinzi la Israeli, (IDF),
Jibril,
Jizyah,
Jerusalem,
Jeremiah,
Jonathan Pollard,
John F. Kennedy
Judaizm,
Joshua,
Judy Shelton,
Ka'aba,
Kaleem Siddiqui,
Kambi ya wakimbizi ya Jenin,
Kashmir
Kaskazini,
khalil,
Khazer,
Khilafah,

Khorasan,
Kinneret,
Konstantinopol,
Khilafa,
Knesset,
Kosovo,
Krusedi,
Kufr
Kumbukumbu ya Taurati,
Lawrence of Arabia,
Libya,
Los Angeles Times,
Lu't
Ludd,
Louis Farrakhan,
M. Asad,
M. Saeed,
Madina,
Maimunah ibn Sa'ad,
Makka
Mapinduzi ya kijinsia,
Masjid al-Aqsa,
Masihi,
Maut,
Mesopotamia,
Mfereji wa Suez,
Mgogoro
Michael Avi-Yonah,
Milenia,
Mirza Ghulam Ahmad,
Mizinga ya Cuba,
Morocco,
Mu'adh ibn Jabal,
Muhammad,
Muhammad Iqbal,
Muqaddamah,
Musa,
Muslim Institute for Research Planning,
Najd,
Nathan,
Nawaaz Sharif,
Nebuchadnezz,
Noah,
Pakistani,
Paundi ya Uingereza,
Pesa,
Qaryah,
Qiblah

Qital,

Qur'an, al Nahl,

Quraish,

R.W. Tawney,

Rabbi Ovadia Yosef,

Riba,

Richard Friedman

Ya'juj na Ma'juj

Saddam Hussein,

Safar al-Hawali,

Saffat,

Sahih Bukhari,

Sahih Muslim,

Sahl bin Sad,

Siku moja kama mwezi,

Siku moja kama wiki,

Siku moja kama mwaka,

Sinai,

Shuaib,

Sunnah,

Suleyman,

Samueli,

Samura ibn Jundad,

Sarayevo,

Saudi Arabia,

Saum,

Shaaban,

Shaikh,

Shamir,

Shirikisho la Kaskazini,

Shirk,

Shetani,

Sura al-Kahf,

Sura ya Banu Israil,

Syria,

Tabariyyah,

Ta Ha,

Taha Jabir,

Taifa la Israeli,

Taifa Tawala,

Talibani,

Tamim al-Dari,

Tashbih,

Taubah,

Tirmidhi,

Uchumi wa Marekani,

Ufalme wa Kiislamu wa Ottoman,

Ufalme wa Kirumi,

Ujerumani,

Ukristo,

Ulaya,

Umoja wa Mataifa,

Umm Salama,

Umm Sharik,

Umar,

Urusi,

Usama ibn Laden,

Usama ibn Zayd,

Utamaduni wa kimagharibi,

Utatu,

Uturuki,

Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia,

Vita Kuu ya Pili ya Dumia,

Vita ya Ghuba,

Wafaat

Warithuddin Muhammad,

Wayahudi wa Israeli,

William Shakespeare,

Wana wa Israeli

Wayahudi wa Kizungu (Ulaya)

Wazayonisti,

Watiberiani,

Ya'juj na Ma'juj

Yassir Arafat,

Yakub,

Yankee,

Yemeni,

Yohana,

Yufretis,

Yunus,

Yuda,

Yusuf,

Yusuf Ali,

Zaburi,

Zainab bint Jahsh,

Zakaria,

Zam zam,

Zughar,